

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Ishirini na Saba – Tarehe 11 Mei, 2021

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

#### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu

**NDG. MOSSY LUKUVI - KATIBU MEZANI:**

#### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,  
WAZEE NA WATOTO (MHE. MWANAIDI ALI KHAMISI):**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA - K.n.y. MWENYEKITI WA  
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO  
YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge, Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Katibu.

**NDG. MOSSY LUKUVI - KATIBU MEZANI:**

### **MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Maswali Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, Mbunge wa Rungwe, sasa aulize swali lake.

Na. 224

**Barabara ya Ibungu – Kafwafwa – Kyimo**

**MHE. ANTON A. MWANTONA** aliuliza:-

Je, ni lini barabara ya Ibungu – Kafwafwa hadi Kyimo itafanyiwa upembuzi yakinifu na kuanza ujenzi kwa kuwa imetajwa kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa *Engineer Godfrey Kasekenya Msongwe*, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, Mbunge wa Rungwe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Ibungu – Kafwafwa – Kyimo ni barabara ya mkoa yenye urefu wa kilometra 68.2 ambapo kilometra 21.8 zipo Mkoa wa Mbeya na kilometra 46.4 zipo katika Mkoa wa Songwe. Barabara hii ni ya changarawe na udongo na inapita sehemu zenye

miinuko mikali hivyo kupitika kwa shida wakati wa mvua kutokana na utelezi. Barabara hii ni muhimu kwa kuwa imekuwa ikitumika katika usafirishaji wa mazao mbalimbali ya chakula na biashara kwa kuwa imepita katika maeneo ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika llani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, Ibara ya 55(c)(iv): Chama cha Mapinduzi kiliahidi kuielekeza Serikali kukamilisha/kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara mbalimbali hapa nchini zenyе jumla ya urefu wa kilometra 7,542.75 ambapo mionganoni mwa hizo ni hiyo Barabara ya Ibungu – Kafwafwa – Kyimo yenye urefu wa kilometra 68.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Ibungu – Kafwafwa – Kyimo ili hatimaye iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, kwa kutambua umuhimu wa barabara hiyo Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) imekuwa ikifanyia matengenezo mbalimbali ili kuhakikisha inapitika majira yote ya mwaka. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, swali la nyongeza.

**MHE. ANTON A. MWANTONA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Wizara. Hii barabara ni muhimu sana kwa upande wa Rungwe lakini pia kwa upande wa lleje. Ni barabara kwa upande wa Rungwe inapita kwenye Kata ya Kyimo, Iponjola pamoja na Ikuti ambapo kuna milima mikali, barabara muda mwingu inakuwa sio nzuri. Kwa hiyo naomba Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ituambie *exactly* ni lini hii barabara itaanza kufanyiwa upembuzi yakinifu ili ijengwe kwa kiwango cha lami? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni lini barabara ambayo pia ipo kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi 2020 - 2025 kutoka Kiwira kupitia Kata ya Kinyala, Igogwe mpaka

Mbalizi itafanyiwa pia upembuzi yakinifu na kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi *Engineer Msongwe*, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kwa pamoja ya Mheshimiwa Anton Mwantona, Mbunge wa Rungwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ya Ibungu - Kalembo - Katengele - Sange - Luswisi - Kafwafwa - Ikuti hadi King'o ni kweli ni barabara ambayo ni muhimu sana kwa wananchi wa lleje na Rungwe. Nataka nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutahakikisha kwamba katika awamu hii ya miaka mitano barabara hii inafanyiwa usanifu na upembuzi yakinifu na mimi ni mnufaika kwa sababu inapita kwenye Jimbo langu na kwenye Kijiji changu pia cha Kalembo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mbunge kwamba barabara hii itafanyika kama tulivyoahidi kwenye llani ya Uchaguzi. Pia, barabara hii ya Kiwira - Kinyala - Igogwe hadi Mbalizi nayo pia iko kwenye llani ambayo nayo pia imeainishwa kati ya barabara zile ambazo zitafanyiwa usanifu wa kina. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Rungwe na wa lleje kwamba barabara hizi tutahakikisha kwamba zinafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ikiwa ni maandalizi ya ujenzi wa lami kadri fedha zitakavyopatikana. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Kabla sijamuita Mbunge atakayeuliza swali la nyongeza, jana niliwakumbusha matakwa ya Kanuni ya 49(2), lakini inaonekana Wabunge bado hamjaisoma. Mbunge mwenye swali lake humu la msingi anatakiwa kusema maneno yafuatayo bila ya kuongeza jambo lingine lolote. Kanuni zetu tulizopitisha; naomba swali langu halafu atataja namba ya swali lake lililopo kwenye orodha ya

shughuli, sasa lijibiwe. Hayo ni matakwa ya Kanuni ya 49(2), tuyazingatie hayo. Mheshimiwa Moni.

**MHE. MOHAMED M. LUJUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa muda ili niulize swali langu la nyongeza. Barabara inayounganisha Wilaya ya Kiteto na Makao Makuu ya Mkoa wao wa Manyara inapita kwenye Jimbo langu, lakini sehemu ya barabara hiyo Kijiji cha Kelema Maziwani daraja limekatika na ni miezi sita sasa. Sasa, naomba kujua ni lini daraja hili litajengwa? (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Moni, Mbunge wa Chemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, *TANROADS* wanafanya tathmini ya barabara zote ambazo zimepata changamoto ya mvua ikiwa ni pamoja na madaraja. Wizara kuitia *TANROADS* kutokana na uzoefu uliotokea miaka miwili, mitatu iliyopita tumeandaa madaraja ya muda kwa ajili ya kutatua changamoto za madaraja ambayo yamesombwa ama kuharibika. Sasa hivi inakuwa ni ngumu kurekebisha hayo madaraja kwa sababu yanahitaji kutengeneza tuta halafu madaraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hata ungeweka sasa hivi ni wazi kwamba daraja hilo litasombwa kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba daraja hilo ambalo liko katika hiyo barabara ya Kiteto Manyara litakuwa ni kati ya madaraja ambayo yatahakikishwa kwamba yanajengwa ili kurudisha mawasiliano ambayo yamekatika kwa kipindi alichokitaja Mbunge. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 225

## **Matukio ya Moto kwenye Shule na Masoko Nchini**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND** aliuliza:-

(a) Je, ni matukio mangapi ya moto yametokea kwenye Shule na masoko katika kipindi cha miaka mitano iliyopita?

(b) Je, uchunguzi uliofanyika ulibaini vyanzo vya moto huo ni nini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita kuanzia mwaka 2016 hadi 2020 ilipokea taarifa 175 za matukio ya moto kwenye Shule na taarifa 55 za matukio ya moto kwenye masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika chunguzi na tafiti mbalimbali za vyanzo vya matukio ya moto katika masoko na mashulenii, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lilibaini vyanzo vya moto kuwa ni migogoro baina ya wanafunzi na menejimenti za shule, lakini matumizi ya umeme yasiyo sahihi, uhalifu, uchomaji wa makusudi (hujuma), hitilafu za umeme, uchakavu wa mifumo ya umeme na uzembe wa kuacha moto kwenye majiko ya mkaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kudhibiti matukio hayo, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaendelea na mikakati ya

kuzuia majanga ya moto kwa kufanya ukaguzi wa majengo na kutoa ushauri na mapendekezo ya kitaalam, yakilambatana na utoaji wa elimu ya kinga na tahadhari dhidi ya majanga ya moto na pia kusisitiza kuwepo kwa vifaa vyaa awali vyaa kuzimia moto yaani (*fire extinguishers*) na vifaa vyaa kung'amu moto yaani (*fire detectors*) na uwepo wa Walinzi katika maeneo husika. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nina maswali mawili ya nyongeza, swali la kwanza; kwa kuwa katika majibu yake ya msingi ameeleza wazi kwamba, Zimamoto huwa wanahusika sana katika kutuliza moto huo endapo majanga yanatokea. Hata hivyo, sio siri mara nyingi Jeshi hilo likifika linakuta magari hayana maji au wamechelewa sasa swali langu kwa Serikali, imejipangaje kuimarisha Jeshi hilo la Zimamoto ili wawe *more efficient?* (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, mioto hiyo ipo katika maeneo yetu tunayoishi au vijijiini au kwenye kata zetu au mitaa yetu, lakini wananchi hao nikiweko mimi hatujapatiwa mafunzo ya kutosha kwenye kuzima mioto mikubwa kama hiyo. Wengi ni waathirika wa maeneo hayo na sitaki kurudi nyuma kukumbusha vilivo ya Shauritanga na mashule mengine ambayo sitaki kutaja ikaja kuharibu sifa za shule hizo kupata wanafunzi. Je. Serikali itatoa lini mafunzo na kwa msisitizo kabisa ili watu hawa wapate elimu ya kusaidia kuzima mioto hiyo? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nachukua fursa hii kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shally Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii kwanza ameuliza, je, ni nini sasa Serikali inafanya au hatua ambazo inazichukua katika kuhakikisha kwamba inapunguza haya majanga ya moto ambayo yanajitokeza mara kwa mara? Ziko hatua nyingi ambazo kama Serikali tumezichukua ili kuona namna ambavyo tunapunguza, hatuwezi kuondosha moja kwa moja kwa sababu, mengine yanakuja, lakini tunapunguza. La kwanza, ni kuendelea kutoa elimu ama kuendelea kutoa taaluma kwa jamii, kwa sababu tunaamini jamii ikipata taaluma ama ikishiba taaluma ya kutosha majanga haya yatapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine tunaendeleza ukaguzi wa majengo. Yapo majengo lazima tuyakague kwanza, yako majengo ya binafsi, yako majengo ya Serikali na yako majengo mengine. Kwa hiyo, tunakuwa tunafanya ukaguzi wa kwenye majengo ili kuona namna ambavyo tunawaelimisha namna ya kujikinga na haya majanga ya moto. Kikubwa zaidi tunao mpango na tumeshaanza, wa kuongeza visima vya dharura kitaalam tunaviita *fire hydrants* ili ikitokezea taharuki kama ya moto tuwe tuna maeneo ya kuweza kuchota maji na kuweza kuokoa maisha ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwamba Je. taaluma huko vijijini inafikaje? Tunavyo vitu vingi ambavyo tumeviandaa ambavyo vinaendelea kutoa taaluma, tunazo zile *fire clubs* ambazo ziko huko vijijini kwenye kata kwenye vijiji, kwenye shehia ambazo zinaendeleza kutoa taaluma kwa watu. Pia hivi karibuni nimewahi kusema sana tu, hivi karibuni tulifanya makubaliano na watu wale wa skauti ambaao wengi wao ni wanafunzi na wako vijijini huko ambaao wanafanya kazi kubwa ya kuendelea kutoa taaluma na kuelimisha jamii namna bora ya kujikinga na haya majanga. Vile vile kuelimisha jamii namna bora ya kutoa taarifa mapema kwa sababu changamoto inakuja kwenye utoaji wa taarifa. Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Mtanda, swalii la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kuuliza swali la nyongeza; kwanza nishukuru kwa majibu ya Serikali, lakini nataka kujuu namna ambavyo Wizara ya Mambo ya Ndani inashirikiana na Wizara ya TAMISEMI wenyewe shule kuhakikisha kwamba matukio haya sasa yanakoma kwa sababu, yamekuwa yakisumbua mara kwa mara katika shule zetu hasa za mabweni. Ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Hamza Hamis Hamis, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimtoe hofu tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunao ushirikiano wa karibu baina ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na TAMISEMI na hata hawa watu wa Wizara ya Elimu katika kuhakikisha kwamba tunapunguza idadi kubwa ya majanga ya moto na majanga mengine hasa katika maeneo ya shule na maeneo mengine. Tayari tumeshakuwa tunakaa vikao mbalimbali, tumeshapanga mipango mbalimbali ambayo ni mikakati ya kuhakikisha kwamba tunapunguza haya majanga.

Kwa hiyo, hilo Mheshimiwa asiwe na wasiwasi juhudii zinaendelea kazi inaendelea na tutahakikisha kwamba tunapunguza haya majanga kwa kiasi kikubwa. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Hai, sasa aulize swali lake.

Na. 226

**Kufufua Zao la Kahawa Hai**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE** aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la Kahawa limekuwa likilimwa kwa wingi katika Jimbo la Hai lakini zao hili kwa sasa limekosa tija.

Je, Serikali haioni kuwa ni wakati sahihi wa kufufua zao hilo katika Jimbo la Hai?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo. Majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saashisha Elinikyo, Mbunge wa Hai kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshaanza kuchukua hatua za kufufua zao la Kahawa katika mkoa wa Kilimanjaro likiwemo Jimbo la Hai. Hatua hizo zinatokana na kushuka kwa uzalishaji kutoka tani 3,486 mwaka 2014/2015 hadi kufikia tani 1,428 mwaka 2020/2021 sawa na asilimia 59. Kushuka huko kumechangiwa na baadhi ya wakulima kuacha kuyahudumia mashamba kulikosababishwa na kuzorota uliokuwa muhimili wa uzalishaji wa kahawa Mkoani Kilimanjaro. Sababu nyingine iliyochangia ni mabadiliko ya tabia nchi yaliyopelekea ukame na kukosekana kwa maji ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na jitihada za kufufua zao la kahawa Mkoani Kilimanjaro likiwemo Jimbo la Hai kwa kufanya mambo yafuatayo:-

(i) Kukifufua na kukijenga upya Chama Kikuu cha Ushirika wa Kahawa Mkoaa wa Kilimanjaro *KNCU* kwa kurejesha mali zilizouzwa kiholela na kuwachukulia hatua za kisheria waliosababisha ubadhilifu wa mali za Ushirika;

(ii) Kuimarisha Taasisi ya Utafiti wa kahawa Tanzania (*TaCR*) kwa kuipa rasilimali ili itekeleze majukumu yake

kikamilifu ya utafiti wa zao la kahawa na uzalishaji wa miche bora ya Kahawa;

(iii) Kuhamasisha upandaji wa miche bora ya kahawa kwa kuwauzia wakulima kwa bei ndogo ya shilingi 100 ambapo jumla ya miche 1,203,300 imesambazwa kwa wakulima 3,270 na miche 810,000 imesambazwa katika Wilaya ya Hai;

(iv) Kumaliza migogoro ya kimkataba iliyopo kati ya Vyama vya Ushirika na Wawekezaji katika mashamba 17 ya kahawa; na

(v) Kufufua na kuimarisha viwanda 12 vya kati vya kuchakata kahawa *CPU* vinavyomilikiwa na wakulima wadogo, Viwanda vyote hivyo viro katika Wilayani Hai.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hizi zinazochukuliwa na Serikali zitachochea ufufuaji wa zao la kahawa Mkoani Kilimanjaro ikiwemo Wilaya ya Hai na maeneo mengine nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante. Naomba sasa kwa kuwa bei ya kahawa kwenye soko la dunia kwa kilo moja inaenda takribani shilingi 9,660 lakini mkulima ambaye anakwenda kuuza kahawa yake kuititia Vyama vya Ushirika kilo moja ananunua kwa shilingi 2,000 bila bakaa.

Je, Serikali haioni iko haja ya kutoa au kuondosha au kupunguza tozo zinazotokana na zao la kahawa ili mwananchi yule ambaye ni mkulima aweze kunufanika na bei hii ya kahawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Lakini swali la pili, kwa kuwa sasa wananchi wa Jimbo la Hai wako tayari kulima kahawa.

Je, Serikali ipo tayari kusambaza pembejeo kwa bei ambayo ni Rafiki kwa wakulima? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni kweli leo katika soko la dunia kwa bei ya mpaka jana wastani wa *Arabica* ilikuwa ni Dola 3 wakati wastani wa *Robusta* ilikuwa Dola 1.5. Na sisi kama wizara na Serikali tumeanza kupitia mjengeko wa bei ambao unahusisha tozo mbalimbali na leo mimi binafsi nitaongoza kikao kitakachohusisha Vyama vya Ushirika hasa vya Mkoa wa Kagera ndio tunaanza navyo. Kwa hiyo, hili la kwamba kuangalia suala la tozo wanazotozwa wakulima katika bei tutalipitia ili wakulima waweze ku-*benefits* na bei na zao lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu pembejeo, Serikali sasa hivi inachukua hatua njia pekee ya kuwasaidia wakulima wadogo wadogo ni kupitia ushirika. Tumefanya majaribio katika sekta ya pamba tumeona wakulima wamepata pembejeo za kutosha katika msimu uliopita kupitia Vyama vya Ushirika. Tumefanya majaribio katika tumbaku, wakulima wamepunguza gharama za pembejeo kwa zaidi ya asilimia 40 kwasababu zinanunuliwa in *bulk* badala ya mkulima mmoja mmoja kwenda sokoni kununua. Kwa hiyo tunajenga Vyama vya Ushirika na nimuahidi Mheshimiwa Mbunge na niwaahidi Waheshimiwa Wabunge wote kwamba tutaangalia njia bora ya wakulima wa zao la Kahawai li Ushirika wao uweze kuwa imara waweze kupata pembejeo katika mfumo wa *bulk* na waweze kuzinunua kwa bei *competitive* ya soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakiri mkulima mmoja mmoja kwenda dukani kununua pembejeo moja moja gharama yake inakuwa ni kubwa na wengi wanashindwa kuhudumia mazao. Kwa hiyo, tupokee wazo la Mheshimiwa Mbunge tutatafuta *mechanism* sahihi ya kuwashudumia wakuliwa wa Kilimanjaro kupitia ushirika wao waweze

kununua pembejeo kwa pamoja na hiyo itawapunguzia gharama.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Judith Kapinga swali la nyongeza.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa swali la nyongeza. Wilaya ya Mbanga ni mojawapo ya wilaya zinalima zao la kahawa kwa wingi lakini Vyama vya Ushirika vimekuwa vikichelewesha malipo na hivyo wakulima kushindwa kununua pembejeo za kuhudumia mazao yao kwa wakati.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha utendaji kazi wa vyama vya ushirika ili wananchi wa Wilaya ya Mbanga waweze kulipwa fedha kwa wakati na hivyo kuwawezesha kununua pembejeo za kuhudumia zao lao kahawa kwa wakati?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kumekuwa na changamoto kwasababu mfumo wa ulipaji siku zote umekuwa ni kwamba baada ya mnada fedha zinalipwa kwenye Chama Kikuu cha Ushirika, Chama Kikuu cha Ushirika kina hamishia fedha katika Chama cha Msingi. Kwa hiyo tumefanya kikao mwezi Aprili na Vyama vya Ushirika vya Mkoa wa Ruvuma kwa maana ya Wilaya ya Mbanga, utaratibu tunaoelekea sasa hivi kuutekeleza katika vyama vya msingi na vyama vikuu vya ushirika ni kwamba mnada unapoisha mnunuzi anatakiwa alipe malipo ndani ya saa 48 na malipo yale yatakwenda moja kwa moja kwa mkulima hayatopitia kwenye ukiritimba wa kwenda kwenye chama kikuu chama kikuu kwenda kwenda kwenye chama cha msingi. Kwa hiyo nimuahidi Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wengine tuna-*perfect system* ya kulipa baada yam nada malipo yaende moja kwa moja kwa mkulima badala ya kupitia kwenye vyama kwasababu huko kunaleta ukiritimba na kuchelewesha malipo.

**NAIBU SPIKA**, Mheshimiwa Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante sana kwa kunipa fursa. Shirika la Utafiti wa Kahawa *Tanzania Coffee Research Institute* limezalisha aina chotara za kahawa ambazo huwa huzaa mara tano zaidi ya zile kahawa za asili zilizokuwa zinaitwa Kent. Wakulima wengi wanalima hizi kahawa za zamani ni lini Serikali itaanlisha program maalum ya kuwafundisha wakulima umuhimu wa hizi kahawa mpya chotara kutoka Lyamungo ili waweze kuongeza tija? Wanahitaji mafunzo sana. Ahsante. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Moshi Vijijini na kwa niaba ya Serikali na Wizara ya Kilimo ni-*acknowledge* kazi alioifanya katika sekta ya kilimo akiwa bado chuoni. Ni kwamba Serikali imekwisha anza kazi na tumeanza kuwatumia wataalam wetu wa *TaCRI* na tumeshaanza *multiplication*ya miche la kisasa ambayo tunaanza kuipeleka kwa wakulima. Tumeanza kuigawa miche hii kwa baadhi ya wakulima na kuwapa elimu. Kwa hiyo program hiyo imeshaanza na elimu imeshaanza kutolewa kwa wakulima umuhimu wa kwenda kwenye hybrid ili waweze kuongeza mapato yao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Assa Makanika, swali la nyongeza.

**MHE. ASSA N. MAKANIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa changamoto ambazo zinakabili zao hili la kahawa katika Jimbo la Hai zinafanana pia changamoto ambazo zinakabili wakuliwa katika Jimbo letu la Kigoma Kaskazini. Ukiangalia moja wapo ya changamoto ni soko na mkulima kuwa na uhuru wa zao hili kahawa kuza anapotaka. Vyama

hivi nya Ushirika vinawafunga wakuliwa wetu, hawawezi kuza kahawa zao endapo mnunuzi huru atafika katika maeneo husika. Je Serikali inaweza kutupa tamko leo juu ya hilo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni vizuri Waheshimiwa Wabunge tukaelewa kwamba kuna *miss conception* juu dhana ya ushirika. Ushirika haumzui mnunuzi binafsi kwenda kununua zao la mkulima. Ushirika ni mfumo wa wakulima wanaokusanya zao lao pamoja na wakulima wale wanauza kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, *experience* imeonesha kwamba pale ambapo kunakuwa hakuna mfumo wa ushirika hasa katika mazao haya kama kahawa, pamba, korosho na mazao mengine yote wakulima wamekuwa wakiiza zao lao bei ndogo sana. Kesi iliyoko Kigoma Kaskazini na Mheshimiwa Mbunge tumeongea naye mimi zaidi ya moja mara mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema kama kuna mnunuzi binafsi anataka kununua zao la mkulima hasa kahawa, hasa Kigoma Kaskazini na wewe mwenyewe nimekwisha kwambia mlete tutamruhusu atakwenda kununua kwenye Chama cha Msingi atuambie bei anayonunulia ni shilingi ngapi na *volume* anayotaka kununua ni kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka *transparent* kwenye mfumo huu, hatulazimishi kwenda kwenye Chama Kikuu cha Ushirika. Tunamruhusu kwenda kwenye Chama cha Msingi na yoyote anayetaka aje hata jana nimekaa na wanunuzi wanaotaka kununua kwenye Vyama vya Msingi kwenye Wilaya ya Karagwe, Wilaya ya Kyerwa sasa hivi wanasantini makubaliano na Vyama vya Msingi ili waweze kununua kwa bei inayofanana na soko tusipofanya hivyo tutarudisha mifumo isiyokuwa rasmi na wakulima watanyonywa sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tuendelee na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini sasa aulize swali lake.

Na. 227

### **Kuanza Utekelezaji Mradi wa Maji Katerela**

**MHE. OSCAR I. KIKOYO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Katerela kwa ajili ya Kata za Kasharunga na Rulanda.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Engineer Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante. kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini Kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jitihada za kuhakikisha wananchi Wilayani Muleba wanapata huduma ya maji, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali imekamilisha miradi ya maji ya Bulembo, Kasharunga, Ruteme, Illogero na Kyota. Pia, utekelezaji wa miradi ya Nshamba, Kishamba na Kashansha unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Mei, 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia RUWASA katika mwaka wa fedha 2021/2022 imepanga kuanza ujenzi wa mradi wa maji kutoka chanzo cha maji Katerela utakaowanufaisha wakazi wapatao 19,619 katika Kata za Kasharunga na Rulanda. Mradi huu unatarajiwa kugharimu kiasi cha shilingi million 700 ambapo utahusisha ujenzi wa chanzo cha maji, ujenzi wa matanki mawili ya maji ukubwa wa litu 200,000 na litu 300,000, ujenzi wa nyumba ya mtambo,

vituo vya kuchotea maji 25 na ujenzi wa mtambo wa bomba za maji umbali wa mita 40,130.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Lakini ninalo swali moja tu la nyongeza. Kutokana na uhaba mkubwa wa maji katika Wilaya ya Muleba na jioagrafia ya Wilaya ya Muleba inapakana na Ziwa Victoria. Serikali inao mpango wowote wa kutumia Ziwa Victoria kuvuta maji kwa ajili ya Wilaya ya Muleba? (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, *Engineer Maryprisca Mahundi*, m ajibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mhehsimiwa Naibu Spika, Mradi wa Ziwa Victoria ni mradi wa kimkakati na ni mradi ambao tunautarajia uhudumie maeneo mengi sana kwasababu ni mradi unaopita katika majimbo mengi na mikoa mbalimbali. Hivyo niweze kumwambia Mhehimiwa Mbunge kwamba maeneo yake ambayo bomba hili kubwa litakuwa likipita basi na yeye atanufaika katika vijiji vile ambavyo viko kilometra 12 kutoka kwenye bomba kwa pande zote kulia na kushoto.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Felista D. Njau, swali la nyongeza.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nilikuwa nataka niiulize Serikali ni lini itamaliza kero ya maji ambayo imekuwa ni sugu katika Kata ya Wazo, Mitaa ya Nyakasangwe, Mitaa ya Salasala na Mivumoni Kata ya Mbezi Mtoni, Sakurveda na Mabwepande Mtaa wa Mbopo?.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, *Engineer Maryprisca Mahundi*, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia *DAWASA* wanafanya kazi nzuri sana maeneo yote ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja. Na tayari mikakati kabambe inaendelea na kufikia mwaka ujao wa fedha maeneo mengi sana ya maeneo hayo yote uliyoyataja Mheshimiwa Mbunge yatakuwa yamefikiwa na maji bombani.

**NAIBU WAZIRI:** Waheshimiwa sasa tuelekee kwenye swali la Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi.

Na. 228

### **Kuwasaidia Wananchi wa Mji wa Itigi Kuvuna Maji**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE** aliluliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya kuwasaidia Wananchi wa Mji wa Itigi kuweza kuvuna maji katika Mbuga inayozunguka Mji huo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Engineer Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Itigi ni miongoni mwa miji miwili iliyopo katika Wilaya ya Manyoni. Mji huu unakadirwa kuwa na wakazi wapatao 32,000. Serikali imeendelea kutekeleza ahadi ilioitoa kwa kuwasaidia wananchi wa maeneo yanayozunguka Mji wa Itigi kuweza kuvuna maji ambapo imekamilisha utambuzi wa awali wa maeneo ambayo yanafaa kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa katika Mji wa Itigi na katika Kijiji cha Kayui, Kata ya Magandu, Kijiji cha Muhanga, Kata ya Ipande pamoja na Kijiji cha

Kaskazi, Kata Kitaraka ambayo yameonekana yanafaa kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali itakamilisha usanifu wa kina na kuainisha ukubwa wa mabwawa yatakayojengwa kuanzia mwezi Januari, 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika mwaka wa 2020/2021 katika kuimarisha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Mji wa Itigi Serikali imekamilisha ujenzi wa mradi wa maji mkubwa unaohudumia vijiji sita vya Songambele, Mlowa, Majengo, Tambukareli, Zinginali na Itigi. Mradi huu umekamilika mwezi Disemba, 2020 na kugharimu shilingi bilioni 2.64. Mradi umewezaresha upatikanaji wa maji katika Mji wa Itigi kufikia asilimia 80.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Omary Massare swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii niulize maswali madogo mawili ya nyongeza. pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali juu ya upatikanaji wa maji katika maeneo yetu hasa Mji wa Itigi ambapo mimi ndio Mwakilishi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi hii ya kuvuna maji katika Mji wa Itigi, ni swali la pili nauliza katika Bunge hili, Bunge lililopita niliuliza swali kama hili. Majibu yalikuwa tunajiandaa, dalili inaonesha kwamba watafanya.

Je, ni lini sasa uvunaji huu utaenda kufanya katika Mji wa Itigi na maeneo ambayo umeyataja ya Kayui, Muhamaga na Kaskazi kujenga mabwawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Lakini swali la pili, nashukuru pia Serikali kwa kukamilisha mradi mkubwa wa maji katika Mji wa Itiga ambao una manufaa makubwa kwa wananchi lakini unawatua akina mama ndoo kichwani. Lakini gharama za kuunganisha maji yale kwenda ndani ni gharama kubwa sana. kwa hiyo, mtu wa kijijini kwa shilingi 200,000 ni hela nyingi. Je, Serikali ipo tayari kupunguza gharama za uunganishaji maji ili wananchi wanufanike na mradi huu

mkubwa ambao Mbunge wao amehangaika nao kuupata na wizara imesaidia? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, *Engineer Maryprisca Mahundi*, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, uvunaji huu wa maji tunautarajia kuutekeleza katika mwaka wa fedha ujao kwa maana mwaka 2021/2022. Mheshimiwa Mbunge ahadi hii imekuwa ikitolewa toka huko awali lakini kwa sasa hivi kama tulivyokuwa tumeendelea kuongea *RUWASA* imekuwa ni mkombozi, *RUWASA* imekuwa ni chachu ya mageuzi ya utekelezaji wa miradi ndani ya Wizara. Hivyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge ili sasa linaingia kwenye utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusiana na ghamra za uunganishaji, hili nalo limekuwa ni tatizo sugu. Hata hivyo, kama tulivyomsikia Mheshimiwa Waziri wakati wa uwasilishaji wa bajeti, ni suala ambalo tayari lipo katika uangalizi mkubwa ambapo tunahitaji kuona wananchi wanaenda kupata nafuu kubwa katika uunganishwaji wa huduma ya maji sio tu katika Mji wa Manyoni bali kwa Tanzania nzima.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimuite Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero, sasa aulize swali lake.

Na. 229

#### **Mradi wa Maji Kiburubutu Ifakara**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Mradi wa Maji wa Kiburubutu katika Jimbo la Kilombero?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, *Engineer Maryprisca Mahundi*, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilipata mkopo kutoka Serikali ya India kupitia Benki ya Exim India jumla ya dola za Marekani millioni 500 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi katika miji 28 nchini ukiwemo Mji wa Ifakara ambao utapata maji kupitia chanzo cha Lumemo. Mradi utahudumia jumla ya Kata tisa na vijiji tisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu za kupatikana kwa wakandarasi watakaotekeleza mradi huu zimeshakamilika na unatarajiwu kuanza wakati wowote katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 na ujenzi wa mradi umepangwa kutekelezwa kwa miezi 24.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kilombero, napenda kushukuru kwa majibu mazuri ya Wizara na tunaombea kweli huu mkopo upatikane na mradi huu ufanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, je, ni lini Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kutembelea Jimbo la Kilombero ili apite angalau kuzungumza na wananchi wa Zinginai, Magombera, Kanyenja, Mpanga na Muhelule ambao wana shida kubwa ya maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kutokana na hali ya udharura wakati tukisubiri mradi huu wa maji tayari Serikali ilishachimba kisima kikubwa katika Kata ya Lumemo

ambapo kinatoa lita 30,000 kwa saa. Changamoto ni tenki la kuhifadhi maji yale kuwasambazia wananchi. Katika hali hii ya udharura, je, Serikali haiwezi kutujengea tenki wakati tunasubiri mradi wa maji wa Kiburubutu - Ifakara? (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Engineer Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la kwenda Kilombero ni moja ya majukumu yangu. Mheshimiwa Mbunge mara baada ya Bunge hili tutaweka utaratibu mzuri ili niweze kufika hapo. Naamini mpaka mwisho wa Bunge hili hata mradi huu utekelezaji utakuwa umeanza, kwa hiyo, nitakuja nikwiwa na bashasha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na ujenzi wa tenki kwa kisima kile ambacho tumekichimba, nia na dhamira kabisa ya Wizara ni kuona wananchi wanapata maji kwa umbali mfupi. Tumeshaweza kutoa fedha ya kuchimba kisima ni dhahiri lazima tutoe fedha ya ujenzi wa tenki. Nimuahidi Mheshimiwa Mbunge, kabla ya mwaka huu wa fedha kuisha, ujenzi wa tenki utaanza kufanyika. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tuelekee Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalii lake.

Na. 230

### **Kuunganisha Mfumo wa Gesi Soko La Feri - Manispaa ya Mtwara Mikindani**

**MHE. TUNZA I. MALAPO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaunganisha mfumo wa gesi asilia kwa ajili ya kupata nishati ya kukaangia samaki katika Soko la Feri Manispaa ya Mtwara Mikindani?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Stephen Lujwahuka Byabato, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (*TPDC*) inaendelea na kazi ya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia katika mikoa mbalimbali nchini ukiwemo Mkoa wa Mtwara kwa ajili ya matumizi ya viwandani, majumbani na taasisi za umma na binafsi. Katika Mkoa wa Mtwara, mradi huu unahuisha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia kwa njia za mabomba na vituo vya kuongeza mgandamizo wa gesi (*Compressed Natural Gas (CNG) Stations*).

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia katika Soko la Feri katika Manispaa ya Mtwara Mikindani upo katika hatua ya kukamilisha usanifu wa kina wa kihandisi, utakaofuatiwa na hatua ya kumpata mkandarasi wa ujenzi wa mradi huo. Kazi ya usanifu inatarajiwaa kukamilika mwezi Agosti, 2021 na ujenzi kuanza Desemba, 2021 na kukamilika Juni, 2022. Gharama za mradi ni takribani shilingi bilioni 10.11.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Malapo, swalii la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la kwanza, nataka kujua ni sababu zippi zinazosababisha kusuasua kwa usambazaji wa gesi kwa matumizi ya binadamu katika Mkoa wa Mtwara hususan Manispaa ya Mtwara Mikindani?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, sisi watu wa Mtwara kabla hatujapata gesi kwa matumizi yetu, gesi imepelekwa Dar es Salaam na watu wameunganishiwa majumbani. Kwa nini wameanza Dar es Salaam badala ya Mtwara ambako gesi inatoka kwa sababu na sisi pia tuna matumizi nayo? Nakushukuru. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kwa pamoja ya Mheshimiwa Tunza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kusema kwamba usambazaji wa gesi katika Mkoa wa Mtwara hausuisui. Tulianza kuzalisha gesi katika Mkoa wetu wa Mtwara mwaka 2015 na mpaka sasa tunatumia umeme wa gesi peke yake kwa Mkoa wa Mtwara, Lindi na mikoa mingine yote ya Kusini. Umeme wote unaotumika kule unatokana na nishati ya gesi. Mpaka kufikia mwezi Julai mwaka huu, tayari nyumba 425 zitakuwa zimeunganishwa na huduma ya gesi majumbani kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ni la kufurahisha, watumiaji wakubwa sana wa gesi Tanzania wa kwanza ni *TANESCO* na wa pili ni kiwanda chetu cha Dangote ambacho kiko Mtwara. Kiwanda hicho kinatoa ajira kwa vijana wetu, watu wanalipa kodi na Serikali inapata manufaa makubwa sana. Kwa hiyo, ni mojawapo ya faida kubwa sana ambayo inapatikana kule. Tunazo taasisi kama nne, Magereza, *VETA*, shule moja ya sekondari na chuo kingine kimoja, zinatumia gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda kusema kwa kweli Serikali imejitahidi sana kuhakikisha wananchi wa Mtwara wananufaika na nishati hii. Hata hivyo, kwa sababu nishati ni kwa ajili ya Watanzania wote basi nyngine kidogo inatoka na kwenda kwingineko mpaka hapa Dodoma tutaweza kuifikisha kwa wakati. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa tunaendelea na swalii la Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Mbunge wa Longido.

Na. 231

**Fidia kwa Wananchi Waliopitiwa na Njia ya Umeme wa Msongo Mkubwa wa KV 400**

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA** aliuliza:-

Umeme wa msongo mkubwa wa KV 400 toka Singida hadi Namanga umepita katika baadhi ya maeneo ya wazi na malisho ya mifugo 6 kwenye Vijiji vya Engikaret, Ranchi, Orbomba, Kimokouwa na Eorendeke; na fedha za fidia ilipendekezwa zitolewe kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ya Vijiji husika pamoja na watu binafsi ambao umeme huo umepita kwenye makazi yao:-

Je, ni lini fedha hizo zitatolewa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Shirika la TANESCO inaendelea kukamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 400 kutoka Singida hadi Namanga. Lengo kuu la mradi huu ni kuimarisha umeme katika Gridi ya Taifa na kuunganisha Tanzania na nchi za Zambia na Kenya katika gridi ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mradi huu mwezi Septemba, 2020 Serikali kupitia TANESCO ililipa fidia jumla ya

shilingi bilioni 11.33 kwa wananchi wapatao 645 katika Wilaya ya Longido ikiwamo Vijiji vya Engikaret, Ranchi, Orbomba, Kimokouwa na Eorendeke. Malipo hayo yamelipwa kama ifuatavyo; Kijiji cha Eorendeke jumla ya shilingi 439,780,320, Kijiji cha Kimokouwa jumla ya shilingi 165,564,000, Kijiji cha Orbomba jumla ya shilingi 343,662,080 na Kijiji cha ranchi jumla ya shilingi 720,754,200.

Mheshimiwa Spika, malipo ya fedha hizi yalifanyika kwa njia ya hundi kupitia Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niullize maswali madogo mawili ya nyongeza. Kabla sijaauliza maswali yangu, naomba tu niweke wazi kwamba sijaridhishwa na majibu ya Serikali kwa swali langu kwa sababu nilitegemea kwamba nitapewa mchanganuo wa hii bilioni 11.33 kwa kuonesha katika kila kijiji ni watu wangapi wamefidiwa kiasi gani na kiasi gani kimekwenda kwenye maendeleo ya vijiji husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini haiishii hapo Kijiji hiki cha Engikaret mahesabu yake hayapo katika jibu moja kwa moja. Ukiangalia hiyo bilioni 11.33 kwa mchanganuo uliotolewa inaonesha ni shilingi bilioni 1.669 tu ndiyo imefika na hiyo bilioni 9.660 sijaelewa kwamba mahesabu yake yamekwenda wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo swali langu la kwanza la nyongeza ni kuhusu kijiji cha Engikaret. Kwa kuwa, kulikuwa na wananchi 46 ambao walileta malalamiko yao kwamba wako kwenye njia ya umeme na wakaenda wakafanyiwa tathmini na kuna wengine 66 waliletwa hivi karibuni.

Je, watu hawa ambao kwa ujumla wao sasa ni zaidi ya watu 112 watalipwa lini hiyo fidia?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kuna umeme ambaao ulielekezwa Tarafa ya Ketundeine, umeme wa *REA* ukifanywa na kampuni yetu ya *TANESCO*. Kasi ya umeme huo ni ndogo sana na tulitegemea mwezi Julai mwaka jana ungewashwa katika vijiji 10 vya awali kwenye Tarafa hiyo yenye vijiji 19. Je, umeme huu wa Ketundeine utakamilishwa lini? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba njibju maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Steven, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatilaji mkubwa ambaao ameendelea kuufanya katika eneo lake. Niseme tu kwamba huo mchanganuo aliousema wa *item* moja moja kwa ajili ya wananchi baada ya hapa nitauagiza utengenezwe na nitaweza kumpatia kwa ajili ya kuona nani amelipwa nini ili aweze kuwasemea wananchi wake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika eneo la malipo nieleze tu kwamba tulipata changamoto kidogo. Katika kijiji cha Engikaret tulivyofanya tathmini mara ya kwanza ilionekana kwamba ni eneo la kijiji lakini wakati pesa imekwenda kulipwa wakaja wananchi wengine takriban 40 na zaidi wakasema wana haki katika eneo hilo na sisi tukawafanya tathmini kutoka kwenye ile ya kijiji ili wao walipwe. Kabla ya pesa ile hajalipwa wakajitokeza wananchi wengine zaidi ya 50 wakiwa na malalamiko hayo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo, yakawepo makubaliano kati ya *TANESCO* na Ofisi ya Mkurugenzi na Mkuu wa Wilaya kwamba kwa kuwa lile eneo lote liliifanyiwa tathmini likiaminika ni la Serikali basi Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Halmashauri zitathmini ni nani anastahili kulipwa nini katika eneo hilo na pesa ile ambayo tayari ipo katika akaunti ya Halmashauri iweze kutumika kwa ajili ya

malipo hayo. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, pesa tayari imeshalipwa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri na yeye anaendelea na utaratibu wa kuhakiki ni nani anastahili kulipwa kama mmojawapo wa wale ambao wako katika eneo hilo.

Katika swali la nyongeza la pili, ni kweli kwamba mradi huo wa vijiji 19 umechelewa. Tulikubaliana na mkandarasi ukamilike kabla ya mwezi Juni mwaka huu na siku siyo nydingi Mheshimiwa Waziri wa Nishati atakuja kuzindua mradi huo kabla ya Mwaka huu wa Fedha kuisha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimruhusu sasa Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Mpanda Mjini anayeuliza swali lake kwa Wizara ya Afya sasa aulize swali lake.

Na. 232

### **Kusuasua kwa Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa Katavi**

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamaliza ujenzi wa Hospitali ya Rufaa Katavi kwani ujenzi huo unakwenda kwa kusuasua?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Mpanda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea na ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Katavi ambapo kwa sasa ujenzi umekamilika kwa wastani wa asilimia 70. Ujenzi kwa upande

wa maabara umefikia asilimia 98 na jengo kuu la hospitali umefikia asilimia 42. Mradi huo unagharimu jumla ya shilingi bilioni 9.82 ambapo hadi sasa kiasi cha shilingi bilioni 3.97 kimetolewa na kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2021/2022, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 57 kwa ajili ya ukamilishaji wa miundombinu ya Hospitali za Rufaa za Mikoa, ikiwemo Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi, ambapo kiasi cha shilingi bilioni 5.85 zitatumika kukamilisha ujenzi huu ifikapo Januari 2022.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sebastian Kapufi, swali la nyongeza.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFİ:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, mbele ya Rais kwa maana ya Hayati Rais Dkt. John Pombe Magufuli, Mheshimiwa Waziri Ummy alituhakikishia kwamba itakapofika mwezi Julai, 2020 hospitali hiyo itakuwa imekamilika. Serikali inasema nini kwa Wanakatavi kutokana na ahadi hizi zisizoteklezeka? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili Mkoa wa Katavi umbali kutoka Katavi ikitokezea amepatikana mgonjwa, anahitaji tiba na madaktari bingwa ama umpeleke Mbeya, Mwanza au Dar es Salaam. Umbali huu ukiwa salama na katika mazingira ya amani unaweza ukaenda bila matatizo, lakini ukiwa katika hali ya mahtuti, umbali unakuwa ni mrefu zaidi. Serikali inasemaje katika namna ya kuwanusuru Wanakatavi kuja na suala zima la dharura nikizingatia yapo maeneo mengine hospitali zimejengwa kwa fedha ambayo ni zaidi ya hiyo bilioni tisa? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Dkt. Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,  
WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL):**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji mkubwa sana wa hali ya afya ya Mkoa wake na Wabunge wa Mkoa huo kwa sababu wamekuwa wakija Wizarani na nakumbuka alikuja pamoja na Wabunge wenzake. Waziri wa Afya alinituma nikaja Mkoani kwao, ni kweli kama Mbunge anavyosema kwa rufaa tu pale kwao wanatumia shilingi milioni 250 kwa mwaka kwa ajili ya *ambulance* tu kupeleka watu rufaa. Kwa hiyo, anachosema ni kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii lake la kwanza anasema hospitali hiyo iliahidiwa kumalizika mwaka jana na bahati mbaya hajafanyika kama ahadi ilivyokuwepo. Kama unakumbuka tulikwenda Wizarani na tayari Waziri wa Afya ameunda timu na imechunguza sababu ambazo zimesababisha hizi hospitali zichelewe na sababu hiyo utaletewa Mheshimiwa Mbunge. Vilevile tumeshatengeneza *strategy* ambayo kwa uhakika kabisa Januari, 2022 hospitali hiyo inakwenda kumalizika ili kuondoa wananchi katika adha hiyo ambayo tayari ulishakwenda kunionesha Mkoani kwako.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili umezungumzia umbali, tulipokwenda mkoani kwako ulielezea suala la ramani ambayo mlitaka hasa kwenda kwenye hospitali za kanda. Ile ramani ambayo ulikuwa unaizungumzia Mheshimiwa Mbunge, tayari Waziri ameshakaa na timu yake na hata yale mapendekezo yenu ya kupunguza rufaa hasa kuelekea kwa hospitali za kanda inatafutiwa suluhisho na itafanyiwa kazi vizuri kama ambavyo mlitegemea ifanyike Wabunge wa Mkoa wenu. Ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, swalii la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini sasa Serikali italeta mashine za *CT-scan* na *MRI* kwa ajili ya Hospitali za Mikoa

hususan Mkao wa Manyara kwa kuwa gharama ni kubwa za wagonjwa wa magonjwa makuu kwenda kwenye Hospitali za kKnda? (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na watoto Mheshimiwa Dkt. Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kutoka Mbulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama anavyosema hata kwenye bajeti ya mwaka huu Serikali imejipanga, siyo tu kuweka *CT-Scan* kwenye hospitali za kanda, bali pia kwenye hospitali za mikoa. Tayari Hospitali ya Mkao kama Mwananyamala; na sasa hivi tunavyozungumza nilikuwa naongea na Meneja wa *MSD*, kuna *CT-Scan* mbili ambazo ziko njiani kwa ajili ya kufunga kwenye hospitali mbili za mikoa; na jinsi fedha zitakavyokuwa zinapatikana, Serikali itahakikisha kwamba hospitali zote za mikoa zinapata *CT-Scan* na hasa tutazingatia umbali kutoka *CT-Scan* moja kwenda nyingine ili kuhakikisha kwamba zinawekwa kwenye *angle* ambazo zitapunguzia wananchi adha ya kwenda mbali kufuata *CT-Scan*.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai, Mbunge wa Karatu, sasa aulize swali lake.

Na. 233

### **Mgogoro wa Wananchi wa Bugeli na Hifadhi ya Manyara**

**MHE. DANIEL A. TLEMAI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua mgogoro wa Wananchi wa Bugeli na Hifadhi ya Manyara pamoja na mauaji ya Wananchi yanayotokea mara kwa mara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Daniel Tlemai Awack, Mbunge wa Karatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Bugeli, hasa wafugaji wanapoingiza mifugo hifadhini na kukamatwa na Askari wa Hifadhi, wamekuwa na tabia ya kukataa kutii sheria bila shuruti na kupiga yowe maalum ijulikanayo kama "*hayodaa*" ikiwa ni kiashiria cha hatari kubwa kwa kabile la Kiiraki. Hivyo, baada ya yowe hiyo kupigwa, wananchi wengi hupata morali na kujitokeza wakiwa na silaha za jadi zikiwemo fimbo, mishale, mapanga na mikuki ili kipinga ukamataji huo wa mifugo na kuchukua mifugo yao kwa kutumia nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kumekuwepo na baadhi ya matukio ya Askari kunyang'anywa silaha au mifugo iliyokamatwa hifadhini na wananchi ambapo husababisha kutokuelewana kati ya Askari wa Hifadhi na wananchi. Pamoja na taharuki hizo, kumekuwepo pia na mauaji ya Askari wapatao wawili na majeruhi kwa Askari watatu katika eneo hilo. Aidha, matukio kama haya yamekuwa yakijitokeza katika maeneo mengine yanayozunguka hifadhi mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikiunda Kamati mbalimbali kuchunguza matukio hayo ili kubaini chanzo cha changamoto hizo. Kwa ujumla, imebainika kuwa tatizo kubwa ni wananchi kutoheshimu makubaliano ambayo yamekuwa yakifanywa mara kwa mara kati ya Uongozi wa Wilaya, Hifadhi, Serikali ya Kijiji na wananchi kuhusu taratibu za kufuatwa na wananchi hao pindi wao wenyewe au mifugo yao inapokamatwa ndani ya hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imedhamiria kwa dhati kuleta mahusiano mazuri kati ya wananchi na maeneo ya hifadhi kwa kuchukua hatua mbalimbali, zikiwemo kufanya vikao vya kutafuta suluhu pamoja na kupanga matumizi bora ya ardhi katika maeneo husika. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itahakiki mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara na kuandaa Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi kwa Kijiji cha Bugeli. Utekelezaji wake kwa sasa upo katika hatua za kukabidhi hati kwa wananchi wa kijiji husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa rai kwa wananchi wanaopakana na maeneo yaliyohifadhiwa kuepuka uvunjifu wa sheria za nchi na za uhifadhi na hivyo kudumisha amani kwa jamii husika na Taifa kwa ujumla.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Awack, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na kwamba sijaridhika na majibu ya Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mauaji yamekuwa yakinoteka mara kwa mara katika Hifadhi ya *Lake Manyara*; imetoka mwaka 2005, ikatokea mwaka 2015 na ikatokea tarehe 28/10/2020 ng'ombe wapatao zaidi ya 10 walipigwa risasi wakikutwa kijijini wakidai kwamba wamefuata nyayo. Askari wa *Game Reserve* wakaenda mpaka nyumba ya mtu huko kijijini na ng'ombe kumi kupigwa risasi.

Vilevile tarehe 28 mwezi wa Novemba, walipigwa risasi watu wanne kule msituni na kuchomwa moto. Nami ni shahidi, nikaenda msituni kule kuwatafuta wananchi hawa na kupata mabaki na mabaki yale yakapelekwa kwa Mkemia Mkuu wa Serikali:-

Je, ni lini wananchi wale watapata majibu ya Mkemia Mkuu wa Serikali? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa, Hifadhi ile ya *Lake Manyara* ikihamishwa mipaka mara kwa mara kila mwaka kutoka Hifadhi ya *Lake Manyara*:-

Je, Waziri yuko tayari kufuatana nami kwenda kujionea mpaka jinsi unavyohamishwa katika *Lake Manyara National Park*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ujibu swali la nyongeza la pili. Swali la nyongeza la kwanza utamjibu kwa maandishi kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 45 fasili ya (10) kwa sababu imetaja terehe mahususi na unaweza ukawa huna hapo. Labda kama unazo, ulijibu kama huna utajibu kwa maandishi, kanuni zetu zinaruhusu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza niendelee kutoa pole kwa wananchi wa Karatu kwa kadhia hii ambayo waliipata. Niwakumbushe tu kwamba, wananchi kwa asilimia kubwa wanatumia nguvu ikiwemo kutotii sheria za uhifadhi na hivyo kusababisha hawa Askari sasa kujichukulia sheria ambazo kimsingi wananchi wangetii kusingetokea vurugu yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, tuendelee kushirikiana kuelimisha hawa wananchi. Hili suala la tarehe 28/11/2020 naomba tu waendelee kuwa subira kwa sababu ni taarifa za kuchunguzi na Askari tayari walishachukua *sample* na wakapeleka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali. Hivyo, majibu yatatolewa na Jeshi la Polisi baada ya kufanya uchunguzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili. Niko tayari kuongozana naye kwenda kuangalia maeneo haya na kuonesha mipaka halisi kama ambavyo ameomba. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Robert Chacha Muboto, swali la nyongeza.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Mji wa Bunda ina Kata 14 na wakulima wake mazao yao yameathirika sana na wanyamapori, hasa tembo; Kata ya Nyatwali, *Bunda Store*, Mcharo na Sazila:-

Je, ni lini Waziri atatembelea Halmashauri hii ili aweze kujionea uharibifu huo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nianze kwanza kwa kuwapongeza Wabunge wote ambao wanazungukwa maeneo ya uhifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sheria ambayo tulishapitisha kwamba wananchi wanapokutana na kadha hii ya tembo na wanyama wengine tunatoa kifuta machozi. Nampongeza Mheshimiwa Robert Chacha kwamba ameendelea kulizungumzia suala hili la wananchi wake kuhakikisha wanapata kifuta machozi, lakini pia nimwahidi kwamba, nitafika kwenye eneo hilo ili tuweze kuzungumza na wananchi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ubarikiwe sana. Kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inawajali sana wananchi wake wakiwemo wale wanaoishi kwenye Vijiji vya Kata ya Kirua Vunjo, Kilema, Marangu, Mamba na Mwika na wanaoishi kwenye vijiji vinavyozunguka msitu wa Mlima Kilimanjaro:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kutathmini upya msimamo wake na kuwaruhusu wanavijiji hawa kutumia eneo la nusu maili ambalo limeainishwa kwenye mipaka? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nitoe rai tu kwa Mheshimiwa Mbunge kwamba maeneo ambayo tayari yanakuwa yameshatangazwa kuwa Hifadhi ya Taifa haturuhusiwi kufanya kitu chochote. Isipokuwa kama ana maombi ambayo anahitaji ifanyike tathmini, basi naomba kupitia Serikali ya Wilaya na Vijiji walete maombi kwenye Wizara, halafu tutaangalia tathmini kama itawezekana; na pale ambapo haiwezekani pia, tutawapa majibu. Ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha Maswali kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na Majibu kutoka Serikalini. Nilete matangazo niliyonayo hapa, tutaanza na Tangazo la Wageni walioko Bungeni humu. (*Makofii*)

Kwanza ni wageni waliopo Jukwaa la Spika; na hawa ni wageni tisa wa Mheshimiwa Dorothy Gwajima, Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, ambao ni mume wake, Watendaji Wakuu wa Wizara ya Afya na Katibu Mkuu wa *UWT*. Kwa majina yao ni Ndugu Methusela Gwajima ambaye ni muwe wake, karibu sana. Nimeona wamesimama wengi, Methusela Gwajima ndio yupi hapo jamani? Haya, ahsante sana. (*Makofii*)

Yupo pia Profesa Abel Makubi ambaye ni Katibu Mkuu Idara Kuu, Afya, karibu sana. Yupo pia Dkt. John Jingi ambaye ni Katibu Mkuu, Idara Kuu Maendeleo ya Jamii, karibu sana. Yupo pia Dkt. Grace Maghembe ambaye ni Naibu Katibu Mkuu Afya TAMISEMI. Naye yupo ama hayupo! Sawa. Dkt. Aifelo Sichalwe Mganga Mkuu wa Serikali, karibu sana. (*Makofii*)

Yupo pia Meja Jenerali Dkt. Gabriel Mhidize ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa Bohari ya Dawa *MSD*, karibu sana. Yupo pia Dkt. Naftali Ng'ondi ambaye ni Kamishna wa Ustawi wa Jamii, karibu sana. Yupo pia Ndugu Vickness Mayo ambaye ni Msajili wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali, karibu sana.

Yupo pia Mwalimu Queen Mlozi ambaye ni Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake Tanzania. Karibu sana. (*Makofi*)

Wapo pia wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge. Yupo mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile ambaye ni Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kutoka *Fei Fashion Tanzania*; hawa ni watengenezaji wa bidhaa za ngozi, hasa mabegi ya kisasa na kwa ujuzi kutoka Japan ambaye, ni Ndugu Gregory Mlay. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Mwanahamisi Said ambao ni watoto wake kutoka Mjini Zanzibar; na hawa ni Ndugu Asha Kombo, Ndugu Zainab Mohamed na Ndugu Zakiwi Abdallah. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni watano wa Mheshimiwa Justin Nyamoga ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Kilolo mkoani Iringa wakiongozwa na Ndugu Karume Mhanila. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Neema Lugangira ambao ni wadau wa lishe wa Shirika la Kimataifa QUAM kutoka Jijini Dar es Salaam ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji, Ndugu Michel Dalesandro na Afisa Mshauri Dkt. Ezekiel Mkuya. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wapo pia wageni 10 wa Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyi na Mheshimiwa Charles Mwijage ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Jimboni Muleba, Mkoani Kagera, wakiongozwa na Ndugu Revocatus Augustine. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Saasisha Mafuwe, ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Hai kutoka Mkoani Kilimanjaro, yeye ni Ndugu Lengai Ole-Sabaya. Karibu sana. (*Makofi*)

Eeh, naona makofi yanaashiria umaarufu. (*Makofi/ Kicheko*)

Mgeni wa Mheshimiwa Luhaga Mpina ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Meatu Mkoani Simiyu na huyu ni Ndugu Christopher Ndamo. Karibu sana. Pia wapo wageni wengine 10 wa Mheshimiwa Luhaga Mpina ambao ni wanafunzi wa vyuo vikuu kutoka Jimbo la Kisesa, Wilaya ya Meatu, Mkoa wa Simiyu, wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Sitta Kuzenza. Karibuni sana. (*Makof!*)

Tunao pia wageni 15 wa Mheshimiwa Anna Lupembe na Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ambao ni wanamaombi kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na Mchungaji Obadia Chitalya. Karibuni sana. (*Makof!*)

Tunao pia wageni wanne wa Mheshimiwa Irene Ndyamukama ambao ni wafanyakazi kutoka Kiwanda cha A -Z kutoka Jijini Arusha wakiongozwa na Afisa Mtendaji Mkuu Ndugu Kalpesh Shah. Karibuni sana. (*Makof!*)

Tunao pia wageni walio tembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; na hawa ni wageni wanne kutoka Baraza la Vijana la SADC lenye Makao Makuu yake Jijini Lusaka, Zambia, ambao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyoendesha shughuli zake. Hawa ni Ndugu Tumaini Makole ambaye ni Mwakilishi wa Jukwaa la Vijana la Dunia walio Mstari wa Mbele Kukabiliana na Magonjwa ambayo Hayapewi Kipaumbele. Tumaini Makole, karibu sana. (*Makof!*)

Tunaye pia Ndugu Aloyce Urassa ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Vijana (*African Leaders Malaria Alliance*). Karibu sana. Tunaye pia Ndugu Isack Kaniki ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Kuongeza Ufahamu. Karibu sana. (*Makof!*)

Eeh, hii Kamati ya Kuongeza Ufahamu, ni ufahamu wa mambo yote au ufahamu wa mambo gani? Huyu ni Mjumbe jamani wa Kamati ya Kuongeza Ufahamu.

Haya, Ndugu Maxmilian Godwin ambaye ni Kiongozi wa Kikosi Kazi Maalum cha Baraza la Vijana la SADC kinachoshughulikia ugonjwa wa Malaria na magonjwa

mengine ambayo hayapewi kipaumbele. Karibuni sana.  
*(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hawa ndio wageni tulionao Bungeni siku ya leo, lakini pia lipo tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge. Mnatangaziwa kwamba siku ya jana tarehe 10 Mei, 2021 Kamati ya Uongozi ilikuwa na kikao ambapo wajumbe waliridhia yafanyike mabadiliko ya Ratiba ya Mkutano wa Tatu wa Bunge unaoendelea. Mabadiliko haya yametokana na makubaliano ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kusoma hotuba za bajeti za nchi zao Alhamisi, tarehe 10 Juni, 2021. Ratiba iliyofanyiwa mabadiliko tayari imeshawekwa kwenye vishkwambi vyetu na Waheshimiwa Wabunge mtaikuta hiyo ratiba kwenye kisanduku kilichoandikwa Ratiba ya Mkutano.

Waheshimiwa Wabunge, Kwa hiyo, muiangalle hiyo ratiba ili mjipange vizuri katika zile Wizara mnazotaka kuchangia, mfahamu mabadiliko yametokea katika ratiba hiyo. Kwa hiyo, Bajeti Kuu ya Serikali itasomwa siku ya tarehe 10 mwezi Juni badala ya tarehe iliyokuwa imewekwa awali.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tunaendelea na ratiba ilio mbele yetu. Katibu.

#### **NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

#### **HOJA ZA SERIKALI**

#### **MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimuite sasa Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Mheshimiwa Gwajima. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE  
NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya

Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ndani ya Bunge lako Tukufu, iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kutoa hoja Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Wizaraya yangu kwa mwaka 2020/2021 na vipaumbele vyake kwa mwaka 2021/2022. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida pamoja na Miradi ya Maendeleo ya Wizara kwa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuwasilisha hotuba yangu. Aidha, kwa masikitiko makubwa, natoa pole kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge Wote, Chama Cha Mapinduzi pamoja na Watanzania wote kwa kuondokewa na mpPENDWA wetu, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile natoa pole kwa wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuondokewa na Viongozi Wakuu, Hayati Benjamin William Mkapa, aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Maalim Seif Sharif Hamad, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar; na Balozi Mhandisi John Herbert Kijazi, aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi. Kazi ya Mungu haina makosa, Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, naomba kutoa pole kwako, Bunge lako Tukufu, familia na wananchi wa Mkoa wa Manyara kwa kifo cha Mheshimiwa Martha Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum CCM. Aidha, natoa pole kwako na familia kwa kifo cha Mheshimiwa Atashasta Nditiye, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Muhambarwe CCM. Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahala pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuapishwa kuwa Rais

wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu na kuwa Rais wa Kwanza Mwanamke shupavu kuiongoza nchi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kipekee sana, namshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kunitfea kuendelea kuiongoza Wizara hii kubwa na muhimu sana kwa nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri amba ni chachu kwenye kuiongoza sekta yangu. Aidha, nampongeza kwa hotuba yake aliyoiwasilisha kwenye Bunge lako Tukufu tarehe 13 Aprili, mwaka huu ambayo imetoa mwelekeo wa majukumu ya Serikali kwa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Spika kwa kuendelea kuiongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ufanisi mkubwa. Vilevile, nitumie fursa hii kuwapongeza Wenyeviti wa Bunge kwa kusimamia vyema mijadala ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Mawaziri wenzangu kwa ushirikiano walionipatia, nami naahidi nitaendelea kushirikiana nao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yangu ili kutimiza dhamira ya Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha kuwa sekta ya afya na sekta nyingine zote zinajibu matamanio ya kujenga uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyeviti wake Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge na Makamu wake, Mheshimiwa Aloyce John Kamamba Mbunge, kwa ushauri

na maelekezo yao waliyoyatoa wakati wa maandalizi ya bajeti hii. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mzuri wanaonipatia naahidi nitaendelea kuwa msikivu na kuzingatia ushauri wao siku zote. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, naomba hotuba yangu na viambatisho vyake viingizwe kwenye *Hansard*. Aidha, naomba kutoa maelezo ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2020/2021 Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi pamoja na maombi ya fedha ya kutekeleza vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Nasibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wadau wake wote ilipanga kutekeleza vipaumbele 16 kupitia Fungu 52 - Idara Kuu ya Afya na Fungu 53 - Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii kama inavyoonekana kwenye ukurasa wa sita hadi wa tisa wa hotuba yangu,

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa ya yaliyokuwa Makadirio ya Mapato Fungu 52 - Idara Kuu ya Afya; katika mwaka 2020/2021, Fungu hili lilikusanya mapato kutokana na huduma za Tiba za Hospitali na tozo za huduma katika Taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ada za Vyuo na uuzaji wa Zabuni; makadirio ya makusanyo kwa mwaka 2020/2021 yalikuwa shilingi Bilioni 467.8 hadi kufikia Aprili 2021, jumla ya Shilingi Bilioni 327.7 zimekusanywa, sawa na asilimia 70 ya makadirio kama ilivyoainishwa kwenye ukurasa wa tisa hadi wa kumi wa hotuba yangu. Aidha, taarifa ya makusanyo haya inaonesha kuwa usimamizi katika hospitali za rufaa za mikoa unahitaji juhudzi zaidi. Hivyo, Wizara itaendelea kuboresha mikakati na ufuatilaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sura ya Bajeti; Fungu 52 - Idara Kuu ya Afya ya mwaka 2021, Wizara iliandaa bajeti ya jumla ya Shilingi 900.1 na kupitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama ilivyoainishwa kwenye ukurasa wa 11 wa Hotuba yangu. Hadi kufikia Aprili 2021,

Wizara ilipokea jumla ya Shilingi Bilioni 667.9, sawa na asilimia 74 ya bajeti iliyoidhinishwa kama inavyoonekana kwenye ukurasa wa 11 hadi wa 12 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa maelezo mafupi kuhusu Fungu 53 la Maendeleo ya Jamii. Wizara kupitia Fungu 53, ilitarajia kukusanya Shilingi 5.4 kutokana vyanzo mbalimbali vya mapato. Hadi kufikia Aprili 2021, Wizara imekusanya kiasi cha Shilingi 3.5, sawa na asilimia 65 ya makadirio kama inavyoonekana katika ukurasa wa 13 wa Hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kuhusu sura ya bajeti ya Fungu hili 53. Fungu hili liliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya shilingi Bilioni 32.2 na hadi kufikia Aprili, 2021, Wizara imepokea jumla ya Shilingi Bilioni 22.9 sawa na asilimia 69 ya bajeti kama ilivyoainishwa kwenye Ukurasa 13 hadi 14 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kutoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu nikianzia na Fungu 52 - Idara Kuu ya Afya ambazo taarifa zipo ukurasa 15 hadi 188 wa hotuba yangu. Kuhusu huduma za Kinga utekelezaji wa majukumu umefanyika kwa mafanikio, naomba kurejea maeneo machache. Huduma za chanjo zimefanikiwa kwa zaidi ya asilimia 95 katika kuwapatia chanjo walengwa wake wote. Mahudhurio ya wajawazito kliniki yalikuwa mazuri kwa asilimia 93.4. Hata hivyo, tuna changamoto moja kwamba asilimia 36 tu waliohudhuria kliniki kwa mara ya kwanza ndio walihudhuria kwa wakati ndani ya wiki 12 za mwanzo wa ujauzito. Hivyo, tuna kazi kubwa ya kuendelea kuelimisha watu wetu waendelee kuwahi kliniki kipindi cha ujauzito ndani ya wiki 12.

Mheshimiwa Naibu Spika, fanikio lingine ni upatikanaji wa dawa muhimu za Afya ya Uzazi ulikuwa wa kuridhisha ambapo kati ya wajawazito milioni 1.1 sawa na asilimia 63 waliohudhuria kliniki walipata dawa zinazostahili mama mjamzito kuzipata idadi ya waliojifungulia kwenye vituo iliongezeka kutoka asilimia 63 mwaka 2015/2016 hadi asilimia

81 mwaka 2020/2021, jambo ambalo linachangia vizuri kabisa kupunguza vifo vya wajawazito na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya shilingi bilioni 24 zimetumika kukarabati vituo 813 kwa kujenga upya miundombinu ya maji na usafi wa mazingira. Kampeni ya Kitaifa ya utoaji wa matone ya Vitamin A ilifanikiwa kwa asilimia 97 ya lengo ambapo watoto walio chini ya miaka mitano walipata matone haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapambano ya UKIMWI kupitia utekelezaji wa mpango 90-90-90 yalifanikiwa vizuri katika 90 zote hususan asilimia 92 ya watu wenye VVU milioni 1.36 walianzishiwa dawa na waliweza kufubaza virusi ya UKIMWI. Mapambano dhidi ya *malaria*; nayo yalifanikiwa kwa kupunguza visa vipyta kwa asilimia 35 na kupunguza idadi ya vifo kwa asilimia 61. Kuhusu kifua kikuu napo tulifanikiwa ambapo kampeni za uchunguzi zilifanyika na kuchunguza wagonjwa 60,000 na 68,000 sawa na asilimia 90 ya lengo ambapo pia tulikwenda kwenye magereza 34 na kuchunguza wafungwa 7,418 na kati yao 2,279 walihisiwa kuwa na ugonjwa huku 24 waliothibitika wakipatiwa matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tishio la *Ebola* kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Uganda. Tumeendelea kuwa salama kwa sababu tuliimarisha mikakati mizima ya kuthibiti tishio hili. Vile vile mlipuko wa kipindupindu Mkoani Kigoma ulidhibitiwa kati ya Julai, 2020 hadi Machi, 2021 haukuweza kusambaa nchini kote. Aidha, mapambano dhidi ya maambukizi ya *COVID*, tumepambana vizuri kwa ushirikiano na wananchi na sekta zote na tumeweza kufanya kwa ufanisi ukilinganisha na nchi zingine duniani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma za tiba; idadi ya vituo imeongezeka kutoka vituo 8,446 mwaka 2019/2020 hadi vituo 8,458 Machi, 2021. Jumla ya wagonjwa waliohudumiwa katika Hospitali zetu za Kibingwa na Ubingwa Bobezi ni wagonjwa milioni 4.5 ikilinganishwa na wagonjwa milioni 5.3 waliohudumiwa kipindi cha mwaka 2019/2020.

Ukiangalia hapo ni upungufu wa asilimia 15, lakini haya ni mafanikio yatokanayo na kuimarisha kwa huduma za tiba katika ngazi ya mkoa na katika ngazi ya halmashauri kwa jinsi ambavyo tumejenga vile vituo na vimeanza kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya upatikanaji wa dawa muhimu 321 katika vituo vya huduma za Afya ilifikia asilimia 75.6 na katika maghala yaani *MSD* asilimia 21. Hata hivyo ili kupandisha upatikanaji wa dawa Serikali iliongeza mtaji wa dawa kufikia Aprili, 2021 Shilingi Bilioni 151.38 zilitolewa na Hazina. Serikali inatambua kuwa upatikanaji endelevu wa bidhaa za afya sio tu ajenda ya kuongeza mtaji wa dawa kila siku, bali ni ajenda ya uwajibikaji mpana kwenye mnyororo wa ugavi wa bidhaa za afya nchini ngazi zote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kubainika kuwepo kwa uzembe katika maeneo mengi ya mnyororo wa ugavi Wizara inaendelea kufanya mabadiliko makubwa eneo hili ili kudhibiti changamoto zinazodidimiza mtaji wa dawa licha ya Serikali kuwa inaongeza mtaji huo mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upatikanaji wa damu salama pia tulijitahidi kufanya vizuri ambapo kufikia Machi, 2021 chupa 250.9 za damu salama na bora zilikusanywa sawa na asilimia 67 ya lengo, lakini hapa utaona kwamba bado watu wengi hawajaitikia wito wa kujitolea kutoa damu, hivyo tutaendelea kuhamasisha ili lengo letu liwe linatimia angalau hata kwa asilimia 90.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya wagonjwa milioni 1.6 walihudumiwa kwenye Hospitali za Kanda Maalum na za Kibingwa ambapo kati yao 2,041.1 walihudumiwa kwa msamaha wenyewe thamani ya Shilingi Bilioni 30.1. Vile vile katika hospitali za mikoa wagonjwa 2,800,000 walihudumiwa ambapo wagonjwa 3,053.1 walihudumiwa kwa msamaha wa thamani ya Shilingi Bilioni 4.0. Utaona kwamba misamaha bado iko mingi na hii inaonesha kwamba Serikali ya Tanzania

chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan inajali wanyonge, inahakikisha kwamba wanapofika kwenye vituo vyetu wanapata huduma. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya miradi 22 ya ujenzi wa hospitali mpya, ukarabati wa majengo na upanuzi wa miundombinu ikiwemo TEHAMA umefanyika kwenye Hospitali za Rufaa za Mikoa, Hospitali za rufaa Kanda na Hospitali Maalum na utekelezaji unaendelea. Thamani ya miradi hii ni bilioni 193.3 ambapo hadi kufikia Machi, 2021 Shilingi Bilioni 130.6 zilishatolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ufupi naomba nitaje hatua zillizofikiwa kwa baadhi ya miradi mikubwa, mingine imeelezwa kwenye hotuba yangu ukurasa wa 266 hadi 270, kiambatisha namba 14.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Kanda ya Kusini Mtwara imefikia asilimia 90 na mpango ni kabla ya Desemba, 2021 ianze kazi; Hospitali ya Kanda Burigi Chato awamu ya kwanza imefikia asilimia 98 na maandalizi ya kuanza huduma yameanza; Hospitali ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Jengo la Meta imefikia asilimia 80. Hivyo naomba kwa maelezo ya miradi mingine yote turejee kiambatisho namba 14. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kutoa utekelezaji wa majukumu kwenye Fungu hili 53 Maendeleo ya Jamii kwenye ukurasa 188 hadi 232 imeelezwa. Wizara imeendelea kuhamasisha na kuelimisha wananchi kuhusu dhana ya kushiriki kwenye shughuli za maendeleo kwa kutumia rasilimali zilizopo katika maeneo yao ambapo mambo yamefanyika mengi ikiwemo ujenzi wa miundombinu mbalimbali kama madaraja, shule na ofisi mbalimbali maelezo zaidi yapo ukurasa 189 hadi 190 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufuatiliaji wa upatikanaji wa haki usawa na ulinzi wa watoto umeendelea kufanyika ambapo kufikia Aprili, 2021 madawati ya ulinzi wa watoto 182 yamefunguliwa katika shule za msingi na sekondari na jumla ya wasimamizi wa madawati shulen 360 wameweza

kuandaliwa na kufanya kazi hii. Aidha, Wizara imeendelea kufanya kampeni ya kutokomeza mimba za utotoni katika mikoa mbalimbali nchi ambapo jumla ya wanafunzi 8,978 katika shule za msingi na wanafunzi 345 wamepata elimu ya madhara ya mimba na ndoa za utotoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajenda ya Kitaifa ya kuwekeza katika afya na maendeleo ya vijana balehe imezinduliwa. Mkakati huu ni wa mwaka 2021/2020 hadi 2024/2025; mkakati huu ulizinduliwa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 17 Aprili, 2021, hapa Jijini Dodoma. Ajenda hii inalenga kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili vijana wetu balehe hapa nchini kama ilivyofafanuliwa zaidi kwenye ukurasa 197 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuwawezesha wanawake kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni Wizara imeendelea kuratibu utoaji wa mikopo kwa wanawake wajasiriamali nchini ambapo mikopo ya thamani ya bilioni 22.3 ilitolewa kwa wanawake wajasiriamali 6,326 kuitia dirisha la wanawake lilioanzishwa katika Benki ya Posta Tanzania. Hii ni fedha nydingi ukilinganisha na kiasi cha Shilingi Bilioni 3.6 kilichotolewa kwa wanawake hawa ambao walikuwa 14,271 wakati huo mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kupinga na kuzuia ukatili dhidi ya wanawake na watoto Wizara imeendelea kutoa elimu ya jamii kwa kuitia kampeni na shughuli mbalimbali za kijamii ikiwemo Kampeni kubwa kabisa ya Twende Pamoja Ukatili Tanzania Sasa Basi. Juhudi nyiningine zimeelezwa kwenye ukurasa 219 hadi 220 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufuatiliaji wa mashirika yasiyo ya Kiserikali umeendelea kufanyika sambamba na kuuhisha taarifa zake, kama inavyosomeka ambapo sasa kufikia Aprili, 2021 mashirika 4,000 ndio yalionekana kuwa hai. Hivyo, nitumie fursa hii kutoa rai kwamba Serikali haitamvumilia mtu au kikundi chochote

kitakachojishughulisha na uendeshaji wa mashirika yasiyo ya Kiserikali ambayo hayajasajiliwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niende kwenye vipaumbele vya Wizara Fungu 52 kwa mwaka 2021/2022; katika utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2021/2022, Wizara imepanga kutekeleza vipaumbee vilivyoainishwa kwenye ukurasa 232 hadi 235 kwenye hotuba yangu, vipaumbele vyote ni muhimu hata hivyo kutokana na muda naomba kuvitaja vichache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kipaumbele cha kwanza kabisa kwenye Wizara yangu ni suala la Bima ya Afya kwa wote. Wizara imedhamiria kuhakikisha inawasilisha Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote mwezi Juni, 2021 kwenye Bunge lako Tukufu. Jumla ya shilingi milioni 231.7 tumetenga kwa ajili ya kuratibu hizi shughuli ili ziweze kutokea bila kikwazo. Vile vile tumedhamiria kukamilisha miradi 22 ya upanuzi, ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma za afya katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Kanda na Maalum. jumla ya shilingi Bilioni 193.2 tumezitenga na zipo kwenye ukurasa wa 266 hadi 270 wa hotuba yangu na kiambatisho namba 14. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tumedhamiria kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba na vitendanishi ambapo jumla ya Bilioni 263.8 tumezitenga, lakini sambamba na fedha hizo Wizara itaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji kwenye viwanda vya dawa na vifaa tiba nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango ambao hivi sasa tayari umewezesha kupatikana kwa viwanda 11 vya dawa kutoka tisa mwaka 2019/2020 na vingine 16 vipo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Vile vile viwanda vya vifaa tiba vimefikia 15 kutoka sita mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la dawa ni ajenda pana inayoangalia mambo mengine, hivyo tutaimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa mnyororo wa ugavi wa bidhaa za

afya kwa kutumia TEHAMA ili kudhibiti matumizi ya bidhaa za Afya yawe kwa usahihi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tutazidi kusimamia ubora wa huduma ili kuvutia wananchi wengi wajunge na bima ya afya na wavitumie vituo vyetu na vitu vyetu viweze kunufaika na bima hizi, hivyo kuwa na uwezo endelevu wa kununua dawa kwa mwongozo wa kulipa na kuchukua dawa toka bohari yetu, badala ya kufanya masuala ya kukopa na kuchelewa kulipa yaani tunafanya *cash and carry* ili kufanya mtaji wa *MSD* usife. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tumedhamiria kuongeza kasi ya upatikanaji wa wataalamu bingwa na bobesi kwa kutumia utaratibu wa mafunzo ya wataalamu wakiwa kazini (*fellowship training program*) mpango huu utawezesha upatikanaji wa madaktari bingwa wengi zaidi na kwa gharama nafuu zaidi na hivyo kutatua changamoto ya upungufu katika Hospitali za Rufaa za Mikoa kama inavyosomeka kwenye Kiambatisho Na. 13 cha hotuba yangu ukurasa 265 utaona upungufu ni mkubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimwa Naibu Spika, tumedhamiria kuimarisha huduma za matibabu ya kibingwa na ubingwa bobesi kwenye hospitali zetu za kibingwa na ubingwa bobesi, ambapo jumla ya shilingi bilioni nane tumetenga kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kibingwa na ubingwa bobesi kama vile vipandikizi kwa ajili ya kuunga mifupa iliyovunjika (*implants*) na ujenzi wa *bankers* kwa ajili ya matibabu ya saratani. (*Makofii*)

Mheshimwa Naibu Spika, tumedhamiria kuimarisha huduma za afya nchini kwa kulenga kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi, Watoto wachanga na Watoto wenye umri chini ya miaka mitano. Jumla ya shilingi bilioni 63.5 tumetenga kwa ajili ya kuimarisha mnyororo mzima wa huduma za chanjo ikiwemo kununua majokofu 1,200 na magari 60. Hivi sasa Wizara inaendelea na usambazaji wa vifaa na vifaa tiba kwaajili ya kuvizezesha vituo vya afya vile vilivyoboreshwu ambavyo vilikuwa havijaanza kazi ya

kufanya huduma za upasuaji ili viendelee kufanya upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni pindi mama anapokabiliwa na uzazi pingamizi. (*Makof*)

Mheshimwa Naibu Spika, tumedhamiria kuimarisha huduma za dharura katika hospitali za rufaa za mikoa nane jumla ya shilingi bilioni 4 tumetenga eneo hili kwa kwaajili ya ujenzi wa jengo la huduma za dharura (*EMD*) na wodi za wagonjwa mahututi (*ICU*).

Mheshimwa Naibu Spika, naomba kwa ridhaa yako niendelee kusoma vipaumbele vya Wizara Fungu 53 Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii kwa mwaka 2021/2022. Katika mwaka 2021/2022 Wizara itatekeleza vipaumbele kama vilivyoainishwa katika ukurasa 236 hadi 238 kwenye hotuba yangu naomba nitambue baadhi hapa kama ifuatavyo;

Mheshimwa Naibu Spika, kwanza tutaendelea kuratibu kukuza ari ya jamii uzalendo na kujenga moyo wa kujitolea katika kujiletea maendeleo ya jamii na kiuchumi kwa kutumia nguvu kazi na rasilimali zinazowazunguka wananchi wetu. Tumetenga milioni 350.7 kwa ajili ya kuamsha ari ya jamii kujenga nyumba bora za gharama nafuu na teknolojia rahisi.

Mheshimwa Naibu Spika, tutaendelea kutekeleza dhana ya uanangezi (ubunifu na ushirikishwaji kwenye jamii kwenye taasisi na vyuo) ili kuzalisha wanafunzi wanaoajirika na kujajiri ili wawe chachu ya maendeleo badala ya kuwa na wanafunzi ambaao wanamakaratasi tu hawawezi kujajiri wala kuajirika kirahisi.

Mheshimwa Naibu Spika, tutaendelea kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia, katika taasisi zetu ili kutoa mafunzo yanayokidhi mahitaji ya soko tumetenga bilioni 10.4 kwaajilii ya jukumu hili ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya taasisi. Tutaendelea kuratibu uwezeshaji wa wanawake kiuchumi na uingizaji wa masuala ya jinsia katika sheria, sera mipango na mikakati jumla tumetenga

bilioni 1.6 kwa ajili hiyo ikiwa ni Pamoja na kuwawezesha kupata mikopo yenyé masharti nafuu. (*Makofí*)

Mheshimwa Naibu Spika, tutaendelea kuhamasisha ushiriki wa wanawake katika ngazi za uongozi na nafasi mbalimbali za maamuzi. Tutaendelea kuratibu kampeni mbalimbali za kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na Watoto jumla ya shilingi milioni 791 tumetenga eneo hili kwaajili ya uratibu wa kampeni hizi.

Mheshimwa Naibu Spika, tutaendelea kuimarisha huduma za ustawi wa jamii na haki kwa familia na Watoto ikiwemo malezi ya kambo na kuandaa walezi wa kuaminika malezi makuzi na maendeleo ya awali ya watoto waweze kutolewa, ulinzi na usalama kwa watoto uweze kutolewa dhidi ya vitendo vya ukatili Pamoja na huduma za utengamao katika familia kwa watoto tumetenga millioni 530.

Mheshimwa Naibu Spika, tutaendelea kuratibu uanzishwaji wa vikundi vya malezi katika ngazi ya jamii ambapo tumetenga milioni 78 kwaajili hii tutaendelea kuratibu uundwaji wa kamati za ulinzi wa wanawake na watoto Pamoja na kuzijengea uwezo.

Mheshimwa Naibu Spika, vilevile kuna migogoro mingi kwenye maeneo ya ndoa hapo, tutaendelea kuimarisha huduma za usuluhisho wa migogoro ya ndoa na familia. Tutawapatia msaada wa kisaikolojia na kijamii familia hizi jamii na makundi mbalimbali wakiwemo wazee, Watoto walio katika mazingira hararishi Pamoja na wahanga wa ukatili na majanga mbalimbali tumetenga million 265.6 eneo hili. (*Makofí*)

Mheshimwa Naibu Spika, naomba kwa ufupi sana kutoa shukrani zangu kama ifuatavyo kwenye ukurasa wa 246 hadi 249 wa hotuba yangu. Natambua kwamba tumekuwa tukipata ushirikiano mkubwa kutoka nchi rafiki mashirika ya Kimataifa, Mashirika ya dini Asasi zisizo za kiserikali, Taasisi za Serikali, taasisi za Elimu, Serkta binafsi na sekta

nyingine zote zinazosaidia kuchangia katika huduma za afya maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii.

Mheshimwa Naibu Spika, yote haya nimeyataja kwa moja moja kwenye hizo kurasa nilizozisema. Vile vile naomba kutambua utendaji wangu kwamba umekuwa ukipata ushirikiano mkubwa sana kutoka kwa viongozi wenzangu naomba niwataje baadhi Mheshimiwa Dkt Godwin Mollel Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Mwanaidi Ally Hamis Naibu Waziri Maendeleo ya Jamii, Profesa Abel Makubi - Katibu Mkuu Afya, Dkt John Jingu Katibu Mkuu Maendeleo ya Jamii, Dkt Alfello W. Sichalwe Mganga Mkuu wa Serikali. Naomba pia nitambue kupitia wao watumishi wote wa Idara zote na Taasisi zote katika sekta yetu na watumishi wote. (*Makofii*)

Mheshimwa Naibu Spika, naomba nitambue mchango pla wa Ofisi ya Rais TAMISEMI kuanzia Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri Manaibu Katibu Wakuu kwa mchango wao katika kutekeleza majukumu ya Sera yetu. (*Makofii*)

Mheshimwa Naibu Spika, pia nichukue fursa hii kuishukuru familia yangu, mume wangu mpPENDWA Advocate Metusela Gwajima na Watoto wetu kwa uvumilivu wao wa kunikosa kama mama muda wote niko kazini hawajaacha kunitia moyo niendelee kufanya kazi hii wamethamini mchango wangu kama mwanadamu kwenye taifa hili nitaendelea kuwapenda daima. (*Makofii*)

Mheshimwa Naibu Spika, nawashukuru wananchi wote wa Tanzania wa Taifa letu walioko ndani ya nchi nan je ya nchi wamekuwa wakinipa ushirikiano mkubwa sana kupitia simu niliyoitangaza na kwa pamoja kazi inaendelea sisi na wao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nichukue fursa hii kuombi maombi ya bajeti ya fedha kwa mwaka 2021/2022 Fungu 52 la Idara Kuu ya Afya kama ifuatavyo. Katika mwaka 2021/2022 Wizara na Taasisi zilizo chini ya Fungu 52 zinakadiria kukusanya shilingi 507,218,152,321 ambapo kati ya fedha hizo, Shilingi 81,717,635,624 zinatarajiwa kukusanywa

kutoka vyanzo vya ndani Makao Makuu ya Wizara, shilingi 92,044,336,376 kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa na shilingi 333,456,180,321 zinatarajiwा kutoka Taasisi zilizo chini ya Wizara na Hospitali ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2021/2022 Wizara kupitia Fungu 52 imepanga kutumia shilingi 557,303,059,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo kati ya hela Shilingi 252,523,260,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na kiasi cha shilingi 304,779,799,000 ni kwa ajili ya Mishahara ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2021/2022 Wizara imetenga kiasi cha shilingi 476,830,236,000 kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo, ambapo shilingi 351,700,000,000 ni fedha kutoka vyanzo vya ndani, na shilingi 125,130,236,000 ni fedha kutoka vyanzo vya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2021/2022 Wizara Fungu 52 (Idara Kuu ya Afya) tunaomba shilingi 1,034,133,295,000 ili tuweze kuvitekeleza vipaumbele nilivyovasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii (Fungu 53) naomba kuwasilisha maombi ya bajeti ya fedha kwa Mwaka 2021/2022 kama ifuatavyo katika mwaka 2021/2022, Fungu hili tumekadiria kukusanya shilingi 6,000,000,000 kutockana na ada na tozo mbalimbali za usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, mapato ya ada za mitihani na uuzaji wa mitaala ya Mafunzo ya Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii na mapato mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2021/2022, Fungu hili tunakadiria kutumia shilingi 28,725,929,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 12,985,672,000 ni Mishahara ya watumishi na shilingi 15,740,257,000 ni Matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa shughuli za maendeleo, Wizara Fungu 53 tunakadiria kutumia shilingi

14,900,000,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 4,900,000,000 ni Fedha za Ndani na shilingi 10,000,000,000 ni Fedha za Nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2021/2022, Fungu hili Wizara tunaomba jumla ya shilingi 43,625,929,000. Jumla ya fedha zote zinazozioomba Wizara yangu kwa Mafungu yote mawili ni shilingi 1,077,759,224,000. Kwa maelezo haya naomba kutoa taarifa kwamba hotuba hii inapatikana pia katika tovuti za Wizara kama zinavyoonekana kwenye hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,  
WAZEE NA WATOTO, MHE. DKT. DOROTHY GWAJIMA (MB),  
KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA  
MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2021/22 - KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**A. UTANGULIZI**

1. ***Mheshimiwa Spika***, kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ndani ya Bunge lako Tukufu, ambayo imechambua Bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ninaomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka 2020/21 na Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2021/22. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida pamoja na Miradi ya Maendeleo ya Wizara kwa mwaka 2021/22.

2. ***Mheshimiwa Spika***, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. Aidha, kwamasikitiko makubwa, napenda kutumia fursa hii

kutoa pole kwa **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge Wote, Chama Cha Mapinduzi pamoja na Watanzania wote kwa kuondokewa na mpendwa wetu, **Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli**, aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, napenda kutoa pole kwa wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuondokewa na Viongozi Wakuu, **Hayati Benjamin William Mkapa**, aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Maalim Seif Sharif Hamad**, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na **Balozi Mhandisi John Herbert Kijazi**, aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi. Kazi ya Mungu haina makosa, hili ni pigo kwetu sote na inatulazimu kulikubali na kuendelea pale walipoishia. Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi.

3. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, naomba kutoa pole kwako, Bunge lako Tukufu, kwa familia na wananchi wa Mkao wa Manyara kwa kifo cha **Mheshimiwa Martha Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum (CCM)** aliyeferiki tarehe 20 Januari, 2021 katika Hospitali ya HCG Mumbai, nchini India alikokuwa akipatiwa matibabu. Aidha, natoa pole kwako na familia kwa kifo cha **Mheshimiwa Atashasta Justus Nditiye** aliyekuwa **Mbunge wa Jimbo la Muhamwe (CCM)** aliyeferiki tarehe 12 Februari, 2021. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahala pema peponi.

4. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa pongezi kwa **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan** kwa kuapishwa kuwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu na kuwa Rais wa Kwanza Mwanamke Shupavu kuiongoza nchi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninampongeza Makamu wa Rais **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango** kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kipekee sana, namshukuru **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuonesha imani yake kubwa kwangu na kunitfea kuendelea kuiongoza Wizara kwa maslahi mapana ya nchi.

5. ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii kumshukuru **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri uliowezesha kuleta tija na ufanisi katika utendaji na kuimarisha huduma zinazotolewa katika Sekta ya Afya na Sekta ya Maendeleo na Ustawi ya Jamii. Aidha, ninampongeza kwa hotuba yake aliyoiwasilisha kwenye Bunge lako Tukufu tarehe 13 Aprili, 2021 ambayo imetoa mwelekeo wa majukumu yatakayotekelezwa na Serikali katika mwaka 2021/22.
6. ***Mheshimiwa Spika***, ninapenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuendelea kutekeleza majukumu yako kwa ufanisi mkubwa katika kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninampongeza Naibu Spika **Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb)** katika utekelezaji wa majukumu yake. Vilevile, nitumie fursa hii kuwapongeza Wenyeviti wa Bunge kwa kusimamia vyema mijadala ndani ya Bunge.
7. ***Mheshimiwa Spika***, ninapenda kuwashukuru Mawaziri wenzangu kwa ushirikiano walionipatia ambao umeiwezesha Wizara ninayoiongoza kuendelea kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma za Afya, Ustawi na Maendeleo ya Jamii. Wizara itaendelea kushirikiana nao na kuhakikisha tunatimiza dhamira ya Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha kuwa Sekta ya Afya inaratibiwa vyema na watanzania wanakuwa na afya bora ili washiriki kikamilifu katika kujenga uchumi wa viwanda.
8. ***Mheshimiwa Spika***, kipekee ninapenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyeviti wake **Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo (Mb)**, na Makamu wake, **Mheshimiwa Aloyce John Kamamba (Mb)** kwa ushauri na maelekezo waliyoyatoa wakati wa maandalizi ya Bajeti hii. Aidha, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mzuri wanaonipatia ikiwemo kutoa ushauri na maoni mbalimbali yenye lengo la kuboresha huduma za Afya, Ustawi na Maendeleo ya Jamii. Ninawaahidi kwamba, Wizara ninayoiongoza itazingatia ushauri wao na kuendelea kuwapa ushirikiano katika kutekeleza majukumu na kazi zetu za kuwatumikia wananchi ndani na nje ya Bunge.

9. ***Mheshimiwa Spika***, baada ya kutoa maelezo ya awali, ninapenda sasa kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2020/21 (Fungu 52 na Fungu 53), Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi pamoja na Maombi ya Fedha ya kutekeleza Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2021/22 (Fungu 52 na Fungu 53).

#### **B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2020/21**

10. ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza majukumu yake, Wizara imeendelea kuzingatia Sera, Mpango Mkakati pamoja na Makubaliano ya Kitaifa na Kimataifa yenyе lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za afya, ustawi na maendeleo ya jamii nchini. Sera hizo ni pamoja na Sera ya Maendeleo ya Jamii (1996); Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000); Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2001); Sera ya Taifa ya Wazee (2003); Sera ya Afya (2007); na Sera ya Maendeleo ya Mtoto (2008). Vilevile, katika kuandaa mpango na bajeti, Wizara imezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Mpango wa Tatoo wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26), Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020-2025, Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (2017/18 – 2021/22) na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs 2030).

11. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/21, Wizara ninayoismamia kwa kushirikiana na Wizara nyingine, Idara na Taasisi za Serikali, Wakala wa Serikali na Wadau wa Maendeleo ilipanga kutekeleza afua mbalimbali zenyе lengo la kuboresha utoaji huduma za afya, ustawi na maendeleo ya Jamii katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kuendelea kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma za chanjo ili kuwakinga watoto chini ya miaka 5, akina mama wajawazito na kutoa chanjo nyinginezo za kimkakati za kukinga na kudhibiti magonjwa yanayozuilkia kama Homa ya Ini, kichaa cha mbwa na mengineyo;

- (ii) Kupunguza vifo vyatika mama na watoto wachanga vinavyotokana na uzazi;
- (iii) Kuimarisha Huduma za Lishe na Kuboresha Usafi wa Mazingira nchini;
- (iv) Kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa yanayoambukiza ikiwa ni Malaria, Kifua Kikuu na UKIMWI pamoja na magonjwa yasiyoambukiza kama vile magonjwa ya Moyo, Kisukari na Saratani;
- (v) Kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vyote vyatika kutolea huduma za afya nchini;
- (vi) Kuimarisha utoaji wa huduma za afya za kibingwa na ubingwa bobezi;
- (vii) Kuendelea kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma katika Hospitali ya Taifa, Maalum, Rufaa za Kanda na Mikoa;
- (viii) Kuimarisha mpango wa Taifa wa utayari wa kukabiliana na magonjwa ya milipuko, ajali na majanga;
- (ix) Kuimarisha mafunzo na maendeleo ya wataalam katika Sekta ya Afya;
  
- (x) Kuamsha ari ya wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo;
- (xi) Kukuza usawa wa jinsia na uwezeshaji wa wanawake;
- (xii) Kuimarisha upatikanaji wa haki na maendeleo ya mtoto;
- (xiii) Kuimarisha huduma za ustawi wa jamii kwa wazee na watoto wakiwemo wale walio katika mazingira harishish;
- (xiv) Kusimamia na kuratibu utendaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika kuleta maendeleo ya jamii;

(xv) Kuwezesha utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (2017/18 – 2021/22); na

(xvi) Kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, Taasisi ya Ustawi wa Jamii pamoja na Chuo cha Ustawi wa Jamii Kisangara.

## **MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA**

### **IDARA KUU YA AFYA (FNGU 52)**

12. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kuptitia Idara Kuu ya Afya (Fngu 52) inalo jukumu la kusimamia upatikanaji na utoaji wa huduma za Afya nchini. Katika kutoa huduma hizo, Wizara pia hukusanya mapato katika kutekeleza sera za uchanglaji wa huduma kutokana na huduma za Tiba zitolewazo na Hospitali zilizo chini yake, tozo za huduma katika Taasisi mbalimbali, ada za Vyuo na uuzaji wa zabuni.

13. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/21, Wizara na Taasisi zilizo chini yake ilikadiria kukusanya kiasi cha **Shilingi 467,799,587,522** ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi 51,171,533,981** zilitarajiwaa kukusanywa kutoka vyanzo vya ndani Makao Makuu ya Wizara, **Shilingi 103,875,213,018** kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa na **Shilingi 312,752,840,523** zilitarajiwaa kukusanywa kutoka Hospitali ya Taifa, Hospitali Maalum, Hospitali za Kanda na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Hadi kufikia Aprili 2021, jumla ya **Shilingi 327,723,075,210.60** sawa na asilimia 70 ya makadirio zilikusanywa ambapo **Shilingi 38,269,215,667.55** zilikusanywa kutoka vyanzo vya ndani makao makuu sawa na asilimia 75, **Shilingi 45,369,636,115.27** kutoka hospitali za Rufaa za mikoa sawa na asilimia 44 na **Shilingi 244,084,223,427.78** kutoka Hospitali ya Taifa, Hospitali Maalum, Hospitali za Kanda na Taasisi zilizo chini ya Wizara sawa na asilimia 78. Mchanganuo wa makadirio na makusanyo kutoka Wizarani Makao Makuu, Mabaraza, Hospitali na Taasisi umeainishwa katika **Kiambatisho Na. 1, 2 na 3.**

14. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi kilichobakia cha mwaka 2020/21, Wizara itaendelea kusimamia na kuboresha ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali kwa kuendelea na utaratibu wa kulipia huduma kuititia Benki, kuimarisha mfumo wa malipo kwa njia ya ki-elektroniki, udhibiti wa Makusanyo na kuwachukulia hatua stahiki watendaji wazembe ambao hawakuweza kufikia malengo yaliyopangwa, kuwaongezea ari watendaji waliofikia malengo ili kuongeza ufanisi na kuboresha huduma za bima.
15. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21, Wizara kupitia Fungu 52 iliandaa bajeti ya jumla ya **Shilingi 900,088,240,000**na kupitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Shilingi 539,128,874,000** ikiwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 360,959,366,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, kiasi cha **Shilingi 181,562,950,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 357,565,924,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya watumishi.
16. **Mheshimiwa Spika**, kati ya **Shilingi 360,959,366,000** zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, jumla ya **Shilingi 280,700,000,000** sawa na asilimia 78 ni fedha za ndani na **Shilingi 80,259,366,000** sawa na asilimia 22, ni fedha za nje kutoka kwa Wadau wa Maendeleo wanaochangia katika Sekta ya Afya.
17. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu mapokezi ya fedha, katika kipindi cha Julai hadi Aprili 2021, Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 667,881,320,030.23**ya bajeti iliyoidhinishwa ya **Shilingi 900,088,240,000** sawa na asilimia 74 kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake. Fedha zilizopokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, ni **Shilingi 392,986,857,719.88** sawa na asilimia 73 ya fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida kwa mwaka. Kati ya fedha hizo kiasi cha **Shilingi 126,865,793,541.26** sawa na asilimia 70 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Shilingi 266,121,064,178.62** sawa na asilimia 74 ni kwa ajili ya Mishahara ya watumishi.

18. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, hadi kufikia Aprili 2021, kiasi cha **Shilingi 274,894,462,310.35** sawa na asilimia 76 kilipokelewa kati ya fedha zilizoidhinishwa kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Shilingi 268,244,197,289.20** sawa na asilimia 96 ni fedha za ndani na **Shilingi 6,650,265,021.15** ni fedha za nje zilizopokelewa kupitia mfumo wa *Exchequer* wa Hazina. Aidha, Wizara ilipokea kiasi cha **Shilingi 117,787,305,378.97** kupitia mfumo wa *D-Fund*.

#### **IDARA KUU YA MAENDELEO YA JAMII (FNGU 53)**

19. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/21, Wizara kupitia Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii (Fngu 53), ilitarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 5,419,250,000** kutohana na ada za wanafunzi kutoka katika Vyuo nane (8) vya Maendeleo ya Jamii vya Buhare, Uyole, Rungembra, Mlale, Msungwi, Ruaha, Mabughai na Monduli, ada za wanafunzi katika Chuo cha Ustawi wa Jamii Kijitonyama pamoja na ada za mwaka na faini za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Hadi kufikia Aprili 2021, Wizara pamoja na Taasisi zake imefanikiwa kukusanya kiasi cha **Shilingi 3,525,722,868** sawa na asilimia 65ya makadirio ya mapato.

20. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/21, Wizara kupitia Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii (Fngu 53) iliidhinishiwa na Bunge lako tukufu Jumla ya matumizi ya **Shilingi 33,195,739,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 26,491,375,000** sawa naasilimia 79.8 ya bajeti ni kwa ajili ya **Matumizi ya Kawaida** ambapo **Shilingi 13,649,294,000** ni fedha za Matumizi Mengineyo (OC) na **Shilingi 12,842,081,000** ni kwa ajili ya Mishahara. Aidha, kiasi cha **Shilingi 6,704,364,000** kilikuwa nikwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi 4,000,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 2,704,364,000** ni fedha za nje.

21. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Aprili 2021, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 22,906,093,357** sawa na asilimia 69ya bajeti kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha zilizopokelewa, Matumizi ya

Kawaida ni **Shilingi 21,268,090,181**sawa naasilimia 80ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 11,374,411,666**ni Matumizi Mengineyo na **Shilingi 9,893,678,515**ni kwa ajili ya Mishahara. Aidha, **Shilingi 1,638,003,175** ni Fedhaza Maendeleosawa na asilimia 24 ya bajeti ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,000,000,000** ni Fedha za Ndani na **Shilingi 638,003,175** ni Fedha za Nje.

### **C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA**

22. ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa majukumu ya Wizara umegawanyika katika Idara Kuu mbili ambazo ni Idara Kuu ya Afya (Fungu 52) na Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii (Fungu 53). Afua zilizotekelawa kwa mwaka 2020/21 ni kama ifuatavyo:-

#### **IDARA KUU YA AFYA (FUNGU 52)**

23. ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na vipaumbele iliyojiwekea kwa mwaka 2020/21,Wizara ilitekeleza afua mbalimbali katika maeneo ya utoaji wa huduma za kinga, tiba, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali watu na fedha, uratibu na usimamizi wa taasisi na mabaraza ya kitaaluma yaliyo chini ya Wizara. Maeleo ya utekelezaji wa maeneo tajwa ni kama ifuatavyo:-

#### **HUDUMA ZA KINGA**

24. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inalo jukumu la kusimamia utoaji wa Huduma za Kinga ili kuikinga jamii dhidi ya magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza. Afua kuu zinazotekelawa katika eneo hilli ni 11 ambazo ni pamoja na: Huduma za Chanjo; Afya ya Uzazi na Mtoto; Afya ya Usafi na Mazingira; Huduma za Lishe; Elimu ya Afya kwa Umma; Udhibiti wa VVU/ UKIMWI; Kifua Kikuu na Ukoma; Udhibiti wa Malaria; Udhibiti wa Magonjwa ya Milipuko; na Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipauambele.

## Huduma za Chanjo

25. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Wizara ilipanga kuwapatia huduma za chanjo Watoto 1,602,391 wenyе umri wa mwaka mmoja, wasichana 523,592 wenyе umri wa miaka 14 na wajawazito 1,733,430 ambao ni walengwa wa huduma za hizo.

26. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha chanjo na vifaa vya kutolea huduma hiyo vinapatikana kulingana na mahitaji, Serikali ilitoa fedha kiasi cha **Shilingi bilioni 30** kwa ajili ya ununuzi wa aina nane (8) za chanjo na vifaa vya kutolea chanjo katika kipindi cha Julai 2020 hadi sasa. Aidha, fedha hizo zilitumika kununua chanjo zifuatazo: dozi 4,000,000 za BCG kwa ajili ya kuwakinga watoto wachanga na ugonjwa wa Kifua Kikuu; dozi 6,000,000 (bOPV) za kuzuia virusi mbalimbali vinavyosababisha ugonjwa wa kupooza; dozi 4,000,000 (Td) za kuzuia ugonjwa wa Pepopunda kwa mama wajawazito; dozi 4,118,800 (PCV-13) za kuwakinga watoto dhidi ya magonjwa ya Nimonia na homa ya uti wa mgongo; dozi 4,339,500 (Rota) za kuwakinga watoto dhidi ya ugonjwa wa kuhara; dozi 815,110 za HPV; kwa ajili ya kuwakinga wasichana dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi; dozi 2,313,800 za IPV kwa ajili ya kuzuia ugonjwa wa kupooza kwa Watoto; na dozi 5,402,900 za Penta kwa ajili ya kuzuia magonjwa ya Dondakoo, Kifaduro, Kupooza, homa ya ini na homa ya uti wa mgongo.

27. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya watoto 1,522,272 sawa na asilimia 95 ya watoto 1,602,391 wenyе umri chini ya mwaka mmoja walichanjwa dozi ya tatu ya Penta. Jumla ya wasichana 502,375 sawa na asilimia 96 ya wasichana 523,592 wenyе umri wa miaka 14 walipatiwa chanjo na wajawazito 1,701,322 sawa na asilimia 98 ya wajawazito 1,733,430 walipatiwa chanjo. Aidha, Wizara imeendelea kutoa chanjo za Homa ya Manjano kwa wasafiri ambapo jumla ya wasafiri 3,354 kati ya waliolengwa 15,000 walipata chanjo ya Homa ya Manjano. Idadi hii ni pungufu kutokana na kupungua kwa wasafiri kwa sababu ya tishio la mlipuko wa COVID-19 duniani.

28. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Serikali imeimarisha huduma za mnyororo baridi kwa kununua majokofu 1,514 ya kutunzia chanjo kwa Halmashauri 104 zilizokuwa na mahitaji nchini na zoezi la ufungaji wa majokofu hayo linaendelea. Wizara kwa kushirikiana na wadau itaendelea kuimarisha upatikanaji wa chanjo nchini ili watoto, wajawazito na wasichana waendelee kukingwa kulingana na miongozo ya Kitaifa inavyoelekeza.

### **Afyaya ya Uzazi na Mtoto**

29. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuimarisha huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto kwa kuboresha huduma kabla, wakati wa ujauzito na kujifungua, baada ya kujifungua, huduma kwa Watoto chini ya miaka mitano na vijana balehe. Afua mbalimbali zimetekelizwa ikiwemo upatikanaji wa bidhaa muhimu kwa ajili ya huduma za afya ya uzazi na mtoto nchini.

30. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kupiga hatua katika kuongeza watumiaji wa njia za uzazi wa mpango ambaao ni muhimu katika kulinda afya ya mama, kuimarisha makuzi ya mtoto, na kumwezesha mama kushiriki katika shughuli za kuongeza uchumi wa familia na nchi. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, takwimu zinaonesha kuwa akina mama 4,926,183 kati ya akinamama 13,841,430 sawa na asilimia 36 walikuwa wanatumia huduma za uzazi wa mpango za kisasa. Aidha, upatikanaji wa dawa na bidhaa za uzazi wa mpango ulifikia asilimia 92 ya mahitaji halisi. Dawa na bidhaa hizo ni pamoja na vichocheo za homoni ambavyo ni vidonge,sindano ya *Depo-provera* na vipandikizi. Bidhaa zingine za uzazi wa mpango ni pamoja na vitanzi, kondomu za kike na kiume ambazo zilinunuliwa na kusambazwa katika vituo mbalimbali hapa nchini. **Matumizi ya Uzazi wa Mpango yamewezesha Familia kupanga uzazi wa watoto na kufanya uzazi uwe salama, malezi kuwa rafiki, mtoto kuwa na afya njema na Taifa salama.**

31. ***Mheshimiwa Spika***, jumla ya wajawazito 1,760,707 walihudhuria kliniki katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi

2021 ambao ni zaidi ya tarajio la wajawazito 1,650,000 sawa na ongezeko la asilimia 6.7 waliotegemewa katika kipindi hicho. Hii inaonesha mwamko wa jamii juu ya umuhimu wa kuhudhuria Kliniki wakati wa ujauzito. Hata hivyo, kati yao ni asilimia 36 tu walihudhuria kliniki kwa mara ya kwanza ndani ya wiki 12 za mwanzowa ujauzito. Kiwango hiki kidogo cha mahudhurio ya kwanza ndani ya wiki 12 za mwanzo kinachangiwa na mila na desturi za kutotoa taarifa za mimba changa katika kipindi hiki. Aidha, kumekuwa na maendeleo makubwa katika ongezeko la wajawazito waliofanya mahudhurio manne au zaidi ya kliniki. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, asilimia 93.4 ya wajawazito walihudhuria klinikiikilinganishwa na asilimia 84yakipindi kama hicho kwa mwaka 2019/20. **Hivyo, natoa rai kwa kila mjamzito kuhudhuria kliniki mapema mara tu anapogundua kuwa ni mjamzito ili aweze kupatiwa huduma za uchunguzi wa maendeleo ya ukuaji wa mimba pamoja na kukinga na kuzuia matatizo kama vile upungufu wa damu na dalili kuelekea kifafa cha mimba mambo ambayo ndiyo yanachangia vifo katika kipindi cha ujauzito na uzazi kwa kiasi kikubwa.**

32. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, takwimu zinaonesha wajawazito waliojifungulia kwenye vituo vyta kutolea huduma iliongezeka hadi kufikia asilimia 81 ikilinganishwa na asilimia 63 kwa takwimu za mwaka 2015/16. Aidha, kwa upande mwingine, katika kipindi hiki, akinamama waliojifungua na kurudi kliniki siku mbili baada ya kujifungua ilikuwa ni asilimia 62 ikilinganishwa na asilimia 34 kwa mwaka 2015/16. Wizara inawapongeza akina mama wajawazito kwa kuendelea kupokea elimu na maelekezo ya afya na kuyafanya kazi kama tunavyoona mwitikio unazidi kuwa mkubwa wa kwenda kujifungua kwenye vituo vyta afya na pia kurejea tena kliniki baada ya kujifungua. Mwitikio huu ni muhimu katika **kuhakikisha usalama wa mama na mtoto, kwa kuwa asilimia 60 ya vifo vitokanavyo na uzazi hutokea kipindi cha baada ya kujifungua kutokana na matatizo ya kupoteza damu, kifafa cha mimba na maambukizi ya bakteria.**

33. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na wadau wake inaendelea kufanya ufuatiliaji wa takwimu za vifo vitokanavyo na uzazi. Aidha, kwa mujibu wa matokeo ya Utafiti wa Hali ya Afya na Watu (TDHS) yalijotolewa mwaka 2015/2016 ilionesha kuwa vifo vitokanavyo na uzazi ni 556 kwa kila vizazi hai 100,000. Katika kipindi hicho hadi sasa Wizara imetekeleza afua mbalimbali zenyе lengo la kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi. Afua hizo ni pamoja na; utekelezaji wa Kampeni ya Jiongeze Tuwavushe Salama, ujenzi na upanuzi wa vituo vya kutolea huduma za afya na kuvizezesha kutoa huduma za dharura za upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni pindi mama anapokabiliwa na uzazi pingamizi, ujenzi wa vituo vya ukusanyaji wa damu salama na mazao ya damu. Kwa hali hiyo ni matarajio ya Wizara kwamba utafiti wa TDHS unaotarajiwa kufanyakia kuanzia mwezi Novemba 2021 utatoa matokeo yenye kupungua kwa vifo vitokanavyo na uzazi.

34. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa dawa muhimu za Afya ya uzazi, taarifa zinaonesha kuwa katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, dozi 4,330,607 za dawa ya kukinga na kuzuia upungufu wa damu kwa wajawazito zilinunuliwa na kusambazwa katika vituo vya kutolea huduma za Afya nchini. Jumla ya wajawazito 1,101,830 sawa na asilimia 63 ya wajawazito 1,760,707 waliohudhuria kliniki walipatiwa dawa za kutibu minyoo ya tumbo, na wajawazito 1,669,122 sawa na asilimia 95.6 ya waliopimwa kipimo cha Malaria, kati yao asilimia 8.5 walikutwa na maambukizi ya malaria na kuanzishiwa matibabu.

35. ***Mheshimiwa Spika***, dawa nyingine muhimu ambazo ziliendelea kupatikana katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021 ni pamoja na dozi 327,220 za sindano ya *Magnesium Sulphate* kwa ajili ya kukinga na kutibu kifafa cha mimba, dozi 87,300,000 za vidonge vya *Fefokwa* ajili ya matibabu ya upungufu wa damu, dozi 2,946,770 za sindano ya *Oxytocin*, inayotumika kuzuia na kutibu kutokwa na damu nyingi baada ya kujifungua zilinunuliwa na kusambazwa na kuwezesha upatikanaji wake kufikia asilimia 95 ya mahitaji. Vilevile, dawa za sindano za *Dexamethasone* ambazo

hupewa mama kumsaidia mtoto kupumua inapotokea mama mjamzito yuko kwenye hatari ya kujifungua mtoto njiti, ilipatikana kwa asilimia zaidi ya 90 ya mahitaji katika vituo vya kutolea huduma za Afya nchini.

36. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa matibabu ya ugonjwa wa kuharisha kwa watoto walio chini ya miaka mitano, dawa aina ya Zinki na ORS dozi 103,050 zilizofungashwa pamoja zilinunuliwa na kusambazwa. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuhakikisha upatikanaji wa kidonge myeyuko cha *Amoxicillin* kwa ajili ya matibabu ya Nimonia, ambapo jumla ya dozi 30,782,700 zilinunuliwa na kusambazwa.

37. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inaendelea kufanya ufuatiliaji endelevu wa afya ya Watoto. Kwa mujibu wa matokeo ya Utafiti wa Hali ya Afya na Watu (TDHS) yaliyotolewa mwaka 2015/2016 ilionesa kuwa vifo vya Watoto vilipungua kama ifuatavyo: Vifo vya Watoto chini ya miaka mitano vilipungua kutoka vifo 81 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2010 hadi vifo 67 kwa kila vizazi hai 1,000; Vifo vya Watoto chini ya mwaka mmoja kutoka vifo 51 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2010 hadi vifo 43 kwa kila vizazi hai 1,000; na vifo vya Watoto wachanga vilipungua kutoka vifo 26 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2010 hadi vifo 25 kwa kila vizazi hai 1,000. Hivyo, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Wizara imetekeleza afua mbalimbali zenyе lengo la kupunguza vifo vya watoto. Afua hizo ni pamoja na; kusisitiza umuhimu wa wajawazito kuhudhuria kliniki ipasavyo, kujifungulia kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, utekelezaji wa Kampeni ya Jiongeze Tuwavushe Salama na kufanya tathmini na uanzishaji wa vyumba maalum kwa ajili ya matibabu ya Watoto wachanga wagonjwa. **Kwa hali hiyo ni matarajio ya Wizara kwamba utafiti wa TDHS unaotarajiwa kufanya kuanzia mwezi Novemba, 2021 utatoa matokeo yenye kupungua kwa vifo vya Watoto.**

38. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha huduma za afya kwa mtoto mchanga na kupunguza vifo vya Watoto wachanga nchini, Wizara imejiwekea lengo la kufikia asilimia 80 ya

hospitali 350 (zinazomilikiwa na Serikali, Taasisi za Dini, Mashirika na watu binafsi) kuwa na vyumba maalum kwa ajili ya matibabu ya Watoto wachanga wagonjwa ifikapo mwaka 2025. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya hospitali 61 zilifanyiwa tathmini na kuagizwa kuanzisha vyumba hivyo. Hospitali zilizofanyiwa tathmini na kuanzisha vyumba maalum kwa ajili ya Watoto wachanga wagonjwa zinatoka katika Mikoa 12 ambayo ni; Mbeya, Ruvuma, Pwani, Simiyu, Shinyanga, Mwanza, Manyara, Tabora, Kagera, Mara, Dodoma na Geita. **Natoa rai kwa Tawala za Mikoa yote nchini, kusimamia uanzishwaji wa vyumba hivyo kwa kila Hospitali kulingana na mpango kazi uliowekwa na kuhakikisha uwepo wa vifaa na watoa huduma wenye stadi na ujuzi wa kuhudumia watoto wachanga, njiti na watoto wagonjwa wanaohitaji huduma hiyo.**

39. ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza vidokezo muhimu vya Umoja wa Mataifa vya kuwa na wigo mpana wa upatikanaji wa huduma za dharura za afya ya uzazi na mtoto, umefanyika ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya 487 ili kuwezesha kutoa huduma kwa wajawazito wanaopata matatizo mbalimbali ya uzazi yakiwemo kupoteza damu wakati wa ujauzito na baada ya kujifungua, kifafa cha mimba na uzazi pingamizi. Hadi kufikia Machi 2021, jumla ya vituo 258 sawa na asilimia 52 vilikuwa tayari vimeanza kutoa huduma kamili za dharura za afya ya uzazi na mtoto ikiwamo ya upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni. Wizara kwa ushirikiano wa karibu na Ofisi ya Rais TAMISEMI inaendelea kuhakikisha vituo vyote vya afya vilivyojengwa ambavyo havijaanza kutoa huduma vinapata watumishi wenye ujuzi wakiwemo madaktari, watoa dawa za usingizi, na wakunga pamoja na vifaa tiba kwa nia ya kuharakisha kuanza utoaji wa huduma.

40. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, watumishi wa vituo vya afya vilivyokarabatiwa katika mikoa nane ya Mtwara, Lindi, Singida, Geita, Simiyu, Mara, Katavi na Kigoma walipata mafunzo kazini, kutoka kwa wabobezi wa masuala ya ganzi na usingizi kutoka "Society of Anaesthesiology Tanzania, Association of Obstetrics and Gynecology" na Wauguzi na Wakunga wabobezi kwenye

uendeshaji wa vyumba vya upasuaji. **Wito unatolewa kwa Mikoa na Halmashauri kuhakikisha kuwa haya majengo ambayo yameshakamilika yaanze kutumika kutoa baadhi ya huduma za afya ya uzazi na mtoto katika kipindi hiki cha mpito ambapo Serikali inakamilisha uwezeshaji wa vituo hivi kutoa huduma zote.**

41. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeweeka nia thabitii ya kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma za uchunguzi na matibabu ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi kufikia vituo 2,123 ifikapo mwaka 2024. Hadi kufikia Machi 2021, asilimia 30 ya lengo ambayo ni sawa na vituo 794 vya uchunguzi wa awali wa saratani ya mlango wa kizazi vilikuwa vimeanzishwa na kuanza kutoa huduma, ikilinganishwa na vituo 623 mwaka 2019/20. Aidha, jumla ya akina mama 332,620 sawa na asilimia 43.4 ya lengo walifanyiwa uchunguzi wa awali wa saratani ya mlango wa kizazi, kati ya lengo la kufikia akina mama 766,370 katika kipindi hicho. ***Saratani ya mlango wa kizazi inazuilika hivyo, wanawake jitokezeni kufanya uchunguzi ili tuweze kupunguza kwa kiasi kikubwa vifo na madhara yatokanayo na saratani ya mlango wa kizazi.***

42. ***Mheshimiwa Spika***, katika kupambana na matukio ya ukatili Serikali imeendelea kutoa huduma jumuishi za afya kwa waathirika wa vitendo mbalimbali vya ukatili hapa nchini kupitia vituo jumuishi 13 (One Stop Centres) vilivyoanzishwa katika Mikoa ya Arusha (Mount Meru RRH), Shinyanga (Shinyanga RRH, Hospitali ya Wilaya Kahama na Kituo cha Afya Nindo), Tabora (Kitete RRH), Mbeya (Hospitali ya Magereza), Dar es Salaam (Mwananyamala na Amana RRH), Mwanza (Sekou Toure RRH), Kilimanjaro (Hospitali ya Wilaya ya Hai), Pwani (Tumbi RRH), Iringa (Hospitali ya FFU) na Simiyu (Hospitali ya Wilaya Simiyu). Katika Kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla walihudumiwa wahanga 134,310 (wanawake 106,196 na wanaume 28,114). ***Ukatili kwenye jamii yetu haukulaliki hivyo, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali na kupitia Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000) itaendelea kutoa mchango wake wa kuimarisha mifumo ya kusaidia kuibua wote wanaofanya na kufanyiwa ukatili kwa ajili ya hatua stahiki. Aidha, huduma***

ya vituo jumuishi kwa waliofanyiwa ukatili itaendelea kusogezwa kwenye mikoa mingine.

### Afya ya Usafi na Mazingira

43. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa awamu ya pili ya Kampeni ya Taifa ya Usafi wa Mazingira yenye kaulimbiu isemayo "**USICHUKULIE POA NYUMBA NI CHOO**" yenye lengo la kuhimiza ujenzi na matumizi ya vyoo bora na vifaa vya kunawia mikono vyenye maji tiririka na sabuni katika ngazi ya kaya na taasisi. Kupitia kampeni hii, idadi ya vyoo bora imeongezeka kutoka asilimia 64 mwezi Juni, 2020 hadi kufikia asilimia 68 mwezi Machi, 2021. Vilevile, kaya zenyе vifaa vya kunawia mikono vyenye maji tiririka na sabuni zimeongezeka kutoka asilimia 40 Juni, 2020 kufikia asilimia 42 Machi, 2021. Hata hivyo, mwitikio wa jamii bado hauna kasi nzuri hivyo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara nyingine itaimarisha Elimu ya Afya pamoja na matumizi ya Sheria ya Afya ya Jamii ya mwaka 2009 na kufanya ufuatiliaji wa kina.

44. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha vituo vya kutolea huduma za afya nichini vinafikia lengo la Malengo ya Maendeleo Endelevu kuhusu huduma endelevu za maji na usafi wa mazingira kwa wote, Wizara kwa kushirikiana na sekta nyingine za Maji na Elimu imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mradi wa Huduma Endelevu za Maji na Usafi wa Mazingira vijiji yaani *Sustainable Rural Water Supply and Sanitation (SRWSS)*. Kwa upande wa sekta ya afya, utekelezaji huu umejikita katika kuwezesha ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maji na usafi wa mazingira kwenye vituo vya kutolea huduma za Afya katika mikoa 17 na Halmashauri 86. Mikoa hiyo ni; Kagera, Mwanza, Geita, Simiyu, Mara, Shinyanga, Singida, Manyara, Tabora, Kigoma, Katavi, Rukwa, Songwe, Iringa, Lindi, Mtwara na Ruvuma. Kiasi cha **Shilingi 24,024,379,125** zimetumika ambapo hadi Machi, 2021 vituo 813 vimekarabatiwa au kujengwa upya miundombinu ya maji na usafi wa mazingira na kazi inaendelea.

45. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2020/21, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo iliweza kufanya tafti ya ufanisi wa uteketezaji wa makondo ya nyuma (Placenta disposal). Utafiti huo ulifanyika katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mwananyamala na Hospitali ya Halmashauri ya Ubungo (Sinza Palestina) mkoani Dar es Salaam kwa kutumia njia ya kibaolojia ijlukanayo kama *bio-digester system* ambapo aina hii ya taka huwekwa kwenye tanki duara liliojengewa chini ya ardhi na kuchanganywa na mabaki ya chakula ili kuwezesha uchakataji ulio sawia kuzalisha gesi asilia (bio-gas) ambayo sasa inatumika kama nishati ya kupikia na kuchemshia maji kwa ajili ya matumizi ya hospitali. **Teknolojia hii inasaidia kupunguza changamoto ya wapi zitupwe taka hizo lakini pia inaongeza tija katika kutunza mazingira na nishati ambayo ingehitaji pengine kulipa gharama ili kuipata.**

46. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inakusudia kuendeleza teknolojia hii kwenye hospitali 10 za rufaa za mikoa ya Dodoma, Njombe, Iringa, Ruvuma, Kigoma, Manyara, Mbeya, Arusha, Mwanza na Geita. Aidha, Wizara imepanga kuongeza kasi ya uboreshaji wa mfumo wa udhibiti salama wa taka hatarishi zinazozalishwa kutokana na huduma za afya. Wizara itashirikiana na OR-TAMISEMI ili kuongeza idadi ya viteketezi taka vinyavyokidhi viwango vya afya na mazingira. Vilevile, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau pamoja na sekta binafsi ili kuanzhishwa kwa *Centralized Biomedical Waste Treatment Centers* kwa lengo la kuongeza udhibiti salama wa taka kwenye maeneo ya mijini ili kuziwezesha hospitali na vituo vya kutolea huduma za afya kupeleke taka walizozalisha katika eneo hilo.

### **Huduma ya Lishe Nchini**

47. ***Mheshimiwa Spika***, lishe bora ni muhimu kwa uhai, ukuaji na maendeleo ya binadamu kiakili na kimwili na hivyo huchangia kuongeza tija katika uzalishaji mali kwa kaya na kuimarisha uchumi wa Taifa kwa ujumla. Katika kuhakikisha hilo linafanikiwa, Wizara imekuwa ikitekeleza Mpango Jumuishi wa Kitaifa wa Lishe (National Multisectoral Nutrition

Action Plan 2016/17 – 2020/21) ambao kwa sasa umeanza kufanyiwa mapitio. Kupitia Mpango huo Serikali imekuwa ikitekeleza afua mbalimbali ili kukabiliana na matatizo ya utapiamlo wa lishe duni na ule wa lishe ya kuzidi. Afua hizo ni pamoja na: utoaji wa matone ya vitamin A na dawa za kutibu minyoo ya tumbo; matibabu ya utapiamlo mkali kwa watoto; utoaji wa vidonge vya madini chuma na *folic acid* kwa wajawazito; uongezwaji wa virutubishi vya madini na vitamini kwenye vyakula vinavyoliwa kwa wingi kwenye jamii ikiwemo unga wa ngano, unga wa mahindi na mafuta ya kula; utoaji wa elimu ya lishe; uhamasishaji masuala ya ulaji unaofaa kwa kutumia vyakula vinavyopatikana kwenye maeneo yetu; na kufanya mazoezi.

48. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuimarisha afya na lishe ya watoto wachanga na wadogo kwa kuendelea kutekeleza Kampeni ya Kitaifa ya utoaji wa matone ya Vitamin A kwa watoto walio chini ya miaka mitano. Malengo ya kampeni ya mwaka 2020/21 yalikuwa ni kutoa matone ya Vitamin A kwa watoto 8,591,810 wa katи ya umri wa miezi (6 – 59). Zoezi hili llikamilika kwa kuweza kuwafikia walengwa 8,334,056 sawa na asilimia 97. Vilevile, Wizara imeendelea kuimarisha huduma za matibabu ya utapimlo mkali kwa watoto kwa kuimarisha upatikanaji wa chakula dawa, upatikanaji wa vifaa vya kufanya tathmini ya hali ya lishe pamoja na kuboresha miundombinu ya kufanya matibabu ya utapiamlo mkali kwa watoto. Aidha, vituo vinavyotoa matibabu ya kulaza ya utapiamlo mkali vimeongezeka kutoka vituo 330 mwaka 2019/20 kufikia vituo vya kutolea huduma za afya 365 Machi 2021. **Lishe bora ni mojawapo ya misingi imara ya kufikia afya njema.** Hivyo, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji makini wa afua zote zinazohusu afya ya lishe kwa kushirikiana na wadau wake wote.

#### **Elimu ya Afya kwa Umma**

49. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuimarisha mikakati ya kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu magonjwa mbalimbali ya kuambukiza na milipuko ikiwemo ugonjwa wa COVID-19 na magonjwa yasiyoambukiza.

Maeneo muhimu yanayozingatiwa katika utoaji elimu kwa umma ni pamoja na faida za lishe bora na umuhimu wa kufanya mazoezi, athari za utapiamlo kwa makundi mbalimbali, Afya ya mama na mtoto na Afya ya Mazingira.

50. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ilikuwa na malengo ya kutoa elimu ya afya kwa jamii kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, ambapo vipindi 320 vilipangwa kufanyika kupitia Radio na Runinga (TV). Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya vipindi 104 vimefanyika katika vituo vya Azam, TBC, ITV, Cloud, Clouds Plus, Channel 10, Star TV, East Africa TV, Mlimani TV, Imaan TV na Uhai TV pamoja na Redio za Kijamii katika Mikoa 12 nchini. Aidha, jumla ya machapisho 203,000 yalitolewa kupitia mitandao ya Kijamii (Facebook, Instagram na Twitter). Pia, Makala 46 ziliandikwa na kuchapishwa kupitia magazeti ya Nipashe, Uhuru, Fahari Yetu, *Daily News*, Mwananchi, Majira na Habari leo. Vilevile, Wizara ilianda Video 1,200 zenye jumbe mbalimbali zilizohusu masuala ya afya na kurushwa kwenye mitandao ya kijamii na Tovuti ya Wizara na Taasisi zake ambapo jumla ya wafuatiliaji (followers) 78,819 walisoma jumbe hizo. Kati ya wafuatiliaji hao, *Facebook* walikuwa 70,790, *Instagram* 5,350, *Twitter* 1,407 na Tovuti ya Taasisi 1,272.

51. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inaendelea kuimarisha Kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma ili kuweza kuandaa machapisho yenye ujumbe wa picha, katuni, video na sauti kwa lengo la kuelimisha Jamii. Aidha, katika kuhakikisha wananchi wanajibowi maswali yao na kuboresha huduma za afya, Wizara imeanzisha Kituo cha Huduma kwa Wateja (Afya Call Centre) ambapo mwananchi anaweza kupiga Namba 199 bure na kuongea na wataalam wa afya moja kwa moja. Kituo hiki hufanya kazi saa 24, ambapo kimekuwa kikipokea simu kati ya 20,000 hadi 30,000 kwa siku. Wananchi wamefaidika na kituo hiki hasa katika kipindi hiki dunia ikikabiliwa na mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19, wananchi hujibowi maswali na hutoa maoni yao. Mfumo uliowekwa katika huduma hii ya simu unaruhusu mwananchi kupiga na kuchagua kupata elimu kuhusu magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza bila kulazimika kuongea na

mhudumu. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi sasa, jumla ya simu 36,254,764 zilipigwa kutoka kwa wateja na kati ya hizo simu 33,226,000 zilipokelewa na kufanyiwa kazi.

Aidha, katika kuimarisha uwajibikaji wa pamoja na kuwatia moyo wananchi, mimi na wasaidizi wangu (Manaibu Waziri) tumetoa namba zetu za simu za mkononi ili zижilikane kwa wananchi pale inapoonekana wanahitaji rufaa wasikose fursa hiyo kwa kutuma walau ujumbe mfupi. **Hivyo, Wizara inashirikiana vema na wananchi na mambo mengi ya kero za wananchi yamekuwa yakipatiwa ufumbuzi sambamba na kuwaimarisha zaidi watoa huduma za afya katika kuhudumia wananchi.**

#### **Udhibiti wa VVU/UKIMWI**

52. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kutekeleza Mpango Mkakati Mtambuka wa UKIMWI wa Nne (2018 – 2023) na Mpango Mkakati wa UKIMWI wa Sekta ya Afya wa Nne (2018 – 2022) ambapo ilitekeleza malengo ya Tisini Tatu (90-90-90) hadi mwisho wa mwaka 2020. Malengo yalikuwa ni kufikia asilimia 90 ya Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (WAVIU) wawe wamepimwa na kujua hali zao za maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU), asilimia 90 kati ya waliotambua hali zao za maambukizi wawe wanatumia tiba endelevu ya ARV na asilimia 90 ya walio kwenye tiba wawe wamefubaza VVU kwenye damu. Kwa mwaka 2020, Tanzania ilikadiriwa kuwa na watu 1,700,000 WAVIU.

53. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia mwezi Machi 2021, WAVIU milioni 1.4, sawa na asilimia 83 ya WAVIU wote walikuwa wametambua hali zao za VVU. Kati yao, WAVIU Milioni 1.36 sawa na asilimia 98 walikuwa katika tiba endelevu ya ARV na asilimia 92 walikuwa wamefubaza virusi. **Haya ni mafanikio makubwa ya Serikali yaliyofikiwa katika kupambana na VVU na UKIMWI.** Aidha, Serikali imeendelea kuhakikisha huduma za utoaji wa dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI (ARV) zinakuwa karibu zaidi na wananchi na kutanua wigo wa huduma hiyo mijini na vijijini ili kupunguza gharama za nauli na kuondoa msongamano katika vituo vya kutolea huduma

hiyo. Hadi kufikia Machi 2021, vituo vipya 299 vimeongezeka vinavyotoa dawa za kupunguza makali ya VVU na hivyo kufikia vituo 6,828 ikilinganishwa na vituo 6,529 vilivyokuwa vinatoa huduma hiyo mwaka 2019/20.

54. ***Mheshimiwa Spika***, huduma za kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT), zimeendelea kutolewa kuititia vituo mbalimbali kama ilivyoelezwa hapo juu, ambapo kwa mwaka 2020/21, jumla ya akina mama wajawazito 1,695,594 sawa na asilimia 98 ya lengo la akina mama 1,729,952 walipatiwa huduma za ushauri nasaha na upimaji wa VVU. Aidha, kati yao akina mama 57,569 sawa na asilimia 3.3 waligundulika kuwa wanaishi na VVU. Akina mama 56,712 sawa na asilimia 98 ya akina mama wenye maambukizi ya VVU walipatiwa dawa (ARV) kwa ajili ya kufubaza VVU. **Wito wangu kwa akina mama wajawazito wazingatie kupata huduma ya vipimo hivi kliniki ili atakayegundulika kuwa na maambukizi ya VVU aweze kupatiwa huduma stahiki.**

55. ***Mheshimiwa Spika***, kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya watoto 47,465 sawa na asilimia 68 walipata kipimo cha awali cha utambuzi wa maambukizi ya VVU ambapo watoto 949 sawa na asilimia 2 walikutwa na maambukizi ya VVU. Kiwango hicho cha maambukizi kinaashiria Tanzania ipo katika kasi sawia ya kuweza kufikia maambukizi chini ya asilimia 2 ifikapo mwaka 2025. Hii ni kama inavyoainishwa katika mpango mkakati wa kutokomeza kabisa maambukizi ya VVU kwa watoto. Maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto baada ya kuacha kunyonya sasa ni asilimia 8 kutoka asilimia 9 mwaka 2019/20.

### **Udhibiti wa Kifua Kikuu na Ukoma**

56. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, lengo la Wizara lilikuwa ni kufanya ugunduzi wa wagonjwa 67,000 wa Kifua Kikuu ambapo jumla ya wagonjwa 60,068 sawa na asilimia 90 ya lengo waligundulika kuwa na Kifua Kikuu. Sababu zilizochangia kufikia mafanikio hayo ni pamoja na kufanya kampeni za uchunguzi kwa kushirikisha

watoa huduma ngazi ya jamii na ununuzi na usambazaji wa mashine za *GeneXpert* 259 katika halmashauri 158 kati ya 184 zilizopo. Aidha, katika kipindi hiki, Wizara ilianza awamu ya pili ya utekelezaji wa afua ya kuboresha huduma za kuzuia maambukizi ya Kifua Kikuu katika Magereza, afua hii inahusisha uanzishaji wa uchunguzi wa Kifua Kikuu kwa wafungwa wapya na uchunguzi wa wafungwa gerezani kila baada ya miezi mitatu na tayari magereza 34 yametembelewa. Katika ziara hizi, jumla ya wafungwa 7,418 walichunguzwa, 2,279 walihisiwa kuwa na Kifua Kikuu na 24 waligundulika kuwa na Kifua Kikuu na kuanzishiwa matibabu. **Hivyo, katika kupambana na kudhibiti Kifua Kikuu Serikali inafanya kazi kuhakikisha inayafikia makundi yote ya jamii bila kusahau walioko magerezani.**

57. ***Mheshimiwa Spika***, katika juhudini za kutanua wigo wa uibuaji wa wagonjwa wa Kifua Kikuu, Wizara ilifanikiwa kuongeza idadi ya maduka ya dawa muhimu na famasi zenye uwezo wa kuwaibua wagonjwa wa Kifua Kikuu kuititia mfumo wa rufaa kwa wahisiwa kwenda kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kwa uchunguzi na ugunduzi, kutoka maduka 300 katika Mikoa 10 mwaka 2019/20 hadi maduka 870 katika Mikoa 19 Machi 2021 sawa na ongezeko la asilimia 190 ya maduka. Kuititia afua hii jumla ya wagonjwa 500 wa Kifua kikuu walibuliwa na kuanzishiwa matibabu katika kipindi husika.

58. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea na uboreshaji wa miundombinu ya vituo vya kutolea huduma za upimaji wa Kifua Kikuu. Hadi mwezi Machi 2021, jumla ya vituo 1,613 nchini vilikuwa na uwezo wa kupima ikilinganishwa na vituo 1,201 vilivyokuwepo mwaka 2019. Aidha, kwa upande wa Kifua Kikuu sugu Wizara imeongeza ugatuvi wa huduma za kifua Kikuu sugu, na hadi kufikia mwezi Machi 2021, jumla ya vituo vya huduma za afya 177 nchini vilikuwa vimewezeshwa kutoa huduma hizi ikilinganishwa na vituo 145 vilivyokuwa vinatoa huduma hizi mwaka 2019.

59. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, upande wa huduma za Ukoma, jumla ya kaya

269 zilitembelewa (contact tracing) na kufanya uchunguzi wa Ukoma katika Halmashauri za Wilaya 10 za Chato, Ifakara Mji, Kilombero, Lindi DC, Liwale, Mkinga, Muheza, Morogoro DC, Mvomero na Nanyumbu. Kupitia zoezi hili wagonjwa wapya 59 wamegunduliwa na wameanzishiwa matibabu ya Ukoma. Hadi kufikia Machi, 2021 idadi ya wagonjwa 832 wamegunduliwa nchi nzima ikilinganishwa na wagonjwa 1,151 kwa kipindi kama hicho mwaka 2019/20. Aidha, idadi ya watoto wanaougua Ukoma imepungua kwa asilimia 50 kutoka watoto 53 mwaka 2019/20, hadi kufikia watoto 27 mwezi Machi, 2021.

### **Udhhibit wa Malaria**

60. ***Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na ugonjwa wa Malaria, Serikali imeendelea kutekeleza afua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya Kampeni maalum ya usambazaji wa vyandarua vyenye dawa kwenye kaya bila malipo ambapo ililuhisha jumla ya Halmashauri 50 katika Mikoa 10 nchini. Kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya vyandarua 8,578,562kati ya 8,733,089 vilisambazwa sawa na asilimia 98 ya lengo. Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa, dawa za kutibu malaria na vitendanishi zinapatikana wakati wote kwenye vituo vya kutolea huduma za Afya nchini. Kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Wizara imenunua na kusambaza jumla ya dozi 6,455,970 za Dawa Mseto za malaria (ALu), Sindano Artesunatevichupa 1,079,247 kwa ajili ya matibabu ya Malaria kali (severe Malaria), vitendanishi 30,676,000 na Dawa ya SP dozi 2,136,000 kwa ajili ya tiba-kinga kwa wajawazito. **Natoa wito kwa wananchi kuhudhuria** vituo vya afya kupata huduma za vipimo kutambua asili ya ugonjwa husika kwani si kila homa ni malaria. Serikali imeweuka mazingira mazuri ya uwepo wa vipimo na dawa kwa ajili ya utambuzi wa homa za malaria.

61. ***Mheshimiwa Spika***, kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, wagonjwa waliothibitishwa kuwa na vimelea vya Malaria kwa kutumia vipimo vya mRDT imeongezeka hadi kufikia asilimia 99 mwezi Desemba, 2020 ikilinganishwa na asilimia 98 mwaka 2019. Ongezeko hili limetokana na

upatikanaji wa muda wote wa vitendanishi vyakupimia malaria kwenye vituo vyakutolea huduma za afya na uelewa sahihi wa watoa huduma kutokana na mafunzo yaliyotolewa. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Serikali imeendelea kutekeleza afua ya kupulizia dawa ukoko katika makazi ambapo, jumla ya nyumba 552,643 kati ya 592,428 sawa na asilimia 93 zimepuliziwa dawa ukoko katika Halmashauri 6 zenyetmaambukizi makubwa ya Malaria ambazo ni Bukombe, Ukerewe, Bihamulo, Kakonko, Kibondo na Kasulu ikijumuisha Kambi tatu za Wakimbizi za; Mtendeli, Nyarugusu na Nduta. **Nachukua fursa hii kutoa wito kwa wananchi kupokea teknolojia ya upulizaji wa dawa ukoko kwenye nyumba zao pamoja na matumizi ya mbinu za kudhibiti mazalia ya viluwiluvi vyambu karibu na makazi wakati Serikali ikitekeleza mikakati mikubwa zaidi ya kudhibiti Malaria nchini. Tanzania bila Malaria inawezekana.**

62. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeanzisha afua mpya ya ufuatiliaji wa wagonjwa wa Malaria hadi ngazi ya kaya (Case Based Malaria Surveillance - CBS) kwa mikoa yenye kiwango kidogo sana cha maambukizi ya malaria nchini ambayo ni Kilimanjaro, Arusha na Manyara. Aidha, mikutano ya viongozi wa dini imefanyika katika mikoa sita ikijumuisha viongozi 72 wa kidini ambao wamehamasishwa juu ya afua mbalimbali za udhibiti wa malaria kwa ajili ya kuwafikia waumini wao. Vilevile, urushaji wa matangazo 629 ya redio kupitia vituo mbalimbali ulifanyika kwa lengo la kuhamasisha jamii juu ya upatikanaji wa dawa mseto ya Malaria kwa bei punguzo kwa sekta binafsi.

63. ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na utekelezaji wa afua mbalimbali za kudhibiti malaria nchini, visa vipyta vyamalaria (Incidence) vilipungua kwa asilimia 35 kutoka visa 162 kati ya watu 1,000 mwaka 2015 hadi visa 106 mwaka 2020, idadi ya vifo vitokanavyo na malaria vimepungua kwa takriban asilimia 61 kutoka vifo 6,311 mwaka 2015 hadi vifo 2,460 mwaka 2020.

### **Udhibiti wa Magonjwa ya Mlipuko**

64. ***Mheshimiwa Spika***, nchi yetu imeendelea kuwa salama licha ya tishio la kuwepo kwa Ugonjwa wa Ebola katika nchi jirani za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na nchi ya Uganda. Wizara ilichukua tahadhari na imeendelea kulinda mipaka yake dhidi ya magonjwa ya milipuko. Serikali imeendelea kudhibiti mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu ambapo katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, ni Mkoa mmoja tu wa Kigoma ndio uliripoti uwepo wa wagonjwa 77 kati yao Wagonjwa 75 walitibiwa na kupona na vifo viwili vilitokea.

65. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kupambana na maambukizi ya COVID-19, ambapo jitihada mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa ikiwemo kutoa miongozo zaidi ya 15 ya namna bora ya kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo ikiwa ni pamoja na kuhamasisha wananchi kunawa mikono mara kwa mara kwa maji safi tiririka na sabuni; kutumia vipukusi (sanitizer) mara kwa mara pale ambapo hakuna maji safi tiririka na sabuni; kufanya mazoezi mara kwa mara pamoja na lishe bora ikiwemo matunda na mbogamboga. Vilevile, Serikali imekuwa ikijielekeza kuwalinda wale wote walio katika makundi ya hatari zaidi dhidi ya ugonjwa huu kama vile wazee na wenye magonjwa ya muda mrefu.

66. ***Mheshimiwa Spika***, afua nyininge zilizoendelea kutekelezwa na Serikali ni pamoja na kuhamasisha jamii kuimarisha matumizi ya Tiba Asili zilizosajiliwa kwa matumizi mbalimbali ikiwemo kujifukiza; uvaaji wa barakoa za kushona na zile za viwandani hasa zinazotengenezwa ndani ya nchi; na kuwahi katika vituo vya kutolea huduma za afya mara mwananchi anapoona dalili za maradhi ili watoa huduma wapate nafasi nzuri zaidi ya kuhudumia. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Wadau iliendelea kutoa elimu ya kujikinga na magonjwa mbalimbali yanayotolewa taarifa kulingana na miongozo ya Shirika la Afya Duniani (WHO).

67. ***Mheshimiwa Spika***, katika hatua za kuimarisha udhibiti wa ugonjwa huu na magonjwa mengine ya milipuko, Wizara

imenunua na kusambaza vipimajoto 590 (Handheld 569 na Walkthrough thermal Scanners 21), Barakoa boksi 100,000, sanitizer lita 10,000, Pampu 48 za kutakasa vyombo vya usafiri na vifaa vya kunawia mikono (ndoo 500, tenki 12 za lita 5,000) na kuvisambaza kwenye mipaka 40 iliyoko kwenye mikoa 14 ya Dar es Salaam, Mwanza, Kagera, Kigoma, Mbeya, Mara, Arusha, Kilimanjaro, Rukwa, Katavi, Mtwara, Ruvuma, Tanga na Lindi. Aidha, jumla ya wasafiri 6,446,710 walifanyiwa uchunguzi katika maeneo yote ya mipakani. Wale waliobainika kuwa na changamoto za kiafya walipatiwa huduma na kuruhusiwa kuendelea na shughuli zao. Aidha, Wizara katika jitihada za kuimarisha udhibiti wa magonjwa yenye hatari ya kusambaa kimataifa immeanzisha mfumo wa kidigitali wa ufuutiliaji wa afya za wasafiri. Mfumo umeanza mwezi Aprili, 2021 na unapatikana katika wavuti *afyamsafiri.moh.go.tz*.

68. ***Mheshimiwa Spika***, licha ya Ugonjwa huu kuisumbua Dunia kwa kiwango kikubwa hasa Mataifa Makubwa Duniani, Tanzania imeendelea kupiga hatua kubwa katika kuudhibiti na kutosababisha tahiruki kwa wananchi, ikiwemo kutowafungia (lockdown) bali kuwapa elimu na kusimamia utekelezaji wa afua za kujikinga. Kwa dhati tunawashukuru sana Viongozi wetu **Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli** aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano na **Mheshimiwa Samia Suluhi Hassan** Rais wa Awamu ya Sita kwa Uongozi Imara kwenye eneo hili katika kipindi chote Nchi ilipokuwa inapita katika janga la ugonjwa wa COVID-19. **Nichukue fursa hii kuwashukuru kwa dhati watoa huduma wote, Timu zetu za kitaalam, Viongozi wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau kwa jinsi walivyojitoa katika kuwashukuru wote waliopata matatizo mbalimbali yatokanayo na ugonjwa huo.**

Vilevile, Wizara inawashukuru Watanzania wote kwa kushikamana kwenye kuitikia na kutekeleza ushauri wa kitaalam na maelekezo ya viongozi wetu kuhakikisha kuwa tunapigana vita hivi bila kuleta athari na hasara kubwa zaidi zitokanazo na maamuzi ya jinsi gani tupigane vita hivi. Niwahakikishie Watanzania wenzangu kuwa tupo vizuri na mafanikio ni makubwa na tuendelee kushikamana katika

kuudhibiti ugonjwa huo na kuendelea kuchukua tahadhari zote zinazotolewa na wataalam wa afya.

### **Udhibiti wa Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele**

69. *Mheshimiwa Spika*, tangu mwaka 2009, Wizara imekuwa ikitekeleza Mpango Mkakati wa Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele (2021 – 2026). Magonjwa hayo ni pamoja na; ugonjwa wa Matende na Mabusha ulioathiri halmashauri 119 nchini, Ugonjwa wa trakoma ambao umeathiri halmashauri 71, ugonjwa wa usubi ambao umeathiri halmashauri 28na magonjwa ya kichocho na minyoo ya tumbo ambayo yameathiri halmashauri zote 184 nchini. Mafanikio makubwa ya Mpango huu kwa ujumla ni pamoja na kuwa, halmashauri zote zilizoathirika na magonjwa haya zimeweza kuendesha zoezi la umezeshaji wa dawa za kingatiba mara moja kila mwaka ili kuyadhibiti na hatimaye kuyatokomeza magonjwa haya.

Tathmini zilizofanyika kati ya mwaka 2015 na 2020 ili kubaini ni kwa kiwango gani magonjwa hayo bado yameathiri jamii yetu matokeo yalionesha kwamba halmashauri 112 kati ya 119 zilizokuwa zimeathirika na ugonjwa wa matende na mabusha zimefanikiwa kutokomeza ugonjwa huo hali ambayo imewaondoa wananchi wapatao milioni 25.1 katika hatari ya kupata madhara ya ugonjwa wa matende na mabusha. Kwa upande wa ugonjwa wa trakoma, tathmini zimeonesha kuwa halmashauri 65 kati ya 71 zilizokuwa zimeathirika na ugonjwa wa trakoma zimefanikiwa kutokomeza ugonjwa huo hali ambayo imewezesha wananchi milioni 17.1 kuondokana na hatari ya kupata madhara yanayotokana na ugonjwa huo.

70. *Mheshimiwa Spika*, katika kudhibiti magonjwa ya usubi, kichocho na minyoo ya tumbo shughuli za umezeshaji wa kingatiba na mipango ya kufanya tathmini ya kiwango cha maambukizikatika halmashauri zote zilizoathirika nchini inaendelea. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi, 2021 umezeshaji wa dawa (kingatiba) kwa magonjwa ya kichocho na Minyoo ya Tumbo zilitolewa kwa watoto wenye umri wa

kwenda shule wapatao 5,097,937 katika Halmashauri 92 za Mikoa 19 ikiwa ni asilimia 95 ya walengwa. Mafanikio haya yametokana na upatikanaji wa dawa, rasilimali fedha, uhamasishaji na mwitikio mzuri wa jamii. Aidha, jumla ya wagonjwa 753 wa Mabusha walifanyiwa upasuaji katika Halmashauri tatu za Lindi, Kilwa na Ruangwa katika Mkoa wa Lindi. Vilevile, Wagonjwa 868 wa trakoma walifanyiwa usawazishaji wa Vikope katika Mikoa mitano ya; Pwani, Mtwara, Lindi, Ruvuma na Singida. Mafanikio haya yametokana na ushirikiano mzuri kati ya Wizara, Halmashauri, Wadau na mwitikio chanya wa jamii katika kupokea huduma hii ya usawazishaji wa vikope.

## HUDUMA ZA TIBA

71. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kusimamia upatikanaji wa huduma za tiba nchini zinazotolewa kupitia vituo vya kutolea huduma za Afya vya Serikali, binafsi na mashirika ya dini. Katika kutekeleza jukumu hili, Wizara inasimamia na kuratibu utoaji wa huduma katika Vituo vya kutolea huduma za afya katika ngazi zote, Upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi, Huduma za uchunguzi wa Magonjwa, Huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala, Upatikanaji wa damu salama na uimarishaji wa huduma za kibingwa na kibingwa bobezi.

### Usimamizi wa Vituo vya Kutolea Huduma za Afya

72. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, vituo vya kutolea huduma za afya viliongezeka na kufikia vituo 8,458 ikilinganishwa na vituo 8,446 mwaka 2019. Kati ya vituo hivyo, Serikali inamiliki vituo 6,225 sawa na asilimia 73.6; mashirika ya dini yanamiliki vituo 917 sawa na asilimia 10.8 na Mashirika mengine na watu binafsi wanamiliki vituo 1,316 sawa na asilimia 15.6. Kati ya vituo 8,458 viliwyopo nchini, hospitali ni 369, vituo vya afya ni 926 na zahanati 7,163. Aidha, jumla ya wagonjwa 4,500,785 walihudumiwa katika Hospitali ya Taifa, Hospitali Maalum, Taasisi, Hospitali za Rufaa za Kanda na za Mikoa ikilinganishwa na wagonjwa 5,305,891 walihudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2019/2020, ikiwa ni upungufu

wa asilimia 15.2. Kati ya wagonjwa 4,500,785 wagonjwa wa nje (OPD) walikuwa 3,999,618 na wagonjwa wa ndani (IPD) walikuwa 501,167. Kupungua kwa idadi ya wagonjwa waliohudumiwa, ambako kumeonekana katika ngazi ya rufaa (Mkoa, Kanda, Maalum na Taifa) kunatokana na kuimarike kwa huduma ngazi ya msingi na kutekelezwa kwa kampeni za usafi, kufanya mazoezi na ulaji bora wa vyakula ili kuimarisha kinga ya miili ya wananchi na kujikinga na maradhi; jambo ambalo ni shabaha kuu ya Wizara ya Afya hapa nchini. Naomba nitumie nafasi hii kuwahimiza wananchi kuendelea kufuata maelekezo ya wataalam wa Afya ili kujikinga na milipuko ya maradhi kwani Kinga ni Bora kuliko Tiba.

#### **Upatikanaji wa Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi**

73. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia Bohari ya Dawa hununua, hutunza na husambaza zaidi ya aina 2,545 za dawa, vifaa tiba na vitendanishi. Kati ya hizo, dawa aina 1,865 ni dawa zilizo katika utaratibu wa Miradi Msonge na aina ya dawa 680 ni dawa muhimu. Dawa za aina 312 ndizo zimeainishwa kuwa ni dawa muhimu na za kipaumbele cha Wizara kwa lengo la kuhakikisha kuwa zinapatikana nyakati zote katika Bohari ya Dawa (MSD). Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, hali ya upatikanaji wa aina hizo 312 katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini ilifika asilimia 75.6 na katika maghala ya MSD ni asilimia 21 ikilinganishwa na hali ya upatikanaji wa dawa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2019/20, ambapo upatikanaji ulikuwa ni asilimia 80 katika vituo vya kutolea huduma na asilimia 56 katika maghala ya Bohari ya Dawa. Aidha, kwa upande wa upatikanaji wa *tracer medicine* aina 30 ulikuwa umefikia asilimia 87 katika ngazi ya vituo vya kutolea huduma za afya, ikilinganishwa na asilimia 92.5 mwaka 2019/20. Mchanganuo wa upatikanaji wa dawa kimko umeainishwa katika **Kiambatisho Na.4.**

74. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha kuanzia Julai 2020 hadi Aprili 2021, Wizara ilipokea kiasi cha **Shilingi bilioni 151.38** kutoka Hazina. Mchanganuo wa fedha hizo umeainishwa

katika **Kiambatisho Na. 5.** Aidha, Wizara imepokea kiasi cha **Shilingi bilioni 111.23** kutoka kwa wadau wa chanjo kwa ajili ya ununuzi wa chanjo, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi na hivyo kuwezesha kuongezeka kwa upatikanaji wa dawa katika vituo vya kutolea huduma za afya.

75. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021,Wizara kupitia Bohari ya Dawa imepokea na kusambaza dawa za miradi msonge zenye thamani ya **Shilingi bilioni 510.9** ikillinganishwa na dawa za Miradi Msonge zenye thamani ya **Shilingi bilioni 361.5** zilizosambazwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2019/20. Dawa hizo zilisambazwa moja kwa moja hadi vituo vya kutolea huduma za afya 6,931 kwa gharama ya **Shilingi bilioni 19.9**.

76. ***Mheshimiwa Spika***, katika juhudzi za kuimarishe upatikanaji wa bidhaa za afya kwa gharama nafuu iklwemo dawa, vifaa tiba na vitendanishi Serikali imekuwa mstari wa mbele kuitikia mwito wa kuhakikisha Tanzania inakuwa nchi ya viwanda na kuendelea kuimarika katika uchumi wa kat. Wizara kwa kushirikiana na Kituo cha Uwekezaji Tanzania, Taasisi husika pamoja na wadau, imepitia na kurekebisha baadhi ya miongozo na taratibu ambazo zilikuwa ni kikwazo kwa wawekezaji wanapotaka kuwekeza katika eneo la viwanda vya dawa na vifaa tiba. Hali hii imeboresha mazingira ya uwekezaji, ambapo katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, idadi ya viwanda vinavyozalisha/kutengeneza dawa vimeongezeka na kufikia 11 kutoka viwanda tisa (9) kwa mwaka 2019/20. Pamoja na viwanda hivyo 11 ambavyo vinafanya uzalishaji wa dawa, kuna viwanda 16 ambavyo viro katika hatua mbalimbali za ujenzi, na katika siku za hivi karibuni vingi vitaanza uzalishaji. Aidha, viwanda vya ndani vya vifaa tiba vimeongezeka hadi kufikia viwanda 15 kutoka viwanda sita (6) vilivyokuwepo mwaka 2019/20.

77. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na Wizara kutengeneza mazingira wezeshi kwa wawekezaji wakubwa na wa kat. wanaotaka kuwekeza katika viwanda vya dawa na Vifaa Tiba, pia iliandaa miongozo na kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji wadogo wenye nia ya kuanzisha viwanda vidogo

hasa katika kipindi hicho wakati dunia ikiwa imekabiliwa na janga la COVID-19 huku uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi ukiwa na changamoto. Uboreshaji wa Mazingira haya kwa wawekezaji wadogo uliwezesha kuanzishwa kwa viwanda vidogo 181 vya vipukusi (sanitizers), viwanda vidogo 77 vya barakoa na viwanda 23 vya majitiba (infusions) ambavyo pia vinapatikana katika baadhi ya hospitali za rufaa za kanda na mikoa.

78. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kubuni mikakati ya kuboresha upatikanaji wa bidhaa za Afya, ikiwemo kuhakikisha Hospitali zote za Rufaa za Mikoa nchini zinaanza kuzalisha bidhaa za afya hasa majitiba. Maelekezo haya yameanza kutekelezwa na tayari Hospitali zimewasilisha maandiko (Business Plan) yao, ambapo Hospitali sita (6) zinatarajiwा kuanza uzalishaji kabla ya kufikia mwisho wa mwaka 2021. Hospitali hizo ni pamoja na Hospitali za Rufaa za Mikoa ya; Dodoma, Kigoma (Maweni), Kagera (Bukoba), Kilimanjaro (Mawenzi), Rukwa (Sumbawanga) na Mwanza (Sekou Toure). Wizara imejikita katika kufanya ufuatiliaji wa karibu wa utekelezaji wa mipango hiyo ili kuhakikisha kuwa hadi ifikapo mwishoni mwa mwaka 2022 Hospitali zote za Rufaa za Mikoa ziwe zimeanza uzalishaji.

79. ***Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na changamoto ya upatikanaji wa dawa katika maghala ya MSD, Wizara illiagiza MSD iangalie namna ya kuanzisha viwanda vya dawa hapa nchini, kufufua viwanda vya Serikali ambavyo vilikuwa vimesimama uzalishaji au kuingia katika ubia na sekta binafsi. Katika kutekeleza agizo hilo, Bohari ya Dawa (MSD) ilianzisha kiwanda cha kuzalisha mipira ya mikono (Gloves Manufacturing Plant) kilichopo Idofi Wilaya ya Makambako mkoani Njombe. Uanzishwaji wa kiwanda hiki umedhamiria kukabiliana na ukosefu mkubwa wa bidhaa hii uliopo duniani ambapo kwa sasa bei ya kununulia *Surgical Gloves* imefika wastani wa **Shilingi 19,500** kutoka wastani wa **Shilingi 5,300** kwa kifungashio cha idadi ya 50 iliyokuwa mwaka 2019. Aidha, uanzishwaji wa kiwanda hiki utakidhi mahitaji ya ndani ya nchi na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Pamoja

na kupunguza uhitaji, ujenzi wa kiwanda hiki utaipunguzia Serikali mzigo wa fedha za kigeni wastani wa **Dola za Kimarekani milioni 7.9** zinazotumika sasa kwa mwaka kwa ununuzi wa bidhaa hizi kutoka kwa wazalishaji wengine nje ya nchi au washitiri.

80. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Bohari ya Dawa ipo katika hatua za mwisho za kuanzisha viwanda vya kuzalisha vidonge (Tablets), vimiminika (syrup) na *Capsules* katika eneo la viwanda, Idoifi, Wilayani Makambako Mkoani Njombe ili kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa hizi kwa wakati na kwa bei nafuu. Kiwanda hiki kitakuwa na uwezo wa kuzalisha vidonge 24,000,000 kwa siku, sawa na mahitaji ya nchi kwa miezi mitatu. Hivyo, kiwanda hiki kina uwezo wa kutosheleza mahitaji ya vituo vya afya nchini kwa kuzalisha siku nne tu. Kutokana na uwezo huu mkubwa, kiwanda kitazalisha bidhaa hizo kwa ajili ya mahitaji ya nchi za Jumuia ya Afrika Mashariki, SADC na nchi nyingine duniani zitakazohitaji bidhaa hizo. Kiwanda hiki kitaiwezesha Serikali kuokoa fedha za kigeni zaidi ya **Dola za Kimarekani milioni 15.6 (Shilingi bilioni 36)** kwa mwaka ambazo zinatumika kwa sasa kununua bidhaa hizo.

81. ***Mheshimiwa Spika***, Bohari ya Dawa pia imeanzisha kiwanda cha kuzalisha Barakoa katika Makao Makuu yake yaliyopo Dar es Salaam. Kiwanda hiki kinaendeshwa na wataalam wa Bohari ya Dawa na kina uwezo wa kuzalisha Barakoa 48,000 kwa siku. Kutokana na uhitaji wa bidhaa hii nchini, Serikali imeongeza mtambo mwingine ambao utakuwa una uwezo wa kuzalisha Barakoa 100,000 kwa siku na hivyo kufanya jumla ya Barakoa 148,000 kuzalishwa kwa siku. Aidha, Bohari ya Dawa inatarajia kuanzisha kiwanda cha kutengeneza Krimu (Ointment & Cream) katika eneo lake la Makao Makuu. Kiwanda hiki kitakuwa na uwezo wa kuzalisha Krimu kulingana na mahitaji maalum ya madaktari na yaliyothibitishwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa (TMDA). Uamuzi huu utaipunguzia Serikali mzigo mkubwa wa fedha za kigeni wastani wa **Dola za Kimarekani milioni 5.7 (Shilingi bilioni 13)**.

82. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeingia ubia wa hisa asilimia 70 katika kiwanda cha dawa cha Keko na asilimia 30 ni hisa za kampuni ya Diocare Ltd. Kiwanda kimeanza kazi mwezi Oktoba 2020 chini ya Menejimenti ya Wizara kikiwa na uwezo wa kuzalisha dawa za aina 10 za vidonge. Katika kuongeza ufanisi wa kiwanda ili kiweze kuzalisha bidhaa za aina nyingi na kwa kiwango cha juu, Wizara imeamua kufunga mtambo mpya ambao utakiwezesha kiwanda kufungasha dawa zote zinazozalishwa kwa wakati na kuzalisha dawa aina 13 zaidi. Aidha, Wizara imedhamiria kukifungua kiwanda cha Tanzania Pharmaceuticals Industries Ltd (TPI) ambacho kina mitambo yenye teknolojia ya kisasa zaidi kilichoko mkoani Arusha. Kwa sasa, Wizara inafanya upembuzi yakinifu ili kubaini aina ya bidhaa zinazoweza kuzalishwa katika kiwanda hicho.

83. ***Mheshimiwa Spika***, ongezeko hili la Viwanda vya ndani vya dawa, litapunguza kwa kiwango kikubwa gharama ambayo Serikali imekuwa ikiingia kwa kuagiza dawa hizi kutoka kwa wazalishaji wa nje, lakini pia itapunguza sana matumizi makubwa ya fedha za kigeni ambazo zimekuwa zikitumika kuagiza dawa hizi nje ya nchi. Vilevile, viwanda hivi vitawezesha upatikanaji wa ajira kwa vijana na wataalam wengi wa kitanzania.**Hivyo, Wizara inawasihi watu binafsi, taasisi na mashirika ya fedha, ambayo yana uwezo wa kuwekeza katika eneo hili la viwanda, waje wafanye hivyo, kwa kuwa mazingira ya uwekezaji katika eneo hili kwa sasa ni rafiki na wezeshi.**

84. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha huduma bora za dawa zinasogezwa karibu zaidi na wananchi, Wizara imefanya marekebisho ya Mwongozo wa Matibabu na orodha ya kitaifa ya dawa kwa kuruhusu dawa zinazohitajika kwa huduma za ubingwa kutolewa na Hospitali za Rufaa za Mikoa pamoja na kuruhusu baadhi ya dawa kutolewa katika ngazi ya vituo vya Afya ambapo hapo awali zilikuwa hazitolewi katika ngazi hiyo. Mabadiliko haya yamesaidia kusogezwa huduma za dawa karibu zaidi na Wananchi. Hatua zilizochukuliwa katika kuhakikisha udhibiti wa huduma za dawa ni pamoja na kuboresha mfumo wa maoteo ya dawa, vifaa na vifaa tiba na vitendanishi kuanzia ngazi ya vituo vya

kutolea huduma za Afya. Lengo ikiwa ni kuhakikisha vituo vinawasilisha mahitaji halisi ya dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi ili kuepusha changamoto ya dawa kuchina na matumizi mabaya ya fedha za umma.

85. ***Mheshimiwa Spika***, zoezi la maoteo limekuwa likifanyika kila mwaka na kuiwezesha vituo kuwasilisha mahitaji halisi ya dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kwa miradi misonge na dawa muhimu. Aidha, Wizara imefanya mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya, namna ya kuandaa maoteo ya dawa kwa mwaka kwa kupitia utaratibu wa ngazi ya chini kuandaa maoteo na kuwasilisha ngazi ya juu (Bottom up quantification). Lengo ni kuiwezesha Bohari ya Dawa kuandaa mpango wa manunuvi unaoendana na mahitaji halisi ya dawa katika vituo vya kutolea huduma.

86. ***Mheshimiwa Spika***, katika suala zima la upatikanaji wa bidhaa za afya zikiwemo dawa, vifaa tiba na vitendanishi, ipo changamoto ya nidhamu isiyofaa katika kutunza na kutumia kwa uadilifu bidhaa hizo kuanzia kwenye ngazi ya kununua, kusafirisha, kupokelewa kwenye taasisi husika na hatimaye kutolewa kwenda hatua ya kumfikia mgonjwa. Hivyo, ikumbukwe kuwa, suala la upatikanaji wa bidhaa za afya siyo ajenda ya kuongeza bajeti tu bali pia ni uadilifu wa kusimamia mfumo mzima wa bidhaa hizi kuanzia kupatikana kwake hadi kumfikia mtumiaji. Wizara kupitia Taasisi zake imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuinua uadilifu kwenye myororo wa ugavi wa bidhaa hizi kwa kuwachukulia hatua mbalimbali wote wanaobainika kuhujumu kwa namna moja au nyingine kupitia wizi au rushwa. Hadi sasa watumishi wawili (2) wa MSD wameshushwa vyeo na mshahara na wengine 24 wamefukuzwa kazi.

87. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa ngazi ya vituo vya kutolea huduma za afya kwa kipindi cha Januari - Machi 2021, Wizara kwa kushirikiana na wadau wake ilifanya tathmini katika halmashauri zote 184 na hospitali za rufaa za mikoa kuhusu ufanisi wa mfumo wa ugavi wa dawa na kubaini kuwa karibia kila kituo kinakabiliwa na tuhuma za usimamizi duni

wa mnyororo wa ugavi jambo linalosababisha kiasi cha kutosha cha bidhaa za afya kutowafikia wagonjwa hususan dawa, vifaa tiba na vitendanishi. Muhtasari wa matokeo ya tathmini hiyo ni kama inavyoonesha katika **Kiambatisho Na. 6**. Aidha, sambamba na tathmini hiyo, yapo matukio mbalimbali ya ubadhirifu na wizi wa bidhaa hizi ambayo yameripotiwa na hatua kuchukuliwa. Wizara kwa kushirikiana na wadau wake wote na vyombo mbalimbali ipo kwenye hatua ya kuhakikisha tathmini hiyo inafanyiwa kazi sambamba na kuboresha mifumo mbalimbali ya udhibiti wa rasilimali hizi zinapopita kwenye hatua zake zote za mnyororo wa ugavi. **Sambamba na hatua mbalimbali za kisheria na Kitaalam, Wizara itatoa elimu kwa wadau wote wakiwemo Waheshimiwa Madiwani na Wabunge ili wanaposimamia utekelezaji wa majukumu yao wajue nini wahoji kwenye taarifa za utekelezaji wanazoletewa.**

88. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha matunzo yenye tija ya bidhaa za afya, Wizara kwakushirikiana na Bohari ya Dawa, imepitia miongozo ya uendeshaji wa Bohari ya Dawa ili kuangalia namna bora ya kuboresha na kusimamia sheria, kanuni na miongozo husika kwa ajili ya kuwezesha kulinda mtaji wa MSD unaotokana na mauzo ya bidhaa hizo za wateja wake ambao ni vituo vya kutolea huduma nchini. Mojawapo ya miongozo hiyo ni utaratibu wa *Cash and Carryambapo*, vituo vya kutolea huduma za Afya vitapewa huduma baada ya malipo kufanyika Bohari ya Dawa. Kufanikiwa kwa utaratibu huu kutasaidia kupunguza deni la MSD inalovidai vituo vya kutolea huduma na hivyo kutunisha mfuko wa MSD. Utaratibu huu utawezesha kukua kwa mtaji wa MSD na kudhibiti ongezeko la madeni.

89. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha hali ya upatikanaji wa bidhaa za dawa inaendelea kuimariika katika kipindi cha mwaka 2021/22, Wizara itatekeleza yafuatayo:-  
(i) Kuimariisha mifumo ya kielektroniki kwa ajili ya usimamizi wa bidhaa za afya sambamba na kuimariisha mfumo wa uthibitisho wa stakabadhi ya mgonjwa kupokea bidhaa husika ya afya hususan dawa na vifaa tiba (rejea **Kiambatisho Na. 7**);

- (ii) Kuingia mikataba ya ufanisi wa mfumo wa ugavi kati ya Wizara na Wakuu wa Taasisi kuititia wizara zinazoshirikiana katika eneo hili;
- (iii) Kujenga uelewa wa pamoja na viongozi wote wanaohusika na kusimamia utekelezaji wa eneo la afya likiwemo hili la bidhaa za afya hususan Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Waheshimiwa Wabunge na Madiwani wote pamoja na vyombo vyote vinavyohusika na ukaguzi wa matumizi sahihi ya rasilimali za umma;
- (iv) Kuendelea kuweka mazingira rafiki ya uanzishwaji wa viwanda vyta dawa na vifaa tiba;
- (v) Kuongeza ajira ya wataalam wa dawa katika ngazi zote za kutolea huduma za dawa ikiwa ni pamoja na Bohari ya Dawa ili iweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi;
- (vi) Kuwasiliana na vyuo vikuu kuhusu aina ya wataalam wanaohitajika kudahiliwa ili kukidhi mahitaji ya wataalam wa uzalishaji wa bidhaa za afya; na
- (vii) Kuimarisha mahusiano na Vyuo Vikuu na NIMR kwa ajili ya kuendelea kufanya tafiti mbalimbali zitakazoimarisha upatikanaji wa bidhaa za afya kwa kutumia rasilimali zilizoko kwa ufanisi zaidi.

#### **Huduma za Uchunguzi wa Magonjwa**

90. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuboresha huduma za uchunguzi wa magonjwa ili kuboresha huduma ya matibabu kwa wananchi. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara imefanya mambo mengi ikiwemo utekelezaji wa Mradi wa *Harmonization and standardization of Laboratory Equipment* na utekelezaji wa programu ya kuboresha huduma za Maabara nchini, yaani *Laboratory Accreditation program*.

91. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeteketeza mradi wa *Harmonization and Standardization of Laboratory Equipment*

kwa kusimika mashine za Maabara katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Maabara za Hospitali za Wilaya na Vituo vya Afya. Aidha, ununuzi wa vitendanishi vitakavyotumika na mashine hizo umefanyika na kusambazwa kwenye vituo 220 vya kutolea huduma za afya nchini.

92. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Wizara imetekeleza programu ya kuboresha huduma za Maabara nchini, yaani *Laboratory Accreditation Program*, ambapo hadi kufikia Machi 2021 jumla ya maabara 14 (sawa na asilimia 83.4) kati ya 17 zilipata ithibati ya Kimataifa ya ISO 15189:2012 na kufikisha jumla ya maabara za Afya 26 zilizo na ithibati (ISO Accreditation). Aidha, jumla ya Maabara 28 kati ya 29 (sawa na asilimia 96.6) zimekidhi viwango vya Kimataifa vya ISO 15189 na zimeshatuma maombi ya ukaguzi wa Kimataifa (application for assessment) na ziko tayari kukaguliwa. Maabara zote ambazo hazikufikia malengo zinaendelea na kukamilisha mipango kazi yao.

93. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kusimamia na kuratibu uboreshaji wa huduma ya uchunguzi wa magonjwa kwa kutumia radiolojia. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Wizara iliwezesha upatikanaji wa *X-ray*mpya za Kisasa (digital X-ray) katika vituo vya kutolea huduma 53 (Hospitali za Rufaa za Mikoa 18, Hospitali za Wilaya 33 na Vituo vya Afya viwili). Hadi kufikia Machi 2021, *Digital X-ray* 49 kati ya 53 zimesimikwa na kuanza kutoa huduma. *Digital X-ray* nne zimefika katika hospitali za; Musoma RRH, Kisarawe, Namtumbo na Mwambani, ambazo zinakamilisha ukarabati wa chumba ili mashine hizo zisimikwe. Aidha, mashine maalum za kufanya uchunguzi na matibabu kwa njia ya mionzi (Fluoroscopy) tatu (3) zimesimikwa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa za Mwananyamala na Amana (Dar es Salaam) na Maweni (Kigoma) na zimeanza kutoa huduma. Pia CT scan mbili (2) zimesimikwa katika Hospitali za rufaa za Mikoa za Sekou Toure (Mwanza) na Mwananyamala (Dar es Salaam). Vilevile, usimikwaji wa *Magnetic Resonance Imaging* (MRI) unaendelea katika hospitali ya Kanda ya Bugando na Vifaa vingine vya uchunguzi hasa vya radiolojia vimenunuliwa (ultrasound, digital X-ray na Fluoroscopy) vyenye thamani ya

**Shilingi bilioni 6.5** ambavyo vitasambazwa katika hospitali tisa (9) za Rufaa za Mikoa na Wilaya.

### **Kuimarisha Huduma za Tiba Asili na TibaMbadala**

94. ***Mheshimiwa Spika***, huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala ni mionganoni mwa huduma za afya zinazosimamiwa na Serikali kupitia Sera ya Afya (2017). Katika kuboresha huduma hizi Wizara imekuwa inatoa elimu kwa waganga wa Tiba Asili na Tiba Mbadala kupitia vyombo vya habari. Uhamasishaji huo unahusu usajili wa waganga wa Tiba Asili na Tiba Mbadala, usajili wa vituo na usajili wa dawa za asili. Aidha, Wizara kupitia Vyuo vya Afya na Sayansi Shirikishi vya Muhimbili, Mirembe na Morogoro vimetoea mafunzo ya kuijendeleza kwa waganga wa Tiba Asili, ambapo katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya waganga wa Tiba Asili 86 wamepata mafunzo hayo.

95. ***Mheshimiwa Spika***, katika kupambana na ugonjwa wa COVID-19, jumla ya dawa za asili 23 ziliidhinishwa baada ya kupimwa na Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Dawa hizo ni pamoja na; NIMR-CAF, Mashimo Hero Corona, Lishe, Dawa ya Asili, COVOTANXA, BINGWA, MGENDELANDAA, NUT, TULSI PLUS, NIGELLA SATIRAT, NIGELLA PLUS, COVIDOL, PM Jilambe Lemon Juice, Shentembo Herbal, Shekilindii, ÓLARAMI, Tinga Tinga, BAYCARO, Mtihaki Mtemi, Planet ++, BUPIJI, UZIMA HERBAL DROPS na Dawa Asili. Pamoja na matumizi ya dawa za kunywa, dawa za kujifukiza zilitumika kwa wingi baada ya uhamasishaji mkubwa na utengenezaji wa mafuta tete (Essential oils) na Taasisi za SIDO-DSM, Vingunguti, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Dodoma. Serikali itaendelea kuimarisha huduma ya Tiba Asili na Tiba Mbadala kwa kuendelea kuwaelimisha wataalam wa dawa za Tiba Asili kuona umuhimu wa kusajili dawa zao. Aidha, kupitia Taasisi ya NIMR, Serikali inaendelea kuzifanyia utafiti wa kina wa kitaalam dawa mbalimbali zilizotumika katika kipindi cha mapambano dhidi ya COVID-19.

96. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha hali ya upatikanaji wa huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala katika kipindi cha mwaka 2021/22, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi za Utafiti

NIMR na ITM-MUHAS, Vyuo Vikuu vya UDSM, SUA na MUHAS, itaendelea na tafiti mbalimbali, kutengeneza *formula* za dawa zitokanazo na mimeadawa, na kuandaa mfumo wa Utengenezaji dawa hizo kiviwanda. Aidha, Wizara itaendelea kuratibu mafunzo ya kuijendeleza kwa waganga wa Tiba Asili kupitia Vyuo vya Afya na Sayansi Shirikishi vya Muhimbili, Mirembe na Morogoro. Vilevile, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa waganga wa Tiba Asili na Tiba Mbadala na wananchi kwa ujumla kuhusu Tiba Asili na matumizi sahihi ya dawa za asili.

### **Upatikanaji wa Damu Salama**

97. *Mheshimiwa Spika*, Wizara, kupitia Mpango wa Taifa wa Damu Salama ilipanga kukusanya chupa za Damu Salama 375,000 ili kukidhi mahitaji ya Damu Salama nchini katika kipindi cha mwaka 2020/21. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya chupa 250,933 zilikusanywa na kusambazwa sawa na asilimia 67 ya lengo. Makusanyo hayo ni sawa na ongezeko la chupa 5,879 sawa na asilimia 2.4 ikilinganishwa na idadi ya chupa za damu salama 245,054 katika kipindi cha mwaka 2019/20. Damu zote zilizokusanywa zilipimwa makundi ya damu, pamoja na magonjwa makuu manne ambayo ni UKIMWI (HIV), Homa ya ini B na C (HBV &HCV) na Kaswende (Syphilis). Katika kipindi cha 2021/22, Wizara imepanga kukusanya jumla ya chupa za damu 375,000.

98. *Mheshimiwa Spika*, pamoja na juhudu kubwa zinazofanywa na Wizara katika ukusanyaji wa chupa za damu salama na kuhakikisha damu salama inapatikana kwa wahitaji wa damu katika vituo vyote vya afya vya kutolea huduma za Afya, Wizara pia inazalisha aina tatu za mazao ya damu ambazo ni Chembe Sahani (Platelates) ambazo husaidia damu kuganda hasa kwa wagonjwa wa saratani, chembe nyekundu (Packed red cells) ambazo husaidia kubeba oksijeni mwilini na Plasma (Fresh frozen Plasma) ambazo husaidia kugandisha damu isiendelee kutoka hasa kwa mama wajawazito wanaotokwa damu wakati wa uzazi/kujifungua. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya chembe sahani 2,480, chembe nyekundu 50,925, na plasma zilizogandishwa 8,863 zilizalishwa kwa ajili ya kuweza kutumika

katika hospitali mbalimbali. Mazao haya ya damu huzalishwa kuititia kanda saba za Mpango wa Taifa wa damu salama. Aidha, Mpango unaendelea na mkakati wa kuongeza uzalishaji wa mazao hayo kuititia hospitali zote za Rufaa za Mikoa kwa kuwajengea uwezo na kuwanunulia vifaa kwa ajili ya uzalishaji. **Nitoe wito kwa wananchi kuendelea kujitolea kuchangia damu ili kuwezesha upatikanaji wa damu nchini ili kukidhi mahitaji ya damu nchini.** Wizara itaendelea kutekeleza kampeni mbalimbali za kuchangia damu ikiwa na lengo la kuendelea kuhamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi zaidi.

#### **Uimarishaji wa Huduma za Matibabu ya Kibingwa na Ubingwa Bobezi Nchini**

99. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarishe huduma za matibabu ya Kibingwa na Ubingwa Bobezi nchini, Wizara inasimamia na kuratibu Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) Upanga na Mloganzila, na Hospitali Maalum tano (5) ambazo ni za Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe na Hospitali ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto. Aidha, Wizara inasimamia utendaji wa Hospitali za Kanda za Rufaa tano (5) ambazo ni Hospitali ya Rufaa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini-Mbeya, Hospitali ya Benjamini Mkapa-Dodoma, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa-Bugando na Hospitali ya Rufaa ya Kanda Kaskazini (KCMC) na Hospitali ya CCBRT.

100. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Wizara kuititia hospitali ngazi ya Taifa, Maalum hadi Kanda imehudumia jumla ya wagonjwa 1,686,395. Kati ya hao, wagonjwa wa nje (OPD) walikuwa 1,452,136 na wagonjwa wa kulazwa (IPD) walikuwa 234,259 ikilinganishwa na wagonjwa 2,013,788 waliohudumiwa katika kipindi cha mwaka 2019/20, ikiwa ni upungufu wa asilimia 16. Mchanganuo wa wagonjwa waliohudumiwa umeainishwa katika **KiambatishoNa. 8.** Wagonjwa waliohudumiwa kwa misamaha walikuwa 241,836 kwa gharama ya **Shilingi 30,072,385,262** kama ilivyoainishwa katika **KiambatishoNa. 9.**

## Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)

101. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali ya Taifa Muhimbili ni Hospitali ya Rufaa inayotoa huduma za tiba za kibingwa na bobezi. Huduma zinazotolewa ni pamoja na upandikizaji wa figo, uwekaji wa vifaa vya usikivu na tiba ya radiolojia. Hospitali ina jumla ya vitanda 1,530 ikiwa ni pamoja na vitanda 77 vya wagonjwa mahututi (ICU), vitanda 42 kwa ajili ya huduma za kuchuja damu (renal dialysis), vitanda 35 kwa ajili ya wagonjwa wenyewe mahitaji maalum (HDU) na vitanda 22 kwa ajili ya wagonjwa wa saratani. Kwa sasa idadi ya vitanda inakidhi nafasi na majengo yaliyopo. Aidha, hospitali ina jumla ya wafanyakazi 2,968 ambapo 2,737 wapo katika ajira ya Serikali na watumishi 231 ni wa mkataba ambao wanalipwa na hospitali.

102. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya wagonjwa 323,544 walihudumiwa ikilinganishwa na wagonjwa 367,913 mwaka 2019/20. Kati ya wagonjwa 323,544 wagonjwa wa nje (OPD) walikuwa 282,751 na wagonjwa wa kulazwa (IPD) walikuwa 40,793. Hospitali imeimarisha upatikanaji wa dawa za aina zote zinazohitajika ambapo hadi Machi 2021 upatikanaji wa dawa umefikia asilimia 94 ikilinganishwa na asilimia 95 mwaka 2019/20. Vilevile, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya wagonjwa 73,044 walipata msamaha wa matibabu yenye gharama ya **Shilingi 9,149,349,105**.

103. ***Mheshimiwa Spika***, huduma za kibingwa Bobezi zinazotolewa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ni pamoja na huduma za upandikizaji wa figo ambazo zilianza kutolewa Novemba 2017, ambapo katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya wagonjwa sita (6) walipata huduma na hivyo kufanya jumla ya wagonjwa 62 waliopatiwa huduma hiyo tangu kuanzishwa. Jumla ya **Shilingi 1,860,000,000** zilitumika ikiwa ni wastani wa **Shilingi milioni 30** kwa mgonjwa mmoja. Gharama za kupandikiza figo kwa mgonjwa mmoja nje ya nchi (India) ni wastani wa **Shilingi 120,000,000**. Hivyo wagonjwa 62 waliopata huduma hii katika Hospitali ya Taifa Muhimbili wangegeharimu jumla ya **Shilingi 7,440,000,000**. Kwa

kuanzisha huduma hiyo hapa nchini Serikali imeokoa jumla ya **Shilingi 5,580,000,000**.

104. ***Mheshimiwa Spika***, Huduma ya kupandikiza vifaa vya usikivu (Cochlear Implants) ilianza kutolewa mwezi Juni, 2017, ambapo mpaka kufikia Mwezi Machi, 2021 jumla ya watoto 34 wamepatiwa huduma hii. Kabla ya hapo huduma hii ilikuwa inapatikana nje ya nchi kwa gharama ya **Shilingi milioni 100** kwa mtoto mmoja. Katika Hospitali ya Taifa Muhimbili gharama ni **Shilingi milioni 40** kwa hiyo jumla ya **Shilingi 2,040,000,000** zimeokolewa kwa kutibu watoto 34.

105. ***Mheshimiwa Spika***, Huduma za tiba ya radiolojia (Interventional Radiology) zinahusisha matumizi ya X-ray, MRI, CT-scan na *Ultrasound* katika kutibu magonjwa moja kwa moja au kutoa sampuli kwa ajili ya uchunguzi. Huduma za tiba ya radiolojia zinawezesha upasualji wa shingo na kichwa, kuondoa uvimbe kwenye sehemu ya kinywa, uso na shingoni, kuweka mirija kwenye figo, kuzibua mirija ya nyongo iliyoziwa, kuzibua mirija ya uzazi na kuondoa usaha ndani ya tumbo. Jumla ya wagonjwa 1,064 wamepata huduma hii toka kuanzishwa kwake mwezi Novemba 2018 ambapo katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya wagonjwa 123 walipata huduma hii, ikilinganishwa na wagonjwa 231 mwaka 2019/20. Gharama ya kumpeleka mgonjwa mmoja nje ya nchi ni **Shilingi milioni 98** wakati katika Hospitali ya Taifa Muhimbili ni **Shilingi milioni 8** tu. Gharama za kutibiwa nje ya nchi ni kubwa kwani mgonjwa hutibiwa kwa awamu na analazimika kwenda si chini ya mara nne (4). Hivyo jumla ya **Shilingi bilioni 95.76** zimeweza kuokolewa. Hospitali itaendelea kutoa huduma hii na kuwafikia wagonjwa wengi zaidi, kwani kwa sasa wataalam wazalendo wameshapata ujuzi wa kutoa huduma hii.

106. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali imeendelea kufanya uchunguzi na tiba ya ugonjwa wa homa ya ini (Hepatitis B) ambapo katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya wagonjwa 2,963 wamechunguzwa na kati yao 250 wanaendelea na dawa, ikilinganishwa na wagonjwa 2,640 waliochunguzwa mwaka 2019/20.

107. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ikishirikiana na wadau wa afya *Novo Nodisk Haemophilia Foundation* (NNHF) imezindua rasmi mradi utakaosaidia upatikanaji wa haraka na ukaribu wa huduma, vipimo na matibabu kwa wagonjwa wenye matatizo ya kuvuja damu (*Haemophilia*) na Selimundu. Uzinduzi huo ulifanyika mnamo tarehe 18 Novemba, 2020. Mradi huu wenye thamani ya **Shilingi bilioni 1.5** ni wa miaka mitatu ambao utatekelezwa kwa ushirikiano kati ya nchi ya Tanzania na Kenya. Miongoni mwa malengo ya mradi huu ni kuboresha huduma za afya kwa wagonjwa wenye matatizo ya damu kupitia ujenzi wa kliniki maalum za magonjwa ya *hemophilia* na selimundu katika vituo 16 nchini Tanzania katika kipindi cha miaka mitatu. Mradi huu pia unalenga kuwajengea uwezo wataalam wa afya nchini kuhusu njia bora za utoaji wa huduma ya afya kwa wagonjwa wa *hemophilia* na selimundu nchini. Hadi kufikla mwezi Machi 2021 hospitali imepokea msaada wa dawa zenye thamani ya **Shilingi bilioni 5** kwa ajili ya kuwahudumia wagonjwa wa *hemophilia*.

108. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali ya Taifa Muhimbili inatibu watoto wote wenye saratani ambapo hupelekwa hospitali ya Ocean Road pale wanapohitaji mionzi na baadaye kurudishwa Muhimbili. Vilevile, inatibu saratani ya damu kwa watu wazima. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, hospitali imewahudumia wagonjwa 2,101 wanaohitaji tiba ya *Chemotherapy* ambao wanakuja kupewa dawa na kurudi nyumbani (chemoday care). Hospitali kwa kushirikiana na Shirika Lisilo la Kiserikali linaloitwa Tumaini la Maisha (TLM) huwafanya wagonjwa uchunguzi na kupewa dawa na chakula bure. Aidha, Hospitali na TLM wamejenga hosteli yenye vitanda 22 kwa ajili ya watoto wanaohitaji matibabu ya muda mrefu. Vilevile, Hospitali kwa kushirikiana na TLM wanatoa huduma za dawa, vipimo na ushauri wa kitaalam kwa watoto wenye saratani katika hospitali nyingine nchini zikiwemo hospitali za Kanda Bugando, Mbeya na KCMC, pamoja na Mnazi Mmoja Zanzibar.

109. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali imeendelea kutoa huduma za mkoba (outreach services) ambapo kupitia Idara ya

Macho pamoja na Idara ya *Urology*, katika Hospital ya Mnazi Mmoja Zanzibar na Turiani mkoani Morogoro. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, wagonjwa 188 walionwa na madaktari bingwa na kati yao wagonjwa 55 walifanyiwa upasuaji.

110. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali ya Taifa Muhimbili imeendelea kutoa huduma za kibingwa kwa wagonjwa kutoka nchi ya nchi. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Hospitali imetua huduma za kibingwa kwa wagonjwa 198 kutoka nchi za Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi, Malawi, Zambia, Misri, Ujerumani, Norway, Swedeni na Marekani.

111. ***Mheshimiwa Spika***, katikakuwajengea uwezo wataalam, Hospitali imeendelea kudhamini mafunzo ya shahada za uzamili kwa wataalam wake. Jumla ya wataalam 90 wapo masomoni katika vyuo mbalimbali nchini na nje ya nchi, ambapo kati yao 29 wapo nje ya nchi. Nchi walizoenda kwa ajili ya mafunzo ni pamoja na Cuba, Misri, Afrika Kusini, India, Uganda, Uturuki, Ethiopia, Australia, China na Kenya. Hospitali hutumia **Shilingi milioni 450** kwa mwaka kugharamia mafunzo ya wataalam hawa.

112. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha huduma za dharura, Hospitali imeweza kufanya upanuzi mkubwa wa huduma za dharura kwa watoto ikiwemo uwekaji wa mfumo wa kufua hewa ya *oxygen*. Uboreshaji wa kitengo hiki cha dharura kwa watoto unaifanya hospitali kuwa mionganini mwa hospitali zillizoimarika katika eneo hilo ukanda wa Afrika Mashariki. Watoto 20 wanaweza kuhudumiwa kwa wakati mmoja. Aidha, Hospitali inaendelea na ujenzi wa Wodi za kulaza wagonjwa binafsi (IPPM Building) ili kukidhi mahitaji ya wagonjwa wanaohitaji huduma binafsi. Aidha, Hospitali imenunua mashine mpya za CT-Scan na MRI, mashine za kisasa za *X-ray*, mashine za usingizi (anaesthesia machines), ventilators, mashine za utasishaji, mashine za maabara, mashine za kufua umeme, lifti pamoja na mashine na taa za upasuaji.

113. ***Mheshimiwa Spika***, Ili kuimarisha utoaji wa huduma katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Hospitali itatekeleza yafuatayo:-

- (i) Kupandikiza uloto (bone marrow transplant) kwa wagonjwa wenyewe kansa ya damu;
- (ii) Kuanza kutoa huduma za upandikizaji wa mimba (IVF);
- (iii) Kuendelea na ujenzi wa jengo la wagonjwa binafsi (private wards) lenye vitanda 200; na
- (iv) Kuendeleza huduma zote za kibingwa kama vile upasuaji kwa kutumia tundu dogo, upasuaji wa kichwa, shingo na koo.

114. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara itaendelea kuiwezesha Hospitali ya Taifa Muhimbili kuwa kituo bora katika utoaji wa huduma za ubingwa na ubingwa bobesi, mafunzo na utafiti wa tiba. Aidha, hospitali itaendelea kutoa tiba za ubingwa na ubingwa bobesi kwa wagonjwa waliopewa rufaa kutoka ndani na nje ya nchi.

### **Hospitali ya Mloganzila**

115. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali ya Mloganzila ni sehemu ya Hospitali ya Taifa Muhimbili, ambayo pamoja na utoaji wa huduma za tiba za kibingwa na kibobezi katika fani za tiba, upasuaji, tiba shirikishi, uuguzi, pia hutumika kama hospitali ya utafiti na mafunzo. Hospitali ina jumla ya watumishi 652 ikijumuisha madaktari bingwa 53, madaktari wa kawaida 40 wauguzi 306 na wataalam kutoka kada zingine 253. Vilevile, Hospitali ina jumla ya vitanda 608 vikiwemo vitanda 31 vya wagonjwa mahututi (ICU) na vyumba 13 vya upasuaji.

116. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya wagonjwa 82,339 walihudumiwa katika Hospitali ya Mloganzila ikilinganishwa na wagonjwa 84,298 mwaka 2019/20 ambapo wagonjwa 7,644 walikuwa ni wakulazwa (IPD) na wagonjwa 74,695 walikuwa ni wa nje (OPD). Hali ya upatikanaji wa dawa za aina zote umeendelea

kuimashwa ambapo hadi kufikia Machi 2021, upatikanaji wa dawa umefikia asilimia 90.6 ikilinganishwa na asilimia 85 iliyokuwepo mwaka 2019/20. Vilevile, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya wagonjwa 73,044 walipata msamaha wa matibabu yenyeye gharama ya **Shilingi 9,149,349,105**.

117. *Mheshimiwa Spika*, baadhi ya huduma za kibingwa zilizotolewa katika Hospitali ya Mloganzila katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021 ni pamoja na huduma za kuondoa mawe kwenye mfumo wa mkojo kwa kutumia mawimbi mshtuko (Extra Corporeal Shock Wave Lithotripsy) ambapo jumla ya wagonjwa 120 wameshapatiwa huduma. Gharama ya huduma hii hapa nchini ni **Shilingi 500,000** ambapo huduma hiyo hugharimu wastani wa **Shilingi 10,000,000** nje ya nchi. Huduma ya upimaji wa utendaji kazi wa kibofu cha mkojo (Uroflow Dynamic), ambapo jumla ya wagonjwa 152 wamepewa huduma. Huduma nyingine zilizotolewa ni pamoja na: huduma za kibingwa za mifumo ya mishipa ya fahamu na ubongo na uti wa mgongo (wagonjwa 85); Huduma za kibingwa za magonjwa ya ndani (wagonjwa 30,236); Huduma za kibingwa za upasuaji (wagonjwa 2,810); Huduma za kibingwa za magonjwa ya dharura (wagonjwa 5,081); Huduma za kibingwa za macho (wagonjwa 1,034); na Huduma za kibingwa za magonjwa ya ngozi (wagonjwa 1,212).

118. *Mheshimiwa Spika*, Hospitali ya Mloganzila ipo katika maandalizi ya kuanza kutoa huduma za kupandikiza uloto (Stem Cells Transplant) kwa kushirikiana na Hospitali ya Taifa Muhimbili – Upanga. Hadi kufikia Machi 2021, matengenezo ya vyumba 6 ambavyo ni maalum kwa ajili ya kulazwa wagonjwa hawa imekamilika kwa asilimia 98.

119. *Mheshimiwa Spika*, katika kuhakikisha Hospitali inakuwa na wataalam wa kutosha na wenye ujuzi, imekuwa ikitoa udhamini wa masomo ya muda mrefu na mfupi kwa wataalam wake kwenda kuijiendezeza katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa kutumia fedha zake za makusanyo ya ndani, lakini pia wengine wamekuwa

wakipata udhamini kupitia Wizara. Hadi kufikia Machi 2021 wataalam zaidi ya 52 wapo katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

120. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma, Hospitali imeboresha mfumo wa kuhifadhi kumbukumbu za matibabu (HIS) ambao umeimarisha ukusanyaji wa mapato, usimamizi wa vitendanishi na kutunza taarifa za wagonjwa. Pia Hospitali imejenga eneo maalum kwa ajili ya kupumzika ndugu wa wagonjwa wanaposubiri kuingia wodini. Jengo hili lina uwezo wa kuhudumia watu 150. Katika kuboresha utoaji huduma, Hospitali imefanya matengenezo kinga ya vifaa tiba mbalimbali ikijumuisha *MRI, CT-Scan, Mammography, Laparoscope, Dental X-Ray, Fluoroscopy* pamoja na vifaa vya maabara ambapo hadi sasa jumla ya **Shilingi 590,295,566** zimetumika.

121. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Hospitali imehudumia jumla ya wagongwa 15 kutoka nchi za China, India, Kenya na Visiwa vya Comoro (Medical Tourism). Wagonjwa hao walipatiwa huduma mbalimbali zikiwemo huduma za kibingwa za mifumo ya mishipa ya fahamu, ubongo na uti wa mgongo, huduma za kibingwa za magonjwa ya dharura, macho, mifupa pamoja na magonjwa ya mapafu ikiwemo *pneumonia*.

122. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Hospitali itaananza kituo cha upandikizaji wa viungo mbalimbali (transplant centre) ikijumuisha uloto (Bone Marrow), figo (kidney), ini (liver), macho (corneal) pamoja na upandikizaji wa ujauzito (In Vitro Fertilization - IVF). Uanzishwaji wa kituo hiki utafanya huduma hizi ziwe endelevu.

### **Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)**

123. ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi ya Mifupa Muhimbili inatoa huduma za Kibingwa na ubingwa bobezi za matibabu ya Mifupa, Ubongo, Mgongo na Mishipa ya Fahamu. Taasisi hii inajumla ya vitanda 362 vikiwemo 18 vya wagonjwa mahututi (ICU) na vitanda 16 vya *High Dependent Unit* (HDU). Taasisi

ina Wafanyakazi 784, wakiwemo Madaktari 102 na Wauguzi 474.

124. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Taasisi ya MOI imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kutoa huduma ya matibabu ya mifupa, upasuaji mishipa ya fahamu na ubongo. Katika kipindi hicho, Taasisi imetoa matibabu kwa wagonjwa 155,843 kati ya hao wagonjwa wa nje (OPD) ni 149,633 na wagonjwa wa kulazwa (IPD) ni 6,210 ikilinganishwa na wagonjwa 196,210 waliopatiwa huduma mwaka 2019/20. Vilevile, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya wagonjwa 13,086 walipata msamaha wa matibabu yenyе għarama ya **Shilingi 409,500,169**.

125. **Mheshimiwa Spika**, Taasisi iliendelea kutoa huduma za kibingwa za upasuaji ambapo katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, wagonjwa 5,212 waliopatiwa huduma za upasuaji wa kubadilisha nyonga 102, goti 87, upasuaji wa goti kwa kutumia matundu 216, upasuaji wa mfupa wa kiuno 58, upasuaji wa mfupa wa paja (femur) 459, upasuaji wa uti wa mgongo 203, ubongo 123, upasuaji mifupa mingine 1,924, watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi 314, na wagonjwa wa dharura 1,726. Hii ikilinganishwa na wagonjwa 5,549 waliopatiwa huduma za upasuaji mwaka 2019/20,

126. **Mheshimiwa Spika**, Taasisi imeendelea kuboresha upatikanaji wa dawa na vitendanishi, ambapo katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, hali ya upatikanaji wa dawa imefikia asilimia 85 ikilinganishwa na asilimia 79 mwaka 2019/20. Vilevile, Taasisi imekamilisha ununuzi na usimikajji wa mtambo mpya na wa kisasa (Angiosuite) kwa ajili ya kutibu matatizo ya mishipa ya damu kwenye ubongo uliogħarimu jumla ya **Shilingi 7,915,788,606** ambazo zimetolewa na Serikali. Hadi kufikia Machi 2021, jumla ya wagonjwa 17 wamepatiwa huduma kupitia mtambo huo. Kufungwa kwa mtambo huu kutaiwezesha Taasisi kuweza kuwahudumia wagonjwa wa ndani na nje ya nchi kwani hadi sasa Tanzania ni nchi pekee yenyе mtambo huu katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na katika SADC ni Tanzania na Afrika Kusini.

127. ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi iliendelea kutoa huduma za mkoba katika sehemu mbalimbali hapa nchini. Taasisi imeendelea kupeleka huduma za kibingwa za Upasuaji Mifupa katika Hospitali ya Nyangao mkoani Lindi ambapo kila baada ya wiki mbili Daktari Bingwa Mmoja huenda Hospitalini hapo. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Taasisi imefanya upasuaji wa kibingwa kwa wagonjwa 248. Vilevile, Taasisi iliendesha Kambi ya upasuaji katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa - Bugando. Kambi hiyo ililenga kuboresha upatikanaji wa huduma za kibingwa za upasuaji wa nyonga na magoti kwa wakazi wa mkoa wa kanda ya ziwa ambapo wagonjwa 300 walionwa na kupatiwa matibabu na wagonjwa 5 walifanyiwa upasuaji wa kibingwa.

128. ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi imeanzisha huduma za kibingwa za upasuaji wa Ubongo na Mgongo katika Hospitali ya Rufaa ya KCMC kwa lengo la kuwapunguzia adha wakazi wa Mikoa ya Kaskazini kufuata huduma hiyo Dar es Salaam, ambapo wagonjwa 23 walionwa na madaktari bingwa na upasuaji wa kibingwa ulifanyika kwa mgonjwa mmoja (1) kutolewa uvimbe kwenye ubongo, wagonjwa watatu (3) walitolewa uvimbe wa damu kwenye ubongo, wagonjwa wanne (4) walifanyiwa upasuaji wa uti wa mgongo na mtoto mmoja (1) alifanyiwa upasuaji wa kutoa maji kichwani. Aidha, Taasisi ilipeleka madaktari bingwa katika Hospitali ya rufaa Mbeya ambapo wagonjwa watatu (3) walifanyiwa upasuaji wa kibingwa wa mifupa wa kiuno na nyonga. Pia, Taasisi imeingia ushirikiano na Hospitali ya Ndanda, Mkoa wa Mtwara kwa ajili ya kutoa Huduma za kibingwa za Mifupa ambazo zimeanza mwezi Aprili 2021. Kwa sasa yupo Daktari Bingwa wa mifupa ambaye anaendelea kutoa huduma hizo.

129. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Taasisi itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kuendelea kuboresha upatikanaji wa huduma mpya za kibingwa za mifupa, Ubongo, Mgongo na Misipa ya Fahamu ili kuondoa kabisa rufaa za kupeleka wagonjwa nje ya nchi;

- (ii) Kuendelea kusogeza huduma hizo kwa wananchi kupitia huduma ya mkoba ili kuwapunguzia wananchi waliopo mkoani gharama za kumsafirisha mgonjwa na mtu wa kumhudumia kuja MOI kupata huduma za kibingwa;
- (iii) Taasisi itaimarisha upatikanaji wa huduma za dawa na vitendanishi ili kuboresha huduma kwa wananchi na kupunguza usumbufu kwa wagonjwa;
- (iv) Taasisi ya Mifupa MOI itaendelea na upanuzi wa huduma awamu ya nne ambapo imeanza hatua za awali za ujenzi wa kituo cha tiba tengemano (Rehabilitation Center) - Mbweni Mpiji;
- (v) Kuungeza eneo la kutolea huduma kwa wagonjwa wa nje (OPD); na
- (vi) Kuanza kutoa huduma za mkoba katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara Kwangwa.

#### **Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI)**

130. ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) ni hospitali maalum inayotoa tiba ya magonjwa ya moyo, mafunzo na utafiti. Taasisi ina jumla ya watumishi wa kudumu 312, wa kujitolea 22 na wa mkataba 15, ikiwa na upungufu wa watumishi 55 ukilinganisha na mahitaji halisi ambayo ni watumishi 367 kulingana na lkama. Kati ya watumishi hao madaktari bingwa bobesi wapo 19, madaktari bingwa wapo 23, madaktari wa kawaida wapo 17, wauguzi 155, wafamasia na maabara 29, utawala na ufundi 69. Aidha, kwa sasa Taasisi ina jumla ya vitanda 150, lakini mahitaji halisi ni vitanda 400.

131. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete imehudumia jumla ya wagonjwa 74,712 ambapo kati yao, wagonjwa wa nje walikuwa 72,080 na wagonjwa wa kulazwa walikuwa 2,632 ikilinganishwa na wagonjwa 77,200 waliohudumiwa katika kipindi cha mwaka 2019/20. Idadi hii inahusisha pia wagonjwa kutoka nchi za DRC, Comoro, Uganda, Malawi, Rwanda,

Burundi na Afrika Kusini. Vilevile, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya wagonjwa 1,580 walipata msamaha wa matibabu yenye gharama ya **Shilingi 476,940,233**.

132. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Taasisi ilifanya upasuaji wa moyo kwa kufungua kifua kwa wagonjwa 251. Aidha, jumla ya wagonjwa 950 walipatiwa matibabu kwa kufanyiwa upasuaji wa moyo kupitia tundu dogo kwa kutumia mtambo maalum *Catheterization Laboratory*, ikiwa ni ongezeko la asilimia 3.8, ukilinganisha na wagonjwa 915 waliofanyiwa upasuaji katika kipindi cha mwaka 2019/20. Vilevile, wagonjwa wengine 81 ambao ni watu wazima wenye matatizo ya mishipa ya damu walifanyiwa upasuaji kwa njia ya teknolojia ya kisasa (Vascular Surgery). Upasuaji huu wa kibingwa bobezi ullifanyiwa na wataalam wa ndani.

133. ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi imeweza kupunguza rufaa ya wagonjwa kwenda kutibiwa nje kwa asilimia 80. Hii imetokana na kuboresha miundombinu na kuongezeka kwa wataalam bingwa bobezi kwenye huduma za uchunguzi na matibabu ya magonjwa ya moyo. Gharama za upasuaji kwa mgonjwa mmoja katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete ni **Shilingi milioni 35** wakati mgonjwa akipelekwa nje ya nchi ni **Shilingi milioni 80**. Hivyo Serikali ingetumia zaidi ya **Shilingi bilioni 161** kwa ajili ya kupeleka wagonjwa wenye matatizo ya moyo nje ya nchi. Kwa wagonjwa hawa kutibiwa hapa nchini, Taasisi imeokoa kiasi cha **Shilingi bilioni 91** lakini pia kwa matibabu haya kufanyika hapa nchini, wataalam wengi zaidi wa ndani ya nchi wamepata ujuzi huu.

134. ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi imeendelea kuboresha huduma za famasia kwa kutoa dawa muhimu za matibabu ya moyo kutoka asilimia 80 kwa mwaka 2019/20 hadi asilimia 96 kwa mwaka 2020/21. Vilevile, huduma ya famasia inapatikana kwa saa 24. Taasisi imeendelea kuboresha huduma za famasia kwa kuhakikisha dawa muhimu zinapatikana kwa kuongeza bajeti ya fedha za ununuzi ya

dawa kutoka kiasi cha **Shilingi bilioni 2.2** mwaka 2019/20 hadi **Shilingi bilioni 4.4** kwa mwaka 2020/21.

135. **Mheshimiwa Spika**, Taasisi imeweza kuwa chachu ya ongezeko la Madaktari bingwa nchini kupitia mafunzo ya *fellowship program* mbalimbali kama *Fellowship in Adult and Pediatric Cardiology* ambapo wataalam mabingwa wanaopatikana katika program hizi wamesaidia kupunguza uhaba wa wataalam mabingwa katika maeneo mbalimbali ya huduma za kitabibu nchini. Aidha, Taasisi ina mpango wa kuanzisha programu mpya ya mafunzo ya kibingwa ya udaktari wa upasuaji wa moyo (Cardiothoracic & Vascular Surgery), udaktari bingwa wa dawa za usingizi wa moyo (Cardiothoracic Anaesthesia), udaktari bingwa wa wagonjwa mahututi na wanaohitaji uangalizi maalum (Critical Care), na Udaktari bingwa wa *Perfusion* (Cardiothoracic Perfusion).

136. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imefanikiwa kununua mtambo wa kisasa wa pili wa *Cathlab na Carto 3* wenye thamani ya **Shilingi bilioni 4.6** Mtambo huu utatumika kwa kufanya uchunguzi na kutibu magonjwa ya moyo na hivyo kuifanya Tanzania kuwa kinara katika nchi za Afrika Mashariki na Kati kwa kuongeza uwezo wa kufanya upasuaji kwa wagonjwa wa moyo bila ya kufungua kifua. Vilevile, mtambo huo, utapunguza rufaa za matibabu nje ya nchi na inategemewa kuwa raia wengi wa nchi zinazotuzunguka watakuja kufuata huduma hii hapa Tanzania (Medical Tourism).

137. **Mheshimiwa Spika**, katika kutoa huduma bora hususan kwa watoto wenye matatizo ya moyo, Taasisi imefanya jitihada za kuongeza wodi kwa ajili ya watoto yenye jumla ya vitanda 33 pamoja na vitanda nane (8) vya chumba cha uangalizi maalum. Kuongezeka kwa wodi hii kumeboresha huduma bora kwa watoto wenye matatizo ya moyo, Ukarabati wa jengo hili umetumia **Shilingi bilioni 1.3**.

138. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarishta utoaji wa huduma kwa kipindi cha mwaka 2021/22, Taasisi itatekeleza yafuatayo:-

- (i) Kuboresha huduma za famasia kwa kutoa dawa muhimu za matibabu ya moyo kwa asilimia 97;
- (ii) Kuongeza chumba cha wagonjwa mahututi (Coronary Care Unit - CCU) chenye vitanda nane (8);
- (iii) Kujenga chumba cha upasuaji maalum kwa ajili ya watoto;
- (iv) Kujenga jengo litakalotumika kwa ajili ya huduma za vipimo vya Radiolojia; na
- (v) Kufadhili mafunzo kwa watumishi ili kuwaongezea ujuzi na hivyo kuweza kutimiza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

### **Hospitali ya Benjamin Mkapa**

139. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali ya Benjamin Mkapa inatoa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi katika kufanya uchunguzi na matibabu katika magonjwa ya moyo, Saratani, figo, Magonjwa ya macho, Mifupa, Magonjwa ya njia ya mfumo wa mkojo, Magonjwa ya kinamama na uzazi, magonjwa ya watoto, Magonjwa ya upasuaji, matibabu kwa kutumia teknolojia ya *endoscopy* kama vile upasuaji wa kutumia matundu madogo (*laparoscopic surgery*), kuelimisha jamii, mafunzo na tafiti kwa kutumia sayansi na teknolojia ya kisasa. Aidha, Hospitali ina vitanda 325 (Hospital ward beds) ikiwa ni pamoja na vitanda sita (6) vya ICU na tisa (9) vya uchunguzi na uzibuaji wa mishipa ya moyo (*Coronary Care Unit - CCU*). Hospitali ina watumishi 467 kati ya 741 wanaohitajika ambapo kati ya madaktari waliopo, madaktari bingwa waliopo ni 45. Hali ya upatikanaji wa dawa muhimu na maalum katika Hospitali umefikia asilimia 90 na katika kuongeza upatikanaji wa dawa Hospitali tayari imetenga duka la dawa la nje (community pharmacy) ili kuhakikisha dawa zinapatikana kwa urahisi.

140. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Hospitali imeendelea kutoa huduma ambapo jumla ya wagonjwa 129,963 walihudumiwa, sawa na

ongezeko la asilimia 28 ikilinganishwa na wagonjwa 101,899 kwa kipindi cha mwaka 2019/20. Kati ya hao, wagonjwa 123,356 walikuwa wa nje (OPD) na wagonjwa waliolazwa (IPD) 6,607. Wagonjwa wanaopatiwa huduma katika hospitali wameendelea kuongezeka kutokana na uboreshwaji wa huduma zinazotolewa na uwepo wa vifaa vyatia kisasa na wataalam wenyewe ujuzi. Vilevile, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya wagonjwa 1,636 walipata msamaha wa matibabu yenyewe gharama ya **Shilingi 265,957,800**.

141. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali imeendelea kutoa huduma za kibingwa ambapo katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, huduma za kibingwa zilizotolewa ni pamoja na magonjwa ya Upasuaji (4,412); huduma za kibingwa za magonjwa ya ndani (11,113); huduma za kibingwa za Magonjwa ya kina mama na uzazi (6,137); huduma za kibingwa za Magonjwa ya watoto (4,437); huduma za kibingwa za Magonjwa ya mfumo wa chakula (1,786); huduma za kibingwa za Meno (2,172); huduma za kibingwa za magonjwa ya Mifupa (9,334); huduma za kibingwa za mifumo ya mishipa ya fahamu na ubongo (Neuro Surgery) (2,903); huduma za kibingwa za magonjwa ya: Macho (3,590); Moyo (7,881); dharura (38,763); figo (898); mfumo wa mkojo (5,068); yanayoathiri mfumo wa damu (694); na masikio, pua na koo (4,555).

142. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Hospitali ilifanikiwa kufanya upasuaji wa kibingwa kwa wagonjwa 3,255 ikiwemo upasuaji wa Mifupa (418), Upasuaji wa Ubongo na mishipa ya fahamu (200) na Upasuaji wa mfumo wa mkojo (459), *General surgery* (897), *Obstetric and Gynecology* (631), Masikio, pua na koo (379), Macho (262) na Meno (9). Jumla ya wagonjwa 27 walipata huduma ya matibabu ya mawe kwenye mfumo wa mkojo (Extracorporeal Shockwave Lithotripsy) na hivyo kufikia idadi ya wagonjwa 45 waliohudumiwa toka huduma hii ilipoanza kutolewa mwezi Machi 2020. Vilevile, Hospitali ina vyumba sita (6) vyatia upasuaji kwa kutumia matundu madogo (Laparoscopic Surgery) ambapo katika kipindi husika, jumla

ya wagonjwa 506 walipatiwa huduma hiyo. Aidha, hospitali ilitoa huduma za mkoba katika mkoa wa Singida na Jiji la Dodoma ambapo jumla ya wagonjwa 3,013 walihudumiwa katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021.

143. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya wagonjwa wanne (4) walipandikizwa figo (Kidney Transplant) kwa kutumia Madaktari wazawa na kufikisha jumla ya wagonjwa sita (6) waliopandikizwa. Hadi Machi 2021, jumla ya wagonjwa 17 wamenufaika na huduma hii kwa gharama ya **Shilingi milioni 425** ikiwa ni wastani wa **Shilingi milioni 25** kwa mgonjwa mmoja tangu huduma hiyo ilipoanzishwa mwezi Machi 2018. Kama wagonjwa hawa wangepelekwa nje ya nchi, inakadiriwa kuwa Serikali ingetumia **Shilingi bilioni 2.04**, sawa na wastani wa **Shilingi milioni 120** kwa mgonjwa mmoja. Vilevile, huduma za uchujaji damu (Haemodialysis) kwa wagonjwa ambao figo zao hazifanyi kazi vizuri zimeendelea kuimarika ambapo jumla ya wagonjwa 117 walipata huduma hii.

144. ***Mheshimiwa Spika***, huduma za ubingwa wa juu wa kutumia maabara maalum (CathLab) ya kuchunguza na kutibu magonjwa ya moyo nazo zilianzishwa mwezi Februari, 2019 ambapo kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya wagonjwa 161 walinufaika na huduma hii, hivyo kufanya idadi ya wagonjwa 340 waliohudumiwa toka ilipoanza kutolewa. Gharama ya huduma hii kwa wastani ni **Shilingi milioni 4.5** hadi **milioni 6** hapa nchini ikilinganishwa na zaidi ya milioni 30 hadi 40 nje ya nchi, hivyo uanzishwaji wa huduma hii imeokoa fedha za Serikali. Aidha, Hospitali kwa kuimarisha huduma za kibingwa za uchunguzi wa magonjwa ya moyo inatoa huduma mbali mbali zikiwemo *Holter ECG*, *Stress ECG/Exercise* (Treadmill test) na *Ambulatory BP Monitoring*. Jumla ya wagonjwa 229 walihudumiwa, kati ya hao, wagonjwa 159 ni wagonjwa wa *stress ECG*, Wagonjwa 27 ni wagonjwa wa *Holter ECG* na wagonjwa 43 walifanyiwa *Ambulatory BP Monitoring*.

145. ***Mheshimiwa Spika***, mnamo mwezi Machi 2020, Taasisi ilianzisha chumba cha uangalizi maalum kwa ajili ya

uchunguzi na uzibuaji wa mishipa ya moyo. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya wagonjwa 188walihudumiwa. Aidha, Hospitali imeanza kutoa huduma kwa watoto wachanga na watoto waliozaliwa kabla ya muda wao (Njiti). Huduma hiyo, imeanza kutolewa mwezi Mei, 2020 ambapo jumla ya watoto 80 wamehudumiwa.

146. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali imeanza kutoa huduma za uchunguzi wa saratani (Histopathology) tangu mwezi Oktoba, 2020 ambapo jumla ya wagonjwa 803 walihudumiwa hadi sasa. Uboreshaji wa huduma hii umegharimu kiasi cha **Shilingi 1,113,470,078**. Aidha, Hospitali imeendelea kuboresha huduma za kibingwa kwa kuanza kutoa matibabu ya Saratani kwa kutumia dawa (Chemotherapy) na wagonjwa 568 walihudumiwa kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2021.

147. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, hospitali ilifanya uboreshaji wa miundombini katika maeneo mbalimbali kama vile ukarabati katika maeneo ya utoaji huduma eneo la upandikizaji uloto uliogharimu kiasi cha **Shilingi 76,562,082.43** ambapo hospitali pia imenunua vifaa vyta kisasa vya maabara ya meno bandia na huduma nyingine kwa garama ya kiasi cha **Shilingi 700,137,680.42**. Aidha, Hospitali ilinunua vifaa vyta kisasa vya kutolea huduma za mazoezi kwa garama ya **Shilingi 399,026,600**.

148. ***Mheshimiwa Spika***, katika bajeti ya mwaka 2021/22 Hospitali imepanga kufanya yafuatayo:-

- (i) Kuendelea kuboresha utoaji wa huduma ya upandikizaji wa figo (Kidney transplant complex);
- (ii) Kuanza kutoa huduma ya matibabu ya saratani kwa kutumia mionzi;
- (iii) Kuanza kutoa huduma za Matibabu ya mfumo wa hewa (Pulmonology Service);

(iv) Kuanza kutoa huduma za matibabu ya upasuaji wa moyo (Open Heart Surgery); na

(v) Kuanza uzalishaji wa Gesi tiba (Medical Oxygen) kwa ajili kuboresha upatikanaji wa huduma.

### Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI)

149. ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI) inatoa huduma za kibingwa na bobezi katika uchunguzi na tiba ya aina zote za Saratani. Taasisi ina jumla ya watumishi 307ukilinganisha na mahitaji ya Ikama ya watumishi 439. Kati ya watumishi 307, madaktari bingwa 49, Wafamasia 14, Wataalam wa Mionzi ni 29, *Radiographer* ni 13 Waugazi ni 87, Wataalam wa Maabara ni 13 na kada nyinginezo. Katika kukabiliana na upungufu huu wa wataalam Taasisi imeweka watumishi 70 wa kujitolea ili kuimarisha utoaji huduma.

150. ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ili kuhakikisha kila mgonjwa anayekuja kupata huduma katika Taasisi anapata huduma bora za kiuchunguzi, kimatibabu na dawa. Katika kuhakikisha hilo linafanikiwa, Taasisi imekuwa ikitenga zaidi ya **Shilingi bilioni 1** kila mwaka kutoka kwenye mapato ya ndani kwa ajili ya kununua dawa za saratani, lakini pia Serikali imekuwa ikiendelea kuongeza fedha za dawa za saratani na vitendanishi katika Taasisi kutoka **Shilingi milioni 790** mwaka 2015/16 hadi **Shilingi bilioni 6** mwaka 2020/21. Vilevile, Taasisi imefungua duka la dawa la jamii katika eneo la hospitali ili kuongeza upatikanaji wa dawa, ambapo hadi kufikia Machi 2021 upatikanaji wa dawa kwa wagonjwa wa saratani ulikuwa ni asilimia 98, ukilinganisha na upatikanaji wa asilimia 4 mwaka 2015 na asilimia 96 mwaka 2019/20.

151. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya wagonjwa 59,266 walipatiwa huduma sawa na asilimia 80 ya lengo kwa mwaka. Kati ya hao, wagonjwa wa nje (OPD) walikuwa 55,020 na wagonjwa wa kulazwa walikuwa 4,246 ikilinganishwa na jumla ya wagonjwa

58,208 waliohudumiwa katika kipindi cha mwaka 2019/20. Kati ya wagonjwa waliohudumiwa katika kipindi hiki, wagonjwa 22,713 walipatiwa huduma za tiba mionzi, wagonjwa 15,904 walipatiwa huduma ya tiba kemia na wagonjwa 20,649 walipata tiba ya kemia na mionzi. Vilevile, Taasisi imekuwa ikitoa huduma kwa wagonjwa wa misamaha, ambapo katika kipindi cha kuanzia Julai 2020 hadi Machi 2021 wagonjwa wa misamaha 8,227 walihudumiwa kwa gharama ya **Shilingi 8,418,508,741.**

152. ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi imeendelea kuboresha huduma za kibingwa za uchunguzi na tiba kwa wagonjwa kwa kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma ambapo katika kipindi cha 2020/21, Serikali imenunua na kusimika mashine za kisasa za *digital X-ray, Ultrasound* na uwepo wa mashine za kuchunguza matokeo ya tiba saratani kwa njia ya damu (tumor markers). Vilevile, Taasisi ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha ujenzi na ununuzi wa mashine za kisasa za teknolojia ya *nuclear medicine* ya kupima saratani mwilini *Positron Emission Tomography – Computerized Tomography scan (PET/CT - Scan)*. Kiasi cha **Shilingi 15,500,000,000** kimeshatolewa na Serikali kwa ajili ya mradi kwa ajili ya ujenzi wa jengo, kununua na kusimika mashine za PET/CT - Scan na *Cyclotron* ambapo Mradi huu unategemewa kukamilika Oktoba 2021

153. ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali kwenye uboreshaji wa miundombinu na vifaa tiba umesababisha kupungua kwa wagonjwa wanaopatiwa rufaa ya matibabu nje ya nchi kutoka wagonjwa 42 mwaka 2017/18 hadi wagonjwa wawili (2) katika kipindi cha Julai 2020 hadi sasa. Aidha, kuimarishwa kwa utoaji wa huduma hasa tiba mionzi, kumeendelea kuwavutia wagonjwa kutoka nje ya nchi kuja nchini kwa ajili ya tiba. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya wagonjwa wapya 83 kutoka nje ya nchi walipatiwa huduma za uchunguzi na tiba ya saratani.

154. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, uchunguzi wa saratani kwa huduma za mkoba

ulifanyika katika mikoa ya Dar es Salaam, Simiyu, na Tanga. Jumla ya wanawake 30,573 walifanyiwa uchunguzi wa saratani ya matiti na saratani ya mlango wa kizazi; na wanaume 3,660 walifanyiwa uchunguzi wa saratani ya tezi dume. Pia, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Taasisi ilioa mafunzo ya namna bora ya utoaji huduma za uchunguzi na tiba ya saratani (mentorship) kwa watumishi 61 wa afya wanaota huduma za saratani nchini kutoka Hospitali za Mikoa ya Mwanza, Dar es Salaam, Simiyu, na Tanga na hivyo kufanya kuwepo na jumla ya watumishi 511 wenye ujuzi huu. Hii, inasaidia katika uchunguzi wa awali wa saratani na hivyo kupunguza wagonjwa wanaofika katika Taasisi wakiwa katika hatua za juu za ugonjwa. Aidha, katika kipindi hicho Taasisi iliendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu namna ya kujikinga na saratani kwa njia mbalimbali vikiwemo vipindi 96 vya TV, redio vipindi 119 na katika magazeti machapisho 96. Utoaji wa elimu kwa umma ulitekelezwa kwa asilimia 102 ya lengo.

155. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Taasisi kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili iliendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi 72 wa Shahada ya Kwanza ya Tiba ya Mionzi (Bachelor of Science in Radiation Therapy Technology), wanafunzi 18 wa Shahada ya Uzamili ya Onkolojia (Masters of Medicine in Clinical Oncology) na wanafunzi 9 wa Shahada ya Uzamili ya Uuguzi katika Onkolojia (Masters of Science in Nursing Oncology). Mafunzo haya yameongeza uwepo wa wataalam wa huduma za saratani hapa nchini hadi kufikia 30 kutoka 13 waliokuwepo mwaka 2015/16. Vilevile, Taasisi imeandaa mpango wa mafunzo nje ya nchi ambapo zaidi ya wataalam 30 watapatiwa mafunzo ya ubingwa bobez.

156. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, ukusanyaji takwimu sahihi za ugonjwa wa saratani uliendelea kutekelezwa nchini kwa kusimamiwa na Wizara. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya takwimu za wagonjwa 7,290 zimeengizwa katika mfumo na hivyo kufanya takwimu za wagonjwa kuwa 31,811.

157. ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi imepanga kutekeleza yafuatayo ili kuboresha huduma za ubingwa bobezi katika tiba ya saratani:-

- (i) Kupanua wodi za wagonjwa binafsi ili kuwa na uwezo wa vitanda 75 na kununua mashine ya tiba mionzi na MRI kuitia mkopo wa NHIF wa **Shilingi bilioni 3.835**;
- (ii) Kuanzisha kiwanda cha kutengeneza *IV fluids*;
- (iii) Kujenga kituo cha ubingwa bobezi cha huduma ya saratani katika eneo la Mloganzila na pia kujenga hospital ya saratani Mbeya ZRH – kwa utaratibu wa PPP;
- (iv) Kuanzisha huduma za mionzi ya ndani kwa saratani ya kooni katika njia ya chakula (esophageal cancer); na
- (v) Kuanzisha huduma za upasuaji wa saratani kwa ushirikiano na hospitali ya Amana, Temeke na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

#### **Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe**

158. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe inatoa huduma za matibabu kwa wagonjwa wa afya ya akili raia na wahalifu pamoja na huduma kwa wagonjwa wa magonjwa mengine ya kimwili, wakiwemo waathirika wa dawa za kulevyva. Aidha, Hospitali inatoa huduma za ushauri wa kitaalam kwa Mahakama mbalimbali hapa nchini, mafunzo ya vitendo na ya kawaida kwa wanafunzi wa kada za afya na zinginezo. Hospitali ina jumla ya vitanda 590 na ina jumla ya watumishi 278, wakiwemo Madaktari 37 na Wauguzi 94.

159. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya wagonjwa 109,110 walipata huduma za matibabu ikilinganishwa na wagonjwa 105,320 katika kipindi kama hicho mwaka 2019/20. Kati ya hao, wagonjwa wa akili wa nje (OPD) walikuwa 81,833 na wagonjwa wa akili wa kulazwa (IPD) walikuwa 27,277. Jumla ya wagonjwa 2,709

walisajiliwa ili kupatiwa matibabu na wagonjwa 318 wapo kwenye matibabu na elimu ya athari juu ya matumizi ya madawa ya kulevyo. Aidha, Hospitali ilitoa huduma za kibingwa kwa wagonjwa 1,384 ambazo ni huduma za Mifumo ya fahamu (Neuro-Cognitive and Dementia) kwa wagonjwa 674, huduma Watoto na Vijana (Child and Adolescent Psychiatry) kwa wagonjwa 465 na huduma za Saikologia kwa wagonjwa 245. Vilevile, Hospitali imeendelea kutoa huduma za kibingwa katika fani za forensiki (Forensic Psychiatry), ambapo wagonjwa wapatao 160 walifanyiwa uchunguzi na kuandikiwa taarifa za kisheria. Hospitali pia, imeendelea kuimarisha hali ya upatikanaji wa dawa na kufikia asilimia 93, ikilinganishwa na asilimia 92 Mwaka 2019/20.

160. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali imeendelea kutoa fursa za mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi wake kwa kudhamini watumishi katika fani mbalimbali za kibingwa katika vyuo vya ndani na nje ya nchi, ambapo jumla ya Madaktari 9 na muuguzi mmoja (1) wanaendelea na masomo katika ngazi mbalimbali za masomo. Hospitali imeendelea na jitihada endelevu za ukarabati na ujenzi wa majengo ya utoaji huduma katika maeneo mbalimbali ambapo ukarabati mkubwa umefanyika katika chumba cha upasuaji mdogo, chumba cha mitambo ya *X-ray*, jengo la maabara pamoja na chumba kwa ajili ya duka la dawa la jamii.

161. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2021/22, hospitali imepanga kutekeleza yafuatayo:-

- (i) Kukamilisha Mpango Mkakati wa miaka mitano kuanzia mwaka 2021 hadi 2026;
- (ii) Kuongeza huduma za Kibingwa;
- (iii) Kuimarisha na kuboresha huduma za afya za akili pamoja na tafiti kuhusu vyanzo vya athari ya afya ya akili nchini;
- (iv) Kuanzisha huduma tembezi saidizi za tiba (clinical supportive services outreach);

(v) Kuimarisha na kuboresha utoaji wa mafunzo kwa vitendo kwa watarajali wa mafunzo ya afya ya akili; na

(vi) Kuendelea kuimarisha huduma za utengemao kwa wagonjwa wa afya ya akili.

### **Hospitali ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto**

162. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali ya Kibong'oto ni Hospitali Maalum katika ngazi ya Taifa inayoshughulika na Tiba ya Magonjwa Ambukizi nchini (Infectious Diseases Hospital). Wizara ilichagua Hospitali ya Kibong'oto kuwa kituo cha Utafiti pamoja na kutoa tiba kwa wagonjwa wa Kifua Kikuu sugu nchini na kujenga utaalamu kwa watumishi wa afya ikiwa na lengo la kugatua utoaji wa huduma za tiba hiyo nchi nzima. Hospitali ina jumla ya watumishi 263 ambapo mahitaji halisi ya Hospitali kwa sasa ni watumishi 522. Aidha, kuna jumla ya vitanda 300, kati ya hivyo vitanda 120 ni kwa ajili ya wagonjwa wa TB sugu, vitanda 120 kwa ajili ya wagonjwa wa TB ya kawaida na vitanda 60 kwa ajili ya wagonjwa wa magonjwa mengine.

163. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Hospitali illihudumia jumla ya wagonjwa 18,684 ukilinganisha na wagonjwa 22,610 waliohudumiwa katika kipindi cha mwaka 2019/20. Kati ya wagonjwa 18,684, wagonjwa wa nje walikuwa 18,024 na wagonjwa waliolazwa 660. Katika kundi la wagonjwa waliolazwa, wagonjwa wa Kifua Kikuu sugu walikuwa 97, Kifua Kikuu sugu ambata na VVU 17, Kifua Kikuu cha kawaida 429 na Kifua Kikuu ambata na VVU walikuwa 36. Aidha, asilimia 82 ya wagonjwa waliopatiwa matokeo ya tiba kwa mwaka 2018 walithibitishwa kupona Kifua Kikuu sugu. Vilevile, Hospitali imeweza kufanya ufuatiliaji wa vimelea vya magonjwa ambukizi ya Kifua Kikuu kwa usugu wa dawa, ambapo wagonjwa 3,426 walipimwa, na kati yao 621 waligundulika kuwa na Kifua Kikuu na kuanzishwa matibabu.

164. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Hospitali imetekeleza Sera ya Afya nchini kwa

kuanzisha huduma mbalimbali za tiba zenye kulenga kuboresha huduma za matibabu ya Wagonjwa wa kifua kikuu na kusogeza huduma karibu zaidi kwa Wananchi. Huduma za kibingwa bobezi zilizoanzisha ni pamoja na huduma ya utengemao wa mapafu kwa Wagonjwa waliokwishaugua Kifua kikuu na kupona na bado wanapata madhara katika mapafu (Pulmonary rehabilitative services), katika kipindi hiki wagonjwa 260 waliowahi kuugua Kifua kikuu wamechunguzwa na kupata huduma ya utengemao wa mapafu yao.

165. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha matokeo ya matibabu ya aina zote za Kifua Kikuu na magonjwa mengine ambata, Hospitali iliweka lengo la kuchunguza wagonjwa 1,565 kama wahisiwa wa Ugonjwa wa Kifua Kikuu. Katika kipindi cha mwezi Julai 2020 hadi Machi 2021 wateja 2,512 waliokuwa na dalili za ugonjwa wa Kifua Kikuu walichunguzwa, ambapo wagonjwa 621 waligunduliwa kuwa na ugonjwa wa Kifua Kikuu na wagonjwa wote walianzishiwa matibabu. Aidha, wagonjwa 92 wa Kifua Kikuu sugu walipokelewa kutoka katika mikoa mbalimbali nchini na kuanzishiwa matibabu.

166. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali liliwanikiwa kufanya uchunguzi wa usugu wa dawa za Kifua Kikuu kwa sampuli 3,426 za wagonjwa wa Kifua Kikuu waliotoka mikoa ya kanda ya kaskazini, ambapo sampuli 28 zilligundulika kuwa na vimelea vya Kifua Kikuu sugu. Katika mwaka 2020/21, Hospitali imenunua gari ambalo ni kliniki inayotembea (Mobile clinic van) ambalo lina vifaa vya uchunguzi wa Kifua Kikuu, VVU/UKIMWI pamoja na mitambo ya X-ray kwa ajili ya kurahisisha upimaji kwa jamii ambazo zipo hatarini kuugua magonjwa ya mapafu hasa jamii za wachimbaji migodi. Katika lengo la kuifikia jamii, gari hili litatumika kwenda kwenye jamii athirika hasa za wachimbaji wa madini katika Mikoa ya Mara, Geita na Manyara kwa kuanzia ambapo inakadiriwa kuhudumia wachimbaji wa 10,000 kwa kipindi cha mwaka 2021/2022.

167. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa dawa muhimu na dawa maalum za kutibu

Magonjwa ambukizi na Magonjwa yasiyo ambukizi kupitia fedha zinazotengwa na Hospitali kutoka vyanzo vyake vya ndani na fedha zinazopelekwa na serikali kuu kupitia Bohari ya Dawa kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi. Aidha, hali ya upatikanaji wa dawa muhimu na maalum katika hospitali umeendelea kuimarika na umefikia asilimia 80 ikilinganishwa na asilimia 75 kwa kipindi cha mwaka 2019/20.

168. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha utoaji wa huduma katika Hospitali ya Kibong'oto katika kipindi cha mwaka 2021/22, Hospitali itatekeleza yafuatayo:-

- (i) Kukamilisha ujenzi wa maabara ya afya ya Jamii Pamoja na ununuzi wa vifaa vya maabara;
- (ii) Kujenga *OPD complex* itakayokuwa na idara ya dharura (Emergency department); na
- (iii) Kukarabati wodi na miundombinu ya hospitali ikijumuisha njia za kupita wagonjwa na watumishi (Walkways).

#### **Hospitali ya Rufaa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya**

169. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali inahudumia Mikoa saba (7) ya Nyanda za juu kusini ambayo ni; Iringa, Njombe, Ruvuma, Katavi, Rukwa, Songwe na Mbeya. Mikoa hiyo ina takriban wakazi 8,000,000. Hospitali hii imegawanyika katika maeneo makuu matatu ikiwa ni pamoja na; Hospitali Kuu, Hospitali ya wazazi Meta na kijiji cha wagonjwa wa akili Uyole. Majukumu makuu ya hospitali hii ni kutoa huduma za Tiba, Mafunzo kwa kushirikiana na Vyuo Vikuu pamoja na kufanya Utafiti. Hospitali ina jumla ya vitanda 603 ambavyo vinatumika katika maeneo yafuatayo; Hospitali Kuu vitanda 447 na Hospitali ya Meta vitanda 156. Hospitali ina jumla ya watumishi 913 wa kada mbalimbali.

170. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali imeendelea kutoa huduma za matbabu ya kibingwa hususan kwa wananchi wa mikoa ambapo katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021,

Hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa 259,873 ikilinganishwa na wagonjwa 252,034 kipindi kama hicho mwaka 2019/20. Kati ya wagonjwa 259,873 waliohudumiwa, wagonjwa wa nje walikuwa 221,694 na wagonjwa wa kulazwa 38,179. Aidha, katika kuboresha huduma za kibingwa, hospitali ilihakikisha wagonjwa wote waliopaswa kuonwa na madaktari bingwa wamepatiwa matibabu na kupunguza rufaa za kupeleka wagonjwa hospitali za ngazi ya taifa.

171. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha huduma za kibingwa, hospitali ilifanikiwa kutoa huduma kwa jumla ya wagonjwa 259,873 kama ifuatavyo: upasuaji wa jumla (9,968); magonjwa ya akina mama (22,997); magonjwa ya watoto (7,897); magonjwa ya ndani (164,003); kuchuja damu kwa wagonjwa wenyewe matatizo ya figo (2,350); magonjwa ya Masikio, Pua na Koo (8,693); huduma ya macho (8,955); huduma ya afya ya kinywa na meno (5,840); mfumo wa mkojo (7,191); saratani (534); magonjwa ya damu (53); na huduma za magonjwa ya dharura na magonjwa mengine (21,592). Huduma zilizoboreshwa ni upasuaji kwa njia ya matundu (Laparoscopic Surgery), Upimaji kwa kutumia CT-Scan na upimaji wa usugu wa dawa za UKIMWI. Aidha, hali ya upatikanaji wa dawa umeendelea kuimarika na umefikia asilimia 98 ikilinganishwa na asilimia 95 mwaka 2019/20.

172. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali ina jumla ya watumishi 670 ambao wameajiriwa na Wizara. Kati ya hao, watumishi 223 wameajiriwa kwa Mkataba kwa kutumia mapato ya ndani ya Hospitalini. Aidha, Madaktari 108 wameajiriwa katika fani mbalimbali ambapo kati yao, Madaktari Bingwa ni 56, Wafamasia nane (8), Wateknolojia Dawa 10, Wateknolojia Maabara 25, Maafisa Wauguzi 198 na Wauguzi 238. Kwa mujibu wa ikama ya hospitali, kuna upungufu wa zaidi ya watumishi 650 wa kada mbalimbali. Upungufu huu unatokana na kustaafu kazi, kufariki kwa watumishi, pamoja na kuongezeka kwa huduma mbalimbali za kibingwa.

173. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha utoaji wa huduma za afya, hospitali kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Ndaki ya Mbeya (UDSM – MCHAS) imeendelea kutoa

mafunzo ya Uduktari katika ngazi ya shahada. Kwa sasa chuo kina jumla ya wanachuo 1,000 wa mwaka wa kwanza hadi wa tano. Aidha, Hospitali kwa kushirikiana na Wizara, imefanikiwa kuwapeleka masomoni watumishi wa kada mbalimbali kama ifuatavyo; Madaktari 30 kusomea ngazi ya ubingwa, Madaktari Bingwa saba (7) kusomea ngazi ya ubobezi na watumishi 15 kusomea fani mbalimbali kwa mujibu wa miundo yao.

174. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imetenga bajeti ya **Shilingi 9,151,766,914.99** kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya kisasa ya Wazazi Meta ambayo ni sehemu ya Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya. Kuanza kwa ujenzi huu imekuwa ni jambo la kihistoria kwa sababu toka hospitali hii ianzishwe mwaka 1950 haijawahi kuongezewa jengo kwa ajili ya kulaza wagonjwa na hivyo kusababisha kuwepo kwa msongamano mkubwa na wagonjwa wengine kulala chini. Kasi ya ujenzi wa jengo hili ni nzuri na tayari ujenzi umekamilika kwa asilimia 80. Vilevile, Hospitali imeboresha miundombinu kwa kuanzisha kiwanda cha uzalishaji wa majitiba (Infusion). Kiwanda kimekamilika na uzalishaji majitiba umeshaanza ambapo kwa siku moja kiwanda kinazalisha lita 120 za majitiba.

175. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Hospitali imeimarisha maeneo ya utoaji wa huduma za mkoba katika mikoa ya Mbeya, Rukwa na Katavi ambapo jumla ya watu 120 walifanyiwa uchunguzi wa macho kati ya hao wagonjwa 45 walifanyiwa upasuaji (upasuaji mkubwa kwa watu 37 na kutoa mtoto wa jicho kwa watoto nane).

176. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Hospitali inategemea kuleketeteza yafuatayo:-

(i) Kukamilisha ujenzi wa Jengo la Meta litakalokuwa na vitanda 223. Mradi huu unatarajiwu kuchukua kipindi cha miezi 24;

(ii) Kuimarisha huduma za uchunguzi kwa kusimika mtambo wa MRI;

(iii) Kuendelea kutoa mafunzo ili kuwajengea uwezo wataalam wa afya katika ngazi ya ubingwa na ubingwa bobezi; na

(iv) Kuimarisha huduma za saratani.

### **Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa Bugando**

177. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa Bugando imeendelea kutoa huduma za kibingwa kwa wagonjwa kutoka mikoa sita (6) ya Mwanza, Geita, Simiyu, Shinyanga, Kagera, Mara na Kigoma. Hospitali imekuwa ikitekeleza majukumu yake ili kuhakikisha huduma bora za kibingwa na kibingwa bobezi kwa wagonjwa zinatolewa katika kiwango cha juu. Baadhi ya huduma za kibingwa zilizotolewa katika Hospitalini kama ifuatavyo; huduma za kuchuja damu kwa wagonjwa wenyе matatizo ya figo (Renal Dialysis), Magonjwa ya akina mama (Obstetrics and Gynaecology), Upasuaji wa Moyo (Cardiothorasic), Magonjwa ya watoto (Pediatrics and Child Health), afya ya akili (Mental Health), Magonjwa ya ndani (Internal Medicine) na Upasuaji wa jumla (General Surgery). Huduma nyininge za kibingwa zilizoanzishwa ni upasuaji kwa njia ya matundu (Laparoscopic Surgery), Uchunguzi wa magonjwa kwa kutumia CT-Scan, upimaji wa usikivu (Autiometry) Pamoja na Ubadilishaji wa Nyonga. Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa, Bugando ina jumla ya watumishi 1,180 ikilinganishwa na mahitaji ya watumishi 2,560. Aidha, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa, Bugando ina jumla ya vitanda 950 ikilinganishwa na mahitaji ya vitanda 1,120.

178. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa 299,939 ikilinganishwa na wagonjwa 260,394 katika kipindi kama hicho mwaka 2020/2021. Kati ya wagonjwa 299,939, wagonjwa wa nje (OPD) walikuwa 277,485 na wagonjwa wa kulazwa (IPD) walikuwa wagonjwa 22,454.

179. ***Mheshimiwa Spika***, hospitali imeendelea kuboresha huduma za kibingwa kwa kuanza kutoa matibabu ya Saratani

baada ya kununua mashine ya tiba ya mionzi iitwayo *Brachytherapy* kwa **Shilingi bilioni 1.4**. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya wagonjwa 11,878 walipatiwa matibabu ya Saratani ikilinganishwa na wagonjwa 8,433 waliopata huduma hiyo kwa kipindi cha mwaka 2019/20. Kati ya hao, wagonjwa 3,130 walipatiwa tiba ya Saratani kwa kutumia dawa (Chemotherapy), wagonjwa 469 walipatiwa mionzi (Radiotherapy), wagonjwa 628 walipatiwa huduma ya tiba mionzi na kemia na wagonjwa 7,651 walihuduria kliniki ya saratani kwa matibabu ya kawaida.

180. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali ilifanikiwa kufanya upasuaji wa kibingwa kwa wagonjwa 1,934 ikiwemo upasuaji wa Moyo na Kifua (131), upasuaji wa Ubongo (98) na upasuaji wa mifupa (392), upasuaji wa VVF (89) na upasuaji wa Mdomo Sungura (176). Kwa sasa hospitali ipo kwenye hatua za kukamilisha kuanzisha huduma za upasuaji kwa kutumia matundu madogo yaani *Laparoscopic Surgery*. Aidha, huduma za kusafisha damu (Renal Dialysis) zimeendelea kuimarika ambapo jumla ya wagonjwa 2,874 walipata huduma hii. Vilevile, hospitali imeimarisha huduma kwa kuongeza mashine nyingine 11 kutoka mashine 10 za awali na kuwa na jumla ya mashine 21 ambazo zimesaidia upatikanaji wa huduma hii kwa urahisi. Pia, huduma ya uchunguzi kupitia CT-Scan iliendelea kutolewa kwa wagonjwa 6,373 kwa kipindi tajwa ikilinganishwa na wagonjwa 5,671 waliohudumiwa mwaka 2019/20.

181. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, hospitali imeimarisha maeneo ya utoaji wa huduma za mkoba kwa maeneo yanayoizunguka hospitali kwa kuwashudumia wagonjwa kama ifuatavyo; Hospitali ya Sengerema wagonjwa 120, Hospitali ya Songambele wagonjwa 280, hospitali ya Kagondo wagonjwa 208, Hospitali ya Bukumbi wagonjwa 236 na Hospitali ya Kabanga wagonjwa 821. Kuboreshwaa kwa huduma hizo ni faida kwa watumishi kwa vile inawajengea uwezo wa kutoa huduma bora kwa wananchi wanaoishi maeneo ya hospitali hizo.

182. ***Mheshimiwa Spika***, hospitali imeendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi wake kuitia mapato ya ndani. Hospitali imeendelea kudhamini watumishi katika fani mbalimbali za ubingwa bobezi katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya Nchi, ambapo kwa kipindi cha miaka mitano jumla ya Madaktari 64 walirejea kutoka katika masomo ya ubingwa na ubingwa bobezi, Wauguzi 28, Wataalam wa Maabara sita (6) na Wafamasia watatu (3). Jumla ya Madaktari 40 na Wauguzi 20 wanaendelea na masomo. Aidha, hospitali pia inadhamini wataalam 83 wa kada nyingine katika vyuo mbalimbali nchini.

183. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, hospitali ilifanya ununuzi wa mashine aina ya *fluoroscopy* pamoja na kufunga mashine ya MRI. Aidha, Hospitali imefanikiwa kuanza ujenzi wa wodi ya wagonjwa wa macho ambayo itasaidia kupunguza msongamano kwenye wodi. Hospitali imeanza ujenzi wa wodi ya saratani ambayo itakuwa na vitanda 120. Upatikanaji wa huduma hii umepunguza rufaa za wagonjwa wa saratani wa Kanda ya Ziwa kwenda Taasisi ya Saratani Ocean Road kwa zaidi ya asilimia 97. Vilevile, hali ya upatikanaji wa dawa umeimarika kufikia asilimia 96 ya mahitaji yote ikilinganishwa asilimia 84 mwaka 2019/20.

184. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha utoaji wa huduma hospitali ya Bugando katika kipindi cha mwaka 2021/22, itafanya ununuzi wa vifaa vifuatavyo:-

- (i) Mashine za Cobalt 60 (2) kwa ajili ya mionzi ya Nje na Ndani;
- (ii) *Gamma camera* yenye spect CT (1); na
- (iii) *Linear Accelaretor Machine* (2) na CT simulator (1).

#### **Hospitali ya Rufaa ya Kanda Kaskazini (KCMC)**

185. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Kaskazini yenye vitanda 686 inashughulika na utoaji wa huduma za kibingwa na kibingwa bobezi za macho, ngozi, viungo bandia, mfumo wa njia ya mkojo, Masikio, Pua na Koo na

huduma ya upasuaji kwa njia ya matundu. Hospitali ina jumla ya watumishi 1,102. Kati yao, watumishi 877 ni wa kudumu na watumishi 225 ni wa mkataba.

186. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Hospitali imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kutoa huduma ya matibabu ambapo jumla ya wagonjwa 281,716 walihudumiwa ikilinganishwa na wagonjwa 364,613 mwaka 2019/20. Kati yao wagonjwa 165,458 ni wagonjwa wa nje (OPD) na wagonjwa 116,258 walilazwa (IPD). Aidha, kwa upande wa huduma za upasuaji, jumla ya wagonjwa 2,797 walifanyiwa upasuaji ikilinganishwa na wagonjwa 3,987 kwa mwaka 2019/20. Hospitali imeendelea kutoa huduma za kusafisha damu ambapo jumla ya wagonjwa 343 wenye matatizo ya figo walihudumiwa ikilinganishwa na wagonjwa 722 walio hudumiwa mwaka 2019/20. Hospitali iliweza kutoa matibabu ya misamaha kwa wagonjwa 320 ullogharimu **Shilingi 321,675,890**; ikilinganishwa na wangonjwa 412 ambao uligharimu **Shilingi 432,567,980** kwa mwaka 2019/20. Vilevile, hospitali imeweza kutoa huduma za mkoba kwa kuhudumia jumla ya watu 2,890. Hospitali ilitoa huduma kwa wagonjwa 12 kutoka nchi za Kenya, Burundi, Kongo na Rwanda.

187. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, hospitali ilifanya ununuzi wa mashine ya ECHO (GE) inayotumika kwenye kliniki ya magonjwa ya moyo. Gharama za mashine hii ni **Shilingi 118,065,000** fedha ambazo ni mapato ya ndani; Ununuzi wa *Ventilators* 2 katika Idara ya *ICU*, ununuzi huu umegharimu **Shilingi 175,940,000** na ununuzi wa *Patient's monitor* 15 katika idara ya *ICU* ambazo zimegharimu **Shilingi 426,879,999**. Aidha, Hospitali imefanikiwa kuzindua wodi ya wagonjwa wa saratani, yenye jumla ya vitanda 47, ambayo imesaidia kupunguza msongamano wa wagonjwa katika wodi ya utabibu. Vilevile, hali ya upatikanaji wa dawa umeimarika kufikia asilimia 85 ya mahitaji yote ikilinganishwa na asilimia 80 mwaka 2019/20.

188. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Hospitali imepanga kutekeleza yafuatayo:-

- (i) Kuendelea kuboresha idara ya Saratani kwa kujenga na kuanzisha huduma ya tiba kwa mionzi (Bunker for radiotherapy) ujenzi huo utagharimu kiasi cha **Shilingi bilioni 7**;
- (ii) Ujenzi wa idara ya magonjwa ya Moyo (Cadiovascular centre) ambao utagharimu kiasi cha **Shilingi bilioni 6**. Ujenzi huo utafanyika kwa awamu, hivyo unategemewa kukamilika ifikapo mwaka 2024; na
- (iii) Kukamilisha ujenzi wa vyumba vinne (4) vya upasuaji, ambapo kwa sasa ujenzi huo umefikia asilimia 70 ya utekelezaji. Ujenzi huo utagharimu kiasi cha **Shilingi 490,000,000**.

### **Hospitali ya CCBRT**

189. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali ya CCBRT inatoa huduma za utengemao wa ulemavu unaosababishwa na hitilafu ya maumbile ya mifupa na viungo vingine vya mwanadamu ikiwa ni pamoja na midomo sungura, mtoto wa jicho, vifundo vya miguu pamoja na huduma za fistula. Aidha, hospitali hutoa huduma za awali za kuzuia ulemavu majumbani, kufuatilia na kutathmini namna huduma za utengemao zinavyotolewa majumbani. Pia Hospitali hutoa ushauri nasaha kwa watu wenye ulemavu na familia zao, kusaidia familia katika kubadili tabia na kuhimiza watu wenye ulemavu kushiriki katika shughuli za jamii. Hospitali ina jumla ya vitanda 119, vitanda vinavyohitajika ni vitanda 199, ina upungufu wa vitanda 80, pia ina jumla ya watumishi 378 kati ya wanahitajika 405.

190. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Hospitali imeendelea kutoa huduma za tiba maalum, za kibingwa na bobezni ambapo jumla ya wagonjwa 103,038 walihudumiwa kati yao wagonjwa 101,745 walikuwa wa nje (OPD) na 1,293 walikuwa ni wakulazwa (IPD) ikilinganishwa na wagonjwa 128,972 waliohudumiwa katika kipindi cha mwaka 2019/20. Aidha, Hospitali inahudumia

wagonjwa wa nje 460 na kutoa matibabu kwa njia ya upasuaji kwa wagonjwa 35 kwa siku.

191. ***Mheshimiwa Spika***, Huduma za afya zinazotolewa na CCBRT ni pamoja na huduma ya kibingwa kwa matibabu ya macho kwa watoto na watu wazima, huduma za kibingwa za mifupa ikiwemo upasuaji wa nyonga na magoti, miguu kifundo (Clubfoot), huduma za utengemao (health rehabilitation), fistula itokanayo na uzazi (obstetric fistula), mafunzo ya kuwajengea uwezo kiuchumi wanawake waliotibiwa fistula.

192. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali ya CCBRT imeendelea kujikita kwenye kutoa huduma za matibabu ya Fistula ya Uzazi kwa viwango vya juu. Hii ni pamoja na kuendelea kutoa elimu kuhusu tatizo hilo kwenye jamii ili akina mama wasiendelee kunyanyapaliwa katika jamii bali wapate matibabu. CCBRT imekuwa ikiwatafuta akina mama wenye tatizo la Fistula ya Uzazi popote pale walipo nchini na kutoa vikwazo vyote vya akina mama hawa kutopata huduma ikiwa ni pamoja na gharama za usafiri, matibabu, chakula na malazi. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, akina mama 344 walipata matibabu. CCBRT inawafuatilia akina mama hawa walipata matibabu baada ya miezi sita kuhakikisha wamepona na kwa mwaka 2020, asilimia 96 ya akina mama walipata matibabu walipona kabisa. Kiwango hiki kimevuka kiwango cha ubora kilichowekwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) cha asilimia 80 ya akina mama walipata matibabu wawe wamepona kabisa baada ya miezi sita. CCBRT pia ni Hospitali pekee nchini iliyopewa ithibati (accreditation) na Shirikisho la Kimataifa la Vyama vya Madaktari Bingwa wa Magonjwa ya Akina Mama na Uzazi (International Federation of Gynecology and Obstetrics -FIGO).

193. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali ya CCBRT ina uzoefu wa kutoa huduma bora za kibingwa na bobez za macho. Ubora wa huduma hizo umeongezwa na uwepo wa idara ya uchunguzi wa magonjwa ya macho (Eye Diagnostic Unit) yenye vifaa bora na vya kisasa ambapo kwa sasa hospitali ina karakana yenye uwezo wa kutengeneza macho bandia

(artificial eyes). Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, wagonjwa 56,929 wa macho walipata matibabu.

194. ***Mheshimiwa Spika***, Kitengo cha Viungo Tiba Saidizi ni mionganoni mwa vitengo vinavyopatikana katika Hospitali ya CCBRT. Kitengo hiki hutoa huduma za viungo tiba saidizi kwa watoto na watu wazima kutoka ndani na nje ya nchi ikiwa ni pamoja na Comoro, Congo, Kenya, Uganda, Burundi na Tunisia. CCBRT ni mionganoni mwa Taasisi inayotoa vifaa tiba saidizi ikiambatana na mafunzo ya namna ya kutumia vifaa tiba saidizi hivyo. Kwa sasa CCBRT inatoa huduma ya viti mwendo, vifaa tiba saidizi na macho bandia kwa wakimbizi mkoani Kigoma (Kambi za Nyarugusu, Mtendeli, Nduta na Kakonko) na jamii inayozunguka kambi hizo.

195. ***Mheshimiwa Spika***, hali ya upatikanaji wa dawa katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, ulikuwa ni asilimia 80. Katika kupunguza utegemezi wa fedha kutoka kwa wafadhili kwa ajili ya kuendesha shughuli zake za kutoa huduma, hospitali ya CCBRT iliamua kupanua wigo wa huduma za wagonjwa wa nje wenye uwezo wa kulipia matibabu yao (Private Clinic) ambapo fedha inayopatikana katika kliniki hiyo inasaidia kuendesha shughuli za utoaji huduma katika hospitali. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya mapato ya ndani kutoka kwa wagonjwa wa *Private* na wale wanaochangia matibabu ni **Shilingi 7,751,768,940**, wagonjwa wa *Private* wakichangia kwa asilimia 50 ya mapato sawa na **Shilingi 3,896,938,705**. Kuongezeka kwa mapato ya ndani kumeweza CCBRT kupunguza utegemezi wa nje hadi asilimia 55 kulingana na utegemezi wa asilimia 100 hapo awali.

196. ***Mheshimiwa Spika***, kwa kutambua uhusiano uliopo kati ya namna ya kuzuia ulemavu na upatikanaji wa huduma bora za afya ya uzazi na watoto wachanga CCBRT iliamua kwa kushirikiana na Wizara kujenga majengo maalum kwa ajili ya huduma za afya ya uzazi na watoto wachanga ambao ulianza 2011 kwa msaada wa wafadhili. Kwa sasa ujenzi huo umekamilika kwa kiwango kikubwa na huduma zitaanza kutolewa wakati wowote mwaka huu 2021.

197. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Hospitali ya CCBRT kuptitia kituo cha huduma za utengemao kilichopo Moshi Mkoani Kilimanjaro iliendelea kutoa huduma za utengemao. Kituo hicho cha huduma za utengemao (rehabilitation) kinahudumia mikoa ya Kilimanjaro, Tanga, Manyara, Arusha, Dodoma na Tabora. Huduma zilizotolewa ni pamoja na utoaji wa viti mwendo (wheelchairs) 693 kwa watoto wenyewe ulemavu, utoaji wa vifaa saidizi 31 kulingana na ulemavu wa mtoto. Vilevile, kutoa mafunzo kwa watoto wenyewe ulemavu na wazazi namna ya kutumia viti mwendo na vifaa vingine saidizi. Kituo pia kilitoa mafunzo kwa watoa huduma za afya namna ya kumhudumia mtoto mwenye ulemavu.

198. ***Mheshimiwa Spika***, kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, madaktari wanne (4) wa CCBRT waliokuwa kwenye masomo ya shahada ya pilii wamehitimu na mtumishi mmoja (1) anaendelea na mafunzo katika fani ya upasuaji. Aidha, watumishi saba (7) walipelekwa kwenye mafunzo ya muda mfupi yanayofanyika ndani na nje ya nchi.

199. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Hospitali itaendelea kutoa huduma za kibingwa bobesi na imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kuongeza wigo wa huduma za afya ya uzazi na watoto wachanga;

(ii) Kuendelea kuboresha huduma za tiba ya magonjwa ya macho ya Retina (pazia nyuma ya jicho) na upasuaji;

(iii) Kuendelea kuwajengea uwezo watoa huduma katika vituo vya Afya vya Serikali kwenye huduma za afya ya Uzazi na watoto wachanga kutoka vituo 23 hadi 45 kwa Mkoa wa Dar es Salaam;

(iv) Kuanza kufanya upasuaji kwa njia ya matundu madogo (laparoscopic surgeries); na

(v) Kuendelea kutoa huduma za mikoba mikoani (mobile outreaches) ikiwa ni pamoja na kujengea uwezo watoa huduma za afya kwenye maeneo yatakayoflikwa.

### **Hospitali za Rufaa za Mikoa**

200. ***Mheshimiwa Spika***, katika jitihada za Serikali za kusogeza huduma za kibingwa karibu na wananchi, Wizara inasimamia na kuratibu utoaji wa huduma katika Hospitali 28 za Rufaa za Mikoa (RRH) kwa kuhakikisha upatikanaji wa huduma za matibabu ya kibingwa, upatikanaji wa Dawa, Vifaa, Vifaa tiba na Vitendenishi, upatikanaji wa madaktari bingwa, ujenzi na uimarishaji wa miundombinu ya kutolea huduma za afya.

201. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Hospitali 28 za Rufaa za Mikoa zilihudumia jumla ya wagonjwa 2,814,390 ambapo wagonjwa wa nje (OPD) walikuwa 2,547,482 na wagonjwa walilazwa (IPD) walikuwa 266,908 ikilinganishwa na wagonjwa 3,206,347 waliohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2019/20, ikiwa ni upungufu wa asilimia 15. Maelezo ya kina yapo kwenye **Kiambatisho Na. 10**. Aidha, kati ya wagonjwa hao waliohudumiwa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, jumla ya wagonjwa 353,139 walikuwa ni wagonjwa wa misamaha ambayo imegharimu jumla ya **Shilingi 4,286,784,135**. Vilevile, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya akina mama 77,563 walijifungua katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, na vilitokea vifo 272 vinavyohusiana na uzazi kwenye hospitali hizi katika kipindi hicho kama ilivyoainishwa katika **Kiambatisho Na. 11**. Hospitali za RRH zina uwezo wa kuwa na jumla ya vitanda 7,176 ambapo kwa sasa zina jumla ya vitanda 6,773 sawa na asilimia 94.5 ya uwezo wa kawaida wa hospitali hizo.

### **Huduma za Mkoba (Outreach Services)**

202. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuwezesha utoaji wa huduma za kibingwa kwenye mazingira ya karibu na wananchi, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Hospitali za Rufaa za Mikoa 19 zilitoa huduma za mkoba katika fani za ubingwa

zifuatazo; magonjwa ya macho, magonjwa ya watoto, utoaji wa dawa za ganzi, upasuaji wa mifupa, magonjwa ya ndani, upasuaji wa kawaida, afya ya uzazi na magonjwa ya wanawake, magonjwa ya sikio, pua na koo na magonjwa ya meno. Katika kliniki hizo, jumla ya wagonjwa 23,133 walihudumiwa. Kati yao 2,969 walifanyiwa upasuaji kama ilivyoainishwa kwenye **KiambatishoNa. 12**. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, hali ya upatikanaji wa Dawa katika Hospitali hizi ilikuwa asilimia 81 ikilinganishwa na asilimia 91 ya kipindi kama hiki kwa mwaka 2019/20.

### **Upatikanaji wa Madaktari Bingwa**

203. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha huduma zitolewazo na Hospitali za Rufaa za Mikoa, Serikali imetoa kipaumbele katika kuhakikisha kuwa huduma za kibingwa katika fani za Upasuaji wa jumla (General Surgery), Magonjwa ya wanawake na uzazi (Obstetric & Gynaecology), Watoto (Paediatric & Child Health), Magonjwa ya Ndani (Internal Medicine), Radiolojia (Radiology), Huduma za dharura (Emergency Medicine), huduma za Upasuaji wa mifupa na magonjwa ya ajali (Orthopaedic Surgery) na huduma za usingizi (Anaesthesiology) zinapatikana kwa uhakika. Hospitali hizi zimeweza kuongeza idadi ya madaktari bingwa kutoka 194 mwaka 2019/20 hadi 244 mwaka 2020/21. Aidha, Serikali inaendelea kuboresha huduma hizi ili kuhakikisha huduma zote 14 za kibingwa zinapatikana kwa ngazi hii kama ilivyoonesha kwenye **KiambatishoNa. 13**.

204. ***Mheshimiwa Spika***, kuitia maendeleo haya ya uwekezaji wa huduma za kibingwa uliofanywa na Serikali hadi sasa, ni dhahiri kuwa nchi yetu inayo fursa nzuri ya kutoa huduma za kibingwa siyo tu kwa faida ya wananchi wa taifa hili bali hata nchi jirani. Vilevile, nchi yetu inayo fursa nzuri ya kutoa mafunzo ya kibingwa kwa wanafunzi wa taaluma za afya wakiwemo wa kutoka nchi mbalimbali duniani. Hivyo, Wizara inafanya maandalizi ya mpango wa kuwezesha huduma za afya za kibingwa kutambulika zaidi nchi zingine za Afrika ili wenye uhitaji badala ya kwenda mbali zaidi waje Tanzania. Hii itaenda sambamba na kuweka mazingira mazuri

ili tuweze kupokea Bima za Afya za Kimataifa. Kwa kutumia fursa hizi hospitali zitaendelea kuimarika na kuendelea kupunguza zaidi utegemezi kwa Serikali na kikubwa kuboresha zaidi afya za wenge uhitaji wa huduma za kibingwa.

## **UHAKIKI WA UBORA WA HUDUMA ZA AFYA**

205. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kuwa huduma za afya zinazotolewa zinakidhi viwango vya ubora, Wizara imekuwa ikisimamia maadili na utendaji wa wataalam kuititia Mabaraza ya Kitaaluma, Bodi na Timu za Usimamizi wa Huduma katika ngazi ya Taifa, Kanda, Mikoa na Halmashauri ili kuhakikisha utendaji wa watumishi unakuwa na tija (productivity) na kunakuwepo matumizi mazuri ya rasilimali. Katika kufanikisha hayo, Wizara imeanza kuendesha mafunzo kwa wajumbe wa Timu za Uendeshaji wa Huduma za Afya za Mikoa (RHMTs) na Halmashauri (CHMTs) kuhusu namna ya kuboresha huduma kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ikiwa ni pamoja na kukusanya na kushughulikia malalamiko ya wateja na kuzingatia haki na wajibu wa wateja. Jumla ya wajumbe 150 katika mikoa ya Arusha (44), Dodoma (39) na Dar es Salaam (67) wamepatiwa mafunzo hayo.

206. ***Mheshimiwa Spika***, dhana ya huduma bora ni pana na inapimwa na anayepokea huduma na kwa upande mwingine anayetoea huduma. Mara nyingi ubora wa huduma ni majumuisho ya mambo mengi yanayogusa matarajio ya mpokeaji wa huduma. Wizara itahakikisha inaimarisha mifumo yote ya ubora wa huduma kwa kusikiliza zaidi mahitaji wa wapokeaji wa huduma na kuelimisha zaidi wapokeaji wa huduma juu ya ubora wa huduma kwa jicho la kitaalam. Lengo ni wananchi wazidi kufurahia huduma wanazopata na kuhamasika zaidi kujunga na bima za afya bila shuruti na waliojunga wakubali kutumia vituo vya huduma kwa kuzingatia mfumo wa rufaa. Aidha, ili kusukuma kasi ya utoaji wa huduma za afya zilizo bora, Wizara itasimamia kuelimisha watalaam wake juu ya uhusiano wa ubora wa huduma katika kupunguza changamoto zinazokabili Taasisi mbalimbali hasa

zitokanazo na upungufu wa fedha unaochangiwa pia na huduma duni zisizovutia wateja wenyewe uwezo wa kuchangia hususan kwa bima za afya. Hii ni katika maandalizi ya kunufaika na ujio wa bima ya afya kwa wote jambo ambalo linahitaji kuvutia wateja watumie huduma za kituo husika vinginevyo kituo kinawenza kisinufaika na bima husika.

207. ***Mheshimiwa Spika***, katika dhana nzima ya kuboresha huduma kwa kuzingatia usalama wa mtoa huduma, Wizara imeendelea kutoa mafunzo ya kukinga na kudhibiti maambukizi ambapo jumla ya watumishi 1,043 wamepatiwa mafunzo katika mikoa ya Morogoro, Tabora, Dar es Salaam, Dodoma, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Shinyanga, Mwanza, Geita, Tanga, Arusha, Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe, Kagera, Katavi, Pwani, Mtwara na Ruvuma. Wizara imefanya mafunzo maalum (mentorship) katika vituo 25 kwenye mikoa sita ya Mbeya, Dar es Salaam Mwanza, Njombe, Tabora na Morogoro katika maeneo ya kukinga na kudhibiti maambukizi.

208. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha ubora wa huduma za upimaji VVU, Wizara imefanya uhakiki wa nje (external auditing) kwa maeneo 209 ya upimaji VVU kwenye vituo 80 katika Mikoa 14 ambapo maeneo 136 (65%) yalikidhi vigezo. Maeneo 73 (35%) ambayo hayakukidhi vigezo yameandaliwa mpango kazi wa uimarishaji ubora ili kuweza kufikia vigezo. Katika kuimarisha usimamizi shirikishi katika ngazi zote za utoaji huduma, Wizara imekamilisha kutengeneza mfumo wa kidijitali wa usimamizi shirikishi (AfyaSS) ambao utawezesha ufuutiliaji wa shughuli zote za usimamizi shirikishi na kusaidia kuimarisha uratibu, kupeana taarifa na matumizi ya takwimu.

## **MIRADI YA MAENDELEO YA WIZARA**

209. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Wizara imeendelea kupanua wigo wa kuwashudumia wananchi, kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Hospitali mpya, ukarabati wa majengo na upanuzi wa Miundombinu ya kutolea huduma za afya nchini katika Hospitali za Rufaa za

Mikoa, Hospitali za Rufaa ngazi ya Kanda na Hospitali Maalum. Aidha, lengo la ujenzi, ukarabati na upanuzi huo ni kusogeza huduma za afya karibu na wananchi, kuongeza upatikanaji wa huduma za Kibingwa na Ubingwa bobezi kwa gharama nafuu na hatimaye kuokoa uhai wa wananchi. Jumla ya Miradi ya Maendeleo 22 inayogharimu kiasi cha **Shilingi bilioni 193.266** imeanzishwa ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Shilingi bilioni 130.634** zimeshatolewa na kutumika hadi sasa. Maelezo ya kina yametolewakatika **Kiambatisho Na. 14.**

210. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha upatikanaji wa huduma za afya nchini, Wizara imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kujenga Hospitali za Rufaa za Mikoa katika mikoa mipyä ya Njombe, Simiyu, Geita, Songwe na Katavi. Hadi kufikia Machi 2021, utekelezaji wa ujenzi katika Hospitali hizo umefikia hatua mbalimbali za ukamilishwaji kama ifuatavyo: Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe ujenzi umefikia asilimia 80; Simiyu (asilimia 70); na Geita (asilimia 94) ambapo baadhi ya huduma katika Hospitali hizi tayari zimeanza kutolewa. Aidha, ujenzi katika Hospitali ya Rufaa ya Songwe umefikia asilimia 80 na Katavi (asilimia 65). Hadi sasa, Jumla ya **Shilingi bilioni 43.616** zimetumika katika ujenzi wa Hospitali hizo.

211. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea na ukarabati na upanuzi wa miradi ya miundombinu ya Hospitali za Rufaa za Mikoa ilizopokea kutoka Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) mwaka 2017. Mikoa yenye miradi ya aina hiyo ni pamoja na; Singida, Mara (Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere), Shinyanga, Manyara, Kilimanjaro (Mawenzi), na Mbeya. Hadi sasa, ujenzi wa Hospitali hizo umefikia hatua mbalimbali za utekelezaji kama ifuatavyo: Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga (asilimia 47), Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara (asilimia 50), Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida (asilimia 40), Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mbeya (asilimia 52), Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara - Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (asilimia 74), na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Kilimanjaro -

Mawenzi(asilimia 70). Utekelezaji wa ukarabati na upanuzi wa miundombinu hiyo umegharimu kiasi cha **Shilingi bilioni 29.63**.

212. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, katika kuimarisha huduma za afya nchini, Serikali imefanya upanuzi wa majengo katika Hospitali ya Sekou Toure – Mwanza, Mwananyamala - Dar es Salaam, Ruvuma, Tanga, Maweni - Kigoma, Sumbawanga (Rukwa) na Dodoma. Hadi sasa, utekelezaji umefikia hatua mbalimbali kama ifuatavyo:Sekou Toure - Mwanza (asilimia 73), Mwananyamala – Dar es Salaam (asilimia 98), Ruvuma (asilimia 45), Bombo - Tanga (asilimia 75) na Maweni - Kigoma - (asilimia 75), Sumbawanga - Rukwa (asilimia 99), Kitete-Tabora (asilimia 70) na Dodoma (asilimia 100). Utekelezaji wa upanuzi miundombinu hii umegharimu kiasi cha **Shilingi bilioni 16.888**.

213. ***Mheshimiwa Spika***, illi kukidhi mahitaji ya huduma za afya kwa wananchi, Serikali imepanua wigo wa huduma za Kibingwa na Ubingwa bobezi kwa kujenga na kufanya upanuzi katika Hospitali tatu za Rufaa za Kanda nchini. Aidha, Hospitali mbili zinazoendelea na ujenzi ni pamoja na Hospitali za Kanda ya Kusini – Mtwara na Hospitali ya Kanda Chato na Hospitali ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini - Mbeya imefanyiwa upanuzi. Ujenzi na upanuzi wa Hospitali hizi umefikia hatua mbalimbali za utekelezaji kama ifuatavyo: Hospitali ya Kanda Kusini – Mtwara (asilimia 90), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini – Mbeya (asilimia 80) na Hospitali ya Kanda Chato awamu ya kwanza imefikia asilimia 98. Utekelezaji wa ujenzi na upanuzi miundombinu ya Hospitali hizi umegharimu kiasi cha **Shilingi bilioni 40.5**.

## UGHARAMIAJI WA HUDUMA ZA AFYA

214. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea na jitihada za kutafuta rasilimali fedha kwa ajili ya kuboresha huduma za afya nchini kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo ikiwemo **Mfuko wa Afya wa Pamoja(Health Basket Fund)**, ambapo kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, kiasi cha **Shilingi 59,025,084,298**kimepokelewa kuititia Mfuko huo

ikilinganishwa na **Shilingi 86,222,819,841** zilizopokelewa katika kipindi kama hicho mwaka 2019/20. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Shilingi 55,854,356,644**sawa na asilimia 95 ya fedha zote zilizopokelewa zilipelekwa na kutumika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa lengo la kuboresha huduma za afya ngazi ya msingi na **Shilingi 3,170,727,654** zilitumika kwa ajili ya kutekeleza majukumu yaliyoko chini ya Wizara.

215. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 22,832,726,265.86**kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya kutekeleza afua mbalimbali katika Sekta ya Afya ikilinganishwa na kiasi cha **Shilingi 25,867,451,925.22** zilizopokelewa kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020. Kati ya fedha hizo kiasi cha **Shilingi 14,172,736,076** ni kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Malipo kwa Ufanisi (Results Based Financing - RBF)ambao ni ubunifu unaolenga kuongeza uwajibikaji wa Watoa huduma za afya pamoja na kuboresha upatikanaji wa rasilimali fedha ili kuboresha upatikanaji na utumiaji wa huduma za Afya nchini.

216. ***Mheshimiwa Spika***,Mfumo wa Bima ya Afya ni mojawapo ya mifumo muhimu ya kuimarisha hifadhi ya jamii kwa kuimarisha uwekezaji katika rasilimali watu. Kwa hivi sasa, jumla ya watananzania 8,224,271 sawa na asilimia 14.7 ya watananzania wote (takriban milioni 59.4) ndiyo wanaonufaika na huduma za bima ya afya. Kati ya wananchi waliojingga na mfumo wa bima ya afya, asilimia 8 wamesajiliwa na NHIF, asilimia 5.4 wanahudumiwa na iCHF, asilimia 0.3 wanufaika na huduma kupita SHIB-NSSF na asilimia 1 wakiwa wamejingga na bima ya afya inayotolewa na makampuni ya bima binafsi za afya. Kwa kutambua kuwa wananchi wengi (takriban asilimia 85.3) wako nje ya mfumo wa bima ya afya, Wizara inaendelea na hatua za maandalizi ya Sheria ya Bima ya Afya kwa wote, ambapo Muswada wa sheria hiyo unatarajiwa kuwasilishwa Bungeni mwezi Juni 2021. Maudhui ya sheria hiyo ni kutoa fursa kwa wananchi wote kupata huduma za afya bila kikwazo cha fedha na hatimaye kulifiki Lengo Na. 3 la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

## RASILIMALI WATU KATIKA SEKTA YA AFYA

217. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na mambo mengine,Wizara inalo jukumu la kusimamia rasilimali watu kwa kuongozwa na misingi ya Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma kama vile Sera ya Menejimenti ya Ajira Katika Utumishi wa Umma Tolea la 2 la mwaka 2008, Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002, Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003, Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2009 pamoja na nyaraka (Circulars) mbalimbali zinazotolewa mara kwa mara.

218. **Mheshimiwa Spika**,katika kuhakikisha Sekta ya Afya inakua na rasilimali watu ya kutosha, Wizara imeendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambapo katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Wizara iliwasilisha ombi la kibali cha kualjiri watumishi 13,301 kwa ajili ya Zahanati, Vituo vya Afya, Hospitali za Wilaya pamoja na Hospitali za Rufaa za Mikoa na Kanda zinazotoa huduma za kibingwa ili kuendelea kupunguza uhaba wa watumishi katika sekta ya afya. Aidha, Wizara imeendelea kusimamia utendaji wa watumishi katika Sekta ya afya kwa kushirikiana na Bodi na Mabaraza ya kitaaluma. Ili Wizara iweze kufikia malengo yake, watumishi wataendelea kuhimizwa kuwa wazalendo, wabunifu wachapa kazi na wenye kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ya afya nchini.

219. **Mheshimiwa Spika**,katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE), ilifanya uchaguzi wa wanafunzi 25,077 sawa na asilimia 57.2 ya wanafunzi 43,835 waliotuma maombi kuijunga na vyuo vya Afya vinavyotoa mafunzo ngazi ya kati. Kati yao wanafunzi 5,682 sawa na asilimia 22.7 walichaguliwa kwenye vyuo vya Serikali vya afya na wanafunzi 19,395 sawa na asilimia 77.3 walichaguliwa kwenye vyuo binafsi na taasisi za dini katika kozi za Uugazi na Ukunga na Sayansi Shirikishi za Afya. Aidha,Wizara iliendesha zoezi la mitihani ya kitaifa kwa wanafunzi wa afya ngazi ya kati nchini wapatao 41,786 katika vyuo 182 vilivyo sajiliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi

(NACTE). Kati ya vyuo hivyo, 45 ni vya Serikali na vyuo 137 ni vya Binafsi.

220. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea na utaratibu wa kuwajengea uwezo watumishi katika Sekta ya Afya, ili kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma za afya nchini. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya watumishi 642 wameendelea kulipiwa gharama za masomo ya uzamili ndani na nje ya nchi. Aidha, watumishi 311 wamepewa udhamini wa kuanza masomo ya uzamili na uzamivu katika mwaka wa masomo wa 2020/21 ikilinganishwa na watumishi 204 waliopewa udhamini mwaka 2019/20. Kati ya watumishi 642 watumishi 19 wanasoma vyuo vya nje ya nchi, na watumishi 623 wanasoma vyuo vya ndani ya nchi. Katika kipindi hicho, jumla ya watumishi bingwa 182 walihitimu mafunzo ya shahada ya uzamili kwa ufadhili wa Serikali.

221. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeandaa mfumo wa mafunzo kwa njia ya masafa (e-Learning Platform) ili usaidie wanafunzi wa afya ngazi ya kati waliopo kwenye vyuo vya mafunzo ya afya na walioko kazini kujisomea na kujijendeleza kitaaluma. Mfumo huu utasaidia kuwabakiza watumishi sehemu za kazi ili waendelee kutoa huduma kwa wananchi pasipo kwenda kujijendeleza vyuoni kwa kipindi kirefu. Hadi kufikia Machi 2021, jumla ya wanafunzi 34,357 wamesajiliwa kwenye mfumo huo, watumishi walioko kazini 11,507 wanajijendeleza kitaaluma (CPD) kupitia mfumo huo.

222. ***Mheshimiwa Spika***, ni dhahiri kuwa, uzalishaji wa rasilimali watu wenye utaalam na sifa stahiki na ambao wameajiriwa haitoshi kumaliza changamoto ya mahitaji ya watumishi. Sehemu nyingine ya changamoto ni jinsi gani watumishi hawa wanafanya kazi kwa tija mahala pa kazi ikiwemo kuzingatia motisha na stahiki zao. Kumekuwa na changamoto ya mifumo dhaifu ya ufuatiliaji wa ufanisi wa watumishi waliopo kiasi kwamba tija inakuwa ndogo kutokana na wachache kuwa wanafanya sehemu kubwa zaidi ambayo ingefanywa na wengi lakini hawatimizi wajibu wao kikamilifu. **Wizara itaimarisha mifumo ya ufuatiliaji wa tija ya watumishi mahala pa kazi ili Taasisi husika ziweze kupandisha viwango vya**

ufanisi na kuvutia wateja. Jambo hili litaenda sambamba na kuwatambua wote wanaofanya kwa tija, kuwawezesha wale wenye uhitaji na pia kuhakikisha watumishi wanapata stahiki zao na motisha kwa wakati kulingana tija aliyochangia mahala pa kazi.

### **MABARAZA YA WANATAALUMA NA BODI ZA USHAURI ZA AFYA**

223. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ina jukumu la kusimamia utendaji wa wataalam wa Sekta ya Afya. Katika kutekeleza hilo, mabaraza na bodi mbalimbali za kitaaluma ziliundwa kisheria kwa ajili ya kusimamia majukumu hayo. Mabaraza na bodi za kitaaluma ni pamoja na: Baraza la Madaktari Tanganyika; Baraza la Afya Mazingira; Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala; Baraza la Uuguzi na Ukunga; Baraza la Famasia, Baraza la Wataalam wa Optometria; Baraza la Wataalam wa Radiologia; Baraza la Wataalam wa Maabara; Bodi ya Maabara Binafsi za Afya (PHLB); na Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Mabaraza na Bodi hizi zimetekeleza majukumu yafuatayo:-

#### **Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC)**

224. ***Mheshimiwa Spika***, Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania lilianzishwa kwa lengo la kusimamia taaluma ya Uuguzi na Ukunga ili kuhakikisha huduma inayotolewa kwa wananchi ni salama na yenye ubora, ikizingatia viwango vinavyokubalika ili kukidhi mahitaji ya jamii. Majukumu ya Baraza ni kusajili, kuorodhesha na kutoa leseni kwa wauguzi na wakunga wenye sifa kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010; Kuishauri Serikali juu ya masuala ya usimamizi, utoaji huduma na mafunzo ya Wauguzi na wakunga nchini, Kusimamia maadili ya wanataaluma; Kukagua na kusajili vituo ninavyotoa huduma binafsi za uuguzi na Ukunga; na Kufanya jukumu lolote litakalohitajika kulingana na Sheria.

225. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Baraza limesajili jumla ya wauguzi na wakunga

3,871 ambapo kati yao, wauguzi wasaidizi ni 303 na maafisa wauguzi ni 3,568 hivyo kufanya jumla ya wauguzi na wakunga wenye usajili na leseni hai 43,000. Jumla ya vyuo vitatu (3) vya mafunzo ya Uuguzi na Ukunga vimesajiliwa katika kipindi cha Julai 2020 mpaka Machi 2021, hivyo kufanya vyuo vinavyotambuliwa na Baraza kufikia 103. Vyuo hivi viko katika mikoa mbalimbali ya Tanzania bara.

226. ***Mheshimiwa Spika***, jumla ya watahiniwa 5,528 ngazi ya shahada, stashahada, astashahada ya Uuguzi na Ukunga kutoka vyuo mbalimbali walifanya mitihani ya usajili na leseni katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021 ikilinganishwa na watahiniwa 6,877 katika kipindi cha mwaka 2019/20. Baraza lilitoa usajili wa awali(provisional registration) kwa Wauguzi na Wakunga 556.

227. ***Mheshimiwa Spika***, Baraza limeendelea kusimamia miiko ya maadili kwa Wauguzi na Wakunga na kuchukua hatua stahiki kwa wanaokwenda kinyume na maadili. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Baraza lilipokea jumla ya mashauri 34 ya tuhuma za ukiukwaji wa maadili, Wauguzi na Wakunga 16 walitiwa hatiani kati yao 13 walipewa onyo,mmoja (1) alisimamishwa kutoa huduma za uuguzi na Ukunga kwa miaka miwili (2), mmoja (1) alifutiwa usajili na kunyang'anywa vyeti na leseni, na mmoja (1) alitenda jinai amefungwa miaka 30.

228. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania litaendelea kufuatilia na kusimamia maadili ya wauguzi na wakunga na kuchukua hatua pale inapobainika wamekwenda kinyume na maadili; kusimamia programu za kuijendeleza kwa watoa huduma kazini *Continuous Professional Development(CPD)* ili kuhakikisha wanataluma wanakuwa na viwango vya kutoa huduma bora; kubuni vyanzo vipyta vya mapato kwa ajili ya kuongeza kipato cha Baraza. Aidha,Baraza itaendelea kuimarisha ufuatiliaji na usimamizi wa huduma za uuguzi na ukunga na ubora wa vyuo vya mafunzo ya uuguzi na ukunga ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo wasimamizi wa mikoa

na wilaya katika kusimamia kazi za Baraza na utoaji wa huduma zenyе ubora.

### **Baraza la Wataalam wa Radiolojia**

229. ***Mheshimiwa Spika***, Baraza la Radiolojia ni chombo kinachosimamia taaluma na huduma za Radiolojia nchini. Majukumu makuu ya Baraza ni: kusajili, kuorodhesha na kuandikisha Wataalam wa Radiolojia nchini; kusimamia na kuweka viwango vya mwenendo na shughuli za Wataalam wa Radiolojia; na kukuza maslahi na maendeleo ya taaluma kwa Wataalam wa Radiolojia.

230. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Baraza la Wataalam wa Radiolojia limesajili jumla ya Wataalam 266 wa kada mbalimbali za Radiolojia na hivyo kufanya liwe na jumla ya Wataalam 1,443 nchini. Baraza linavitambua Vyuo vinne (4) vinavyozalisha Wataalam wa Radiolojia katika viwango tofauti vya elimu. (Diploma, Advanced Diploma, Shahada ya kwanza na Shahada ya uzamili).

231. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi husika, jumla ya wanafunzi 118 walihitimu mitihani ya vyuo ambapo jumla ya Wahitimu 28 wa Shahada ya Radiotherapy walipangiriwa kufanya mafunzo ya Utarajali katika vituo mbalimbali. Baraza liliendelea kuwasimamia kwa kuwapa miongozo ya Utarajali, miiko na maadili, kufuatilia mienendo na utendaji wao.

232. ***Mheshimiwa Spika***, Baraza limekuwa likifuatilia mwenendo wa Wataalam wa Radiolojia na kutoa elimu juu ya miiko na maadili kuititia semina, mikutano, makongamano na mitandao ya jamii. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Baraza limepokea jumla ya taarifa nne (4) za Wataalam waliofanya uvunjifu wa maadili. Kati yao wawili kesi zao zilipelekwa mahakamani, mmoja suala lake lilipelekwa Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa na mmoja (1) suala lake lilihughulikiwa na Baraza ambapo Baraza liliifikia maamuzi ya kumfutia usajili.

233. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2021/22 Baraza la Wataalam wa Radiolojia limepanga kutekeleza kazi zifuatazo: Kuandaa na kufanya vikao vyaa kisheria vya Baraza; kufanya ukaguzi shirkishi katika vyuo, Hospitali na vituo vinavyotoa huduma za Radiolojia; kupokea na kuwapangia vituo Watarajali; kukamilisha mpango mkakati wa mwaka 2022 - 2027.

### **Baraza la Wataalam wa Optometria**

234. ***Mheshimiwa Spika***, Baraza lilianzishwa kwa lengo kuu la kusimamia upatikanaji wa huduma bora za Optometria kwa wananchi katika ngazi zote. Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2021 Wataalam wa Optometria Watatu (3) walisajiliwa na hivyo kufanya jumla ya Wataalam waliosajiliwa na baraza hadi kufikia Machi 2021 kuwa 345. Baraza linavitambua na kusimamia vyuo viwili (2) na katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021 Baraza halikufanya usajili mpya wa chuo. Jumla ya wanafunzi 17 walihitimu katika fani ya Optometria na liliwasimamia kwa vitendo kazini.

235. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2021/22, baraza la wataalam wa optometria litaendelea kusajili wataalam wa baraza; litasimamia na kuratibu utoaji huduma; na litaendelea kufuatilia ukiukwaji wa maadili katika vituo.

### **Baraza la Wataalam wa Maabara**

236. ***Mheshimiwa Spika***, Baraza la Wataalam wa Maabara liliundwa kwa lengo la kuweka utaratibu wa kusajili na kusimamia Wataalam wa Maabara za Afya ya Binadamu na masuala mengine yanayohusiana na hayo.

237. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya Wataalam waliosajiliwa na Baraza la Wataalam wa Maabara kwa usajili wa kudumu ni 822, usajili wa Awali ni 1,297 na walioandikishwa ni 578. Jumla ya Wataalam wa Maabara waliosajiliwa hadi Machi 2021, ni 12,992. Baraza la Wataalam wa Maabara linavitambua vyuo

48 vinyavyotoa Mafunzo ya Maabara kwenye Mikoa mbalimbali, vikiwemo vyuo Vikuu sita (6) na Vyuo vya kati 42. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya Vyuo vinne (4) vilisajiliwa na Baraza. Baraza liliendesha mitihani kwa Wataalam wa Maabara katika ngazi zote ambapo jumla ya Wataalam 2,585 walitahiniwa. Kati yao 1,917 (74%) walifaulu. Katika kuhakikisha usimamizi unaimarishwa, Baraza liliandika Barua ya kuhimiza Waganga Wafawidhi wa vituo kuhakikisha usimamizi wa watarajali unafanyika kikamilifu na taarifa iwe inawasilishwa Baraza kila mwezi ikielezea pia mienendo ya maadili ya Watarajali.

238. ***Mheshimiwa Spika***, Baraza limeshughulikia mashauri kumi na mbili (12) ya ukiukwaji wa maadili. Kati ya mashauri hayo, Watarajali wawili (2) walipewa onyo na kuruhusiwa kuendelea na mafunzo kwa gharama zao, Wataalam sita (6) walipelekwa TAKUKURU, Mtaalam mmoja (1) amesimamishwa kufanya kazi za taaluma kwa kipindi cha mwaka mmoja (1), Mtaalam mmoja (1) shauri lake linaendelea kusikilizwa na Wataalam wawili (2) wapo kwenye hatua ya uchunguzi wa awali.

239. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Baraza litaandaa viashiria vya utendaji na mwongozo wa kusimamia utekelezaji wake kwa Wataalam wa Maabara za Afya; kukusanya maoni kutoka kwa wadau kwa ajili ya kufanya mapitio ya Sheria ya Wataalam wa Maabara; kuendelea kupokea maombi, kusajili na kuhuisha rejesta ya Wataalam wa Maabara; kuwajengea uwezo Waratibu wa Mikoa kwenye kusimamia utekelezaji wa *Continous Professional Development(CPD)* na kuwajengea uwezo wa kufanya usimamizi shirkishi Waratibu wa Mikoa; kuandaa viwango vya kuanzisha vyuo vya taaluma ya Maabara; kufanya ukaguzi maalum kwa vyuo vyote vinyavyotoa taaluma ya Maabara nchini; na kuandaa na kuendesha mitihani ya usajili kwa Wataalam wa Maabara.

### **Baraza la Wataalam wa Afya ya Mazingira**

240. ***Mheshimiwa Spika***, Baraza la Kusajili Wataalam wa Afya Mazingira lilianzishwa kwa lengo kuu la kusajili Wataalam wa

Afy Mazingira ili kulinda nidhamu na maadili katika Taaluma ya Afya Mazingira. Baraza lina mamlaka ya kuendesha uchunguzi na kumshitaki mwanataaluma na hata kumfutia usajili endapo atabainika kukiuka misingi ya kada.

241. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Baraza lilitisajili Wataalam wapya wa Afya Mazingira 189 na jumla ya Wataalam wa Afya Mazingira waliosajiliwa na Baraza toka kuanzishwa kwake hadi kufikia Machi, 2021 ni 3,478. Baraza linadhibiti ubora wa utoaji wa mafunzo katika Vyuo Viwili (2) vya Shahada (Degree), Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili na Chuo cha Kikatoliki Ruaha. Kwa upande wa Stashahada kuna Vyuo 6 ambavyo ni Kagemu, Muheza, Ngudu, Mpwapwa, RUCU na MUHAS. Baraza la Afya ya Mazingiraliiratibu mafunzo ya vitendo kwa watarajali 64.

242. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2021/22 Baraza limepanga kuanzisha mfumo wa kielectroniki wa usajili (Online system) na tovuti ya Baraza kwa lengo la kuboresha ufanisi; kuchapisha na kusambaza kwa wadau wote *Code of Ethics* ambayo ni mwongozo wa maadili ya wanataaluma; kukamilisha kanuni tatu za mafunzo, matumizi ya fedha na mwenendo wa mashitaka ili kuongeza ufanisi wa shughuli za Baraza; kukamilisha muongozo wa Elimu ya kujiendeleza (CPD) kwa wanataaluma ili kuongeza umakini na ufanisi katika utendaji wao wa kazi; na kuvikagua mara kwa mara vituo vya mafunzo ya vitendo kwa watarajali ili kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa yanakidhi viwango vinavyo kubalika.

### **Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala**

243. ***Mheshimiwa Spika***, Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala lilianzishwa kwa lengo la kusimamia, kudhibiti na kuendeleza Tiba Asili na Tiba Mbadalanchini. Baraza lina majukumu makuu ya kulinda na kusimamia maadili ya Wataalam wa Tiba Asili kupitia; usajili wa Waganga wa Tiba Asili na Tiba Mbadala, Wasaidizi wa Waganga, usajili wa dawa za asili pamoja na usajili wa vituo vya kutolea huduma za Tiba Asili na maduka ya dawa asili.

244. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Baraza lilsajili jumla ya Wataalam 2,037 na kufanya jumla ya wataalam waliosajiliwa na Baraza kuwa 26,853. Aidha, katika kusimamia maadili ya wataalam wa Tiba Asili na Tiba Mbadala, Baraza lilipokea tuhuma za uvunjifu wa maadili manne (4) ya Waganga wa Tiba Asili; wawili (2) walipewa onyo na elimu na wawili (2) walitozwa faini na kupatiwa elimu.

245. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Baraza liliweza kusajili jumla ya Dawa za Tiba Asili 17 ikilinganishwa na dawa 10 mwaka 2019/20. Hivyo hadi sasa kuna jumla ya Dawa Tiba Asili 49 zinazotambuliwa na Baraza. Aidha, jumla ya Kliniki za Tiba Asili na Tiba Mbadala 247 zilisajiliwa na kupewa leseni hivyo kuwa na jumla ya Kliniki 1,003 nchi nzima. Vilevile, jumla ya Wataalam wa Tiba Asili na Tiba Mbadala 228 walipewa elimu na kuhamasishwa kusajili dawa zao.

246. ***Mheshimiwa Spika***,kazi zilizopangwa kufanyika kwa mwaka 2021/22 ni pamoja na; usajili wa wataalam wa Tiba Asili na Tiba Mbadala, maduka na vituo vya kutolea huduma; kuititia na kuboresha sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ambayo hutumika kutoa mafunzo na maelekezo muhimu juu ya Tiba Asili na Tiba Mbadala kitaaluma na kiutendaji; kuimarisha ufuatililaji na usimamizi wa huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala ikiwa ni pamoja na: kuwajengea uwezo Waratibu wa mikoa na wilaya katika kusimamia kazi za Baraza; kufanya ukaguzi katika maduka na vituo vya kutolea huduma na maeneo ya kutengenezea dawa asili; na kuendelea kufanya uhamasishaji wa usajili wa Waganga wa Tiba Asili na Tiba Mbadala, vituo vya kutolea huduma pamoja na dawa za asili.

### **Baraza la Famasi**

247. ***Mheshimiwa Spika***,Lengo kuu la kuanzishwa kwa Baraza la Famasi ni kusimamia taaluma ya famasi na kudhibiti ubora wa huduma za dawa zinazotolewa kwa jamii kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo. Majukumu makuu ya

Baraza ni kusajili wanataaluma wote wa kada ya famasi na kusimamia ubora wa majengo ya kutunzia na kuuzia dawa ziklwemo famasi za jumla, rejareja na Maduka ya Dawa Muhimu.

248. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Baraza lilisajili Wataalam wa famasi 475 na hivyo kufanya jumla ya Wataalam waliosajiliwa na Baraza kufikia 6,231. Katika kipindi hicho Baraza lilisajili vyuo 13 na hivyo kufanya vyuo vyote vilivyosajiriwa na Baraza kufikia 52. Aidha, jumla ya watahiniwa 882 walifanya mitihani ambapo 616 (75.7%) walifaalu mitihani hiyo. Katika kipindi hicho, Baraza lilisimamia mafunzo kwa vitendo kwa watarajali 535 waliopangiwa kufanya mafunzo kwa vitendo.

249. ***Mheshimiwa Spika***, katika kusimamia Miiko na maadili ya kazi, Baraza liliopokea mashauri ya kitaaluma 52 waliolalamikiwa kukiuka miiko na maadili ya kitaaluma kutoka katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya. Wanataaluma 19 wenye makosa waliitwa katika Kamati ya nidhamu na maazimio ya kamati ya nidhamu yatatolewa. Uchunguzi kwa wanataaluma 33 bado unaendelea na taratibu stahiki za kinidhamu zitachukuliwa baada ya hatua za uchunguzi kukamilika.

250. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2021/22 Baraza la Famasi litafanya mapitio ya mitaala ya kozi ya famasi katika ngazi ya NTA L4-6 ili mafunzo yatakayotolewa yaendane na mahitaji ya sasa. Aidha, Baraza katika kuunga mkono juhudhi za upatikanaji wa dawa katika hospitali za rufaa za mikoa, limejikita katika kuwajengea uwezo wafamasia na fundi dawa wa hospitali za rufaa za mikoa 28 kwa kuwapatia mafunzo ya utengenezaji wa dawa kwa kutumia utaalam uliopo katika Chuo cha *Kilimanjaro School of Pharmacy*. Baraza litaendelea kushirikiana na Mabaraza mengine ya taaluma kufanya usimamizi shirikishi katika vituo vya mafunzo kwa vitendo na kusimamia utendaji kazi wa wafamasia katika maeneo yao ya kutolea huduma ili kupunguza kero za wananchi dhidi ya huduma zitolewazo na kushughulikia mmomonyoko wa maadili ya taaluma.

## Baraza la Madaktari Tanganyika

251. ***Mheshimiwa spika***, Baraza la Madaktari Tanganyika lilianzishwa kwa lengo la kuhakikisha kuwa jamii inapata huduma salama na bora kutoka kwa wanataaluma. Kwa msingi huo, Baraza lina wajibu wa kuhakikisha kuwa wataalam wanatenda kazi kwa kuzingatia mwenendo na maadili ya kitaaluma. Baraza linashughulika na ufuutiliaji wa maadili ya kitaaluma ikiwamo kuhakikisha usajili kwa kada za Madaktari, Madaktari wa Meno, Madaktari Wasaidizi, Madaktari wa Meno Wasaidizi, Matabibu, Matabibu Wasaidizi, Wataalam Wazoeza Viungo, Wataalam wa Tiba kwa vitendo (Occupational Therapists), Wataalam wa afya ya akili wasaidizi (Mental health and rehabilitation officers) na wataalam wa tiba ya matatizo ya kuongea (speech therapists).

252. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia mwezi Machi 2021, Baraza llilikuwa na jumla ya wataalam wapya 15,248 ambapo limetoa usajili wa awali kwa wataalam 2,730; usajili wa kudumu 1,456; waliohuisha leseni 1,112; ngazi ya cheti 66; ngazi ya astashahada 1,637; usajili wa muda kwa wataalam wa nje ya nchi 149; usajili wa muda kwa wataalam wa ndani 69 na usajili wa vyeti vya utendaji wenye maadili 41.

253. ***Mheshimiwa Spika***, Baraza limeandaa muongozo wa mitihani kwa wataalam waliomaliza mafunzo ya utarajali na limeweza kutunga na kutoa mitihani kwa watarajali wote waliomaliza mafunzo yao mwaka 2019/20. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2020/21, Baraza limesajili watarajali (interns) 2,732 kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo. Vilevile, Baraza limefanya maboresho ya mfumo wa kielektroniki wa usajili wa wanataaluma ili kuwezesha wanataaluma kujisajili kwa urahisi. Katika kipindi Julai 2020 hadi Machi 2021, Baraza limefanya ufuutiliaji pamoja na kuendesha mafunzo kwa vitendo kwa madaktari katika Mikoa ya Mwanza, Mara, Kagera, Tabora, Ruvuma, Simiyu na Geita kwa lengo la kuhamasisha weledi wa taaluma katika utoaji wa huduma ili kupunguza malalamiko. Katika kusimamia maadili ya

Madaktari, Baraza lilipokea mashauri ya tuhuma 13 ambayo yalisikilizwa na kamati maalum na kisha kufanyiwa kazi.

254. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Baraza la Madaktari Tanganyika litaendelea kupokea, kusikiliza na kuwasilisha mashauri mbalimbali kwenye kikao cha Baraza; kutengeneza na kijiungu na Mfumo wa Uhasibu Serikalini (MUSE); kuratibu uandaaji, usimamizi na usahishaji wa mitihani (Post Internship Examinations); kusimamia mafunzo ya wanataaluma kwa kukagua vyuo vinavyotoa mafunzo na vituo vya mafunzo ya utarajali; kukagua vituo vya kutolea huduma ili kujiridhisha na ubora wa huduma zinazotolewa na kutoa mapendekizo pindi upungufu unapobainika.

### **Bodi ya Maabara Binafsi za Afya**

255. ***Mheshimiwa Spika***, Bodi ilianzishwa kwa Sheria ya kuratibu huduma za Maabara Binafsi za Afya. Majukumu ya Bodi ni pamoja na usajili wa maabara binafsi za Afya; kuandikisha Maabara zote Binafsi zilizoshikizwa kwenye Vituo Binafsi vya kutolea huduma za tiba nchini; kusimamia ubora na usalama wa majengo, miundombinu na majibu ya vipimo vya maabara; na ukaguzi na usimamizi shirkishi wa Maabara Binafsi za Afya baada ya kusajiliwa ili kuhakikisha ubora wa huduma za Maabara zinaboreshwila kila wakati.

256. ***Mheshimiwa Spika***, kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Bodi ya Maabara Binafsi za Afya iliweza kusajili maabara binafsi zipatazo 175 zikiwemo Maabara zinazojishikiza (attached) 74 na maabara zinazojitegemea (autonomous) 101 hivyo kufanya kuwa na jumla ya maabara zinazotambuliwa kufikia 2,513. Katika kusimamia maadili ya utoaji wa huduma za Maabara Binafsi za Afya, Bodi lilipokea tuhuma mbili (2) moja kutoka mkoani Kagera na nyingine Dodoma ambapo Bodi ilisitisha leseni za utoaji huduma za maabara hizo hadi zitakapoweza kufanya maboresho pamoja na kuzingatia kanuni za ubora wa huduma za maabara.

257. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Bodi iliweza kufanya kaguzi katika mikoa minne (4) ya Dar es Salaam, Arusha, Kagera na Morogoro ambapo maabara 556 zilikaguliwa. Kupitia kaguzi hizo, maabara 68 zilikutwa na changamoto na kufungiwa. Kupitia kaguzi hizo Bodi iliweza kupata fursa ya kutoa elimu kwa wamiliki na watendaji wote katika maabara 556 zilizotembelewa kuhusu namna bora ya kuboresha utendaji wao.

258. ***Mheshimiwa Spika***, kazi zilizopangwa kutekelezwa katika kipindi cha mwaka 2020/21 ni kama ifuatavyo:-

(i) Kufanya tathmini ya Mpango Mkakati wa Bodi wa mwaka (2016/17 - 2021/22);

(ii) Kufanya mapitio ya Sheria Na.10 ya mwaka 1997 ya Bodi ya Maabara Binafsi za Afya;

(iii) Kuendelea kuweka na kutekeleza mikakati ya kuhakikisha huduma bora zinatolewa kwenye maabara binafsi za afya kwa kuendelea kutoa elimu kwa wamiliki wa maabara binafsi;

(iv) Kufanya kaguzi kwenye maabara binafsi nchini; na

(v) Kuendelea kushirikiana na Taasisi nyingine na kusambaza sampuli za nje za uhakiki ubora (External Quality Assurance).

#### **Bodi ya Hospitali za Watu Binafsi**

259. ***Mheshimiwa Spika***,lengo kuu la kuanzishwa kwa Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi ni kusimamia na kudhibiti hospitali binafsi ambazo zinasimamiwa na watu au mashirika yaliyoidhinishwa pamoja na utendaji wao ili kuhakikisha jamii inapata huduma za afya bora nchini. Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi ina majukumu makuu ya kuchambua, kuamua na kumshauri Waziri kuhusu maombi ya vibali vyta kufungua hospitali yaliyowasilishwa; kuhifadhi na kuhuishwa rejista ya vituo vilivyosajiliwa.

260. ***Mheshimiwa Spika***,katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi imefanikiwa

kusajili vituo vipatavyo 152 ikiwa ni pamoja na hospitali moja (1) ya ngazi ya Mkao, ngazi ya Halmashauri (9), vituo vya afya vitano (5), zahanati 66, kliniki nane (8), kliniki Maalum moja (1), kliniki tisa (9) za huduma za kibingwa, *Polyclinic* (33), fiziotherapia (2), kliniki ya macho viwili (2), kliniki za kinywa na meno8, vituo vya uchunguziviwili (2), vituo vya kusafisha damu vitano (5) na kliniki moja ya afya ya akili. Hadi kufikia Machi 2021, jumla ya Vituo vya Kutolea Huduma za Afya Binafsi 2,849vimesajiliwa.

261. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Bodi iliweza kufanya kaguzi katika Mikoa Sita (6) ambayo ni Morogoro, Dar es Salaam, Ruvuma, Tanga, Kilimanjaro na Arusha ambapo jumla ya vituo vya kutolea huduma 183 vilikaguliwa ambapo vituo 23 vilibainika kuwa na dosari. Kupitia kaguzi hizo Bodi iliweza kupata fursa ya kutoa elimu kwa wamiliki na watendaji wa vituo vyote 183 vilivyokaguliwa kuhusu namna bora ya kuboresha utendaji wao.

262. ***Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi cha mwaka 2021/22, Bodi itafanya yafuatayo:-

- (i) Kufanya ukaguzi shirikishi na kutoa elimu juu ya Sheria, Kanuni na miongozo ya Hospitali Binafsi katika Hospitali Binafsi zilizoomba usajili;
- (ii) Kutatua malalamiko ya wagonjwa katika Hospitali Binafsi;
- (iii) Kufuatilia madeni ya Kitengo kwa kushirikiana na Waratibu wa PHAB katika ngazi za Mikoa na Wilaya; na
- (iv) Kupokea maombi mapya ya Hospitali Binafsi na Kampuni/Taasisi za Dini/Asasi Zisizo za Kiserikali zinazoomba kuidhinishwa kusimamia na kuendesha huduma za afya nchini.

263. ***Mheshimiwa Spika***, Mabaraza na Bodi hizi ni vyombo muhimu katika usimamizi wa utekelezaji wa masuala ya miiko, tamaduni na maendeleo ya kitaaluma jambo linalochangia kwenye kufikia kutoa huduma bora na salama kwa wateja

wetu. Hata hivyo, ili kuongeza ufanisi wa uratibu na kupunguza gharama za uendeshaji, Wizara imechukua mwelekeo wa kuboresha muundo wa uendeshaji ili kuongeza kasi ya kufikia malengo ya kisekta na kazi hii inaendelea.

#### **UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI CHINI YA IDARA KUU YA AFYA (FUNGU 52)**

##### **Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)**

264. ***Mheshimiwa Spika***, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya una majukumu ya kuandikisha waajiri na wanachama, kukusanya michango, kusajili vituo vya huduma na kuhakiki ubora wa huduma zitolewazo, kufanya uwekezaji wa muda mfupi, malipo kwa watoa huduma, kutoa elimu kwa Umma na kufanya tathmini ya Uhai na Uendelevu wa Mfuko.

265. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Mfuko ulikuwa na lengo la kusajili wanachama wapya 413,368. Mfuko ulifanikiwa kusajili wanachama wapya 418,972 sawa na asilimia 101 ya lengo ikilinganishwa na wanachama 338,236 mwaka 2019/20. Katika kipindi husika Mfuko ulikuwa na wanachama 1,127,956 na wanufaika 4,341,993 sawa na asilimia 8 ya Watanzania wote ikilinganishwa na wanachama 1,050,493 na wanufaika 4,102,144 mwaka 2019/20. Mfuko umeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ili kuweza kufikia lengo ikiwa ni pamoja na juhudzi za kutoa elimu ya dhana ya bima ya afya na umuhimu wa kujinga na bima ya afya.

266. ***Mheshimiwa Spika***, Mfuko umeendelea kuongeza mtandao zaidi wa vituo vya kutolea huduma ambapo hadi Machi 2021 ulikuwa umesajili vituo 9,152 vya kutolea huduma za matibabu katika ngazi mbalimbali mijini na vijijini ili kutoa huduma kwa wanachama na wanufaika ikilinganishwa na vituo 7,940 viliviyosajiliwa mwaka 2019/20. Kati ya vituo hivyo, vituo 6,292 sawa na asilimia 69 vinamilikiwa na Serikali, vituo 909 sawa na asilimia 10 ni vya Mashirika ya Dinina vituo 1,951 sawa na asilimia 21 vinamilikiwa na watu binafsi.

267. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa mapato, mfuko umeendelea na jithada za ukusanyaji kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwepo michango ya wanachama na waajiri, ambapo katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Mfuko ulikuwa na lengo la kukusanya **Shilingi bilioni 396.17** ikiwa ni michango kutoka kwa wanachama ambapo kiasi cha **Shilingi bilioni 372.55** kilikusanya ambayo ni sawa na asilimia 94 ya lengo ikilinganishwa na makusanyo ya **Shilingi bilioni 310.77** mwaka 2019/20. Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya kiasi cha **Shilingi bilioni 365.68** kililipwa kwa vituo vilivyosajiliwa na Mfuko kutoa huduma za afya. Katika malipo hayo, asilimia 33 ililiipwa kwenye Vituo vya Serikali, asilimia 29 kwenye vituo vinavyomilikiwa na Mashirika ya Dini na asilimia 38 kwa Vituo Binafsi, ikilinganishwa na asilimia 35 iliyolipwa kwenye vituo vya Serikali, asilimia 29 kwenye vituo vinavyomilikiwa na Mashirika ya Dini na asilimia 36 kwenye Vituo Binafsi mwaka 2019/20.

268. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na majukumu mengine, Mfuko una jukumu la kuchangia katika uboreshaji wa huduma za matibabu nchini. Maboresho hayo hufanyika kupitia utoaji wa mikopo nafuu ya vifaa tiba, dawa na ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za Afya. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya **Shilingi bilioni 1.29** zilitolewa kwa vituo 28 vilivyokidhi vigezo ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 3.57** zilizotolewa kwa vituo 33 vilivyokidhi vigezo mwaka 2019/20. Utaratibu huu umesaidia kujenga uwezo wa vituo katika kutoa huduma za afya kwa wanachama na wananchi kwa ujumla. **Nitoe rai kwa vituo vya kutolea huduma za afya nchini hasa vinavyomilikiwa na Serikali kutumia fursa hii ya mikopo katika kuboresha upatikanaji wa huduma za matibabu kwa wananchi.**

269. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendeleza harakati za uboreshaji wa ufanisi wa utoaji huduma kwa wateja, Mfuko umeanzisha Mfumo wa Uwasilishaji na Uchakataji wa Madai kwa njia ya Kielectroniki kwa lengo la kuhakikisha madai ya watoa huduma yanalipwa kwa wakati. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, mfuko umelipa madai kwa wastani wa siku 46 ambazo ni ndani ya matakwa ya Sheria,

lengo ni kufikia wastani wa siku 30. Maboresho haya yataendelea kufanyika na hatimaye kuvifikia vituo vyote vilivyojiliwa na Mfuko. Aidha, Mfuko unaendelea kufanya kagazi za mara kwa mara katika vituo vya kutolea huduma kwa lengo kusimamia ubora wa huduma na kutoa elimu na miongozo mbalimbali ya tiba inayotolewa na Serikali. Vilevile, ili kuhamkisha Mfuko unakuwa endelevu utaendelea kufuata mapendekezo yanayotolewa na Taarifa ya Tathmini ya Uhai na Uendelevu wa Mfuko (actuarial valuation).

270. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/22, mfuko umepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

- (i) Kuongeza wigo wa wanachama kwa kutekeleza mkakati wa masoko;
- (ii) Kubuni na kuanzisha vifurushi vya bima ya afya ikiwemo kifurushi cha Wageni wanaoingia nchini;
- (iii) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika shughuli za Mfuko;
- (iv) Kuimarisha mfumo wa huduma kwa wateja na kuendelea kufanya tathmini ya hali ya kuridhika kwa huduma zitolewazo;
- (v) Kufanya maboresho katika kitita cha mafao yatolewayo kwa wanufaika;
- (vi) Kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora kwa wanachama kwa kusimamia utekelezaji wa miongozo mbalimbali ya tiba;
- (vii) Kuendelea kuwekeza katika maeneo yenye tija katika Sekta ya Afya;
- (viii) Kuendelea kutoa mikopo ya vifaa tiba, dawa na ukarabati wa vituo kwa lengo la kuboresha huduma za matibabu kwa wanachama na wananchi kwa ujumla; na
- (ix) Kujenga uwezo wa watumishi wa Mfuko.

## Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba(TMDA)

271. ***Mheshimiwa Spika***, Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ni Taasisi iliyo chini ya Wizara ambayo inashughulika na udhibiti wa utengenezaji, uingizaji, usambazaji na uuzaaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi. Mamlaka pia hushughulika na ukaguzi wa viwanda vya utengenezaji dawa na maeneo ya kuhifadhia, kusambaza na kuuzia bidhaa zinazodhibitiwa na Mamlaka ili kuhahikisha vigezo vilivyowekwa vinafikiwa. Aidha, Mamlaka hufanya tathmini na kusajili bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi ili kuhakikisha zinakidhi vigezo vinavyotakiwa kabla ya kuruhusiwa kwenye soko. Vilevile, Mamlaka ina jukumu la kutoa vibali vya kuendeshea biashara za bidhaa inazozidhibiti, kufanya uchunguzi wa kimaabara kwa lengo la kuhakiki usalama na ubora wa bidhaa zinazodhibitiwa.

272. ***Mheshimiwa Spika***, Majukumu mengine ya Mamlaka ni pamoja na kufuatilia katika masoko ya bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi, kukusanya taarifa na kutathmini madhara yatokanayo na matumizi ya dawa na kuchukua hatua stahiki; kuhamasisha matumizi sahihi ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi na kuelimisha na kutoa taarifa sahihi kwa wadau na wananchi kwa ujumla juu ya bidhaa zinazothibitiwa na Mamlaka. Majukumu yote haya yamelenga katika kuongeza tija na ufanisi katika udhibiti wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi ili kulinda afya ya jami.

273. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya maombi 921 ya usajili wa dawa za binadamu yalipokelewa na kufanyiwa tathmini na Mamlaka, ambapo maombi mapya 438 yaliidhinishwa na maombi 464 yalihuishwa. Aidha, maombi 19 hayakukidhi vigezo na wahusika wamejulishwa ili waweze kufanya maboresho. Vilevile, Mamlaka ilipokea maombi 296 ya usajili wa vifaa tiba na kufanyiwa tathmini ambapo maombi mapya yaliyokidhi vigezo na kuidhinishwa yalikuwa 165 na maombi 110 yalikuwa ya kuhuisha. Jumla ya maombi 21 hayakukidhi vigezo na wahusika wamejulishwa. Mamlaka ilipokea maombi 103 ya usajili wa dawa za mifugo ambapo maombi 45 yalikidhi

vigezo na kusajiliwa na maombi 27 yalihuishwa. Jumla ya maombi 31 hayakukidhi vigezo na wahusika wamejulishwa ili kuyafanyia maboresho.

274. ***Mheshimiwa Spika***, Mamlaka ilifanyia kazi maombi yote 1,102 yaliyopokelewa ya usajili wa maeneo ya biashara za dawa, vifaa tiba na vitendanishi, ambapo maeneo 997 sawa na asilimia 90 yalikidhi vigezo, kusajiliwa na kupewa vibali vyta kuanza biashara za bidhaa hizo. Maombi yote ambayo hayakukidhi vigezo, wahusika walijulishwa ili waweweze kufanya maboresho. Aidha, jumla ya sampuli 2,398 za bidhaa za dawa zilipokelewa, ambapo sampuli 2,321 zilichunguzwa kwenye maabara za TMDA na sampuli 77 bado zinaendelea kufanyiwa uchunguzi. Kati ya sampuli zilizochunguzwa sampuli 2,226 sawa na asilimia 96 zilikidhi vigezo. Vifaa tiba vilivyopokelewa vilikuwa 463 na vifaa 428 vilichunguzwa ambapo vifaa tiba 316 sawa na asilimia 74 ya vilivyochanguzwa vilikidhi vigezo. Aidha, vifa tiba 35 vinaendelea kufanyiwa uchunguzi. Kwa upande wa vitendanishi jumla ya sampuli 288 zilipokelewa, sampuli 286 zilichunguzwa ambapo sampuli 285 sawa na asilimia 99 zilikidhi vigezo. Jumla ya sampuli 115 za vipukusi zilipokelewa ambapo sampuli 70 zilichunguzwa na sampuli 55 sawa na asilimia 79 zilikidhi vigezo. Bidhaa ambazo sampuli zake hazikukidhi vigezo hazikusajiliwa na nyingine kuondolewa kwenye soko kwa njia ya ukaguzi.

275. ***Mheshimiwa Spika***, kila mwaka Mamlaka hufanya ukaguzi wa viwanda vinavyozalisha dawa vyta ndani na nje ya nchi. Hadi kufikia Machi 2021, jumla ya viwanda viwili (2) vyta dawa ndani ya nchi vilikaguliwa. Lengo la ukaguzi katika viwanda ilikuwa ni kufuatilia utekelezaji wa marekebisho yaliyoelekezwa awali na wakaguzi. Katika ujenzi wa viwanda, TMDA hutoa msaada wa kiufundi kwa wamiliki na kuwaelekeza vizuri namna ya kujenga viwanda ili viweze kukidhi matakwa ya Utengenezaji Bora wa Dawa (Good Manufacturing Practices - GMP).

276. ***Mheshimiwa Spika***, jumla ya maeneo ya biashara za dawa, vifaa tiba na vitendanishi 2,628 yalikaguliwa ambapo

2,039 yalikidhidhi vigezo sawa na asilimia 78. Vilevile, jumla ya maombi 9,070 ya kuingiza nchini bidhaa za dawa, vifaa tiba, vitendanishi na malighafi za kutengeneza dawa yalipokelewa ambapo maombi 8,428 sawa na asilimia 93 yaliidhinishwa. Pia maombi 389 ya kusafirisha bidhaa nje ya nchi yalipokelewa ambapo maombi 350 sawa na asilimia 90 yaliidhinishwa. Maombi ya kuingiza bidhaa za dawa, vifaa tiba, vitendanishi na malighafi za kutengeneza dawa yaliyoidhinishwa ni ongezeko la maombi 5,557 ikilinganishwa na maombi 2,851 yaliyoidhinishwa katika kipindi kama hiki mwaka 2019/20. Aidha, maombi ya kusafirisha bidhaa nje ya nchi yaliyoidhinishwa ni ongezeko la maombi 187 ikilinganishwa na maombi 163 yaliyoidhinishwa katika kipindi kama hiki mwaka 2019/20. Maombi yote ambayo hayakukidhi vigezo wahusika walijulishwa ili waweze kufanya marekebisho.

277. ***Mheshimiwa Spika***, katika kulinda afya za watumiaji, Mamlaka ilisimamia uteketezaji wa jumla ya tani 5.7 zenye thamani ya takriban **Shilingi bilioni 2.04** za bidhaa zisizofaa kwa matumizi ya binadamu. Aidha, tani za bidhaa zisizofaa zilizoteketezwa zimepungua kwa takriban tani 0.8 ikilinganishwa na tani 6.5 katika kipindi kama hiki mwaka 2019/20.

278. ***Mheshimiwa Spika***, Mamlaka itaendelea kuhakikisha inatoa huduma bora ambapo katika kipindi cha mwaka 2021/22 kazi zifuatazo zitatekelezwa:-

(i) Kufanya ukaguzi wa viwanda vya utengenezaji na maeneo ya biashara yakiwemo ya kuhifadhia, kusambaza na kuuzia dawa, vifaa tiba na vitendanishi ili kuhahikisha vigezo vilivyowekwa vinafikiwa;

(ii) Kutathmini na kusajili bidhaa za dawa, vifaa tiba, vitendanishi na vipukusi ili kuhahikisha zinakidhi vigezo vinavyotakiwa kwa mujibu wa sheria kabla ya kuruhusiwa kuingia sokoni;

- (iii) Kufanya uchunguzi wa kimaabara wa sampuli za dawa, vifaa tiba, vitendanishi na vipukusi ili kuhakiki usalama na ubora wa bidhaa hizo;
- (iv) Kuanzisha maabara maalum Dodoma ya kuchunguza dawa za mitishamba;
- (v) Kutoa vibali vya kuingiza nchini na kusafirisha nje ya nchi dawa, vifaa tiba, vitendanishi na vipukusi,
- (vi) Kusajili na kutoa vibali vya biashara za bidhaa zinazodhibitiwa na Mamlaka;
- (vii) Kufanya ukaguzi wa bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi na pia kukusanya taarifa na kutathmini madhara yatokanayo na matumizi ya dawa na kuchukua hatua stahiki; na
- (viii) Kuendelea kuelimisha na kutoa elimu sahihi kwa wadau na wananchi kwa ujumla juu ya bidhaa zinazothibitiwa na Mamlaka.

#### **Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA)**

279. *Mheshimiwa Spika*,Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ina majukumu ya kufanya uchunguzi wa kimaabara kwa sampuli/vielelezo mbalimbali; kutoa ushahidi wa kitaalam kwenye mahakama zote nchini kutookana na taarifa ya matokeo ya uchunguzi wa kimaabara; kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi na Udhhibit wa Kemikali za Viwandani na Majumbani Sura 182, Sheria ya Udhhibit wa Vinasaba vya Binadamu Sura 73 na Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Na. 8 ya mwaka 2016.

280. *Mheshimiwa Spika*,katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Mamlaka ilipokea jumla ya sampuli 107,963 kati ya sampuli 60,000 zilizotarajiwa kupokelewa kwa ajili ya uchunguzi wa kimaabara ambazo zinajumuisha sampuli za sumu, dawa za kulevyta, mauaji, majanga, ubakaji, utambuzi wa uhalali wa watoto kwa wazazi na jinsi tawala, matibabu

ya wagonjwa wa figo vyakula, dawa za binadamu na mifugo, dawa asili, maji, kemikali, maji taka, na bidhaa nyingine za viwandani. Sampuli zilizochunguzwa ni 105,929 sawa na asilimia 98 ya sampuli zilizopokelewa na sampuli 2,034 zinaendelea kufanyiwa uchunguzi. Aidha, Mamlaka imeendelea kuchangia katika kulinda afya za wananchi na mazingira pamoja na utoaji wa haki katika vyombo vyaa maamuzi kwa kutoa ushahidi wa kitaalam katika mahakama mbalimbali nchini.

281. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha utekelezaji wa majukumu na kutoa huduma bora kwa wananchi, Mamlaka imewawezesha Watumishi 17 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi na watumishi 132 kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi ili kuwaongezea maarifa na ujuzi katika kutekeleza majukumu yao. Mafunzo haya yatawezesha Mamlaka katika kulinda usalama wa nchi, afya na mazingira kwa kuimarisha udhibiti wa kemikali hatarishi, kupitia usajili wa wadau wanaojishughulisha na biashara au matumizi ya kemikali, ukaguzi wa maghala ya kuhifadhia kemikali, utoaji wa vibali vyaa kuingiza au kusafirisha kemikali na kuelimisha Wadau dhidi ya madhara ya kemikali kwa matumizi yasiyo salama.

282. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya wadau 676 wanaojishughulisha na biashara au matumizi ya kemikali walisajiliwa sawa na asilimia 113 ya lengo la kusajili wadau 600 na maghala 1,705 ya kuhifadhia kemikali yalikaguliwa sawa na asilimia 130 ya kukagua maghala 1,314 yaliyopangwa kukaguliwa. Aidha, Mamlaka iliweza kutoa jumla ya vibali 42,843 sawa na asilimia 180 ya lengo la kutoa vibali 23,776, kutoa elimu kwa jumla ya wadau 4,615 kuhusiana na matumizi salama ya kemikali sawa na asilimia 105 ya lengo la kutoa elimu kwa wadau 4,400 na hivyo kuwezesha kulinda afya na mazingira.

283. ***Mheshimiwa Spika***, Mamlaka itahakikisha kuwa inaendelea kutoa huduma bora ambapo katika kipindi cha Mwaka 2021/22, kazi zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

- (i) Kuchunguza jumla ya sampuli/vielelezo 105,000 kwa lengo la kulinda afya, mazingira na kuchangia katika utoaji haki;
- (ii) Kuendelea na ujenzi wa Ofisi na Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Makao Makuu ya nchi Dodoma;
- (iii) Kuimarisha usimamizi wa kemikali nchini kwa kufanya usajili wa wadau 800 wanaojishughulisha na biashara ya kemikali;
- (iv) Kukagua mizigo ya kemikali katika mipaka 38 nchini na kukagua maghala 1,850 ya kuhifadhiya kemikali;
- (v) Kutoa vibali 34,900 vya kuingiza na kusafirisha kemikali;
- (vi) Kuendelea kuboresha Mifumo ya TEHAMA ili kurahisisha utoaji na upatikanaji wa huduma za Mamlaka kwa Wananchi kwa wakati;
- (vii) Kuendelea na uanzishwaji wa kanzidata ya taifa ya vinasaba vya binadamu (Human DNA Database);
- (viii) Kuimarisha Kituo cha Taifa cha Kuratibu Matukio ya Sumu nchini;
- (ix) Kutoa elimu kwa Wadau 6,650 juu ya huduma zinazotolewa na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali; na
- (x) Kuendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa Watumishi 20 na Watumishi 65 katika mafunzo ya muda mfupi.

#### **Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR)**

284. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Taasisi iliendelea kutekeleza tafiti mbalimbali zinazohusiana na: Malaria, kifua kikuu (TB), UKIMWI, afya ya mama na mtoto, magonjwa ya kitropiki yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, magonjwa ya mlipuko, magonjwa yasiyoambukiza, muungano wa magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza (co-morbidities), viashiria vya afya vya

kijamii pamoja na magonjwa mtambuka ya binadamu na wanyama (One Health). Kwa ujumla, muda wa kukamilika kwa tafti zinazoendelea ni kati ya mwaka mmoja hadi mitano ambapo Taasisi imejipanga kutoa matokeo pindi tafiti hizo zitakapokamilika.

285. ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi ilipokea maombi ya tafiti mpya 249, ukilinganisha na maombi 436 mwaka 2019/20, kushuka huku kumechangiwa na kuwepo kwa mlipuko wa COVID-19 duniani. Maombi yaliyopokelewa yalikuwa kwenye maeneo ya; Usugu wa Dawa - AMR (5), Lishe (2), COVID-19 (38), Mifumo ya afya (37), UKIMWI (14), Malaria (32), Afya ya mama na mtoto (35), Magonjwa yasijoambukiza (20), Mifumo ya kijamii (15), Zoonotiki (7), Magonjwa ambayo yalikuwa hayapewi kipaumbele (7), Kifua Kikuu – TB (20) na mengineyo (17). Kati ya maombi yote yaliyopokelewa maombi 204 yalipewa kibali cha kuanza kufanya utafiti na maombi 43 hayakukidhi vigezo na hivyo wahusika walipewa taarifa ili wafanye maboresho.

286. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2021/22, Taasisi imepanga kuboresha huduma zake kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kukamilisha uanzishwaji wa kituo kikubwa cha utafiti na uchunguzi wa mimea dawa na kuanzisha kiwanda cha kimkakati cha kuzalisha dawa zitokanazo na mimea – NIMR Mabibo. Hii ni pamoja na kuimarisha tafiti katika Tiba Asili kwa kushirikiana na wadau na watalaamu/waganga wa Tiba Asili hapa nchini;

(ii) Kuimarisha ushirikiano na hospitali za rufaa za mikoa (RRHs) na Timu za Usimamizi na Uendeshaji wa Huduma za Afya za Mikoa (RHMTs) katika kutekeleza miradi mbalimbali ya utafiti;

(iii) Kushirikiana na programu za UKIMWI, malaria, kifua kikuuu na NTD katika kufanya tafiti mbalimbali zitakazochangia kuharakisha utokomezaji wa maradhi mbalimbali ya kuambukiza;

(iv) Kuimarisha na kujenga uwezo wa taasisi wa kufanya utafiti kuhusu magonjwa ya mlipuko na mifumo ya afya; na

(v) Kuimarisha usimamizi wa maadili na kufuatilia kwa karibu kazi za utafiti wa Afya zinazofanyika ndani ya nchi.

### **Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC)**

287. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Taasisi ya Chakula na Lishe imeendelea kufanya uchambuzi wa sampuli za vyakula katika viwanda vikubwa, vya kati na vidogo katika ngazi mbalimbali nchini. Hadi sasa, jumla ya viwanda vikubwa 33 vinavyoongeza virutubishi kwenye chakula; viwanda tisa (9) vinaongeza madini joto kwenye chumvi, viwanda 10 vinaongeza virutubishi kwenye mafuta ya kula, viwanda nane (8) vinaongeza kwenye unga wa ngano na sita kwenye unga wa mahindi. Matokeo ya uchambuzi wa sampuli za vyakula kutoka viwandani zilizochukuliwa unaonesha kwamba asilimia 86 ya unga wa ngano una viwango sahihi vya virutubishi ikilinganishwa na asilimia 72 mwaka 2019/20; asilimia 73 ya mafuta yameongezwa vitamini A; na asilimia 7 ya unga wa mahindi umeongezwa virutubishi ukilinganisha na asilimia 5 mwaka 2019/20.

288. ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi imeendelea kukamilisha tafiti nne (4) kubwa zinazohusu kubaini uzalishaji na upatikanaji wa chumvi yenyе madini joto nchini; kutathmini hali ya lishe kwa akina mama wajawazito mkoani Mbeya; kufanya tathmini ya mbinu za kubadili tabia za unyonyeshaji watoto wachanga kwa akina mama katika mikoa ya Njombe na Iringa; na utafiti wa viashiria vya hali ya lishe kwa akina mama walio katika umri wa kuzaa katika kaya mkoani Morogoro. Matokeo ya tafiti hizo yatatumika kuboresha huduma za lishe nchini.

289. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/21, Taasisi imekamilisha na kizindua mfumo rasmi wa upatikanaji wa taarifa na takwimu za lishe nchini kupitia jukwaa la pamoja ambalo litawezesha wadau kupata taarifa mbalimbali za

lishe kwa urahisi kwa njia ya mtandao. Jukwaa hili litaongeza wigo wa matumizi ya taarifa katika maandalizi ya mikakati, mipango na maamuzi mbalimbali ya kisera na kiutendaji ili kuboresha hali ya lishe nchini. Aidha, jukwaa linajumuisha taarifa zinazotokana na viashiria kutoka katika Sekta mbalimbali ikiwemo Afya, Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Maji, Elimu na Maendeleo ya Jamii. Mfumo huu unapatikana katika anuani: [www.mnis.tfnc.go.tz](http://www.mnis.tfnc.go.tz).

290. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuongeza ufanisi katika kufanya tathmini ya huduma za lishe nchini, Taasisi ya Chakula na Lishe iliendesha mafunzo yanayohusu tathmini ya hali ya lishe, unasihi na huduma za lishe kwa watu wanaoishi na virusi nya UKIMWI (Nutrition Assessment Counselling and Support). Mafunzo hayo yalihusishawawezeshaji (63) ambapo Maafisa lishe walikuwa (31), Matabibu (16) na Wauguzi (16) kutoka Mikoa ya Njombe, Iringa, Simiyu, Mara na Geita. Aidha, mafunzo haya yalilenga kuongeza idadi ya watoa huduma za afya wenye ujuzi wa kufanya tathmini ya hali ya lishe, unasihi na huduma za lishe kwa watu wanaoishi na virusi nya UKIMWI.

291. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Taasisi ya Chakula na Lishe kwa kushirikiana na Chuo Kikuu Cha Kilimo cha Sokoine na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbilli imefanikisha kuanzisha mradi wa kutengeneza vyakula nya nyongeza kwa lengo la kusaldia matibabu ya Utapiamlo Mkali na wa kadiri kwa watoto walio na umri wa miezi 6 hadi 24. Vilevile, vyakula hivi vinatarajiwa pia kuweza kutumika katika makuzi kwa watoto wenye umri wa miezi 6 hadi 59. Hadi sasa, tayari aina nne (4) za chakula zimeshatengenezwa na uchunguzi wa kimaabara unaendelea ili kuhakiki usalama wake. Aidha, mradi huu unalenga kuchangia katika mikakati ya kupunguza vifo nya watoto wenye umri chini ya miaka mitano katika jamii.

292. ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi imeendelea kutekeleza mikakati ya kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza, hususan athari za ongezeko la viwango nya tatizo la uzito uliozidi na kiribatumbo mionganoni mwa jamii. Ili kupunguza

athari za magonjwa haya, Serikali imeandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Ulaji (*National Food Based Dietary Guideline*) na kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kubadilisha mtindo wa maisha hususan uli duni.

293. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/22, Taasisi imepanga kutekeleza yafuatayo ili kuboresha huduma kudhibiti na kutokomeza utapiamlo nchini:-

- (i) Kufanya utafiti wa kutambua vyanzo vingine vya madini joto katika vyakula vinavyotumika katika kaya, kwa wanawake walio kwenye umri wa kuzaa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Singida, Simiyu, Mjini Magharibi na Pemba Kusini;
- (ii) Kukamilisha kazi ya kuandaa mwongozo unaohusu tahadhari ya mapema na huduma za lishe wakati wa dharura na maafa ili ujumuishwe katika mfumo wa Taifa unaratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu (*National Disaster Risk Management Framework*);
- (iii) Kuendelea kushirikiana na Taasisi nyingine za Serikali na sekte binafsi kupata teknolojia rahisi ya kunyonyiza virutubishi vya nyongeza wakati wa kusaga unga wa mahindi;
- (iv) Kuendelea kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu faida za lishe bora na athari za utapiamlo kwa makundi mbalimbali kuititia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii (*Radio na Luninga, magazeti, mitandao ya Youtube, Facebook, Instagram, Twitter na Tovuti ya Taasisi*);
- (v) Kukamilisha mandalizi na kusimamia utekelezaji wa Mpango Jumuishi wa Pili wa utekelezaji wa masuala ya lishe wa miaka mitano (*2<sup>nd</sup> National Multisectoral Nutrition Action Plan – 2021/22 – 2025/26*); na
- (vi) Kuhamasisha matumizi ya jukwaa la pamoja la taarifa na takwimu za lishe kwa njia ya mtandao sambamba na kutoa mafunzo ya namna ya kutumia jukwaa hilo na kuhamasisha matumizi ya taarifa na takwimu hizo ili kufanya

maamuzi (*evidence-based decisions*) mbalimbali katika ngazi zote.

### **IDARA KUU YA MAENDELEO YA JAMII (FNGU 53)**

294. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/21, utekelezaji wa majukumu ya Wizara (Fngu 53) ulilenga kwenye maeneo mbalimbali matano yakiwemo; eneo la maendeleo ya jamii, kuimarissha upatikanaji wa haki na maendeleo ya mtoto, kuboresha huduma za ustawi wa jamii, kuchochea maendeleo ya jinsia na uwezeshaji wa wanawake na kuratibu utekelezaji wenye ufanisi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Uratibu wa utekelezaji wa majukumu katika maeneo haya ulifanywa na makao makuu ya Wizara kwa ushirikiano na taasisi zake pamoja na wadau wake wote.

### **ENEO LA 1: MAENDELEO YA JAMII**

295. ***Mheshimiwa Spika***, katika eneo hili Wizara imeendelea kuratibu dhana ya ushirikishaji wananchi katika shughuli za maendeleo ya jamii kwa kuhamasisha ushiriki wa wananchi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia rasilimali zilizopo katika maeneo yao. Jitihada hizo zimevezesha jamii kushiriki katika ujenzi wa daraja kwa nguvu za wananchi kwenye vijiji vya Lughuza na Wangwi, Wilayani Lushoto na ujenzi wa vyumba viwili (2) vya madarasa ya Shule ya Sekondari Sanya Juu, Mkoani Kilimanjaro. Aidha, ujenzi wa Ofisi 16 za Vijiji, Vituo 6 vya Afya na Zahanati 21 unaendelea katika Mikoa ya Katavi, Arusha, Kigoma, Geita, Kagera na Dodoma.

296. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Wizara imeendelea kutekeleza Kampeni ya Ujenzi wa Nyumba Bora kwa Gharama Nafuu zinazotumia teknolojia rahisi. Kampeni hii yenyе Kaulimbiu "***Piga Kazi: Boresha Makazi***", imewevesha kujengwa kwa nyumba bora 751 katika Mikoa ya Pwani, Katavi, Singida na Mwanza. Aidha, jumla ya ramani 360 za nyumba bora na nakala 1,050 za Mwongozo wa Ujenzi wa Nyumba Bora zimesambazwa kwa viongozi wa kijamii wakati wa Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika Mkoani Simiyu.

297. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inatambua na kuthamini mchango wa Maafisa Maendeleo ya Jamii kwa maendeleo ya nchi. Maafisa hao kupitia stadi na maarifa ya kuiendea jamii, hutumia njia za uhamasishaji, uraghabishi na uelimishaji katika kuiandaa jamii kuwa tayari kwa mabadiliko yenyе manufaa kwao na kwa Taifa. Aidha, huwezesha jamii kutambua wajibu wao wa kujilettea maendeleo binafsi na ya kijamii na kubaini fursa zilizopo na changamoto zinazowazunguka ili kutumia rasilimali walizonazo kubuni na kutekeleza mikakati ya ufumbuzi wa changamoto zao. Hivyo, Maafisa Maendeleo ya Jamii wameendelea kujenga jamii endelevu, inayojiamini na yenyе uwezo wa kujituma na kushiriki, kwa misingi ya usawa na kuheshimiana katika kubaini mahitaji, kubuni, kuandaa na kutekeleza mipango ya kujilettea maendeleo na kutumia kikamilifu matokeo ya kazi zao. Katika kuhakikisha jamii inashiriki kikamilifu kujilettea maendeleo ni dhahiri Maafisa Maendeleo ya Jamii wanatakiwa kujengewa uwezo zaidi na kuwezeshwa rasilimali fedha na nyenzo za kazi ili kutekeleza majukumu yao kikamilifu na kuwa chachu ya mabadiliko katika jamii.
298. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha utendaji wa Maafisa Maendeleo ya Jamii, Wizara imeendelea kuboresha utoaji wa mafunzo ya taaluma ya maendeleo ya jamii katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii Buhare, Mlale, Misungwi, Rungembra, Mabughai, Ruaha, Uyole na Monduli kwa kusimamia ubora wa mafunzo na kuboresha miundombinu ambapo udahili wa wanafunzi umeongezeka kutoka wanafunzi 3,986 (Me 1,548 na Ke 2,438) mwaka 2019/20 hadi kufikia wanafunzi 4,644 (Me 1,876 na Ke 2,768) mwaka 2020/21 sawa na ongezeko la asilimia 17. Vilevile, jumla ya wanafunzi 3,953 kutoka Vyuo nane (8) vya Maendeleo ya Jamii walihitimu mwaka 2019/20 ikilinganishwa na wanafunzi 3,307 waliohitimu mwaka 2018/19 ikiwa ni ongezeko la asilimia 19.5.
299. ***Mheshimiwa Spika***, pia Wizara inaendelea kuboresha ya utoaji wa Mafunzo ya Taaluma ya Maendeleo ya Jamii katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru (TICD) na Vyuo nane (8) vya Maendeleo ya Jamii (CDTIs) kwa kutekeleza dhana

ya uanagenzi ili kuzalisha wahitimu wenye weledi na umahiri unaoendana na soko la ajira na kujiajiri. Katika mwaka 2019/20, Wizara imeanzisha Programu za Uanagenzi ambapo wanafunzi na wahitimu 219 wa Taaluma ya Maendeleo ya Jamii wanaendelea na mafunzo ya ujuzi wa kujiajiri unaoendana na soko la ajira kwenye Taasisi, Mashirika na Makampuni. Utaratibu huu unatarajiwa kuwezesha idadi kubwa ya wanafunzi na wahitimu wa TICD na CDTIs kunufaika na programu hii kwa namna mbalimbali ikiwemo kupata ajira za kudumuna ujuzi wa kujiajiri.

300. ***Mheshimiwa Spika***, katika eneo hili la maendeleo ya jamii, Wizara pia imeendelea kuratibu Vituo vya Kidigitali vya Ubunifu na Maarifa vyakuibua na kukuza mawazo na vipaji vya wanafunzi na jamii inayozunguka Vyuo vya Maendeleo ya Jamii. Vituo viwili (2) vya Kidigitali vya Ubunifu na Maarifa vya Buhare CDTI na Mabughai CDTI vimezinduliwa mwaka 2020/21 na kufikia Vituo tisa (9) ambavyo vimeanzishwa kwenye Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na Vyuo nane (8) vya Maendeleo ya Jamii. Vituo hivi vitawezesha kuibua na kukuza mawazo na vipaji vya kibunifu mionganini mwa wanafunzi na jamii ili waweze kuchangia katika maendeleo ya Taifa kwa kuzalisha teknolojia zinazohitajika katika maendeleo ya viwanda, kuboresha mbinu za ujasiriamali na masoko na utatuzi wa changamoto mbalimbali katika jamii ikiwemo ajira.

## **ENEO LA 2: HAKI NA MAENDELEO YA MTOTO**

301. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia utoaji wa haki za mtoto zikiwemo haki ya kuishi, kulindwa, kuendelezwa, kushiriki na kutobaguliwa. Wizara imeendelea kuimarisha Ulinzi wa Watoto kwa kuimarisha mifumo ya ulinzi wa watoto shulen. Aidha, Wizara imeendelea kuratibu uanzishwaji wa Madawati ya Ulinzi wa Watoto katika shule za msingi na sekondari. Hadi kufikia Aprili, 2021, jumla ya madawati 182 yameanzishwa na jumla ya wasimamizi wa madawati shulen 360 walipatiwa mafunzo ya namna ya kusimamia madawati hayo ili kupunguza ukatili wa watoto shulen.

302. ***Mheshimiwa Spika***, Wizarapiaimeendelea kufanya kampeni ya kutokomeza mimba za utotoni katika mikoa ya Shinyanga, Mara, Tabora, Singida, Rukwa, Tanga na Dodoma. Kutokana na kampeni hiyo, jumla ya wanafunzi 8,978 katika shule za Msingi na wanafunzi 345 katika shule za Sekondari na walimu 40 walifikiwa na kupata uelewa kuhusu madhara ya mimba na ndoa za utotoni kiafya, kielimu na kiuchumi. Aidha, katika kuzuia ukatili mtandaoni, Wizara imeandaa jumbe maalum zinazopinga ukatili mtandaoni na kuzitumia kutoa elimu kwa jamii kuhusu athari za ukatili.
303. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara piaimeendelea kuelimisha jamii kuhusu athari za mila, desturi na tamaduni zenye madhara zinazosababisha vitendo vya ukatili dhidi ya watoto nchini. Aidha, kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo Wizara imeendelea kuongeza mwamko kwa jamii kutoa taarifa za vitendo vya ukatili dhidi ya watoto nchini kwa kuratibu huduma ya simu bila malipo kwa namba 116 kwa watoto wanaofanyiwa vitendo vya ukatili na unyanyasaji (Child Helpline). Huduma hizo ni pamoja na kisheria, tiba, unasihi na mahali salama kwa kukaa kwa muda. Hadi kufikia Aprili 2021, jumla ya simu 1,079,891 zilipokelewa na jumla ya watoto 5,228 walipatiwa huduma kupitia simu hiyo ikilinganishwa na watoto 3,044 waliopatiwa huduma kwa mwaka 2019/20.
304. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile,Wizara imetoa elimu kuhusu athari za ukeketaji kupitia mipaka ya Namanga, Holili, Horohoro na Sirari kwa Kamati ya Usalama ya Wilaya katika mipaka husika pamoja na Maafisa wa Halmashauri ili waweze kushughulikia ukeketaji unaofanyika kwa familia moja kuhama kutoka nchi moja kwenda nchi jirani ambapo, jumla ya wataalam 100 kutoka kwenye Wilaya 4 walishiriki.
305. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara pia imeendelea kutoa taarifa ya utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto (CRC) wa mwaka 1989 lengo likiwa ni kupima utekelezaji wa nchi katika kukuza haki na ustawi wa mtoto. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi kufikia Aprili 2021, Wizara imeandaa Taarifa ya sita (6) ya Nchi ya Utekelezaji wa Mkataba wa

Kimataifa wa Haki za Mtoto taarifa ambayo inaonesha hali halisi ya haki za mtoto nchini, mafanikio ya utoaji wa huduma na haki za mtoto ikiwemo mifano bora ya kuigwa katika afua za kuimarisha upatikanaji wa haki za mtoto na changamoto zilizopo katika kutekeleza afua za haki ya mtoto.

306. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu Malezi ya Mtoto na Elimu kwa Familia, Wizara inatambua kuwa Malezi chanya ya mtoto ni hatua muhimu katika Makuzi na Maendeleo ya Mtoto katika hatua ya kufikia utimilifu wake. Hivyo, Wizara imeendelea kuongeza uelewa wa malezi kwa wazazi na walezi ili kumlinda mtoto na aina zote za ukatili bila kuathirika na Makuzi yake kimwili, kiakili, kiroho, kimaadili na Kijamii. Katika kuimarisha malezi chanya ya watoto na elimu kwa familia, Wizara imetua elimu kuhusu malezi chanya kwa jumla ya Maafisa Maendeleo ya Jamii 7,445 na wazazi 110,805. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau inaratibu ujenzi wa Vituo 30 vya Kijamii vya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (Community-Based ECD Centres) katika Halmashauri 6 za Mikoa ya Dodoma na Dar es Salaam.

307. ***Mheshimiwa Spika***, Vituo hivi ni vya majaribio navinajengwa katika Halmashauri za Temeke (5) na Kigamboni (5) katika Mkoa wa Dar es Salaam na Bahi (5), Kongwa (5), Chamwino (5) na Kondoa (5) katika Mkoa wa Dodoma. Lengo ni kuhakikisha kwamba vituo hivi vinajengwa katika Mikoa yote nchini. Vituo hivi vitasimamiwa na jamii yenyewe na vitachukua watoto walio na umri chini ya miaka 4 kwa lengo la kuimarisha makuzi jumuishi ya watoto ikiwa ni pamoja na ujifunzaji wa Awali, ulinzi wa mtoto, lishe bora, Elimu ya Afya Msingi na mawasiliano baina yao na watoa huduma.

308. ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza maazimio ya Mkutano wa Kimataifa wa Idadi ya Watu na Maendeleo (*International Conference on Population and Development*) uliofanyika nchini Kenya mwaka 2019, Tanzania imeandaa Ajenda ya Kitaifa ya Kuwekeza katika Afya na Maendeleo kwa Vijana Balehe (2021/22-2024/25). Ajenda hiyo ilizinduliwa rasmi na **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa**, Waziri Mkuu

wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 17/4/2021 Jijini Dodoma. Ajenda hii ya Kitaifa itaimarisha uwekezaji katika afya na maendeleo kwa vijana balehe nchini ili kuleta uhusiano wa malezi ya watoto wadogo na wale wanaofikia umri wa vijana balehe. Aidha, Ajenda inalenga kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili vijana balehe hapa nchini kupitia nguzo kuu sita (6) ambazo ni: Kupunguza Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI; Kutokomeza Mimba za Utotoni; Kuzuia Ukatili wa Kimwili, Kingono na Kisaikolojia; Kuboresha Lishe; Kuhakikisha Watoto wa Kike na Kiume Wanabaki Shulen; na Kuwajengea Vijana Balehe Ujuzi na Uwezo wa Kuzifikia Fursa mbalimbali za Kiuchumi.

309. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Wizara ipo katika hatua za mwisho za maandalizi ya Programu ya Kitaifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (2021/22-2025/26) yenye lengo la kuratibu na kusimamia utoaji wa huduma jumuishi za malezi chanya kwa watoto, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto katika Halmashauri zote nchini. Aidha, Wizara imeandaa Kitini cha Elimu ya Malezi ya Familia Kuzuia Ukatili dhidi ya Watoto Tanzania (2017) kwa lengo la kuimarisha uwezo na mbinu kwa wawezeshaji wa jamii ili kuwajengea wazazi/walezi maarifa na stadi juu ya mikakati ya kijamii ya kuzuia aina zote za ukatili dhidi ya watoto kupitia elimu madhubuti ya malezi chanya yanayofaa kwa familia. Vilevile, Wizara imeandaa Mwongozo wa Uanzishwaji na Uendeshaji wa Vikundi vya Malezi chanya kwa jamii (2021). Lengo ni kuweka utaratibu wa namna ya kuanzisha na kuendesha vikundi vya malezi katika jamii.

310. ***Mheshimiwa Spika***, uwekezaji kwa watoto katika miaka ya awali ya maisha yana mchango mkubwa katika kuleta mabadiliko chanya ya kielimu, kijamii na kiuchumi katika Taifa letu. Sayansi ya ukuaji wa mtoto inatueleza kwamba msingi madhubuti unaojengwa kwa mtoto katika miaka ya awali unamuwezesha mtoto kujitambua, kujimudu, kujua wajibu wake na kuwa na ujuzi wa kumuwezesha kumudu majukumu mbalimbali ikiwemo ya kiuchumi, kielimu na kijamii. Katika mipango yetu ya kupunguza umaskini nchini, ni muhimu uwekezaji wa mapema kwa watoto ufanyike kama njia

mojawapo ya kufikia malengo ya Taifa. Uwekezaji huu utasaidia kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kijamii kwa kiasi kikubwa kuliko kusubiri kuwekeza katika kipindi cha utu uzima. Pia, uwekezaji huu utasaidia kupunguza matabaka ya kijamii.

### **ENEO LA 3: HUDUMA ZA USTAWI WA JAMII**

311. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inatambua umuhimu wa Maafisa Ustawi wa Jamii katika kuratibu na kusimamia utoaji wa huduma za Ustawi wa Jamii hapa. Majukumu ya Maafisa Ustawi wa Jamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ni pamoja na: kutoa huduma za malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya watoto wadogo na wachanga, kuimarisha ustawi na ulinzi wa familia kwa kufanya unashi kwa wanandoa walio kwenye migogoro na mifarakano; kusimamia huduma kwa familia zenyenye dhiki; kusimamia matunzo kwa watoto; kusimamia huduma kwenye Makao ya Watoto; kusimamia huduma ya malezi ya kambo na kuasili; na kusimamia huduma za malezi, matunzo na ulinzi kwa watoto walio katika mazingira hatarishi.

Aidha, Maafisa Ustawi wana jukumu la kusimamia huduma kwa watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani; kusimamia ulinzi na usalama kwa watoto dhidi ya vitendo vya ukatili; kusimamia haki za mtoto kisheria; kusimamia huduma za marekebisho ya tabia kwa watoto; kusimamia huduma za ustawi wa jamii katika mahakama za watoto; kusimamia huduma kwa wahanga wa usafirishaji haramu wa binadamu; na kusimamia huduma za ulinzi na matunzo kwa wazee pamoja na watu wenye ulemavu. Majukumu mengine ni kusimamia huduma ya msaada wa kisaikolojia na kijamii kutokana na majanga mbalimbali yanayoikumba jamii kama vile matetemeko ya ardhi, ajali mbalimbali pamoja na milipuko ya magonjwa.

312. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha ustawi na maendeleo ya familia nchini, Wizara imeendelea kutoa huduma za ustawi wa jamii kwa watoto walio katika mkinzano na sheria kwenye mahabusu tano (5) za watoto za Mbeya, Kilimanjaro, Tanga, Arusha na Dar es Salaam. Mahabusu hizi zinatoa huduma za msingi ikiwa ni pamoja na huduma za

sheria kwa watoto walio katika mkinzano na sheria ambapo, mwenendo wa watoto walio katika Mahabusu za watoto takwimu zinaonesha kuwa jumla ya watoto 413 waliokinzana na sheria (Me 380 na Ke 33) waliwezeshwa kupata huduma za msingi za chakula, malazi, mavazi, huduma za matibabu na sheria kwa mwaka 2020/21 ikilinganishwa na watoto 138 (Me 120 na Ke 18) waliwezeshwa kupata huduma hizo kwa mwaka 2019/20. Ongezeko la watoto katika Mahabusu za Watoto linatokana na mwamko wa wananchi kutoa taarifa kuhusu makosa yaliyofanywa na mtoto pamoja na kuongezeka kwa Mahakama za Watoto ambazo hutoa hukumu ya mtoto kukinzana na sheria.

313. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kuititia Programu ya Marekebisho ya Tabia kwa Watoto waliopatikana na makosa imeendelea kutekelezwa katika Halmashauri mbalimbali nchini. Lengo la programu hii ni kuwachepusha watoto waliopatikana na makosa mbalimbali hususan makosa ya jinai kutoka katika mfumo rasmi wa haki jinai kwa kuwarekebisha tabia na kuwaunganisha na familia zao. Hadi kufikia Aprili 2021, jumla ya watoto 78 (Me 73 na Ke 5) ambao walikutwa na makosa mbalimbali ya kijinai wamechepushwa ikilinganishwa na watoto 148 (Me 89 na Ke 59) waliochepushwa mwaka 2019/20.

314. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara pia imeendelea kuhakikisha kuwa huduma za msingi, elimu na mafunzo zinaendelea kutolewa kwa watoto waliobainika kufanya makosa ya jinai waliopo katika Shule ya Maadilisho Irambo Mbeya. Hadi kufikia Aprili 2021, watoto 219 (Me 210 na 9 Ke) waliobainika kufanya makosa ya jinai walipatiwa huduma ikilinganishwa na watoto 169 (Me 163 na Ke 6) walipatiwa huduma mwaka 2019/20. Shule hii inatoa marekebisho ya tabia kwa watoto na kuwapatia ujuzi ili wanapokamilisha hukumu zao wawze kujitegemea na kuwa raia wema.

315. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Wizara imeendelea kutoa mafunzo kwa Maafisa 140 wa Mahakama za Watoto wakiwemo Maafisa Ustawi wa Jamii 39, Mawakili 6, Waendesha Mashtaka 16, Mahakimu 62 na Wanasheria 17

kutoka Mikoa ya Kilimanjaro, Geita na Simiyu kuhusu namna bora ya kuendesha mashauri ya watoto katika mahakama za watoto. Lengo la mafunzo hayo ni kuboresha uendeshaji wa mashauri ya watoto katika mahakama za watotozilizopo katika mikoa 24 ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Kagera, Pwani, Morogoro, Dodoma, Singida, Iringa, Njombe, Mtwara, Dar es Salaam, Lindi, Ruvuma, Shinyanga, Simiyu, Mwanza, Mara, Geita, Songwe, Rukwa, Tabora, Kigoma na Tanga. Vilevile, Mahakama za Watoto saba (7) zimeanzishwa na kufikia Mahakama za Watoto 147 nchi nzima. Jumla ya watoto 737 walihudumiwa katika mahakama hizo nchini ambapo watoto 516 (Me 217 na Ke 299) waliachiwa huru na watoto 221 (Me 93 na Ke 128) walikutwa na hatia.

316. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara pia imeendelea kutoa huduma za sheria, marekebisho ya tabia, unasihi na msaada wa kisalkologia kwa watoto walio katika mkinzano na sheria kupitia Mahakama za Watoto. Hadi kufikia Aprili 2021, jumla ya watoto 1,661 (Me 1,061 na Ke 600) walihusika na ukinzani wa sharia. Mikoa 10 iliyoongoza kwa kuwa na watoto wanaokinzana na sheria ni Tanga, Pwani, Arusha, Kilimanjaro, Dar es Salaam, Dodoma, Mara, Mbeya, Singida na Shinyanga.

317. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imefanyia kazi masuala yanayohusu Matunzo na Ulinzi kwa Watoto Walio katika Mazingira Hatarishi na Familia zenye Migogoroambapo, imeendelea kusimamia utoaji wa huduma za Malezi ya Kambo na Kuasili kwa watoto walio katika mazingira hatarishi kwa kupitia na kuhakiki maombi ya watoto kwa ajili ya malezi ya kambo. Hadi kufikia Aprili 2021, jumla ya maombi 149 yalipokelewa ambapo maombi 50 kati ya hayo yalitolewa kibali cha kufanya shughuli hizo. Aidha, jumla ya watoto 38 (Me 18 na Ke 20) walipata huduma za malezi ya kambo na watoto 17 (Me 5 na Ke 12) walipata huduma ya kuasilikama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na.15.**

318. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kutekelezaProgramu ya Kuwatambua Watu wa Kuaminika ili kulea watoto walio

katika mazingira hatarishi wakiwemo watoto yatima katika mikoa ya Dar es Salaam, Iringa, Kilimajaro, Arusha, Dodoma na Mwanza. Jumla ya Watu wa Kuaminika 168 walitambuliwana jumla ya watoto 27 wamewekwa kwa watu wa kuaminika kwa ajili ya hifadhi na malezi ya muda. Aidha, kupitia programu hiyo, idadi ya watoto waliolelewa na Watu wa Kuaminika imeongezeka kutoka watoto 662 mwaka 2019/20 hadi kufikia watoto 689 Aprili 2021. Vilevile, mafunzo kuhusu huduma kwa Watu wa Kuaminika yametolewa kwa Maafisa Ustawi wa Jamii 160 kutoka katika Jiji la Arusha, Jiji la Dodoma, Manispaa za Ubungo, Kigamboni, Temeke, Ilala, Kinondoni, Iringa, Moshi, na Halmashauri za Nyamagana na Ilemela.

319. ***Mheshimiwa Spika***, Uratibu wa Huduma kwa Watoto walio katika Mazingira Hatarishiwanaoishi kwenye makao ya watoto ni eneo liliopewa kipaumbele na Wizara ambapo, Wizara immeendelea kutoa leseni za usajili wa makao kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo. Jumla ya leseni 24za usajili wa makao ya watoto zimetolewa. Usajili wa makao ya watoto umeongezeka kutoka Makao ya Watoto 190 mwaka 2019/20 hadi Makao ya Watoto 214 kufikia Aprili, 2021. Aidha, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Shirika la *ABBOTT Fund Tanzania* imejenga Makao Mapya ya Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi katika Eneo la Kikombo Mkoani Dodoma. Makao haya yana Mabweni 4 ya kuwashudumia watoto 250, nyumba 25 za watumishi, majengo kwa ajili ya karakana ya mafunzo ya ufundi, na kituo cha michezo na burudani.

320. ***Mheshimiwa Spika***, ujenzi wa makao ya Kikombo ni sehemu ya Mpango Mkakati Endelevu wa Wizara wa kuwatengamanisha na kuwaunganisha Watoto na Familia zao kupitia ufadhili wa *ABBOTT Fund Tanzania* (**Dola za Marekani Milioni 5.5**). Ujenzi huu umeiwezesha Serikali kutatta changamoto za huduma katika makao ya watoto Kurasini Dar es Salaam, ikiwemo kukosekana kwa mazingira salama na ongezeko la vibaka katika maeneo yanayozunguka makao, na eneo dogo kwa ajili ya miradi ya karakana za ufundi na michezo kwa watoto, na shughuli za bustani na

ufugaji. Vilevile, Wizara imeendelea kusimamia utoaji wa huduma katika Makao ya Watoto yanayomilikiwa na watu binafsi na Taasisi nyingine. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, jumla ya Makao ya Watoto 36 yamesajiliwa yenye watoto 918 (Me 496 na Ke 422)kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 1**, hivyo kuwa na jumla ya Makao ya Watoto 520 yanayomilikiwa na watu binafsi na Taasisi nyingine.

**Jedwali Na.1:** Makao ya Watoto Yanayomilikiwa na Watu Binafsi na Taasisi nyingine Yaliyosajiliwa kwa Kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021.

Na.	Mwezi	Idadi ya Makao ya Watoto	Idadi ya Watoto		
			Me	Ke	Jumla
1	Julai, 2020	9	124	92	216
2	Agosti, 2020	5	56	59	115
3	Septemba, 2020	4	90	43	133
4	Oktoba, 2020	4	43	55	98
5	Novemba, 2020	1	24	27	51
6	Desemba, 2020	1	7	6	13
7	Januari, 2021	2	16	19	35
8	Februari, 2021	5	35	31	66
9	Machi, 2021	4	14	14	28
10	Aprili, 2021	1	87	76	163
<b>Jumla</b>		<b>36</b>	<b>496</b>	<b>422</b>	<b>918</b>

**Chanzo:** *WAMJW*

321. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa Huduma za Marekebisho na Utengemao kwa Watoto Wanaoishi na Kufanya Kazi Mitaani, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kufanya jitihada za kuwatambua watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani ili kuwaunganisha na familia zao. Katika maandalizi hayo tathmini ya mahitaji na maandalizi ya mpango wa huduma kwa kila mtoto hufanyika. Hadi kufikia Aprili 2021, zoezi hili limefanyika katika mikoa

mitano (5) ya Mwanza, Arusha, Iringa, Mbeya na Dodoma ambapo jumla ya watoto 5,390 (Me 3,852 na Ke 1,538) wanaoishi na kufanya kazi mtaani walitambuliwa na kupewa huduma mbalimbali ambapo watoto 135 (Me 92 na Ke 43) kati ya hao, waliunganishwa na familia zao, watoto 821 (Me 519 na Ke 302) walipewa vifaa vya shule na watoto 75 (Me 58 na Ke 17) walipewa huduma ya kuimarisha uchumi wa kaya.

322. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu Uratibu wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuimarisha huduma hizi kwa kusimamia utoaji wa huduma katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana. Hadi kufikia Aprili 2021, jumla ya vituo 134 vimepatiwa vyeti vya usajili. Aidha, jumla ya vituo 33 vya kulelea watoto wachanga (Crèches) wa chini ya miaka miwili vimesajiliwa. Kupitia vituo vya kulelea watoto wadogo mchana, jumla ya watoto 163,394 (Me 85,175na Ke 78,219) waliandikishwa hadi kufikia Aprili 2021, ikilinganishwa na watoto 159,479 (Me 82,539 na Ke 76,940) walioandikishwa mwaka 2019/20 kama inavyoonesha katika **Kiambatisho Na. 16.**

323. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha huduma za malezi kwenye vituo vya kulelea watoto wadogo mchana, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri inaendelea kufanya ufuatiliaji saidizi kwa lengo la kuhakikisha vinatoa huduma zenye ubora na zinazozingatia viwango. Ufuatiliaji wa vituo hivyo umefanyika katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Tanga, Mwanza, Shinyanga, Kagera, Geita, Kigoma, Rukwa, Simiyu, Morogoro, Mara, Manyara, Kilimanjaro na Songwe. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi kufikia Aprili 2021, jumla ya vituo 2,691 vilikaguliwa vikiwemo vituo 597 vilivyosajiliwa na 2,094 ambavyo havijasajiliwa. Aidha, vituo 290 vilifungwa kutokana na kutokidhi masharti ya uendeshaji na vituo ambavyo havijasajiliwa vinaendelea na taratibu za kupata vyeti vya usajili.

324. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara pia imeendelea kusimamia utoaji wa mafunzo ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali

ya mtoto ili kukabiliana na upungufu wa Walezi wa Watoto nchini kuititia vyuo 26. Kati ya vyuo hivyo, chuo kimoja ni cha Serikali na 25 ni vya Binafsi. Hadi kufikia Aprili 2021, jumla ya wanafunzi 748 walidahiliwa katika vyuo 21 vinavyotoa mafunzo ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto Tanzania Bara. Aidha, Wizara imeendelea kuratibu utoaji wa huduma katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana kwa kutoa miongozo na mafunzo kwa Wamiliki wa Vituo pamoja na Walezi wa Watoto 81.

325. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu Huduma kwa Waathirika wa Vitendo vya Ukatili, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kushughulikia mashauri ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto ikiwemo ukatili wa kimwili, ukatili wa kihisia, kingono na ukatili wa kiuchumi. Hadi kufikia Aprili 2021, jumla ya mashauri 11,270 ya watu wazima na mashauri 6,651 ya watoto yalipokelewa na kufanyiwa kazi kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 17**. Aidha, katika kuimarisha utoaji wa huduma kwa waathirika wa ukatili, Wizara imeongeza idadi ya wataalam 50,304 wanaoshughulikia masuala ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto katika mikoa yote nchini. Kati ya wataalam hao, Polisi Jamii ni 4,542, Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto wa Kujitolea ni 15,255, Wahudumu wa Afya ni 10,534, Maafisa Ustawi wa Jamii ni 3,582, Walimu wa Unasihi/Malezi ni 13,636 na Wasimamizi wa Mashauri ngazi ya Jamii ni 2,755.

326. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, katika kutokomeza utumikishwaji wa watoto, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuwatambua na kuwapatia huduma muhimu watoto wanaotumikisha katika mikoa ya Tabora, Mbeya na Songwe. Hadi kufikia Aprili 2021, jumla ya watoto 900 (Me 522 na Ke 378) wanaofanyakazi katika ajira hatarishi wametambuliwa. Aidha, elimu kuhusu madhara ya utumikishwaji wa watoto katika sekta ya kilimo na shughuli nyiningine za kiuchumi imetolewa kwa wataalam 8,873 (Me 3,948 na Ke 4,925) kutoka sekta mbalimbali kwenye mikoa hiyo.

327. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na mafanikio hayo, changamoto zilizojitekeza ni upungufu wa Maafisa Ustawi wa Jamii katika ngazi mbalimbali hususan Kata na uhaba wa vitendea kazi kama vile kompyuta na usafiri. Aidha, kumekuwepo na changamoto ya upatikanaji wa taarifa kwa wakati kutoka kwa wadau mbalimbali jambo ambalo Wizara itafanya kazi kwa kuimarisha uratibu wa mashirikiano ikiwemo na wadau wa ndani hususan Ofisi ya Rais – TAMISEMI ambaye ni mdau mwenye eneo kubwa zaidi.

328. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu usimamizi wa usuluhishi wa migogoro ya ndoa na matunzo ya watoto, Wizara imeendelea kushughulikia mashauri haya katika jamii kuititia Mabaraza ya Usuluhishi ya Ndoa ya Kamishna wa Ustawi wa Jamii. Hadi kufikia Aprili 2021, jumla ya mashauri ya ndoa 6,588 yalipokelewa ambapo, kati ya mashauri hayo, mashauri 4,747 yalisuluhishwa, mashauri 797 yalipelekwa mahakamani na mashauri 1,044 yanaendelea na usuluhishi.

329. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa Uratibu wa Huduma ya Msaada wa Kisaikolojia na Kijamii Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuratibu uimarishaji wa utoaji wa Huduma za Msaada wa Kisaikolojia kwa Familia na wahitaji mmoja mmoja. Katika kusimamia hili, Wizara iliratibu mafunzo ya kuwajengea uwezo Maafisa katika Halmashauri 43 nchini ambapo Washiriki 1,075 wakiwemo Maafisa Ustawi wa Jamii, Maafisa Maendeleo ya Jamii, Walimu, Manesi na Madaktari walipewa mafunzo ambayo pia, yalijumuisha wajumbe wa Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto.

330. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia utoaji wa huduma za Msaada wa Kisaikolojia na Kijamii wakati wa majanga kwa mfano, hadi kufikia Aprili 2021, Wizara imetoe msaada wa kisaikolojia kwa waathirika 65 (Me 43 na Ke 22) wa ajali ya treni iliyotokea tarehe 02/01/2021 katika maeneo ya Kigwe - Bahi Mkoani Dodoma ambayo ilisababisha vifo vya watu watatu (3) akiwemo mtoto wa miaka miwili. Aidha, kwa kushirikiana na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma, Sekretarieti ya Mkoa wa Dodoma na

wadau wengine Wizara iliweza kutoa huduma za kijamii na msaada wa kisaikolojia kwa majeruhi wa ajali ya treni waliolazwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma.

331. ***Mheshimiwa Spika***,kuhusu huduma za ustawi wa jamii kwa Wazee, Wizara imeendelea kutoa huduma za msingi za chakula, malazi, mavazi na matibabu kwa wazee wakiwemo wazee wasiojiweza wanaoishi katika Makazi ya Wazee 13 yanayomilikiwa na Serikali. Makazi hayo ni; Kibirizi, Njoro, Kolandoto, Bukumbi, Ipuli, Fungafunga, Mwanzange, Misufini, Nunge, Nyabange, Kilima, Sukamahela na Magugu. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, wazee wasiojiweza 267 (Me 167 na Ke 100) walipatiwa huduma ikilinganishwa na wazee 349 (Me 200 na Ke 149) waliopatiwa huduma katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Wazee wasiojiweza wamekuwa wakiongezeka na kupungua kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na baadhi ya wazee kuunganishwa na familia zao pamoja na vifo. Aidha, Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia utoaji wa huduma za chakula, mavazi, malazi na matibabu kwa wazee 451 (Me 216 na Ke 235) wanaoishi katika Makazi ya Wazee 14 yanayomilikiwa na Taasisi binafsi.

332. ***Mheshimiwa Spika***,katika kutambua kuwa Wazee ni hazina ya taifa kutokana na uzoefu na ujuzi waliokuwa nao, Wizara inaendelea kuhakikisha kuwa wazee wanashiriki na kushirikishwa katika mipango na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ushiriki wa Wazee unazingatiwa kupitia utendaji wa Mabaraza ya Wazee ambayo yamekuwa chachu katika maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2021, Mabaraza ya Wazee 458 yameundwa katika ngazi mbalimbali na kufikia Mabaraza ya Wazee 14,883 ukilinganisha na Mabaraza 14,425 yaliyokuwepo mwaka 2019/20. **Nitoe wito kwa familia na jamii kuendelea kuwajali na kuwatunza wazee pamoja na kuwapatia mahitaji yao ya msingi.**

333. ***Mheshimiwa Spika***,Mabaraza haya hutumika kama majukwaa ya wazee kujadili masuala yanayohusu haki zao. Aidha, Wizara imeendelea kuratibu maadhimisho ya Siku ya

Kimataifa ya Wazee Duniani yanayofanyika tarehe 1 Oktoba kila mwaka ambapo kwa mwaka 2020, maadhisho hayo Kitaifa yalifanyika katika Halmashauri ya Kondo Mkoa wa Dodoma. Jumla ya Wazee 226 kutoka katika Halmashauri 8 za Mkoa wa Dodoma pamoja na Wazee kutoka Chama cha Wazee Mkoa wa Dar es Salaam (Dar es Salaam Elders Association - DEA) walishiriki maadhisho hayo ambapo Wazee 101 walipatiwa huduma za afya.

334. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Wadau imekuwa ikifanya kazi ya usimamizi saidizi wa afua za wazee ili kufuatilia na kutathmini utoaji wa huduma. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, usimamizi umefanyika katika mikoa 10 ya Dodoma, Tanga, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Geita, Kagera, Mbeya, Ruvuma na Kigoma. Afua hizo zinazosimamiwa ni pamoja na:-

- (i) Uundwaji na uhuishaji wa Mabaraza ya Ushauri ya Wazee kote nchini;
- (ii) Kuratibu upatikanaji wa huduma za afya kwa wazee wasiojiweza;
- (iii) Kuratibu shughuli mbalimbali za uzalishaji mali zinazofanywa na wazee ili kujingizia kipato; na
- (iv) Kuratibu na kusimamia utoaji wa huduma katika Makazi 13 ya Wazee na wasiojiweza yanayomilikiwa na Serikali.

#### **ENEO LA 4. MAENDELEO YA JINSIA NA UWEZESHAJI WANAWAKE**

335. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ina jukumu la kisera la kuwawezesha wanawake kiuchumi, kisasa na kiutamaduni ili kuondokana na umaskini wa kipato pamoja na ukatili wa kijinsia. Jukumu hili limekuwa likifanyika kwa kuratibu utoaji wa mikopo kwa Wanawake Wajasiriamali. Aidha,jukumu hili linatekelezwa kupitia Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2000 pamoja na Mkakati wake wa Utekelezaji wa mwaka 2005. Kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (WDF) kwa fedha zinazotengwa kupitia vyanzo

vya ndani vya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kipindi cha mwaka 2015 hadi mwaka 2020, kiasi cha **Shilingi Trilioni 2.22** zimetolewa kama mikopo na kunufaisha vikundi vya wanawake wajasiriamali takriban 490,000 vyenye wanawake zaidi ya milioni 4.9. Mafanikio hayo yametokana na Marekebisho ya Sheria ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2018 Kifungu cha 37A kinachoziyekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani (wanawake 4%, vijana 4% na watu wenye ulemavu 2%) kwa ajili ya kutoa mafunzo ya ujasiriamali na mikopo kwa makundi hayo.

336. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, kupitia Dirisha la Wanawake lililoanzishwa katika Benki ya Posta Tanzania (TPB), mikopo imeendelea kutolewa kwa vikundi vyenye wanawake wajasiriamali watano (5) hadi 10 pamoja na Wanawake mmoja mmoja waliofanikiwa (*graduates*) kutokana na mikopo hiyo kwa riba ya asilimia 3 kwa mwezi. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, mikopo yenyeye thamani ya **Shilingi 22,332,385,000** imetolewa kwa jumla ya wanawake wajasiriamali 6,326 kutoka katika mikoa 26 ya Tanzania Bara ikilinganishwa na kiasi cha **Shilingi 3,586,400,000** kilichotolewa kwa wanawake wajasiriamali 14,271 mwaka 2019/20. Idadi ya wanawake wajasiriamali kwa mwaka 2019/20 walionufaika na mikopo ni kubwa ikilinganishwa na walionufaika kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021. Hii ni kutokana na maboresho yaliyofanyika kwenye Mwongozo na Kanuni za Uendeshaji na Utoaji wa Mikopo mwaka 2019 ambapo wigo wa mikopo kwa vikundi umeongezeka hivyo kuruhusu wajasiriamali kukopa kiasi kikubwa.

337. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na mafanikio yaliyopatikana ya kuwafikia wanawake wengi, katika kuwawezesha wanawake kupata mikopo yenyeye masharti nafuu kuna changamoto ya uhitaji mkubwa wa mikopo ikilinganishwa na mtaji uliopo.

338. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu Wizara kuratibu Mafunzo ya Ujasiriamali na Uendeshaji wa Biashara kwenye kuwawezesha wanawake kiuchumi, Wizara imeanzisha mpango wa

kuwajengea uwezo wanawake wajasiriamali katika mikoa yote 26 ya Tanzania bara. Aidha, mafunzo hayo kwa kipindi hiki yametolewa kwa wanawake wajasiriamali wapatao 788 katika Mkoa wa Singida (wanawake 381) na Mkoa wa Pwani (wanawake 407) na mafunzo hayo yataendelea kwa mikoa yote. Katika mafunzo hayo, wanawake wamejengewa uwezo kwa kupata elimu ya kiufundi kwenye baadhi ya maeneo kama vile kodi, urasimishaji wa biashara, elimu ya hifadhi ya jamii na elimu ya viwango na ubora wa bidhaa. Pia, mbinu mbalimbali za kukuza mitaji pamoja na kupata masoko ya uhakika ya bidhaa zao zilitolewa kuititia Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO), taasisi za fedha na Wakala wa Usajili wa Leseni na Biashara (BRELA).

339. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara iliratibu ushiriki wa Wizara katika Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika Kitaifa Mkoani Simiyu kuanzia tarehe 01 - 09 Agosti, 2020. Katika maonesho hayo jumla ya wananchi 1,200 (Me 660 na Ke 540) walitembelea banda la Wizara na kupata elimu kuhusu masuala ya usawa wa kijinsia, madhara ya vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto, mafunzo ya ujasiriamali na uendeshaji wa biashara na huduma nyingine za kisekta. Kutokana na Maonesho hayo, Wizara imebaini kuwa: kuna uhitaji mkubwa wa masoko ya bidhaa za wajasiriamali; kutokana na mwamko mkubwa wa wananchi kujiajiri hususan katika viwanda vidogo, kuna uhitaji mkubwa wa mikopo yenye masharti nafuu; na uhitaji mkubwa wa matumizi ya teknolojia katika uzalishaji na uendelezaji wa shughuli za ujasiriamali. Aidha, Wizara pia iliratibu ushiriki wa wanawake katika Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam maarufu kama "Maonesho ya Sabasaba" ambapo jumla ya wanawake wajasiriamali 203 walishiriki katika Maonesho hayo na kupata fursa ya kuonesha na kuuza bidhaa zao.

340. ***Mheshimiwa Spika***, kwenye eneo la Uratibu wa Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu kupinga na kuzuia ukatili dhidi ya wanawake na watoto kwa kuratibu Kampeni ya "Twende Pamoja: Ukatili

Tanzania Sasa Basi" iliyofanyika katika Mikoa ya Katavi na Mara ambapo jumla ya watu 5,300 walishiriki. Washiriki walikuwa ni pamoja na Viongozi wa Dini, Watu Mashuhuri na Wazee wa Mila. Aidha, Wizara imeratibu Maadhimisho ya Kitaifa ya Siku 16 za Kupinga Ukatili Dhidi ya Wanawake yaliyofanyika katika Mkoa wa Dar es Salaam yaliyokuwa na Kaulimbiu isemayo "Mabadiliko Yanaanza na Mimi". Wizara pia imeratibu Maadhimisho ya Kitaifa ya Siku ya Mwanamke anayeishi Kijiji yaliyofanyika Mkoa wa Pwani – Mkuranga tarehe 15 Oktoba, 2020. Katika utekelezaji wa kazi hii, changamoto ilijojitokeza ni kuendelea kuwepo kwa vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake vinavyotokana na imani na desturi zenye madhara katika jamii zetu. **Nitoe wito kwa Watanzania wenzangu tuendelee kushirikiana katika kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto hapa nchini ikiwemo kutoa taarifa za vitendo hivyo kwa mamlaka husika.**

341. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuratibu uanzishwaji wa Madawati ya Jinsia na Watoto katika vituo vya Polisi, Jeshi la Magereza, Taasisi ya TAKUKURU na Vyuo vya Elimu ya Juu na Vyuo vya Kati. Hadi sasa Jeshi la Polisi limeunda madawati 420, Jeshi la Magereza madawati 153, Dawati moja (1) katika Taasisi ya TAKUKURU, na madawati matano (5) yameanzishwa katika Vyuo vya UDOM, Mzumbe, UDSM, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na Taasisi ya Ustawi wa Jamii. Madawati haya yameongeza mwamko wa wananchi kutoa taarifa za ukatili katika maeneo yao pamoja na kuzuia ukatili wa kijinsia hususan rushwa ya ngono na kuzingatia masuala ya jinsia vyuoni. Aidha, Wizara pia imeendelea kuratibu jitihada za kuimarisha ulinzi wa wanawake na watoto. Jitihada hizi zinahusisha uanzishaji wa Kamati 1,843 za Ulinzi wa Wanawake na Watoto na hivyo kuwa na jumla ya Kamati 18,186 zilizoanzishwa kuanzia ngazi ya Kijiji/Mtaa hadi Taifa.

342. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu uratibu wa Kuimarisha Usawa wa Jinsia na Haki za Wanawake, Wizara imefanya Kampeni kwa njia ya misafara ya kijinsia (*gender caravans*) iliyolenga kutoa elimu ya kijinsia katika Chuo cha Ardhi, Mzumbe, Iringa, Chuo cha Afya Kibena na Chuo Kikuu Shirikishi cha Sayansi -

Njombe. Misafara hii ilihamasisha na kuhimiza uanzishwaji wa Dawati la Jinsia katika Vyuo vya Elimu ya Juu na Vyuo vya Elimu ya Kati. Aidha, Wizara ilifanya ufuatiliaji wa shughuli za uwezeshaji wa wanawake kiuchumi na utokomezaji wa ukatili wa kijinsia katika Halmashauri za Chamwino na Tanganyika na kufanya ukaguzi wa matumizi ya pikipiki 29 zilizotolewa kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri za Tanganyika na Chamwino kwa ajili ya kufuatilia shughuli za uwezeshaji wanawake kiuchumi na masuala ya kutokomeza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

343. ***Mheshimiwa Spika***, wakati wa ufuatiliaji, jumla ya pikipiki 29 zilikaguliwa ili kubaini endapo zinatumika kutoa huduma iliyokusudiwa na kuwarahisishia usafiri Maafisa Maendeleo ya Jamii hususan waliopo kwenye kata zilizo mbali na maeneo ya mjni. Vilevile, Wizara ilifanya tathmini katika shughuli za uwezeshaji wanawake kiuchumi kupitia ufugaji wa kuku na kilimo cha mbogamboga na matunda katika Wilaya za Chamwino-Dodoma, Ikungi-Singida na Kasulu-Kigoma. Kampeni hiyo itaendelea katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara pamoja na Halmashauri zake 184.

#### **ENEO LA 5: URATIBU WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI**

344. ***Mheshimiwa Spika***, katika eneo hili Wizara imeendelea kusimamia usajili, uratibu na ufuatiliaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili yachangie katika kuleta maendeleo ya Taifa. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili 2021, jumla ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 630 yalisajiliwa na kupatiwa vyeti vya usajili na hivyo kufikia idadi ya Mashirika 11,411 yaliyosajiliwa na taarifa zake kuhifadhiwa kwenye mfumo wa usajili. Hata hivyo, kati ya Mashirika hayo yaliyoingizwa kwenye mfumo wa usajili, takriban Mashirika 4,000 tu ndiyo yapo hai kwa mujibu wa mwenendo wa uwasilishaji taarifa za kila mwaka. Aidha, kiasi cha fedha zilizokusanya wa kutokana na ada za usajili wa Mashirika 630 katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021 ni kama inavyoonekana kwenye **Kiambatisho Na. 18.**

345. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inaendelea na zoezi la kuhakiki Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kuhuisha taarifa zilizopo kwenye mfumo na imeendelea kutoa mafunzo juu ya usajili na uratibu wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa Wasajili Wasaidizi 88 kutoka katika mikoa 6 ya Pwani, Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Singida, Dodoma na Tabora. Kupitia mafunzo hayo, Wasajili Wasaidizi wanaendelea kuratibu Mashirika hayo katika maeneo yao kwenye ngazi za Mikoa na Wilaya kwa mujibu ya Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo walijopewa.

346. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kufanya ufuatiliaji na tathmini ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kupima utendaji wa Mashirika na uzingatiaji wa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na.24/2002 kama ilivyofanyiwa urekebu mwaka 2019. Ufuatiliaji wa ana kwa ana ulifanyika kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 79 katika Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Iringa, Pwani, Ruvuma, Dodoma, Manyara na Shinyanga kwa kushirikiana na Wasajili Wasaidizi katika Mikoa hiyo kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 19**. Aidha, ufuatiliaji wa Mashirika 450 ulifanyika kupitia Mikutano mbalimbali ya Wizara na vikao vya majumuisho (*Monitoring Exit Meetings*) na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

347. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, Wizara imefanya uhakiki wa Mikataba ya Fedha 206 iliyowasilishwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 134 na kubaini jumla ya **Shilingi 803,190,166,342.29** zimetumika kutekeleza miradi ya maendeleo inayotekelizwa na Mashirika katika jamii. Kati ya Mashirika hayo, 70 ni ya Kimataifa na 64 ni ya Kitifa. Aidha, sehemu kubwa ya fedha hizo zilipelekwa katika Sekta ya Afya (mikataba 34), Hifadhi ya Jamii (mikataba 72), Uvezeshaji Wananchi Kiuchumi (mikataba 32), Mazingira (mikataba 14) Kilimo (mikataba 21), Elimu (mikataba 15), Utawala Bora (mikataba 8), Jinsia (mikataba 3), Maji (mikataba 3), Nishati (mikataba 3) na Ardhi (mkataba 1). Hii inafanya Mikataba yote iliyohakikiwa tangu Kanuni 609/2018 itungwe kufika 319 yenye thamani ya jumla ya **Shilingi 2,209,574,831,096**.

348. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na utekelezaji huo, Wizara inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na ufinyu wa bajeti, hali inayosababisha kushindwa kuyafikia Mashirika mengi ili kuhimiza uzingatiaji wa sheria, ukusanyaji wa mapato ya Serikali kama ilivyopangwa katika mwaka wa fedha husika. Pia, kwa kuwa uratibu wa usajili na ufuatiliaji wa Mashirika hayo katika ngazi za Mikoa na Wilaya unatekelezwa na Wasajili Wasaidizi katika maeneo hayo, kumekuwa na changamoto ya kuhodhi jukumu la ufuatiliaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika ngazi za Mikoa na Halmashauri na hivyo kukosekana takwimu sahihi ya Mashirika katika maeneo yao.

349. ***Mheshimiwa Spika***, lichaya mafanikio yaliyopatikana, changamoto kubwa iliyopo niuhaba wa Maafisa Maendeleo ya Jamii nchini. Hata hivyo, Serikali imeendelea kuajiri watumishi hao katika Halmashauri zote nchini. Kupitia ajira hizo, idadi ya Maafisa Maendeleo ya Jamii walioajiriwa katika Halmashauri na Mikoa mbalimbali nchini imeongezeka kutoka maafisa 2,846 mwaka 2018/19 hadi kufikia maafisa 2,983 Aprili, 2021 sawa na ongezeko la maafisa 137. Vilevile, takwimu za Halmashauri zinaonesha uwepo wa Maafisa Maendeleo ya Jamii 5,428 katika ngazi mbalimbali za Halmashauri. Hali hii inapelekea kuwepo kwa upungufu wa Maafisa Maendeleo ya Jamii 2,445 katika ngazi zote sawa na asilimia 45.

350. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuajiri Maafisa Ustawi wa Jamii katika maeneo mbalimbali ikiwemo Halmashauri ili kuwezesha upatikanaji wa huduma za ustawi wa jamii kwa wazee na watoto walio katika mazingira hatarishi. Hadi kufikia Aprili 2021, Maafisa Ustawi wa Jamii 740 wanafanya kazi katika ngazi mbalimbali za Serikali ikiwemo hospitali. Idadi hii inaonesha kuna upungufu wa asilimia 97 ya mahitaji halisi nchi nzima.

351. ***Mheshimiwa Spika, napenda kutumia Bunge lako Tukufu kuzielekeza Halmashauri zote nchini kutoa kipaumbele katika kuajiri Maafisa Maendeleo ya Jamii na Maafisa Ustawi wa Jamii katika ngazi zote za Mamlaka za Serikali za Mitaa ili***

**kupunguza uhaba uliopo na kuwezesha uratibu wa afua za maendeleo na ustawi wa jamii.**

352. ***Mheshimiwa Spika***, kama nilivyoeleza awali, Wizara imekuwa ikisimamia utekelezaji wa majukumu yake pia kuitia Taasisi zilizo chini yake ambapo katika mwaka 2020/21, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru ilipanga kukusanya kiasi cha **Shilingi 5,047,293,865** kutoka vyanzo mbalimbali. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, Taasisi imeweza kukusanya kiasi cha **Shilingi 3,157,867,683** sawa na asilimia 63 ya makadirio. Vilevile, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru imeendelea kutoa mafunzo ya maendeleo ya jamii katika ngazi ya Astashahada, Stashahada, Shahada na Shahada ya Uzamili. Katika kipindi cha mwaka 2020/21, Taasisi ilidahili wanafunzi 2,492 katika ngazi zote (Me 821 na Ke 1,671) ikilinganisha na wanafunzi 2,115 waliodahiliwa mwaka 2019/20 kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na.2**

**Jedwali Na.2:** Mwenendo wa Udhili Katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru (TICD)

Aina ya Mafunzo	2019/20			2020/21		
	Ke	Me	Jumla	Ke	Me	Jumla
Astashahada	744	226	970	870	357	1227
Stashahada	223	57	280	229	83	312
Shahada	476	351	827	553	366	919
Shahada ya Uzamili	21	17	38	19	15	34
<b>Jumla</b>	<b>1,464</b>	<b>651</b>	<b>2,115</b>	<b>1,671</b>	<b>821</b>	<b>2,492</b>

**Chanzo:** *TICD*

353. ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi pia imeendelea kuhakikisha Wataalam wa Maendeleo ya Jamii wanaohitimu na kwenda kufanya kazi katika maeneo mbalimbali wanakuwa na weledi wenyewe kukidhi soko la ajira. Taasisi ina jukumu la kuhakikisha kuwa wanafunzi wanamaliza masomo wakiwa na maarifa na ujuzi stahiki. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, wanafunzi 1,003 (Me 262 na Ke 741) walihitimu

katika fani na ngazi mbalimbali. Kati yao, wanafunzi 389 walihitimu katika ngazi ya Cheti (*Basic Certificate Level 4*), wanafunzi 215 katika ngazi ya Cheti (*Technician Certificate Level 5*), wanafunzi 224 katika Stashahada ya Maendeleo ya Jamii, wanafunzi 159 katika Shahada ya Maendeleoya Jamii na wanafunzi 16 katika Shahada ya Uzamili ya Maendeleo ya Jamii.

354. ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi imeshirikiana na Mkoa wa Arusha katika utatuzi wa changamoto mbalimbali za maendeleo katika jamii kwa kuandaa afua mbalimbali katika masuala ya lishe na changamoto zinazokabili maafisa maendeleo ya jamii. Vilevile, Taasisi imehamasisha jamii kushiriki katika utekelezaji wa shughuli na miradi ya maendeleo kwa kutumia rasilimali zinazoizunguka jamii. Mfano, Taasisi inashirikiana na jamii katika kuhamasisha ujenzi wa kivuko cha Mto Malala utakaogharimu **Shilingi 34,000,000**. Aidha, uhamasishaji wa wananchi katika mradi huu umeokoa kiasi cha **Shilingi 12,000,000** kwa jamii kutowana na ari ya kujitolea nguvu kazi.

355. ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi imeendelea kuchochaea na kuendeleza ubunifu (*innovation*) mionganoni mwa wanafunzi kuititia kituo cha Huduma Tandaa na Ubunifu wa Kidigitali. Kuititia kituo, wanafunzi wameunda vikundi vyta ujasiriamali na kuanza kujiajiri wakiwa chuo. Vilevile, Taasisi imeendelea kuwezesha wanafunzi kufanya uanagenzi katika mwaka wa masomo 2019/20, na hivyo kupata ujuzi wa kazi unaowezesha kuajiriwa au kujiajiri. Aidha, kituo hiki huwa kinaratibu na kuunganisha Idara za Kitaaluma na Wadau wa Uanagenzi (*apprenticeship stakeholders*) ili kuwawezesha wanachuo kutekeleza dhana ya uanagenzi. Kwa mfano, Taasisi ilianaa jukwaa la wadau 100 wa soko la ajira (*industry*) kwa ajili ya utekelezaji wa dhana ya uanagenzi. Hadi sasa Taasisi imeandaa kanzi data ya wadau (*apprenticeship stakeholders' database*) yenye wadau zaidi ya 200.

356. ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi kuititia Zahanati yake imeendelea kuwezesha huduma za Afya kwa wanafunzi, watumishi na wananchi walioko maeneo ya karibu. Baadhi

ya huduma zitolewazo na Zahanati ya Taasisi ni utoaji wa tiba kwa magonjwa mbalimbali (*outpatient clinic*), huduma kwa wateja wanaohitaji kulazwa muda mfupi, upimaji (*diagnostic services*), upasuaji mdogo (*minor surgery*), elimu ya afya kwa Jumuiya ya Taasisi na Wananchi na Huduma Tandaa (*outreach services*) kwa jamii katika eneo la afya. Zahanati inatoa huduma kwa kutumia kadi za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).

357. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu Taasisi ya Ustawi wa Jamii chini ya Wizara; Taasisi hii imeendelea kutoa mafunzo katika ngazi ya Astashahada, Stashahada, Shahada, Stashahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamili. Katika mwaka 2020/21, Taasisi ilipanga kukusanya kiasi cha **Shilingi 9,181,417,000** kutoka katika vyanzo mbalimbali. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, Taasisi iliweza kukusanya kiasi cha **Shilingi 7,018,551,123** ikiwa ni sawa na asilimia 76 ya makadirio.

358. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa masomo 2020/21, Taasisi imedahili wanafunzi 2,187 (Me 753 na Ke 1,434) ikilinganishwa na wanafunzi 1,799 waliodahiliwa mwaka wa masomo 2019/20 sawa na ongezeko la asilimia 22 kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na.3**

**Jedwali Na.3:** Wanafunzi Waliodahiliwa katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii

Na.	Aina ya Mafunzo	2019/20			2020/21		
		Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
1	Astashahada	249	671	920	375	545	920
2	Stashahada	48	177	225	145	402	547
3	Shahada	207	404	611	221	469	690
4	Stashahada ya Juu	15	10	25	8	12	20
5	Shahada ya Uzamili	5	13	18	4	6	10
<b>Jumla</b>		<b>524</b>	<b>1,275</b>	<b>1,799</b>	<b>753</b>	<b>1,434</b>	<b>2,187</b>

**Chanzo:** *Taasisi ya Ustawi wa Jamii*

359. ***Mheshimiwa Spika***, aidha, Taasisi imewezesha wanafunzi 1,246 (Me 318 na Ke 928) kuhitimu masomo katika fani na ngazi mbalimbali kwa mwaka 2019/20 ikilinganishwa na wanafunzi 1,368 (Me 393 na Ke 975) waliohitimu mwaka 2018/19. Kati yao, wanafunzi 538 wamehitimu katika ngazi ya

Astashahada, wanafunzi 378 wamehitimu ngazi ya Stashahada, wanafunzi 288 wamehitimu ngazi ya Shahada, wanafunzi 21 wamehitimu ngazi ya Stashahada ya Juu na wanafunzi 21 wamehitimu ngazi ya Shahada ya Uzamili.

360. ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi ya Ustawi wa Jamii imeendelea kufanya kazi kwa karibu na Serikali za Mitaa na Wilaya na katika Kampasi yake ya Kisangara imeratibu ujenzi wa Kituo cha Malezi ya Watoto baada ya jamii kuliibua kama tazito linalowakabili ambapo ujenzi upo katika hatua za kukamilika. Vilevile, Taasisi ina Programu ya Uanagenzi (Apprenticeship) inayounganisha wanafunzi na waajiri ikiwa ni nafasi ya kuwapa wanafunzi mafunzo ya vitendo kwa kipindi cha miezi sita (6). Kwa sasa programu ina wanafunzi 96 walipo katika Taasisi mbalimbali.

361. ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi hii pia imeendelea kutoa ushauri nasaha na upimaji wa VVU kwa wanafunzi, wafanyakazi na jumuiya inayoizunguka. Aidha, imeendelea kutoa msaada wa kisaikolojia na kijamii, ushauri wa kisheria katika malezi na ndoa na ushauri wa matumizi ya dawa za kulevyta katika shule za msingi na sekondari zinazoizunguka. Vilevile, Taasisi imekuwa ikifanya kazi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo Hospitali ya Mwananyamala, Marie Stopes, TAYOA, TACAIDS na WAMATA.

#### **F. VIPAUMBELE VYA WIZARA NA BAJETI YA MAPATO, MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2021/22**

##### **IDARA KUU YA AFYA (FUNGU 52)**

362. ***Mheshimiwa Spika***, katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2021/22, Wizara imeainisha vipaumbele vitakavyozingatiwa katika kuboresha utoaji wa huduma za afya nchini ambavyo ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha huduma za afya nchini zikiwemo huduma zitakazopelekea kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi, watoto wachanga na watoto wenye umri chini ya miaka mitano;

- (ii) Kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kulingana na mahitaji halisi katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya nchini;
- (iii) Kuimarisha utoaji wa huduma za afya kuanzia ngazi ya Afya ya Msingi, hospitali za rufaa ngazi ya Mkoa, Kanda na Taifa kwa kukamilisha ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma za afya;
- (iv) Kuimarisha mfumo wa bima ya afya nchini ili kufikia lengo la Serikali la kuwa na bima ya afya kwa wananchi wote;;
- (v) Kuongeza udahili wa wanafunzi wa kada mbalimbali za afya kwa kuimarisha miundombinu katika vyuo vya afya nchini;
- (vi) Kuimarisha utoaji wa mafunzo ya wataalam bingwa na bobezi katika sekta ya afya ikiwa ni pamoja na kutumia utaratibu wa mafunzo ya kibingwa na bobezi wakiwa kazini (Fellowship Training Programme);
- (vii) Kuimarisha huduma za matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Mifupa MOI, JKCI, Ocean Road Cancer Institute, Hospitali ya Benjamini Mkapa kufikia viwango vya kimataifa ili kukidhi mahitaji ya hapa nchini na kuhudumia wagonjwa kutoka nje ya nchi;
- (viii) Kuweka mazingira wezeshi ya ukusanyaji wa damu salama na mazao yake katika mikoa mitano ya Dodoma, Mbeya, Kigoma, Mtwara na Mwanza ili kukidhi mahitaji;
- (ix) Kuimarisha huduma za dharura katika Hospitali za Kanda ikiwemo Hospitali ya Benjamini Mkapa ili iweze kumudu ongezeko la mahitaji ya huduma za dharura kutokana na Serikali kuhamishia Makao Makuu ya nchi Dodoma;
- (x) Kuimarisha mpango wa Taifa wa utayari wa kukabiliana na magonjwa ya milipuko, ajali na majanga kwa kuboresha huduma za dharura na uokoaji ikiwemo miundombinu na vitendea kazi;

- (xi) Kudhibiti magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza nchini; na
- (xii) Kusimamia ubora, usalama na ufanisi pamoja na kufanya tafiti mbalimbali zinazohusiana na Tiba Asili na Tiba Mbadala Nchini.

363. ***Mheshimiwa Spika***, ili kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika mwaka 2021/22, Wizara imekadria kutumia kiasi cha **Shilingi 1,034,133,295,000** zitakazotumika kutekeleza majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na uendeshaji wa ofisi na miradi wa maendeleo. Baadhi ya maeneo yaliyotengewa fedha kwa mwaka 2021/22 ni pamoja na:-

- (i) Ununuzi na usambazaji wa chanjo **Shilingi bilioni 63.2** zimetengwa;
- (ii) Ununuzi na Usambazaji wa Dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi ambapo **Shilingi bilioni 263.8** zimetengwa ambapo kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 45.8** ni kwa ajili ya Miradi Misonge ambayo ni UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu;
- (iii) Kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma katika Hospitali ya Taifa, Hospitali Maalum, Hospitali za Rufaa za Kanda na Hospitali za Rufaa za Mikoa, **Shilingi bilioni 105.9** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa miundombinu katika Hospitali hizo;
- (iv) Kuendelea kuimarisha huduma za kibingwa na ubingwa bobezi katika Hospitali ya Taifa, Hospitali Maalum, na Hospitali za Rufaa za Kanda ambapo, kiasi cha **Shilingi bilioni 6.8** kimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na vifaa tiba; na
- (v) Kuboresha miundombinu ya vyuo vya afya na kugharamia mafunzo na maendeleo ya wataalam katika Sekta ya Afya, kiasi cha **Shilingi bilioni 11.1** zimetengwa kwa ajili ya kugharamia mitihani, chakula na ukarabati wa miundombinu ya Vyuo vya Afya.

## **IDARA KUU YA MAENDELEO YA JAMII (FNGU 53)**

364. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/22, Wizara kupitia Idara zake zilizo chini ya Fngu 53 itatekeleza vipaumbele 14 ili kuboresha utoaji huduma za ustawi wa jamii na maendeleo ya jamii:-

- (i) Kukuza ari ya jamii, uzalendo na kujenga moyo wa kujitolea katika kujiletea maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa kutumia nguvukazi na rasilimali zinazowazunguka;
- (ii) Kutekeleza dhana ya uanagenzi, ubunifu na ushirikishwaji jamii kwenye Taasisi na Vyuo ili kuzalisha wanafunzi wanaoajirika na kujajiri na kuwa chachu ya maendeleo;
- (iii) Kuratibu uwezeshaji wa wanawake kiuchumi na uingizaji wa masuala ya jinsia katika Sheria, Sera, Mipango, Mikakati, Programu na Bajeti;
- (iv) Kuendelea kuimarisha huduma za ustawi wa jamii na haki kwa familia na watoto ikiwemo malezi ya kambo na kuasili, watu/walezi wa kuaminika, malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya watoto, ulinzi na usalama kwa watoto dhidi ya vitendo vya ukatili pamoja na huduma za utengemao katika familia kwa watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani;
- (v) Kuimarisha huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa na familia, Msaada wa Kisaikolojia na Kijamii kwa familia, jamii na makundi mbalimbali wakiwemo wazee, watoto walio katika mazingira hatarishi pamoja na wahanga wa ukatili na majanga mbalimbali;
- (vi) Kuimarisha ufuatiliaji na uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili yaweze kutoa mchango chanya katika ujenzi wa Taifa;
- (vii) Kuendelea kuratibu kampeni mbalimbali za kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto;
- (viii) Kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii

Tengeru na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ili kutoa mafunzo yanayokidhi mahitaji ya soko;

(ix) Kusimamia, kufuatilia na kuimarisha uanzishaji na uendelezaji wa Vituo vya Kulelea Watoto Wadogo na Vituo vya Kijamii vya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto katika ngazi ya jamii ili kuboresha malezi na makuzi ya kila mtoto;

(x) Kuendelea kuimarisha utoaji wa huduma za msingi katika Vituo vya Ustawi wa Jamii ikiwemo Makazi ya Wazee na Watu wenyewe Ulemavu, Mahabusu za Watoto, Makao ya Watoto na Shule ya Maadilisho;

(xi) Kuimarisha mifumo ya kusimamia, kufuatilia na kutathmini viwango vya huduma za ustawi wa jamii zinazotolewa nchini;

(xii) Kuanzisha na kuimarisha utendaji wa Mabaraza ya Watoto na Dawati la Ulinzi la Watoto Shuleni;

(xiii) Kuendelea kuratibu uundwaji wa Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto pamoja na kuzijengea uwezo;

(xiv) Kuratibu uanzishwaji wa Vikundi vya Malezi katika ngazi ya jamii; na

(xv) Kuhamasisha ushiriki wa wanawake katika ngazi za uongozi na nafasi mbalimbali za maamuzi.

365. ***Mheshimiwa Spika***, ili kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa hapo juu, Wizara kwa mwaka 2021/22 imekadiria kutumia kiasi cha **Shilingi bilioni 43.6** ili kutekeleza majukumu mbalimbali kupitia Idara zake kama ilivyoainishwa kwenye kila Idara kama ifuatavyo hapa chini.

## **IDARA YA MAENDELEO YA JAMII**

366. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza ushiriki wa wananchi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye maeneo yao na maendeleo ya mtu mmoja mmoja katika jamii, katika mwaka 2021/22, Wizara itaendelea kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kuendesha Kampeni ya Kitaifa ya kuamsha ari ya jamii kuhusu ujenzi wa nyumba bora za gharama nafuu na teknolojia rahisi;
- (ii) Kuendesha Kampeni ya kukuza uzalendo kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu na kati;
- (iii) Kukarabati majengo na miundombinu katika Vyuo nane vya Maendeleo ya Jamii;
- (iv) Kuboresha utoaji wa mafunzo ya taaluma ya maendeleo ya jamii ili kukidhi mahitaji ya soko na kutekeleza dhana ya uanagenzi, kukuza ujuzi wa wahitimu na kuwajengea uwezo wa kujajiri na kuajiriwa; na
- (v) Kutekeleza mpango wa ushirikishaji jamii ili kutoa suluhihisho kwa changamoto zinazoilkabili jamii.

#### **IDARA YA MAENDELEO YA MTOTO**

367. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha 2021/22, ili kuimarisha utoaji wa haki za watoto nchini, Wizara itaendelea kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kuratibu uanzishwaji wa madawati ya ulinzi wa watoto shuleni katika Halmashauri zote nchini;
- (ii) Kuendeleza kampeni za kupinga ndoa na mimba za utotoni, ukeketaji na aina zote ukatili kwa watoto kuititia radio za kijamii kwa kutumia jumbe mahsusini katika mikoa ya Mbeya, Iringa, Songwe, Njombe na Kigoma;
- (iii) Kuendelea kutoa elimu ya malezi chanya kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii, Ustawi wa Jamii, Walimu na Watumishi wa Afya katika mikoa ya Tanzania Bara;
- (iv) Kukamilisha Ajenda ya Taifa ya Malezi Chanya kwa Familia na kusambaza nchi nzima; na

(v) Kuratibu utekelezaji wa Ajenda ya Kitaifa ya Kuwekeza katika Afya na Mandeleo kwa Vijana Balehe nchini 2021/22-2024/25.

## **IDARA YA USTAWI WA JAMII**

368. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/22, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaendelea kuboresha utoaji wa huduma za ustawii wa jamii kwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kuimarisha utendaji na kuwezesha upatikanaji wa huduma za msingi katika makao ya Taifa ya Watoto ya Kurasini - Dar es Salaam na Kikombo – Dodoma, Shule ya Maadilisho Irambo, mahabusu 5 za watoto pamoja na Mahakama za Watoto;
- (ii) Kuwezesha uhamisho wa Watoto pamoja na watumishi kutoka Makao ya Taifa ya Watoto – Kurasini kuja Kikombo – Dodoma;
- (iii) Kuwezesha mafunzo ya ufundi stadi, ujasiriamali na stadi za maisha kwa watoto waliokinzana na sheria katika mahabusu za watoto pamoja na Shule ya Maadilisho;
- (iv) Kuwezesha kuwaunganisha na familia zao watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani katika mikoa 26 nchini;
- (v) Kuwezesha upatikanaji wa mahitaji ya msingi kwa wazee 300 pamoja na upatikanaji wa huduma za ustawii wa jamii kwa wazee katika Makazi ya Wazee 13 nchini;
- (vi) Kuwezesha uhamisho wa Wazee katika Makazi ya Wazee 4 yanayotarajiwaa kufungwa;
- (vii) Kuwezesha maadhisho ya siku ya kupinga ukatili dhidi ya Wazee na Siku ya Kimataifa ya Wazee;
- (viii) Kufanya utafiti wa tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Wazee (2003) na Kusambaza Sera ya Taifa ya Wazee iliyofanyiwa Mapitio;

- (ix) Kuwezesha utengamao wa kijamii kwa wazee wanahudumiwa katika makazi ya Wazee;
- (x) Kuwezesha upatikanaji wa bima ya afya ya jamii iliyoboreshwa kwa wazee 411 wanaohudumiwa katika Makazi ya Wazee na maveterani wa vita kuu ya pili ya dunia;
- (xi) Kufanya ukaguzi wa viwango na ubora wa huduma katika vituo vyá kulelea watoto wadogo mchana na Makao ya Watoto katika mikoa 10 nchini;
- (xii) Kuwezesha uendeshaji wa Baraza la Kamishna wa Ustawi wa Jamii la Usuluhihi wa Ndoa ikiwa ni jitihada za kuimarisha malezi chanya na mahusiano katika familia pamoja na kuanzisha huduma ya msaada wa kiasikolojia kupitia Baraza la Kamishna wa Ustawi wa Jamii la Usuluhihi wa Ndoa;
- (xiii) Kuwezesha watumishi kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na ya muda mfupi;
- (xiv) Kuwezesha utungaji wa sheria ya taaluma ya Ustawi;
- (xv) Kuwajengea uwezo maafisa Ustawi wa Jamii wanaohudumia katika mahakama za watoto;
- (xvi) Kufanya mapitio ya mwongozo wa huduma za malezi ya kambo na kuasili;
- (xvii) Kufanya ufuatilaji wa ubora ubora wa huduma za Ustawi wa Jamii katika magereza, shule, vituo vyá afya, madawati ya Jinsia na Watoto ya Polisi na Mahakama za Watoto katika mikoa 26;
  
- (xviii) Kuwezesha Maafisa Ustawi kushiriki Kongamano la Maafisa Ustawi wa Jamii; na
- (xix) Kuweka mazingira bora ya ufundishaji na kujifunza katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii.

## **IDARA YA MAENDELEO YA JINSIA**

369. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/22, Wizara itaendelea kutekeleza afua mbalimbali za kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi kwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kufanya Kampeni ya kupinga vitendo vya Ukatili wa Kijinsia ijulikanayo kama "Twende Pamoja: Ukatili Tanzania Sasa Basi" katika Kanda 7;
- (ii) Kuwezesha ushiriki wa Viongozi na Maafisa wa Wizara kwenye mikutano ya Kikanda na Kimataifa kuhusu masuala ya kijinsia;
- (iii) Kuratibu uanzishaji wa Madawati ya Jinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu na Katil;
- (iv) Kufundisha Wanawake kuhusu uzalishaji wa kuku na kilimo cha bustani;
- (v) Kuwezesha makongamano ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi katika kanda 7; na
- (vi) Kuratibu Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, Siku ya Wajane, Siku ya Siku ya Mwanamke anayeishi Kijijini na Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia.

## **IDARA YA URATIBU WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI**

370. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/22, Wizara itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kushiriki kikamilifu katika kuchangia maendeleo na ustawi wa jamii kwa kutekeleza yafuatayo:-

- (i) Kufanya ufuutiliaji wa takriban Mashirika 1,000 katika maeneo ya Tanzania Bara;

- (ii) Kuwezesha usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 500 na uhuishaji wa vyeti vipyta kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 5,500 kwa mujibu wa Sheria Na. 3/2019 katika ngazi ya Wilaya, Mkoa, Taifa na Kimataifa;
- (iii) Kuwezesha vikao vya Mashirikiano kuhusu uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali baina ya Tanzania Bara na na Zanzibar;
- (iv) Kuwezesha kufanya kwa jukwaa la mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;
- (v) Kufanya utafiti kuhusu mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kuandaa taarifa ya mchango wa Mashirika hayo kwa mwaka;
- (vi) Kuwezesha ulipaji wa gharama za uendeshaji na umiliki wa mfumo wa kielektroniki wa usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;
- (vii) Kufanya mafunzo kwa Wasajili Wasaidizi na wadau wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali juu ya Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo inayosimamia uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali; na
- (viii) Kuwezesha vikao vya Bodi ya uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

## **G. SHUKRANI**

371. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imekuwa ikipata ushirikiano mkubwa kutoka nchi rafiki, Mashirika ya Kimataifa na sekta nyingine zinazosaldia na kuchangia katika huduma za Afya, Maendeleo na Ustawi wa Jamii.

372. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kuchukua nafasi hii ya kipekee kuzishukuru nchi za Canada (DFATD), Denmark (DANIDA), na Ireland (Irish Aid), Uswisi (SDC), Korea Kusini (KOICA) na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa yakiwemo

Benki ya Dunia, UNICEF, kwa kuchangia katika Mfuko wa Afya wa Pamoja (Health Basket Fund), ambao umesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma za afya nchini. Aidha, napenda kuzishukuru nchi za China, Cuba, India, Italia, Japan, Marekani, Misri, Sweden, Uingereza, Ujeruman na Ufaransa na nchi nydingine ambazo zimeendelea kuisaidia Wizara kwa njia mbalimbali.

373. ***Mheshimiwa Spika***, nayashukuru pia mashirika mengine ya Kimataifa kwa ushirikiano wao waliotoa kwa Wizara. Mashirika hayo ni pamoja na: Mashirika yaliyo chini ya Umoja wa Mataifa (UNAIDS, UNDP, UNFPA, UN-Women, WHO na IAEA); Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU); Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB); GAVI; PEPFAR; CDC; USAID; PMI; Abbott Fund; DFID; EED; Elizabeth Glaser Paediatric Aids Foundation (EGPAF); GIZ; Global Fund (for HIV, TB na Malaria); Bill and Melinda Gates Foundation; Good Samaritan Foundation (GSF); HelpAge International; John Snow Incorporation (JSI); JICA; KfW; Save the Children; World Vision; Benki ya STANBIC; na Walter REED.

374. ***Mheshimiwa Spika***, niwashukuru watu binafsi, vyama vyaa hiari na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya ndani ya nchi kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za afya. Mashirika hayo ni pamoja na Benjamin William Mkapa HIV/AIDS Foundation, AGOTA, Aga Khan Foundation, APHFTA, AMREF, AGPAHI, APT, BAKWATA, CSSC, CCT, Counsenuth, ELCT, Ifakara Health Institute, Lions Club, MAT, AFRICARE, Msalaba Mwekundu, MEHATA, MEWATA, TAMWA, TAWLA, TGNP, MDH, MeLSAT, PASADA, PAT, PSI, PRINMAT, Rotary Club International, SIKIKA, Shree Hindu Mandal, TANNA, TPHA, TPRI, Tanzania Surgical Association (TSA), Tanzania Diabetic Association, TANESA, THPS, TUNAJALI, Tanzania Midwife Association, TDA, TAYOA, TISS, TEC, UMATI, USADEFU, White Ribbon Alliance, LSF, Plan International - Tanzania, Kivulini, WiLDAF, TCRF, FSDT, Haki Elimu, SOS Children Tanzania, TWCC, Compassion International, Care International Tanzania, TECDEN na Pact Tanzania.

375. **Mheshimiwa Spika**, nazishukuru Taasisi mbalimbali za Serikali zikiwemo SIDO, BRELA na TBS. Aidha, navishukuru Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam, Muhimbili, Sokoine, Ardhi, Mzumbe, Dodoma, Chuo Kikuu Huria, Kumbukumbu ya Herbert Kairuki, IMTU, Tumaini, St. Agustino, CUHAS, Sebastian Kolowa, St. John, Aga Khan, Morogoro Muslim, Taasisi ya Teknolojia ya Nelson Mandela, Arusha pamoja na Vyuo vyote vilivyo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za afya na maendeleo ya jamii. Aidha, nawashukuru wadau wengine waliota huduma ya elimu kwa njia za radio, televisheni, magazeti na mitandao ya kijamii katika masuala ya afya na maendeleo ya jamii, hususan katika mapambano dhidi ya Corona nchini.

376. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha utendaji wangu wa kazi nikiwa Waziri, nimepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Napenda kumshukuru **Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel (Mb.)**, Naibu Waziri wa Afya, **Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis (Mb.)**, Naibu waziri Maendeleo ya Jamii, kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, naomba kuwashukuru **Prof. Abel N. Makubi** Katibu Mkuu (Afya) na **Dkt. John K.Jingu** Katibu Mkuu (Maendeleo ya Jamii) kwa mchango wao katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu yangu. Vilevile, nawashukuru **Dkt. Alfello W. Sichalwe** Mganga Mkuu wa Serikali, Makamishna, Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo vya Wizara. Nawashukuru pia wakurugenzi wakuu wa Hospitali za Taifa na Kanda ambao ni **Prof. Lawrence M. Museru** (Hospitali ya Taifa Muhimbili), **Dkt. Respicious L. Boniface** (Taasisi ya Mifupa MOI), **Prof. Mohamed Janabi** (Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete), **Dkt. Julius Mwaiselage**, (Taasisi ya Saratani ya Ocean Road), **Dkt. Alphonce Chandika** (Hospitali ya Benjamin Mkapa), **Dkt. Riziki M. Kisonga** (Hospitali ya Kibong'oto), **Dkt. Paul S. Lawala** (Hospitali ya Mirembe) na Wakurugenzi wa Hospitali za Rufaa za Kanda **Dkt. Godlove Mbwanji** (Hospitali ya Rufaa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya), **Dkt. Fabian A. Massaga** (Hospitali ya Bugando) na **Prof. Geleard Masenga** (Hospitali ya KCMC).

377. ***Mheshimiwa Spika***, kipekee naomba kuwashukuru wakurugenzi na wakuu wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ambazo ni MSD, NHIF, TMDA, NIMR, Mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali, TFNC, Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru pamoja na Mabaraza ya Kitaaluma na Bodi za Usajili, Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Waganga Wafawidhi wa Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati, Wakuu wa Vyuo vya Mafunzo vilivyo chini ya Wizara na wafanyakazi wote wa Wizara na Mashirika ya Dini, Mashirika ya Kujitolea na Mashirika Binafsi. Natoa shukrani kwa sekta zote ambazo tunashirikiana nazo katika kutoa huduma za afya, maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii pamoja na wananchi wote kwa ushirikiano wao. Nawaasa waendelee kuzingatia misingi ya huduma bora na kufanya kazi kwa bidii kwa manufaa ya Taifa letu.

378. ***Mheshimiwa Spika***, nichukue fursa hii pia kuishukuru familia yangu, kwa uvumilivu wao na kwa kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa. Aidha, nawashukuru wananchi wote wa Tanzania kwa kunipatia ushirikiano wakati wa kutekeleza majukumu yangu. Naahidi kuwa nitaendelea kuwaenzi na kuwatumikia kwa nguvu zangu zote ili kuleta mabadiliko ya haraka ya kimaendeleo.

## I. MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA 2021/22

### IDARA KUU YA AFYA (FUNGU 52)

#### Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2021/22

379. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/22, Wizara na Taasisi zilizo chini yake inakadiria kukusanya kiasi cha **Shilingi 507,218,152,321** ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi 81,717,635,624** zinatarajiwa kukusanya kutoka vyanzo vya ndani Makao Makuu ya Wizara, **Shilingi 92,044,336,376** kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa na **Shilingi 333,456,180,321** zinatarajiwa kukusanya kutoka Taasisi zilizo chini ya Wizara na Hospitali ya Taifa.

### **Matumizi ya Kawaida**

380. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/22, Wizara kupitia Fungu 52imepanga kutumia **Shilingi 557,303,059,000** nikwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo kati ya hizo kiasi cha **Shilingi 252,523,260,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na kiasi cha **Shilingi 304,779,799,000**ni kwa ajili ya Mishahara ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake.

### **Miradi ya Maendeleo**

381. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2021/22, Wizara imetenga kiasi cha **Shilingi 476,830,236,000** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 351,700,000,000**ni fedha kutoka vyanzo vya ndani, na **Shilingi 125,130,236,000**ni fedha kutoka vyanzo vya nje.

382. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2021/22 Wizara (Idara Kuu ya Afya – Fungu 52) inaomba jumla ya **Shilingi 1,034,133,295,000** ili kuweza kutekeleza na kutimiza malengo iliyojewekea.

## **IDARA KUU YA MAENDELEO YA JAMII (FNGU 53)**

### **Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2021/22**

383. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/22, Wizara imekadiria kukusanya **Shilingi 6,000,000,000** kutokana na ada na tozo mbalimbali za usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, mapato ya ada za mitihani na uuzaji wa mitaala ya Mafunzo ya Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii na mapato mengine.

### **Matumizi ya Kawaida**

384. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/22, Wizara inakadiria kutumia kiasi cha **Shilingi 28,725,929,000**kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 12,985,672,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya watumishi na **Shilingi 15,740,257,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

## Miradi ya Maendeleo

385. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa shughuli za maendeleo, Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 14,900,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 4,900,000,000** ni Fedha za Ndani na **Shilingi 10,000,000,000** ni Fedha za Nje.

386. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2021/22, Wizara (Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii - Fungu 53) inaomba jumla ya **Shilingi 43,625,929,000**.

387. **Mheshimiwa Spika**, jumla ya fedha zote zinazoombwwa na Wizara kwa Mafungu yote (Fungu 52 na Fungu 53) ni **Shilingi 1,077,759,224,000** kama inavyoonesha kwenye Jedwali lifuatalo.

Na	Fungu	Matumizi ya Kawaida	Miradi ya Maendeleo	Jumla
1.	Fungu 52	557,303,059,000	476,830,236,000	<b>1,034,133,295,000</b>
2	Fungu 53	28,725,929,000	14,900,000,000	<b>43,625,929,000</b>
	<b>Jumla</b>	<b>586,028,988,000</b>	<b>491,730,236,000</b>	<b>1,077,759,224,000</b>

388. **Mheshimiwa Spika**, Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto [www.moh.go.tz](http://www.moh.go.tz) na [www.jamii.go.tz](http://www.jamii.go.tz).

389. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimwa Wabunge hoja imeungwa mkono tutaendelea na utaratibu wetu ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa afya. Nimuite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii Mheshimiwa Stanslaus Nyongo.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELO YA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ifuatayo ni taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya bajeti ya Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na maoni ya kamati kuhusu makadirio na mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 118(9) ya kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni 2020 napenda kushukuru kwa kunipa wasaa wa kuweza kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto kwa mwaka 2021 pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya kamati kuhusu makadirio na mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba taarifa ya kamati yote iingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo, Kamati ilichambua na yafuatayo ni maelezo ya uchambuzi huu kuhusu ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Kwa mujibu wa kanuni ya 117(1) ya kanuni za Bunge za kudumu Toleo la Juni 2020 kamati ya kudumu ya Bunge ya huduma na Maendeleo ya Jamii ilifanya ziara ya ukaguzi wa baadhiya miradi ya maendeleo iliyoengewa fedha katika mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipata wasaa wa kukagua miradi mitatu ambayo ni mradi wa taasisi ya saratani ya *Ocean Road*, mradi wa taasisi ya mifupa ya Muhimbili (*MOI*) na mradi wa taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete. Hali ya miradi hiyo Pamoja na maoni na ushauri wa Kamati ni kama ilivyoonekana kwenye taarifa kuanzia ukurasa wa 2 hadi ukurasa wa 9.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifuatacho ni uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti na uzingatiaji wa maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Wizara kuitia fungu 52 Idara Kuu ya Afya katika mwaka wa fedha 2021 ilikadiria kukusanya maduhuli ya shilingi bilioni 467.7 na kufika Februari 2021 makusanyo yalikuwa ni asilimia 53.6 kama inavyoonekana kwenye kielelezo tulichokitoa Na.1 na ukurasa namba 9 hadi ukurasa namba 11 wa taarifa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii Fungu 53 katika mwaka wa fedha 2020/2021 makadirio yalikuwa ni kukusanya maduhuli ya shilingi bilioni 5.4 kufika Februari 2021 makusanyo yalikuwa shilingi bilioni 3.1 sawa na 58% kama inavyoonekana kwenye kielelezo tulichokitoa Na. 2 maeleo ya kina ya sababu za makusanyo hayo kuwa madogo na mengine kuzidi kuwa kwenye taarifa kuanzia ukurasa wa 12 hadi wa 13 wa taarifa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliangalia vilevile upatikanaji wa fedha kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara kuitia Fungu 52 iliidhinishiwa na Bunge lako tukufu jumla ya shilingi bilioni 900 kufika Machi 2021 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 409 sawa na asilimia 45.4% kama inavyoonekana kwenye kielelezo Na. 3 tulichokitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Fungu 53 Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii kufika Februari 2021 imefanikiwa kupokea kiasi cha shilingi bilioni 17.6 sawa na asilimia 53% ya shilingi bilioni 33.195 zilizoidhinishwa kama inavyoonekana kwenye kielelezo namba 4 tulichokitoa. Maeleo ya mchanganuo wa fedha hizi ni kama inavyoonyeshwa kwenye taarifa ya kamati kuanzia ukurasa wa 13 hadi ukurasa wa 18.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulifanya uchambuzi wa mpango wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Kamati imefanya uchambuzi wa mchanganuo wa shughuli za Wizara kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka fedha 2021/2022 makadirio na makusanyo ya maduhuli ya Fungu 52 katika mwaka wa fedha 2021/2022 ni jumla ya shilingi bilioni 507.2 mchanganuo ni kama unavyoonekana kwenye kielelezo tulichokitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa kamati umebaini kuwa makadirio yam waka wa fedha 2021/2022 ni ongezeko la 8.4% ya makadirio ya makusanyo katika mwaka wa fedha 2021. Ongezeko Zaidi linaonekana katika vyanzo vya Wizara ambavyo kuna ongezeko la 59.7%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Fungu 53 katika mwaka wa fedha 2021/2022 imekadirwa kukusanya makusanyo yaani maduhuli ya shilingi bilioni 6 sawa na ongezeko la 10.72% ikilinganishwa na mwaka wa fedha wa 2021/2022 maelezo na sababu ya ongezeko la taarifa ya kamati iko katika ukurasa wa 21.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulifanya uchambuzi wa makadirio na matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022, katika eneo hili kamati imefanya uchambuzi wa aina mbili kama ifuatavyo: uchambuzi wa kwanza ulikuwa ni wa bajeti ya Wizara Fungu 52 na 53 kwa mwaka wa fedha mwaka 2020/2021 na 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara kupitia Fungu 52 Idara Kuu ya Afya inaomba kuidhinishiwa shilingi trillioni 1.03 sura ya bajeti ya Wizara kama inavyoonekana kwenye kielelezo namba 8 tulichokitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa kina wa kamati umebaini kuwa bajeti ya Fungu 52 imeongezeka kwa asilimia 15 kutoka shilingi bilioni 900 ya mwaka 2021 ongezeko Zaidi ni kwneye OC kwa asilimia 39. Fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutoka ndani kwa asilimia 25 na fedha za nje kwa asilimia 56 kama inavyoonekana kwenye kielelezo namba 9 tulichokitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilihoji sababu ya ongezeko hilo na ilielezwa kuwa ni kutokana na mahitaji yaliyopo ya kukamilisha miradi mbalimbali ili ianze kutoa huduma Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hii muhiu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii Fungu 53 katika mwaka wa fedha 2021/2022, inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 43.6 fedha hizo zinajumuisha matumizi ya kawaida asilimia 65.5 na miradi ya maendeleo ambayo ni asilimia 34.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati imebaini kuwa bajeti imeongezeka kwa asilimia 31 ya ongezeko Zaidi ni kwenye miradi ya maendeleo kwa asilimia 122.2 Kamati inaipongeza sana Serikali kwa ongezeko hilli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele kingine cha (b) tulichambua bajeti ya Wizara dhidi ya bajeti ya mpango wa maendeleo wa Taifa ya mwaka 2020/2021 na 2021/2022. Uchambuzi huu ulilenga katika kubaini ni kwa kiwango gani ongezeko au upungufu wa bajeti ya Taifa unaoathiri bajeti ya Fungu 52 katika uchambuzi huo Kamati imebaini yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati bajeti ya Taifa kwa mwaka 2021/2022 imeongezeka kwa 3.95% kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na.11, bajeti ya Fungu 52 imeongezeka kwa 14.9% kama inavyoonekana kwenye kielelezo tulichokitoa cha namba 9. Vilevile, wakati bajeti ya Taifa ya maendeleo imeongezeka kwa asilimia 2.76, bajeti ya Fungu 52 kwa ajili ya maendeleo imeongezeka kwa asilimia 32.1. Wakati bajeti ya Taifa ya matumizi mengineyo imeongezeka kwa asilimia 5.42, bajeti ya matumizi mengineyo ya Fungu 52 imeongezeka kwa asilimia 39.1. Tafsiri tunayopata katika uchambuzi huu ni kuwa, licha ya ongezeko dogo katika bajeti ya Taifa, Iakini bajeti ya Wizara hii imepewa kipaumbele zaidi. Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imefanya pia uchambuzi wa kulinganisha asilimia ya bajeti ya matumizi mbalimbali ya Fungu 52 kati ya mwaka 2020/2021 na 2021/2022 dhidi ya bajeti ya Taifa na imebaini yafuatayo:-

(i) Bajeti ya Fungu 52 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) dhidi ya bajeti ya Taifa imeongezeka kutoka asilimia 4.85 mwaka 2020/2021 hadi kufikia asilimia 6.40 mwaka 2021/2022; na

(ii) Bajeti ya maendeleo ya Fungu 52 dhidi ya bajeti ya Taifa ya maendeleo imeongezeka kutoka asilimia 2.8 mwaka 2020/2021 hadi kufikia asilimia 3.6 mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla bajeti ya Fungu 52 imeongezeka kutoka asilimia 2.58 mwaka 2020/2021 hadi kufikia asilimia 2.85 mwaka 2021/2022 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na.11, (a) na (b) kama tulivyokitoa. Kamati inaendelea kuipongeza sana Serikali na kusisitiza kiasi hiki cha fedha kitolewe chote na kiendelee kuongezwa mwaka hadi mwaka ili kuendelea kuboresha sekta hii muhimu kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla. Mheshimiwa Mahatma Gandhi amewahi kusema "*It is health that is real wealth and not pieces of gold and silver*" maana yake ni kwamba afya ina thamani kubwa kuliko vipande vya dhahabu na fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifuatacho sasa ni maoni na ushauri wa mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, Idara Kuu ya Afya - Vifo vya Mama na Mtoto. Mojawapo ya Vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2021/2022 ni kupunguza vifo vya akina mama vinavyotakana na uzazi pamoja na watoto. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, kiasi cha shilingi bilioni 63. 4 kinaombwa kwa ajili ya kupunguza vifo vya mama na mtoto. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa, bado fedha zinazotengwa kwa mradi huu hazitolewi za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa hotuba nzuri alioitoa siku ya tarehe 22 Aprili 2021 wakati analihutubia Bunge kwa kusema: "Katika miaka hii mitano mpaka 2025, juhudzi za kupunguza vifo vya wajawazito na watoto zitaendelezwa" na kuwa radi huu ni wake wa moyoni kabisa.

Kamati inaendelea kusitiza Serikali kuongeza bajeti lakini pia kuhakikisha fedha zote zinazotengwa zinatolewa kwa wakati ili kupunguza vifo hivi ambapo kwa takwimu za Umoja wa Mataifa za 2018, Tanzania ina vifo 398 kwa kila vizazi hai 100,000 wakati Lengo Namba 3 (1) la *SDG* linataka kufikia mwaka 2030, kupunguza vifo vya akina mama na watoto duniani hadi chini ya vifo 70 kwa kila vizazi hai 100,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili, Huduma Maalum kwa Watoto Njiti. Kamati inasema kuwa upatikanaji wa huduma kwa watoto wachanga wanaozaliwa kabla ya umri wao kutimia na wakiwa na uzito pungufu yaani njiti bado ni changamoto kwani hakuna watumishi, wauguzi na wahudumu wa kutosha, vifaa na vifaa tiba pamoja na bima ya afya. Ili kuondoa changamoto hizo, Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Vifaa na vifaa tiba vya kutosha viwepo vya kusaidia watoto kupumua;

(ii) Serikali iweke utaratibu utakaowezesha watoto njiti kupata huduma ya bima kwa kutumia kadi ya wazazi mpaka kadi ya mtoto itakapokuwa tayari;

(iii) Serikali iandae eneo na kujenga Jengo Maalum kwa ajili ya uangalizi wa watoto njiti ikiwa ni pamoja na watoto njiti wanaohudhuria kliniki ili wasichangamane na wengine ili kuepuka kusababisha maambukizi kwao kutokana na eneo la sasa kuwa dogo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili;

(iv) Ili kuboresha utoaji wa huduma, wauguzi waongezwe katika hospitali zote nchini ikiwemo Hospitali ya Taifa Muhimbili ambayo kimsingi imegawanywa katika maeneo makuu matatu ambayo ni wodi ya watoto njiti, wodi ya watoto wanaohitaji uangalizi maalum yaani *Neonatal Intensive Care Unit* na wodi ya Kangaroo. Maeneo yote matatu kwa sasa yana wauguzi 49 tu na wahudumu 14 wakati mahitaji halisi ni kuwa na wauguzi 180 na wahudumu 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, uhaba wa dawa nchini. Hali ya upatikanaji wa dawa nchini siyo wa kuridhisha. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, kiasi cha shilingi bilioni 200 kiliidhinishwa na Bunge kwa ajili ya dawa. Hadi kufikia Machi 2021 ni asilimia 26.6 tu ya fedha ndiyo zilikuwa zimepokelewa. Licha ya taarifa ya Wizara kuonesha kuwa hakuna uhaba wa dawa na chanjo nchini katika Bohari Kuu ya Dawa, lakini dawa na chanjo hizi bado hazijawafikia wananaachi. Kutokana na hali hii, Kamati inashauri:-

(i) Serikali iharakishe upelekaji wa dawa na chanjo katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini;

(ii) Madeni yote ya dawa kwa vituo vya Afya yaangaliwe upya ikibidi Wizara ya Fedha iyafute ili waweze kupatiwa dawa;

(iii) Bajeti yote inayoidhinishwa na Bunge lako Tukufu itolewe yote kwa wakati ili kuondoa changamoto hiyo. Aidha, mkazo zaidi uwekwe kwenye kinga;

(iv) Serikali iharakishe utekelezaji wa uamuzi wa kuanzisha kiwanda cha kuzalisha dawa na vifaa tiba nchini cha *Simiyu Medical Product* ili kupunguza gharama za kununua dawa nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, Bima ya Afya kwa Wote. Kamati inampongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa uamuzi wake wa kuongeza umri wa wategemezi wa bima ya afya kutoka miaka 18 hadi 21. Ni dhahiri kuwa

Rais ameamua kupunguza mzigo kwa wazazi hasa ikizingatiwa kuwa vijana wengi wenye umri wa miaka 18 kwa tamaduni zetu bado ni tegemezi kwa wazazi wao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bima ya Afya kwa wote imekuwa ni ajenda ya Bunge kwa muda mrefu kuitia Kamati hii. Hata hivyo, bado jambo hili halijatekelezwa na Kamati imekuwa ikiambiwa mchakato unaendelea. Katika vikao vya uchambuzi wa bajeti ya Wizara hii, Kamati ilihoji hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa ushauri huu wa Bunge na ilielezwa kuwa, Serikali itahakikisha inaleta Muswada huu katika Mkutano huu wa Tatu. Kutohana na umuhimu wake, Kamati inashauri yafuatayo:-

- (i) Wananchi washirikishwe vya kutosha ili kutoa maoni yao katika kuboresha Muswada huo;
- (ii) Serikali ione namna ya kushirikisha Sekta Binafsi nchini katika kutoa huduma ya Bima ya Afya; na
- (iii) Kwa kuwa kumekuwepo na malalamiko kwa wateja wa *NHIF* kukosa baadhi ya huduma ikiwemo dawa, Wizara isimamie kuondoa changamoto hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, uhaba wa rasilimali watu. Takwimu zinaonesha kuwa, upungufu wa rasilimali watu katika sekta ya afya ni asilimia 53. Kamati imeshuhudia Taasisi kubwa kama *JKCI, MOI* na *Ocean Road* zote zikiwa na upungufu wa watumishi. Changamoto zaidi inaonekana katika vituo vya afya na zahanati ambako ndiko wagonjwa wengi zaidi wanakwenda kupata huduma. Hali hii kiasi kikubwa inachangia vifo vya akina mama na watoto. Kamati inashauri mkakati wa makusudi wa kuajiri watumishi wa sekta ya afya uanze mara moja. Serikali na hususan Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ihakikishe inatoa vibali vya kuajiri watumishi hasa ikizingatiwa kuwa kuna wataalam wengi mtaani ambao hawajapata ajira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, ugonjwa wa Virusi vya Korona yaani *COVID-19* au UVIKO. Ugonjwa wa virusi vya

*Corona* umekuwa ni tishio duniani kote. Kamati inampongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuamua kuunda Kamati ya Wataalamu ambao kwa kushirikiana na Taasisi za Afya Duniani na vilevile za Kikanda za EAC na SADC wamepanga kuliangalia suala hili kwa undani ikiwa ni pamoja na kufanya uchambuzi wa kina na kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukua na jinsi ya kuendelea kupambana na maradhi hayo. Kamati inaendelea kusisitiza wananchi kuendelea kuchukua tahadhari kwa kufuata miongozo ya kinga ambayo imekuwa ikitolewa nchini na kuendelea kula mboga na matunda kwa wingi pamoja na kutumia tiba asili na pia tiba mbadala ili kupunguza maambukizi ya ugonjwa huo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, saba, magonjwa yasiyoambukiza yaani *Non-Communicable Diseases*. Nchi yetu kama zilivyo nchi nydingine duniani zina matatizo ya afya yanayotokana na magonjwa yasiyoambukiza yaani *Non-Communicable Diseases*. Takwimu zinaonesha kuwa, magonjwa yasiyoambukiza yanachangia kwa asilimia 27 ya vifo vyote nchini. Tafiti za mwaka 2012 zinaonesha kuwa, kwa kila watu 100 wenyewe miaka 25 na kuendelea, watu 9 wana kisukari, watu 26 wana shinikizo la damu, watu 25 wana mafuta yaliyozidi kwenye damu na asilimia 34 wana uzito uliozidi, hili ni ongezeko kubwa ikilinganishwa na ilivyokuwa mwaka 1986. Si hivyo tu, takwimu za Ripoti ya Utafiti wa Hali ya Lishe Nchini ya mwaka 2018 inaonesha kuwa, asilimia 31.8 ya watoto wenyewe umri chini ya miaka 5 wamedumaa na wanatoka katika mikoa 11 ambayo inaongoza kwa uzalishaji wa chakula, asilimia 14 wana uzito pungufu na asilimia 5 wana upungufu wa damu, hivi vyote vinachangiwa na lishe duni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la magonjwa haya linatokana na mabadiliko ya mtindo wa maisha kama kutofanya mazoezi, ulaji usiofaa, matumizi ya pombe kupindukia, tumbaku na madawa ya kulevyaa, msongo wa mawazo pamoja na kutopata usingizi wa kutosha. Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Elimu iendelee kutolewa kwa jamii juu ya mbinu za kujikinga na magonjwa haya pamoja na uzingatiaji wa lishe bora;

(ii) Rasilimali watu ijengewe uwezo wa kuweza kutambua, kuzuia na kutibu magonjwa yasiyoambukiza;

(iii) Kutokana na gharama kubwa za kutibu magonjwa yasiyoambukiza, ni vema Serikali ikasaidia katika kutoa ruzuku ya dawa za kisukari au kupunguza kodi ya uingizaji wa dawa nchini ili zitolewe kwa bei nafuu; (*Makofii*)

(iv) Wizara ya Afya ishirikiane na Wizara nyingine kama Ujenzi, Habari, Elimu ili kuhakikisha ujenzi wa barabara unazingatia sehemu ya watembea kwa miguu na vipindi vya Elimu kwa Umma kuhusu athari za magonjwa yasiyoambukiza na namna ya kujikinga. Mwanazuoni Henry De Bracton wa Uingereza amewahi kusema: "*An ounce of prevention is worth a pound of cure.*" Yaani senti ndogo ya kinga ina thamani kubwa sana kuliko tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nane, Huduma za Kibingwa. Kamati inaipongeza sana Serikali kutokana na ununuzi wa vifaa na mitambo mikubwa na ya kisasa katika sekta ya afya yenye uwezo wa kutibu magonjwa mbalimbali makubwa na yenye gharama kubwa ambayo awali ilikuwa inawalazimu wagonjwa kupelekwa nje ya nchi.

Kamati inaamini kama huduma zitatangazwa ipasavyo, Tanzania itakuwa ni Kitovu cha Utalii wa Matibabu *yaani Hub of Medical Tourism.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, Kamati inashauri:-

(i) Serikali iweke mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutumia Balozi zetu kutangaza Huduma za Kibingwa zinazotolewa na Taasisi zetu kama JKCI, MOI, Ocean Road, Hospitali ya Benjamin Mkapa na nyingine nyingi; na

(ii) Serikali iendelee kufundisha wataalam wake ili kuwa wabobezi zaidi katika kutumia mitambo hii ya kisasa ili kuepuka kutumia wataalam wanaotoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tisa, kuimarisha huduma za Tiba asili na Tiba Mbadala. Kamati imeona na imeshauri kumekuwa na ongezeko ya matumizi ya tiba asili na tiba mbadala nchini kwa sasa jambo ambalo ni jema kabisa. Kamati inapongeza wataalam hawa kwa kuwa wabunifu na kuisaidia jamii yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ili kuepuka uwepo wa watoa huduma hawa wasio waaminifu, Kamati inashauri Wizara iwasajili watoa huduma hawa na dawa zao ambazo zimethibitika kuwa zinatibu magonjwa mbalimbali na kuanza kuzisambaza katika vituo vyetu nya kutolea huduma za afya. Aidha, Serikali iendelee kutoa elimu kwa jamii juu ya tiba asili na tiba mbadala ambazo hazina madhara kwa watumiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi, Hospitali *CCBRT*. Kamati inatambua kazi kubwa inayofanywa na Hospitali ya *CCBRT* katika kutoa huduma za afya nchini. Hospitali hii awali ilisajiliwa kama Hospitali ya kutoa huduma za matibabu zinazolenga kuzuia ulemavu au kupunguza athari za ulemavu. Hata hivyo, ili kuongeza mchango wake katika sekta ya afya ilikubaliwa kuanza kutoa huduma za Afya ya Uzazi na Watoto Wachanga. Mwaka 2012, *CCBRT* ilianza kujenga miundombinu ya kutolea huduma hiyo ikiwa ni pamoja na jengo ambalo tayari limekamilika kwa asilimia 90 na mashine na vifaa tiba baadhi vimeshanunuliwa tayari. Kamati imebaini kuwa, pamoja na *CCBRT* kipeleka maombi ya kubadili usajili wake lakini bado suala hili halijakamilika.

Kamati inashauri Wizara kukamilisha usajili wa hospitali hii mapema ili kuongeza wigo wa utaoji wa huduma za afya nchini kwani Hospitali ya *CCBRT* itapunguza msongamano wa wagonjwa katika Hospitali za Mkoa wa Dar es Salaam na hususan Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi na moja, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii. Kamati imeona kuna uhaba wa Maafisa Ustawi na Maendeleo ya Jamii. Hivyo basi, Kamati inashauri Serikali itoe vibali nya ajira kwa watumishi hawa kwani vyuo vyetu vinazalisha wataalamu hawa wa kutosha na wapo mtaani wakiwa hawana ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi na mbili, miundombinu ya Vyuo nya Maendeleo ya Jamii. Tunasisitiza kuwa, bajeti ya vyuo hivi iweze kutolewa kwa wakati na viweze kuendelezwa na viweze kufanya kazi iliyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi na tatu, Usawa wa Kijinsia. Kamati imebaini kuwa Mradi wa Kuzuia Ukatili wa kijinsia na Afua za Kuwezesha Wanawake Kiuchumi unategemea fedha za nje kwa asilimia 100.

Katika mwaka 2020/2021 fedha zilizopokelewa ni shilingi milioni 90 sawa na asilimia 9 kati ya shilingi bilioni 1.04 zilizotengwa. Kamati imesikitishwa na jambo hili. Lengo Na.5 la Malengo ya Maendeleo Endelevu linasisitiza umuhimu wa kuzuia ukatili wa kijinsia. Kamati inashauri bajeti ya kutosha itengwe na itolewe yote na kwa wakati ili kuwezesha utekelezaji wa mipango ya kuzuia ukatilia wa kijinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nihitimishe kwa kusema kwa mara nyingine napenda kutoa shukrani zangu kwako kwa fursa uliyonipa ya kuwasilisha maoni haya ya Kamati lakini pia kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu Tukufu. Nawashukuru sana Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Manaibu Mawaziri wake Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel na Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis kwa ushirikiano wanaoipa Kamati.

Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Idara Kuu Afya, Profesa Abel Makubi na Naibu Katibu Mkuu, Idara Kuu Maendeleo ya Jamii, Dkt. John Jingu pamoja na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati tangu tulipoanza kufanya nao

kazi na kushiriki vizuri kwenye uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa ushirikiano mzuri ambao wanani. Wajumbe hawa ni wachapa kazi na wameshiriki kikamilifu katika uchambuzi wa Bajeti na kuhakikisha wanahoji ili kupata ufanuzi wa kina. Naomba Majina yao yote yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wetu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema. Pamoja naye, namshukuru Mkurugenzi Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Athuman Hussein na Mkurugenzi Msaидizi, Ndugu Gerald Magili kwa ushirikiano wanaoipa Kamati yetu wakati wote.

Aidha, tunawashukuru sana Makatibu wa Kamati yetu Ndugu Pamela Pallangyo na Ndugu Nyamwanja Chilemeji pamoja na msaидizi wa Kamati Ndugu Jane Ndulesi kwa kuhakikisha shughuli zote za Kamati zinatekelezwa kikamilifu ikiwemo taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maeleo haya sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na watoto pamoja na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kama ilivyowasilishwa na Mto Hoja Fungu Na. 52 jumla ya shilingi 1,034,133,295,000, na Fungu 53 jumla ya shilingi 43,625,929,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. Naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA  
MAENDELEO YA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU  
NA BAJETI YA WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,  
JINSIA, WAZEE NA WATOTO KWA MWAKA FEDHA 2020/2021  
PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA  
MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA  
2021/2022 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

### **SEHEMU YA KWANZA**

#### **1.0      UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 napenda kukushuru kwa kunipa wasaa wa kuweza kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii ya Kamati imejikita katika kueleza maeneo yafuatayo:-

- a) Maeleo na uchambuzi kuhusu ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2020/2021;
- b) Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti na uzingatiaji wa Maoni ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021;
- c) Uchambuzi wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 (Makadirio ya Maduhuli na Matumizi); na
- d) Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati.

## **SEHEMU YA PILI**

### **2.0 MAELEZO NA UCHAMBUZI KUHUSU UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ilifanya Ukaguzi wa baadhi ya Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2020/2021. Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo zilifanywa kwa kuzingatia Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata wasaa wa kukagua miradi mitatu ambayo ipo Dar Es Salaam. Awali, Kamati ilipanga kukagua miradi minne ukiwemo Mradi wa Ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii - Monduli. Hata hivyo, Kamati ilishindwa kukagua Mradi huu kutokana na Msiba uliolikumba Taifa letu wa kuondokewa na aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

**Mheshimiwa Spika**, Miradi iliyotembelewa na Kamati ni pamoja na Mradi wa Taasisi ya Saratani Ocean Road – ORC (**Namba ya Mradi 5412**), Mradi wa Taasisi ya Mifupa Muhimbili – MOI (**Namba ya Mradi 5491**) na Mradi wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete – JKCI (**Namba ya Mradi 5419**). Hali ya Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

#### **2.1 MRADI WA TAASISI YA SARATANI OCEAN ROAD – ORC (**NAMBA YA MRADI 5412**)**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu wa Taasisi ya Saratani Ocean Road ambao Kamati iliutembelea mnamo tarehe 15 Machi 2021, unahusu ujenzi wa jengo maalum la kusimika mashine maalum, maabara za kuchanganyia dawa za nyuklia, na vyumba vyta huu ya Huduma, ununuzi na usimikaji wa mashine ya *cyclotron*, na ununuzi na usimikaji wa mashine ya PET/CT Scan ambapo gharama yake ni **Shilingi 16,783,405,000.00** na bajeti ya mradi huu iliandaliwa kuanzia mwaka wa fedha 2016/17.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa Serikali ilitoa jumla ya **Shilingi 14,500,000,000.00** na Taasisi ilitoa **Shilingi 1,000,000,000/=** kutoka kwenye mapato yake ya ndani kugharamia mradi huu. Hata hivyo, kiasi hiki ni pungufu ya fedha zilizokubaliwa ambazo ni **Shilingi 16,783,405,000.00** na hivyo kuwa na nakisi ya **Shilingi 1,283,405,000.00**. Nakisi hii ikijumlishwa na fedha kwa ajili ya waranti katika mwaka wa pili na gharama za malighafi na uendeshaji wa kuanzia kiwanda, jumla kuu ya nakisi katika mradi huu ni **Shilingi 2,719,005,000.00**. Kiasi hiki cha nakisi ndicho kilichofanya Taasisi kuomba fedha katika bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021 na Bunge liliidhinisha, jumla ya **Shilingi 4,000,000,000.00** kwa ajili ya mradi huu<sup>1</sup>. Hadi Kamati inatembelea mradi huu, fedha hizi zilikuwa hazijatoka.

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ni muhimu sana kwa Taifa letu kutokana na ukweli kwamba:-

- i) Utaboresha huduma za Saratani nchini ziwe katika kiwango cha kimataifa hasa katika uchunguzi, kwani mashine hii ndiyo mashine ya kisasa kabisa katika uchunguzi wa saratani duniani kote;
- ii) Utapunguza rufaa za nje na hivyo kuokoa fedha ambazo Serikali hugharamia wagonjwa nje ya nchi hasa India;
- iii) Utachangia utekelezaji wa Sera ya Serikali ya ujenzi wa viwanda, kwani utahusisha kujenga kiwanda (*cyclotron*) ambacho kitatumika katika kuzalisha mionzi-dawa (*radio-isotopes*) za upimaji katika PET/CT Scan;
- iv) Utaongeza mapato ya Taasisi kwani wagonjwa watalipia huduma za uchunguzi na hivyo kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikalini na pia kuongeza uwezo wa Taasisi kugharamia shughuli za uendeshaji. Aidha, mionzi-dawa itauzwa kwa hospitali nydingine nchini na nchi jirani ambazo zitafunga mashine za PET/CT scan; na

---

<sup>1</sup> Taasisi ya Saratani Ocean Road: Taarifa ya Mradi wa Maendeleo wa Pet/Ct Scan inayowasilishwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii

v) Utaongeza Wagonjwa kutoka nje (***Medical Tourism***) kwani PET/CT Scan haipatikani katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara isipokuwa Afrika ya Kusini. Wagonjwa kutoka katika nchi za jirani ikiwemo Uganda, Kenya, Malawi, Msumbiji, DRC, Burundi, Zambia, Rwanda, Comoro, Sudan ya Kusini na Somalia watakuja nchini. Inakadiriwa kuwa mashine itaweza kuhudumia takriban **wagonjwa 2,000** kwa mwaka kutoka nje ya nchi, ambapo kila kipimo cha PET/CT **Scan ni Shilingi 1,600,000** na hivyo kuingiza mapato ya wastani wa **Shilingi bilioni 3.2** kwa mwaka kwa huduma ya PET/CT Scan kwa wagonjwa kutoka nje ya nchi. Vilevile Taasisi itapata mapato yatakayotokana na takribani **wagonjwa 1,000** walio katika Mfumo wa Bima ya Afya na wale wa binafsi; hivyo kuingiza mapato ya takriban **Shilingi bilioni 1.6** kwa mwaka.

vi) **Mheshimiwa Spika**, pamoja na manufaa hayo, Kamati ilielezwa changamoto zillizofanya kuchelewa kwa mradi huu kuwa ni pamoja na utaratibu za manunuzi katika kumpata mzabuni mwenye uwezo wa kutekeleza mradi huu katika maeneo yote matatu ya jengo, kiwanda cha cyclotron, na mashine ya PET CT scan na kuongezeka kwa gharama za mradi baada ya tenda kwani ni zaidi ya ile bajeti iliyoidhinishwa na Serikali mwaka 2019/20.

Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa Mradi huu na kutoa kiasi cha Shilingi Bilioni 14.5. Hata hivyo, Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kuhakikisha kiasi hicho cha Shilingi Bilioni 4 kinatolewa kwa Taasisi hii muhimu kabla ya mwaka huu wa fedha haujaisha ili mradi huu uweze kukamilika kama ulivyopangwa ifikapo Oktoba, 2021.

## **2.2 MRADI WA TAASISI YA MIFUPA MUHIMBILI – MOI (NAMBA YA MRADI 5491)**

**Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Mifupa MOI inatekeleza Mradi wa MOI Phase III unaohusisha Ujenzi wa Jengo na ununuzi wa Vifaa Tiba na ulianza katika mwaka wa fedha 2017/18 ambapo Serikali ilitoa kiasi cha **Shilingi 16,500,000,000.00**. Upatikanaji wa fedha hizi umewezesha MOI kununua mashine za kisasa kabisa kama za Radiologia, zikiwemo MRI, CT-*Scan*, *Digital X-ray*, CR X-ray, Portable X-Ray, Ultrasound 2, C-arm,

ECHO na ECG *Anaesthesia Machines* 6, vitanda vya kisasa vya ICU, *Monitors na ventilators* pamoja na vitanda vya upasuaji 6 na *Microscope* ya kisasa kwa ajili ya upasuaji wa ubongo na uti wa mgongo na Vifaa vipyta vya kisasa vya mazoezi tiba (*Pysiotherapy*)<sup>2</sup>.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, kiasi cha **Shilingi 5,000,000,000.00** kilitegwa kwa ajili ya uboreshaji wa Huduma katika Taasisi ya Mifupa MOI. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,800,000,000.00** ni kwa ajili ya kulipa deni la NHIF la Ujenzi wa MOI phase III, na **Shilingi 3,200,000,000.00** ni kwa ajili ya ununuzi wa vifaa Tiba.

**Mheshimiwa Spika**, hadi Kamati inatembelea mradi huu, fedha hizo zilikuwa bado hazijatolewa. Kamati ilielezwa kuwa mawasiliano yameshafanyika kati ya Wizara ya Afya na Wizara ya Fedha na Mipango, na kwamba Serikali imejipanga kuhakikisha kuwa fedha hizo zinatolewa kabla mwaka wa fedha wa 2020/2021 haujaisha.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata wasaa wa kutembelea Hospitali hii na kushuhudia Mashine mbalimbali za kisasa zikiwa zimefungwa. Katika Maabara ya Upasuaji Ubongo ijlukanayo kitaalamu kama **Angio Suite**, Kamati ilishuhudia mashine hii yenye uwezo wa kufanya upasuaji wa matatizo ya mishipa ya damu kichwani pasipo kufungua fuvu la kichwa. Kamati ilielezwa kuwa, gharama ya maabara hii **Shilingi Bilioni 7.9 ikijumuisha ujenzi wa maabara (Bilioni 3.2) na ununuzi wa machine (Bilioni4.7)**. Mashine hii imeanza kufanya kazi tarehe 27/01/2021 na tayari wagonjwa 16 wameshatibiwa. Gharama ya upasuaji huu kwa nchi kama India ni **Shilingi Milioni 60** lakini MOI inafanya kati ya **Shilingi Milioni 10** hadi 15.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza sana juhudhi hizi za Serikali kwani kwa hakika uwekezaji uliofanyika ni mkubwa sana na utaendelea kusaidia kupunguza gharama ambazo

---

<sup>2</sup>Taarifa ya Miradi ya Maendeleo ya Taasisi ya MOI inayowasilishwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii

nchi ilikuwa inaingia katika kupeleka wagonjwa nje ya nchi. Si hivyo tu, pia uwekezaji huu utasaidia kuleta wagonjwa kutoka nchi mbalimbali hususan zilizopo Afrika kwani ukiacha Afrika ya Kusini hakuna nchi nyingine yenye Mashine hii.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kazi kubwa ambayo MOI inafanya, Kamati ilielezwa changamoto ambazo ni kikwazo katika utekelezaji wa majukumu ya Taasisi zikiwemo: bajeti finyu ikilinganishwa na mahitaji halisi ya ununuzi wa vifaa na gharama za uendeshajji; miundombinu duni isiyokidhi mahitaji kwani wagonjwa ni wengi; na maslahi duni ya watumishi ambayo yanapunguza morali ya utendaji kazi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatoa RAI kwa Serikali kuhakikisha inatoa fedha hizi kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha haujaisha ili MOI iweze kulipa deni hilo la NHIF na pia iweze kununua vifaa vilivyobaki kwani imebainika kuwa, hata mwaka wa fedha 2019/2020 Taasisi hii haikupelekewa fedha zilizoidhinishwa na Bunge.

**2.3 MRADI WA TAASISI YA MOYO JAKAYA KIKWETE – JKCI (5419)**  
**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) ilitengewa kiasi cha **Shilingi 500,000,000.00** kwa ajili ya ukarabati wa jengo la watoto. Mpaka Kamati inatembelea mradi huo, hakuna fedha yoyote iliyokuwa imepokelewa kutoka Hazina. Hata hivyo, Kamati illijulishwa na kushuhudia ununuzi wa vifaa vya kisasa kwa kutumia fedha zilizoidhinishwa na Bunge katika mwaka wa fedha 2019/2020 kiasi cha **Shilingi 1,000,000,000.00**. Vifaa hivyo ni pamoja na *Anaesthesia Machine*, *ICU Echo Machine*, *Syringe Pump*, *Intra-Aortic balloon Pump*. Pamoja na Vifaa hivi, Kamati ilielezwa kuwa, Serikali ilitoa kiasi cha **Shilingi 4,600,000,000.00** kwa ajili ya ununuzi wa *machine* ya *Cathlab* na *Carto 3* ambazo hutumika kufanya upasuaji wa moyo kwa tundu dogo, kuzibua mishipa ya moyo, kuweka vifaa vya kusuma moyo, kuziba matundu pamoja na kupima mfumo wa umeme wa moyo<sup>3</sup>. Kamati ilishuhudua usimikaji wa

---

<sup>3</sup>Taarifa ya Miradi ya Maendeleo ya Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete Inayowasilishwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii

mtambo ukiendelea na ilielezwa kuwa inatarajiwa kukamilika na kuanza kutumika ifikapo mwezi huu wa Mei, 2021.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza sana Serikali kwa uwekezaji huu mkubwa. Kama ilivyokuwa kwa Taasisi ya Saratani *Ocean Road* na Taasisi ya Mifupa MOI kwani utasaidia kupunguza au kuondoa kabisa rufaa za matibabu ya moyo nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Taasisi hii, Kamati ilielezwa changamoto za uhaba wa dawa na vitendea kazi kutoka Bohari ya Dawa (MSD); milolongo mirefu ya kodi kwa vifaa na vifaa tiba; na uhaba wa Watumishi hususan *Biomedical Engineers* kwani wapo 2 na mmoja anajitolea hivyo kuna haja ya kutoa kibali cha ajira.

#### ***2.4 MATOKEO NA MAONI YA JUMLA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO***

**Mheshimiwa Spika**, Kufuatia ukaguzi huo wa miradi ya maendeleo iliyotembelewa, Kamati imefanya tathmini yake na inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

##### **a) Hali ya Upatikanaji wa Fedha**

Kamati imebaini kuwa bado hali ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi siyo ya kuridhisha. Mpaka Kamati inatembelea miradi hii, fedha ambazo ziliidhinishwa na Bunge katika mwaka wa fedha 2020/2021 zilikuwa bado hazijatoka. **Ni imani ya Kamati kuwa Serikali itatoa fedha hizo kabla mwaka wa fedha kuisha ili miradi iliyopangwa iweze kutekelezwa na kufikia malengo yaliyopangwa.**

##### **b) Uhaba wa Watumishi**

Taasisi nyingi zina changamoto ya Watumishi kama inavyoonekana kwenye changamoto zilizoainishwa. **Kamati inashauri Serikali itoe kibali cha ajira ili taasisi kama JKCI, Ocean Road na MOI ziweze kuajiri watumishi wa kutosha wataoweza kutumia mashine za kisasa zilizofungwa na hatimaye kuboresha upatikanaji wa huduma za afya nchini.**

**c) Kutangaza Huduma nje ya Nchi**

Kamati imebaini kuwa pamoja na Taasisi hizi zote tatu (JKCI, MOI na *Ocean Road*) kuwa na mashine bora na za kisasa katika kupima na kutibu magonjwa mbalimbali, bado taasisi hizi hazijajitangaza ipasavyo. **Kamati inashauri taasisi hizi zianze kujitangaza kote Duniani.** Hii itasaidia kupunguza gharama ambazo wananchi wetu wamekuwa wakiingia katika kuwapeleka wagonjwa nje ya nchi lakini pia hali hiyo itapelekea watu kutoka nchi mbalimbali kuja nchini kwa ajili ya matibabu (*Medical Tourism*) na hivyo kuongeza mapato nchini. Aidha, uwekwe mfumo utakaowezesa Taasisi hizi kukubali kupokea Bima binafsi za ndani na nje ya nchi.

**d) Msamaha wa kodi ya vifaa na vifaa tiba**

**Mheshimiwa Spika**, milolongo mirefu ya kodi kwa ajili ya vifaa na vifaa tiba imekuwa ni kikwazo na mzigo kwa JKCI, MOI na Ocean Road. **Kamati inashauri Serikali itoe msamaha wa kodi kwa vifaa na vifaa tiba vinavyotumika kwenye hospitali hizi.**

**3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Bajeti ya Wizara iliyowasilishwa mbele ya Kamati mnamo tarehe 29 Aprili, 2020, Kamati ilipata wasaa wa kuichambua na kuijadili, lakini pia Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo mbalimbali kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara kama ifuatavyo:-

**3.1 UTEKELEZAJI WA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA MWAKA 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni kuhusu Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo tisa (9). Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kwa kiasi kikubwa Serikali imetekeleza Maoni na Ushauri wa Kamati. **Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanya kazi Maoni na Ushauri wa**

**Kamati.** Aidha, kwa maeneo ambayo bado hayajatekelezwa kikamilifu, Kamati itaendelea kuyasisitiza katika Taarifa hii likiwemo suala la Sheria ya Bima ya Afya kwa wote.

### **3.2 UCHAMBUZI WA UKUSANYAJI WA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia **Fungu 52 - Idara Kuu Afya**, Katika mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiria kukusanya maduhuli ya **Shilingi 467,799,587,522.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 51,171,533,581.00** sawa na **asilimia 10.9** zilikadiriwa kukusanya kutoka Makao Makuu ya Wizara, **Shilingi 103,875,213,018.00** sawa na **asilimia 22.2** kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa na **Shilingi 312,752,840,523.00** sawa na **asilimia 66.9** kutoka Taasisi zilizo chini ya Wizara na Hospitali ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa, kufikia Februari 2021, jumla ya **Shilingi 250,711,009,968.56** zilikuwa zimekusanywa sawa na **asilimia 53.6** ya lengo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 32,620,409,378.26** zilikusanywa kutoka Wizarani, **Shilingi 31,546,086,337.00** kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa na **Shilingi 186,544,514,253.30** kutoka Taasisi na Hospitali za Taifa<sup>4</sup> kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 1.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kuwa, makusanyo makubwa ambayo ni **asilimia 63.7** ya lengo yamekusanywa kutoka kwenye vyanzo vya Wizara. **Kamati inaipongeza Wizara kwa makusanyo hayo mazuri, ni imani ya Kamati kuwa, kufikia mwisho wa mwaka fedha Juni 2021, lengo la makusanyo litafikiwa**. Pamoja na makusanyo hayo mazuri, Kamati imebaini pia kuwa, Hospitali za Rufaa makusanyo yake ni chini ya **asilimia 50 (asilimia 30.3)**. Kamati ilihoji sababu za makusanyo hayo madogo katika Hospitali za Rufaa na ilielezwa kuwa, Hospitali nyingi zilikuwa zikiandaa bajeti zake za makusanyo ya ndani pasipo kuzingatia vigezo halisi vya kibajeti na hivyo kusababisha kuwa na bajeti zisizo


---

<sup>4</sup> Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara (Idara Kuu Afya – Fungu 52) kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Februari, 2021: Mchanganuo wa Makadirio ya Makusanyo ya Mapato kwa kipindi cha Julai hadi Februari, 2021.

na uhalisia. Si hivyo tu, lakini pia kumekuwa na uzembe hali ambayo imefanya Wizara kuamua kuingia mkataba wa utendaji (*Performance Contract*) na viongozi wa taasisi zinazotoa huduma za matibabu na zile ambazo hazitoi huduma za matibabu pamoja na Hospitali zote ili malengo ya ukusanyaji wa maduhuli yaweze kufikiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haikuishia hapo, ilichambua zaidi na kubaini kuwa, makusanyo ya Hospitali ya Benjamina Mkapa kufikia Februari 2021 yalikuwa ni **Shilingi 13,119,781,237.61** sawa na **asilimia 118** ya lengo la kukusanya **Shilingi 11,111,575,793.00**. Tafsiri ni kuwa, kufikia Juni 2021 makusanyo yatakuwa makubwa zaidi. Kamati ilitaka kujua nini siri ya kuvuka lengo na ilielezwa kuwa, ni kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo:- kuanzishwa kwa huduma mpya za upasuaji wa kutoa mawe kwenye figo; kuanza kutumika kikamilifu kwa mtambo wa *Cathlab* kufuatia kupatikana kwa watalaam wa kibingwa; kuanza kutolewa kwa huduma za maabara ya kuchunguza Saratani (*Histopathology*); na kuongezeka kwa idadi ya wataalamu bingwa waliokuwa masomoni na hivyo kuimarisha utoaji wa huduma katika Hospitali. **Kamati inaipongeza sana Hospitali hii kwa kazi kubwa na nzuri inayoendelea kutolewa. Ni imani ya Kamati kuwa, hali ya utendaji na ukusanyaji wa maduhuli itazidi kuimarika katika mwaka wa fedha 2021/2022.**

### Kielelezo Na. 1



**Chanzo: Randama ya Wizara (Machi 2021) na Usanifu wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Idara Kuu Maendeleo ya Jamii (**Fungu 53**), katika mwaka wa fedha 2020/2021, makadirio yalikuwa ni kukusanya maduhuli ya **Shilingi 5,419,250,000.00** kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali ambavyo ni ada za wanafunzi katika Vyuo mbalimbali nya Maendeleo ya Jamii na mitaala ya kozi za maendeleo ya jamii kiasi cha **Shilingi 4,687,056,000.00** sawa na **asilimia 86.49**, ada ya usajili na ada za mwaka za Mashirika yasiyo ya Kiserikali **Shilingi 682,690,000.00** sawa na **asilimia 12.6**, mitaala ya kozi za ustawii wa jamii **Shilingi 48,000,000.00** sawa na **asilimia 0.89** na Mapato mengine **Shilingi 1,504,000.00** sawa na **asilimia 0.03**<sup>5</sup>

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari 2021, Idara ilifanikiwa kukusanya maduhuli ya **Shillingi 3,147,497,573.00** sawa na **asilimia 58** ya lengo. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, makusanyo madogo zaidi ni kutoka chanzo cha mitaala ya kozi za ustawii wa jamii kwani kati ya **Shilingi 48,000,000.00** zilizokadiriwa, zimekusanywa **Shilingi 6,907,000.00** sawa na **asilimia 14.39** ya lengo. Aidha, Kamati imebaini pia ada za usajili wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali makusanyo yake ni **asilimia 31** tu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati illifuatilia ili kujua chanzo cha makusanyo hayo madogo na ilielezwa yafuatayo:-


- a) Kwa upande wa mitaala, ni kutokana na Vyuo 27 ambavyo vilitarajiwa kununua mitaala havikukidhi vigezo nya kupata ithibati ya kutoa mafunzo hayo na hivyo Idara ilifanikiwa kuuza mitaala kwa vyuo vitano (5) tu kati ya vyuo 32 vilivyokadiriwa; na
- b) Kwa Upande wa ada za usajili wa NGO's, ni kutokana na kuondolewa kwa Mashirika yasiyo hai kuititia zoezi la uhakiki linaloendelea kufanyika nchi nzima. Zoezi hilo linatokana na

---

<sup>5</sup> Muhtasari wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Fungu 53 -Maendeleo ya Jamii kwa Mwaka 2020/2021 (Mapato kwa Mwaka 2020/2021)

Wizara kuanza kutumia Mfumo wa usajili wa Kielektroniki mwezi Mei 2020, ambapo mashirika yote yaliyosajiliwa tangu mwaka 2005 yaliingizwa kwenye mfumo tofauti na uhalisia wa mashirika yaliyo hai kwa sasa. Mashirika hayo yameondolewa kwenye orodha kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali kama ilivyofanyiwa urekebu mwaka 2005, inayoelekeza kuwa shirika lisipotoa taarifa kwa miaka miwili mfululizo linatakiwa kuondolewa kwenye orodha. Sambamba na hilo, Kamati ililelezwa kuwa mashirika mengi hulipa ada za mwaka katika kipindi cha Machi hadi Aprili kabla ya tarehe ya ukomo ambayo ni 15 Aprili. Hivyo Wizara ilitarajia ongezeko la makusanyo ya mapato katika kipindi hicho<sup>6</sup>.

### Kielelezo Na. 2



**Chanzo: Randama Wizara (Machi 2021) na Usanifu wa Kamati**

### 3.3 UPATIKANAJI WA FEDHA KWA MWAKA WA 2020/2021

**Mheshimiwa Spika**, katika Bajeti ya mwaka 2020/2021, Wizara kupitia **Fngu 52** (Idara Kuu Afya) iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi 900,088,240,000.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 539,128,874,000.00** sawa na **asilimia 59.9** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 360,959,366,000.00** sawa na **asilimia 40.1** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

---

<sup>6</sup> Fngu 53 (Maendeleo ya Jamii): Majibu ya Hoja za Waheshimiwa Wabunge zilizotolewa wakati wa Kikao cha Kamati ya Kudumu Ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii Tarehe 29 Machi, 2021

**Mheshimiwa Spika**, fedha za matumizi ya kawaida zinajumuisha mishahara ya watumishi **Shilingi 357,565,924,000.00** sawa na **asilimia 66.32** na matumizi mengineyo (OC) **Shilingi 181,562,950,000.00** sawa na **asilimia 33.68** ya bajeti yote ya matumizi ya kawaida. Kwa upande wa fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo, **asilimia 78** ya fedha hizo ambazo ni sawa na **Shilingi 280,700,000,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 80,259,366,000.00** sawa na **asilimia 22** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imejulishwa kuwa, kufikia Machi 2021, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 409,018,849,518.72** sawa na **asilimia 45.4** ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya **Fungu 52**<sup>7</sup>. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, mishahara imepata **Shilingi 212,711,404,212.90** sawa na **asilimia 59.4.9**, matumizi mengineyo **Shilingi 113,154,602,242.67** sawa na **asilimia 62.32**. Kwa upande wa miradi ya maendeleo, **Shilingi 83,152,843,063.15** zimepokelewa sawa na **asilimia 23** ya fedha zilizoidhinishwa kwa mfumo wa Exchequer. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni **Shilingi 76,502,578,042.00** sawa na **asilimia 27.25** ya lengo ambapo fedha za nje ni **Shilingi 6,650,265,021.15** sawa na **asilimia 8.29** ya lengo kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 3.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati illoji ni kwa kiasi gani upatikanaji huo mdogo wa fedha za maendeleo umeathiri miradi ya kipaumbele iliyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2020/2021 kama upatikanaji wa Dawa, kupunguza Vifo vya akina Mama vitokanavyo na uzazi (SMMRP) na Kudhibiti UKIMWI. Kamati ilielezwa yafuatayo:-

- a) Kwa **fedha za ndani**, Wizara imeendelea kuratibu vyanzo mbalimbali vya fedha za dawa ikiwemo fedha za NHIF zinazolipwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya. Katika

---

<sup>7</sup> Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara (Idara Kuu Ya Afya – Fungu 52) kwa kipindi Cha Julai 2020 hadi Februari, 2021: Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kufikia

kufanikisha suala hilo, Wizara ilitoa maelekezo kwa vituo vyote vya kutolea huduma nchini kutumia **asilimia 50** ya fedha zote zinazotoka NHIF kununulia dawa na vitendanishi. Kutokana na hali hiyo, upatikanaji wa dawa na vitendanishi nchini upo katika kiwango cha **asilimia 86** kwa kuzingatia **aina 30** za dawa muhimu sana kukidhi mahitaji ya afya ya msingi. Vilevile, kwa kutumia kipimo cha aina **312 za dawa**, zinazohitajika katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya upatikanaji upo katika kiwango cha **asilimia 70**. Aidha, dawa muhimu kwa ajili ya kuokoa maisha ya wajawazito wanapojifungua pia zinapatikana kwa kiwango cha kuridhisha ikiwa ni pamoja na *Oxytocin, Magnesium Sulphate Injection*, dawa za kuongeza wingi wa damu, misoprostol n.k.

b) Kwa **fedha za nje**, hakuna miradi iliyoathirika kwani, kati ya fedha ambazo hazijajumuishwa katika hesabu ya fedha zilizopokelewa ni pamoja na fedha za ununuzi wa dawa za kupunguza makali ya VVU (Global Fund) na Chanjo (GAVI). Kwa mujibu wa utaratibu uliopo, mara baada ya dawa na chanjoi hizo kupokelewa, thamani ya bidhaa hizo za afya hurasimishwa kuwa fedha. Kwa hali hiyo, Wizara inatarajia kupokea bidhaa hizo kati ya mwezi Aprili na Mei, 2021 na hivyo haitarajiwi kuwepo kwa athari katika utekelezaji wa Miradi inayaogharamiwa na fedha za nje. Pia Wizara ilipokea kiasi cha **Shilingi 109,943,041,708** kuititia mfumo wa D-Fund, na hivyo kufanya fedha zilizopokelewa kutoka kwa wadau wa maendeleo kufikia **shilingi 116,593,306,729.15** na hivyo haitarajiwi kuwepo kwa athari katika utekelezaji wa miradi inayaogharamiwa na fedha za nje<sup>8</sup>.


**Mheshimiwa Spika, Ni imani ya Kamati kuwa dawa hizo pamoja na fedha zote za maendeleo zitatoka kabla ya mwaka wa fedha kuisha ili miradi hii iweze kutekelezwa na hivyo kuboresha Afya za Watanzania kama ilivyoainishwa kwenye Uk.131 wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 yenye dhamira ya kuwa na**

---

<sup>8</sup> Majibu ya Hoja za Kamati ya Bunge zilizoibuliwa wakati wa kuwasilisha Makadirio ya Bajeti ya Wizara (Fungi 52 -Idara Kuu Afya) kwa Mwaka 2021/

wananchi wenye afya bora ili kuwawezesha kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na kutoa huduma kwa kuendelea kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma bora za afya<sup>9</sup>. Si hivyo tu, lakini pia itasaidia katika kutekeleza Lengo Na.3 la Maendeleo Endelevu linalohusu "Good Health and Well being ambalo pamoja na masuala mengine lakini pia linasisitiza umuhimu wa nchi wanachama ikiwemo Tanzania kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya Sekta ya afya ili kupunguza vifo vya mama na mtoto. Mwanasaikolojia kutoka Marekani Bi. Anne Wilson Schaeff amewahi kusema "Good health is not something we can buy, however, it can be an extremely valuable savings account" hivyo yatupasa kuwekeza katika afya za wananchi wetu.

Kielelezo Na. 3




Chanzo: Randama Wizara (Machi 2021) na Usanifu wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia **Fungu 53** (Idara Kuu Maendeleo ya Jamii), kufikia Februari 2021 imefanikiwa kupokea kiasi cha **Shilingi 17,643,080,408.00** sawa na **asilimia 53** ya **Shilingi 33,195,739,000.00** zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa, mishahara ni **Shilingi 7,905,547,900.00** sawa na **asilimia 61.56** ya lengo, matumizi mengineyo (OC) **Shilingi 9,099,529,333.00** sawa na **asilimia**

<sup>9</sup> Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020

**66.67.** Kwa upande wa fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo, kiasi cha **Shilingi 638,003,175.00** kimepokelewa sawa na **asilimia 9.52** ya fedha zote za kutekeleza miradi ya maendeleo zilizoidhinishwa<sup>10</sup>. Kamati imebaini kuwa, fedha hizi zote ni kutoka nje ambayo ni sawa na **asilimia 23.6** ya fedha za nje zilizoidhinishwa kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 4. Kamati ilihoji Wizara ni kwa nini fedha za ndani hazijatoka na ilielezwa kuwa fedha hizo zinatarajiwa kutoka kabla ya Mwaka huu wa fedha kuisha. **Kamati inasisistiza fedha hizi zitoke kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha ili miradi iliopangwa iweze kutekelezwa.**

#### Kielelezo Na.4



**Chanzo: Randama Wizara (Machi 2021) na Usanifu wa Kamati**

#### 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa Mpango wa utekelezaji wa majukumu, mapato na matumizi ya kawaida pamoja na ile ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ya Wizara katika mwaka wa fedha 2021/2022 imepangwa kwa kuzingatia mambo mbalimbali kama vile Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Sera ya Afya ya Mwaka 2007, Mpango

---

<sup>10</sup> Muhtasari wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Fungu 53 -Maendeleo ya Jamii kwa Mwaka 2020/2021 (Fedha zilizopokelewa na Wizara hadi Februari, 2021)


wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Malengo ya Maendeleo Endelevu, na llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020<sup>11</sup> kama yalivyofafanuliwa na Mheshimiwa Waziri.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi wa mchanganuo wa shughuli hizo za Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kama ifuatavyo:-

#### 4.1 UCHAMBUZI WA UKUSANYAJI WA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika**, Makadirio ya makusanyo ya maduhuli kuititia Idara Kuu Afya (**Fungu 52**) katika mwaka wa fedha 2021/2022 ni jumla ya **Shilingi 507,211,162,896.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 81,710,646,199.00** sawa na **asilimia 16** zinakadiriwa kukusanywa kutoka vyanzo vya ndani vya Wizara, **Shilingi 92,044,336,376.00** sawa na **asilimia 18** kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa na **Shilingi 333,456,180,321.00** sawa na **asilimia 66** kutoka Taasisi zilizo chini ya Wizara na Hospitali ya Taifa kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 5

**Kielelezo Na. 5**  
**MAKADIRIO YA MADUHULI 2021/2022 (FUNGU 52)**




**Chanzo: Randama Wizara (Machi 2021) na Usanifu wa Kamati**

<sup>11</sup> Mpango wa Mapato na Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo (Fungu52) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, makadirio ya mwaka 2021/2022 ni ongezeko la **Shilingi 39,411,575,774.00** sawa na **asilimia 8.4** ya makadirio ya makusanyo ya **Shilingi 467,799,587,122.00** katika mwaka wa fedha 2020/2021. Ongezeko zaidi linaonekana zaidi katika vyanzo vya Wizara ambapo kuna ongezeko la **asilimia 59.7** kutoka **Shilingi 51,171,533,581.00** mwaka 2020/2021 hadi **Shilingi 81,710,646,199.00** mwaka 2021/2022. Aidha, Kamati imebaini pia makadirio ya mapato kutoka Hospitali za Rufaa yameshuka kwa **asilimia 11.4** kutoka **Shilingi 103,875,213,018.00** mwaka 2020/2021 hadi kufikia **Shilingi 92,044,336,37.00** mwaka 2021/2022 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 6. Kamati ilhoji na ililezwa sababu za kushuka kwa makadirio kama ilivyoelezwa awali ni kutokana na Hospitali hizo kuanza kuandaa bajeti za makusanyo ya ndani zenye kuzingatia uhalisia wa vyanzo vyao.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa ongezeko la bajeti kwa upande wa Wizara, ni kutokana na mapato yanayokadiriwa kupatikana kutoka Maabara ya Taifa ambayo awali hayakuwepo.


#### Kielelezo Na. 6



**Chanzo:** Randama Wizara (Machi 2021) na Usanifu wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Idara Kuu Maendeleo ya Jamii (**Fungu 53**), katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 imekadiria kufanya makusanyo ya maduhuli ya **Shillingi 6,000,000,000.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 4,704,600,000.00** sawa na **asilimia 78.4** ni kutokana na ada za wanafunzi katika Vyuo vya maendeleo ya jamii na mitaala ya kozi za maendeleo ya jamii, **Shilingi 531,161,000.00** sawa na **asilimia 8.85** kutokana na ada ya usajili na ada za mwaka za Mashirika yasiyo ya Kiserikali, **Shilingi 28,000,000.00** sawa na **asilimia 0.47** ni kutokana na mitaala ya kozi za ustawi wa jamii, **Shilingi 736,235,000.00** sawa na **asilimia 12.27** kutokana na ada ya malazi kwa Wanafunzi wa Vyuo vya maendeleo ya jamii, na **Shilingi 4000.00** sawa na **asilimia 0.0001** kutokana na mapato mengine<sup>12</sup> kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 7.

Kielelezo Na. 7



### Chanzo: Randama Wizara (Machi 2021) na Usanifu wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kuna ongezeko la **asilimia 10.72** la makusanyo ya maduhuli kutoka **Shilingi 5,419,250,000.00** mwaka 2020/2021 hadi kufikia **Shilingi 6,000,000,000.00** mwaka 2021/2022. Kamati imechambua zaidi na kubaini kuwa ongezeko hilo ni kutokana na Ada ya malazi kwa Wanafunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ambayo haikuwepo awali.

<sup>12</sup> Randama Fungu 53 : Makadirio ya Mapato na Maombi ya Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka 2021/22 (Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli)

## **4.2 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa, Bajeti ya Wizara katika mwaka wa fedha 2021/2022 inalenga katika kuchochlea maendeleo ya watu na ustawi wa Taifa. Lengo ni kuhakikisha kuwa, wananchi wanakuwa na siha bora ili kuwawezesha kushiriki katika shughuli za Ujenzi wa Taifa na kuboresha maisha yao. Mipango mbalimbali imepangwa na Serikali kama ilivyoainishwa kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na ule wa Mwaka mmoja pamoja na miongozo mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika**, katika eneo hili Kamati imeanya uchambuzi wa aina mbili kama ifuatavyo:-

### **a) Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara (Fungu 52 na 53) kwa mwaka 2020/2021 na 2021/2022**


**Mheshimiwa Spika**, kama ilivyoolezwa na Waziri mwenye dhamana, lli kuweza kutekeleza malengo mbalimbali ya Wizara kwa mwaka huu wa fedha 2021/2022, Wizara kuititia **Fungu 52** (Idara Kuu Afya) inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi 1,034,133,295,000.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 557,303,059,000.00** sawa na **asilimia 53.89** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 476,830,236,000.00** sawa na **asilimia 46.1** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo<sup>13</sup>.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, sura ya Bajeti ya Wizara inajumuisha **Shilingi 304,779,799,000** sawa na **asilimia 29.5** kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 252,523,260,000.00** sawa na **asilimia 24.4** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC), **Shilingi 351,700,000,000.00** sawa na **asilimia 34** fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo na **Shilingi 125,130,236,000.00** sawa na **asilimia 12.1** fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 8

---

<sup>13</sup> Randama Fungu 52 : Mpango wa Mapato, Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2021/22

## Kielelezo Na. 8



Chanzo: Randama Wizara (Machi 2021) na Usanifu wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haikuishia hapo, ilifanya uchambuzi zaidi na kubaini kuwa, **Bajeti ya Fungu 52** imeongezeka kwa **asilimia 15** kutoka **Shilingi 900,088,240,000.00** mwaka 2020/2021 hadi kufikia **Shilingi 1,034,133,295,000.00** mwaka 2021/2022. Aidha, uchambuzi umebaini kuwa matumizi mengineyo yameongezeka kwa **asilimia 39**, na kwa upande wa fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo kutoka ndani zimeongezeka kwa **asilimia 25** na fedha za nje kwa **asilimia 56**.


**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilihoji sababu za ongezeko hilo na ilielezwa kuwa, ongezeko hilo la fedha limezingatia mahitaji yaliyopo ya kukamilisha miradi mbalimbali ili ianze kutoa huduma. Baadhi ya miradi hiyo ni pamoja na Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mtwara inayotarajija kuanza kutoa huduma za afya kwa mwaka wa fedha 2021/22; Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Chato ambayo inatarajia kuanza kutoa huduma mwezi Aprili, 2021 ikiwemo huduma ya Tiba Utalii (*Medical Tourism*); Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara-Kwangwa ambayo tayari imeanza kutoa huduma; na ujenzi na ukarabati wa vyuo vya mafunzo ya wataalam wa kada za afya vya Mtwara, Kondoa, Dodoma na Nachingwea. **Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi hii muhimu.**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na ongezeko hilo la fedha, Kamati imebaini kuwa mishahara imepungua kwa **asilimia 15**. Kamati llihoji sababu za kupungua na ilielezwa ni kutohana na kusafisha takwimu za watumishi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa watumishi wote wanapokea mishahara yao stahiki na kuondoa watumishi hewa.

**Mheshimiwa Spika**, Kielelezo Na. 9 kinaonesha ulinganisho wa Bajeti kati ya mwaka 2020/2021 na 2021/2022 kwa **Fungu 52** (Idara Kuu Afya).

#### Kielelezo Na. 9

ULINGANISHO WA BAJETI FUNGU 52 2020/2021 NA 2021/2022				
MATUMIZI	2020/2021	2021/2022	ONGEZeko/UPUNGUFU	%
MISHAHARA	357,565,924,000	304,779,799,000	- 52,786,125,000	- 14.8
OC	181,562,950,000	252,523,260,000	70,960,310,000	39.1
MAENDELEO NDANI	280,700,000,000	351,700,000,000	71,000,000,000	25.3
MAENDELEO NJE	80,259,366,000	125,130,236,000	44,870,870,000	55.9
JUMLA	900,088,240,000	1,034,133,295,000	134,045,055,000	14.9



**Chanzo: Randama ya Fungu 52 na Usanifu wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Idara Kuu Maendeleo ya Jamii (**Fungu 53**), Katika mwaka wa fedha 2021/2022, imojiwekeea malengo mbalimbali kama vile kuendelea kuamsha ari ya jamii kushiriki katika Miradi ya Maendeleo, kutoa elimu ya kuzuia ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto na kuhakikisha Maafisa Maendeleo na Ustawi wa Jamii wanaajiriwa katika ngazi mbalimbali ili kusaidia kuleta chachu ya Maendeleo katika Jamii.


**Mheshimiwa Spika**, ili malengo na vipaumbele mbalimbali vya Idara viweze kutekelezwa kikamilifu, rasilimali fedha ni jambo muhimu. Hivyo basi, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Idara Kuu Maendeleo ya Jamii (**Fungu 53**) inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu Jumla ya **Shilingi 43,625,929,000.00**. Fedha hizo zinajumuisha matumizi ya kawaida **Shilingi 28,725,929,000.00** sawa na **asilimia 65.5** na miradi ya maendeleo **Shilingi 14,900,000,000.00** sawa na **asilimia 34.5**. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida, **Shilingi 12,985,672,000 (asilimia 46)** ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na **Shilingi 15,740,257,000 (asilimia 54)** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC). Aidha, kwa upande wa miradi ya maendeleo fedha za ndani ni **Shilingi 4,900,000,000 (asilimia 32.9)** na **Shilingi 10,000,000,000 (asilimia 67.1)** ni fedha za nje<sup>14</sup>.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi kwa lengo la kulinganisha bajeti ya mwaka 2020/2021 na mwaka 2021/2022 kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 na imebaini kuwa, bajeti ya mwaka huu imeongezeka kwa **Shilingi 10,430,190,000** kutoka **Shilingi 33,195,739,000.00** mwaka 2020/2021 hadi kufikia **Shilingi 43,625,929,000.00** sawa na ongezeko la **asilimia 31**. Uchambuzi wa Kamati umeenda mbali zaidi na kubaini kuwa, ongezeko kubwa linaonekana kwenye miradi ya maendeleo kutoka **Shilingi 6,704,364,000.00** hadi kufikia **Shilingi 14,900,000,000.00** sawa na ongezeko la **asilimia 122.2**. Aidha, fedha za nje zimeongezeka kwa **asilimia 270** kutoka **Shilingi**

<sup>14</sup> Randama Fungu 53 : Makadirio ya Mapato na Maombi ya Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka 2021/22

**2,704,364,000.00** hadi **Shilingi 10,000,000,000.00** kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 10. Kamati inapongeza Wizara kwa kuona umuhimu wa Idara hii na kuongeza Bajeti yake. Hii ni muhimu hususan kwenye kuwezesha huduma za ustawi wa jamii na ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii.

### Kielelezo Na.10



**Chanzo:** Randama Wizara (Machi 2021) na Usanifu wa Kamati

b) Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2020/2021 na 2021/2022

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi huu wa Kamati ulilenga katika kubaini ni kwa kiwango gani ongezeko/upungufu wa bajeti ya Taifa unavyoathiri bajeti ya **Fungu 52**. Katika uchambuzi huo, Kamati imebaini yafuatayo:-

- Wakati Bajeti ya Taifa kwa mwaka 2021/2022 imeongezeka kwa **asilimia 3.95** (Kielelezo Na. 11), bajeti ya **Fungu 52** imeongezeka kwa **asilimia 14.9** (Kielelezo Na. 9);
- Wakati bajeti ya Taifa ya maendeleo imeongezeka kwa **asilimia 2.76**, bajeti ya **Fungu 52** kwa ajili ya miradi ya maendeleo imeongezeka kwa **asilimia 32.1**
- Wakati bajeti ya Taifa ya matumizi mengineyo imeongezeka kwa **asilimia 5.43**, bajeti ya matumizi mengineyo ya **Fungu 52** imeongezeka kwa **asilimia 39.1**

Mheshimiwa Spika, tafsiri tunayopata katika uchambuzi huu ni kuwa, licha ya ongezeko dogo katika bajeti ya Taifa, lakini bajeti ya Wizara hii (**Fungu 52**) imepewa kipaumbele zaidi. Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi huu.

### Kielelezo Na. 11

ULINGANISHO WA BAJETI YA TAIFA MWAKA 2020/2021 NA 2021/2022 (KWA MILIONI)				
MATUMIZI	BAJETI KUU YA TAIFA 2020/2021	BAJETI KUU YA TAIFA 2021/2022	PUNGUFU/ONGEZEO	%
OC	3741137.00	3,944,164	203027.00	5.43
MISHAHARA	7762389.00	8,150,509	388120.00	5.00
MAENDELEO	12899433.00	13,255,855	356422.00	2.76
MALIPO MADENI	10476834.00	10,663,278	186444.00	1.78
TANAPA, TAWA NA NCAA	0.00	245,000	245000.00	
JUMLA	34,879,793	36258806.00	1,379,013	3.95

### Chanzo: Mpango wa Taifa 2021/2022 na Usanifu wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya pia uchambuzi wa kulinganisha asilimia ya bajeti ya matumizi mbalimbali ya Wizara (**Fungu 52**) kati ya mwaka 2020/2021 na 2021/2022 dhidi ya bajeti ya Taifa na imebaini yafuatayo:-


- i) Bajeti ya **Fungu 52** kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) imeongezeka kutoka **asilimia 4.85** mwaka 2020/2021 hadi kufikia **asilimia 6.40** mwaka 2021/2022;
- ii) Bajeti ya maendeleo ya **Fungu 52** imeongezeka kutoka **asilimia 2.8** mwaka 2020/2021 hadi kufikia **asilimia 3.6** mwaka 2021/2022

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla bajeti **ya Fungu 52** imeongezeka kutoka **asilimia 2.58** mwaka 2020/2021 hadi kufikia **asilimia 2.85** mwaka 2021/2022 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na.11 (a) na (b). **Kamati inaendelea** kuipongeza Serikali na kusisitiza kiasi hiki cha fedha kitolewe chote na kiendelee kuongezwa mwaka hadi mwaka ili

kuendelea kuboresha Sekta hii muhimu kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla. Mahatma Gandhi amewahi kusema *"It is health that is real wealth and not pieces of gold and silver"*.

**Kielelezo Na. 11 (a)**


MATUMIZI	BAJETI KUU YA TAIFA 2020/2021	BAJETI FUNGU 52 2020/2021	ASILIMIA
OC	3,741,137,000,000	181,562,950,000	4.85
MISHAHARA	7,762,389,000,000	357,565,924,000	4.61
MAENDELEO	12,899,433,000,000	360,959,366,000	2.80
MALIPO MADENI	10,476,834,000,000		0
TANAPA, TAWA NA NCAA	0		
JUMLA	34,879,793,000,000	900,088,240,000	2.58



**Chanzo: Mpango wa Taifa 2021/2022, Randama ya Fungu 52**

**Kielelezo Na. 11(b)**  
**ASILIMIA YA BAJETI YA FUNGU 52 DHIDI YA BAJETI YA  
TAIFA 2021/2022**

MATUMIZI	BAJETI KUU YA TAIFA 2021/2022	BAJETI FUNGU 52 2021/2022	%
OC	3,944,164,00,000	252,523,260,000,00	6.40
MISHAHARA	8,150,509,00,000	304,779,799,000	3.74
MAENDELEO	13,255,855,00,000	476,830,236,000	3.60
MALIPO MADENI	10,663,278,00,000	0	
TANAPA, TAWA NANA C A A	245,000,000,000	0	
JUMLA	36,258,806,000,000	1,034,133,295,000	2.85



**Chanzo: Mpango wa Taifa 2021/2022, Randama ya Fungu 52 Machi 2021 na Usanifu wa Kamati**

### SEHEMU YA TATU

#### 5.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya Uchambuzi huo, Kamati inatoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo yafuatayo kwa lengo la Kuboresha Utendaji kazi wa Wizara hii katika kuwahudumia wananchi:-

#### 5.1 IDARA KUU AFYA

##### a) Vifo vya Mama na Mtoto

Mheshimiwa Spika, Mojawapo ya Vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2021/2022 ni kupunguza vifo vya akina mama vinavyotakana na uzazi pamoja na watoto. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, kiasi cha **Shilingi 63,488,855,480.00** kimeombwa kwa ajili ya kupunguza vifo vya mama na mtoto. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa, bado fedha zinazotengwa kwa mradi huu hazitolewi za kutosha.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzani Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa Hotuba nzuri aliyoitao tarehe 22 Aprili 2021 wakati analihutubia Bunge kwa kusema "**katika miaka hii mitano**

**mpaka 2025, juhudzi za kupunguza vifo vya wajawazito na watoto zitaendelezwa**<sup>15</sup>. Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kuongeza bajeti lakini pia kuhakikisha fedha zote zinazotengwa zinatolewa kwa wakati ili kupunguza vifo hivi ambapo kwa takwimu za Umoja wa Mataifa za 2018 zinaonesha Tanzania ina vifo 398 katika vizazi hai 100,000 wakati Lengo Na.3 la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) hususan Lengo Na. 3 (1) linataka kufikia mwaka 2030, kupunguza vifo vya akina mama na watoto duniani hadi chini ya vifo 70 kwa kila vizazi hai 100,000<sup>16</sup>.

### **b) Huduma Maalum kwa Watoto Njiti**

**Mheshimiwa Spika**, Upatikanaji wa huduma kwa Watoto wachanga wanaozaliwa kabla ya umri wao kutimia na wakiwa na uzito pungufu (njiti) bado ni changamoto kwani hakuna watumishi (waugezi na wahudumu) wa kutosha, vifaa na vifaa tiba pamoja na bima ya afya. Ili kuondoa changamoto hizo Kamati inashauri yafuatayo:-

- i) Serikali ihakikishe kunakuwepo vifaa na vifaa tiba vya kutosha vya kusaidia watoto kupumua kwa kuwa watoto ni wengi na tatizo ni kubwa nchi nzima;
- ii) Serikali iweke utaratibu utakaowezesha watoto njiti kupata huduma ya bima kwa kutumia kadi ya wazazi mpaka kadi ya mtoto itakapokuwa tayari;
- iii) Serikali iboreshe huduma za watoto njiti katika hospitali za pembezoni ili kuepuka tatizo la vifo vya watoto hao ambao wanapoteza maisha wakiwa njiani au wakiwa wamechelewa kupata huduma stahiki kwa kusafirishwa kutoka umbali mrefu kwenda kupata huduma Hospitali ya Taifa Muhimbili;

---

<sup>15</sup> Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, wakati wa kulihutubia Bunge la 12 tarehe 22 Aprili 2021

<sup>16</sup> <https://www.un.org/sustainabledevelopment/health/>

- iv) Bajeti katika Hospitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali nyingine zenyenye kutoa huduma hii ziongezwe ili kuweza kuhudumia watoto hawa ambao wana mahitaji maalum;
- v) Kwa kuwa eneo la sasa wanadolitumia katika Hospitali ya Taifa Muhimbili ni dogo na halikidhi mahitaji, Serikali iandae eneo na kujenga Jengo maalum kwa ajili ya uangalizi wa watoto hawa ikiwa ni pamoja na watoto njiti wanaohuduria kliniki ili wasichangamane na wengine ili kuepuka kusababisha maambukizi kwao; na
- vi) Ili kuboresha utoaji wa huduma, wauguzi waongezwe katika Hospitali zote nchini ikiwemo Hospitali ya Taifa Muhimbili ambayo kimsingi limegawanywa katika maeneo makuu matatu ambayo ni Wodi ya watoto njiti, wodi ya watoto wanaohitaji uangalizi maalum (*Neonatal Intensive Care Unit*)na wodi ya Kangaroo. Maeneo yote matatu kwa sasa yana wauguzi arobaini na tisa (49) na wahudumu kumi na nne (14) wakati mahitaji halisi ni kuwa na wauguzi mia moja themanini (180) na wahudumu thelathini (30).

### c) Uhaba wa Dawa Nchini

**Mheshimiwa Spika**, Upatikanaji wa Dawa nchini bado ni changamoto. Kamati inafahamu kuwa kuimarka kwa huduma ya upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kulingana na mahitaji halisi katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya nchini ni moja ya Vipaumbele vya Wizara hii. Hata hivyo, hali ya upatikanaji wa dawa nchini siyo wa kuridhisha.

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/2021, kiasi cha shilingi **Bilion 200** kiliidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Dawa. Hadi kufikia Machi 2021 ni **asilimia 26.6** tu ya fedha ndiyo zilikuwa zimepokelewa. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, bajeti ya dawa imepanda kwa **asilimia 14.5** hadi kufikia Shilingi **229,160,540,000.00**. Kuongeza bajeti ya dawa tafsiri nyingine ni kuwa tumeshindwa kukinga na ndiyo maana tunajikita kutibu. Pamoja na kuongeza bajeti ya dawa, bado kuna changamoto ya utoaji wa fedha kama ilivyoelezwa na

hivyo kuathiri upatikanaji wa dawa na chanjo katika vituo vyta afya nchini. Licha ya taarifa ya Wizara kuonesha kuwa hakuna uhaba wa dawa na chanjo nchini katika Bohari Kuu ya Dawa, dawa na chanjo hizi bado hazijawafikia wananchi. Kutokana na hali hii, Kamati inashauri yafuatayo:-

- i) Serikali iharakishe upelekaji wa dawa na chanjo katika vituo vyta afya nchini;
- ii) Madeni yote ya dawa kwa vituo vyta Afya yaangaliwe upya ikibidi Wizara ya Fedha iyafute ili waweze kupatiwa dawa;
- iii) Bajeti yote inayoidhinishwa na Bunge lako Tukufu itolewe yote kwa wakati ili kuondoa changamoto hiyo. Aidha, mkazo zaidi uwekwe kwenye kinga;
- iv) Mifumo ya kielektroniki iwekwe katika vituo vyta kutolea huduma za afya ili kudhibiti upotetu wa dawa; na
- v) MSD ianzu kununua dawa kwa wazalishaji na kuanza kuuza dawa hizo kwa Sekta Binafsi ili kuongeza kipato.
- vi) Serikali iharakishe utekelezaji uamuzi wa kuanzisha kiwanda cha kuzalisha dawa na vifaa tiba nchini cha Simiyu Medical Product ili kupunguza gharamaza kununua dawa nje ya nchi

**d) Bima ya Afya kwa Wote**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inampongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa uamuzi wake wa kuongeza umri wa wategemezi wa bima ya afya kutoka miaka 18 hadi 21. Ni dhahiri kuwa Rais ameamua kupunguza mzigo kwa wazazi hasa ikizingatiwa kuwa vijana wa umri wa miaka 18 kwa tamaduni zetu bado ni tegemezi kwa wazazi.

**Mheshimiwa Spika**, Bima ya Afya kwa wote imekuwa ni ajenda ya Bunge kwa muda mrefu kuititia Kamati hii. Hata hivyo, bado jambo hili halijatekelezwa na Kamati imekuwa

ikiambiwa mchakato unaendelea. Katika vikao vya uchambuzi wa bajeti ya Wizara hii, Kamati ilihoji hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa ushauri huu wa Bunge na ilielezwa kuwa, Serikali itahakikisha inaleta Muswada huu katika Mkutano wa Tatu wa Bajeti na tayari **Shilingi Milioni 231** zimetengwa kwa ajili ya kugharamia maandalizi ya kutungwa kwa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote na utoaji wa elimu kwa Umma. Ni imani ya Kamati kuwa Muswada huu utaletwa kama ilivyoahidiwa ili kuhakikisha wananchi wote wanakuwa na uhakika wa upatikanaji wa huduma za afya nchini. Aidha Kamati inashauri yafuatayo:-

- i) Wananchi washirikishwe vya kutosha ili kutoa maoni yao katika kuboresha muswada;
- ii) Serikali ione namna ya kushirikisha Sekta Binafsi nchini katika kutoa huduma ya Bima ya Afya; na
- iii) Kwa kuwa kumekuwepo na malalamiko kwa wateja wa NHIF kukosa baadhi ya huduma zikiwemo dawa, Wizara isimamie kuondoa changamoto hii.

**e) Uhaba wa Rasilimali Watu**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza Serikali kwa hatua iliyofikia ya uboreshaji na ujenzi wa Vituo vya Afya, Zahanati na Hospitali katika maeneo mbalimbali nchini. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa bado changamoto ya rasilimali watu katika Sekta hii ni kubwa. Takwimu zinaonesha kuwa, upungufu wa rasilimali watu ni **asilimia 53**. Kamati imeshuhudia Taasisi kubwa kama JKCI, MOI na *Ocean Road* zote zikiwa na upungufu wa Watumishi. Changamoto zaidi inaonekana katika vituo vya afya na zahanati ambako ndiko wagonjwa wengi zaidi wanakwenda kupata huduma. Hali hii kiasi kikubwa inachangia vifo vya akina mama na watoto.

**Mheshimiwa Spika**, nchi ikiwa inajienda kuwa na Bima ya Afya kwa wote, suala la uwepo wa Watumishi wa kutosha ni muhimu sana kwani utoaji wa huduma hizi unahitaji

wafanyakazi wa kutosha wenye uwezo na ujuzi na ambao watasambazwa kwa usawa katika maeneo yote nchini. Hivyo basi **Kamati inashauri mkakati wa makusudi wa kuajiri watumishi wa Sekta ya afya uanze mara moja**. Serikali na **hususan Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ihakikishe inatoa vibali vya ajira kwa watumishi wa afya hasa ikizingatiwa kuwa kuna wataalam wengi mtaani ambao hawana ajira.**

**f) Ugonjwa wa Virusi vya Korona - UVIKO (COVID-19)**

**Mheshimiwa Spika**, ugonjwa wa virusi vya Corona bado ni tishio duniani kote. Kamati inampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuamua kuunda Kamati ya Wataalam ambao kwa kushirikiana na Taasisi za Afya Duniani na zile za Kikanda za EAC na SADC wamepanga kuliangalia suala hilli kwa undani ikiwa ni pamoja na kufanya uchambuzi wa kina na kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukua na jinsi ya kuendelea kupambana na maradhi hayo. **Kamati inaendelea kusitiza wananchi kuendelee kuchukua tahadhari kwa kufuata miongozo ya kinga ambayo imekuwa ikitolewa nchini na kuendelea kula mboga na matunda kwa wingi pamoja na kutumia tiba asili na tiba mbadala ili kupunguza maambukizi haya.**

**g) Magonjwa Yasiyoambukiza (*Non- Communicable Diseases*)**

**Mheshimiwa Spika**, Nchi yetu kama zilivyo nchi nyininge duniani zina matatizo ya afya yanayotokana na magonjwa yasiyoambukiza (*Non Communicable diseases*). Takwimu zinaonesha kuwa, magonjwa yasiyoambukiza yanachangia kwa **asilimia 27** ya vifo vyote nchini. Tafiti za Mwaka 2012 zinaonesha kuwa, kwa kila watu 100 wenye miaka 25 na kuendelea, watu 9 wana kisukari, watu 26 wana shinikizo la damu, watu 25 wana mafuta yaliyozidi kwenye damu na 34 wana uzito uliozidi. Hata hivyo, takwimu za 1986 zinaonesha kuwa ni mtu 1 kati ya 100 ndiyo alikuwa na kisukari na 5 kati ya 100 walikuwa na shinikizo la damu. Tafsiri ni kwamba,

kumekuwa na ongezeko kubwa la wagonjwa wanaouguwa magonjwa yasiyoambukiza nchini. Ongezeko la magonjwa haya yote linatokana na mabadiliko ya mtindo wa maisha kama kutofanya mazoezi, ulaji usiofaa, matumizi ya pombe kupindukia, tumbaku na madawa ya kulevyia, msongo wa mawazo pamoja na na kutopata usingizi wa kutosha.

**Mheshimiwa Spika**, takwimu za Ripoti ya utafiti wa hali ya lishe nchini ya mwaka 2018 (Tanzania National Nutrition Survey, 2018) zinaonesha kuwa, **asilimia 31.8** ya watoto wenye umri chini ya miaka 5 wamedumaa na wanatoka katika mikoa 11 ambayo inaongoza katika uzalishaji wa chakula (Morogoro, Mbeya, Ruvuma n.k), **asilimia 14** wana uzito pungufu na **asilimia 5** wana upungufu wa damu<sup>17</sup> hivi vyote vinachangiwa na lishe duni.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na ongezeko la magonjwa haya yote, bajeti inayotengwa kukabiliana na magonjwa haya ni ndogo na hivyo haitoshelezi hasa ikizingatiwa kuwa, kutibu magonjwa haya yasiyoambukiza ni gharama kubwa. Kutokana na hali hii Kamati inashauri yafuatayo:-

- i) Elimu iendelee kutolewa kwa jamii kuititia njia mbalimbali kama kufundishwa mashulen, vipindi vyya redio na televisheni juu ya mbinu za kujikinga na magonjwa haya pamoja na uzingatiaji wa lishe bora;
- ii) Rasilimali watu ijengewe uwezo wa kuweza kutambua, kuzuia na kutibu magonjwa yasiyoambukiza;
- iii) Kutokana na gharama kubwa za kutibu magonjwa yasiyoambukiza, ni vema Serikali ikasaidia katika kutoa Ruzuku ya dawa za kisukari au kupunguza kodi ya uingizaji wa dawa nchini ili zitolewe kwa bei nafuu;
- iv) Wizara ya Afya ishirikiane na Wizara nyingine kama Ujenzi, habari, Elimu ili kuhakikisha ujenzi wa barabara unazingatia

---

<sup>17</sup> Ripoti ya utafiti wa hali ya lishe nchini ya 2018

sehemu ya watembea kwa miguu na vipindi nya Elimu kwa Umma kuhusu athari za magonjwa yasiyoambukiza na namna ya kujikinga. Mwanazuoni Henry De Bracton wa Uingereza amewahi kusema “**An ounce of prevention is worth a pound of cure.**”

#### **h) Huduma za Kibingwa**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza sana Serikali kutokana na ununuzi wa vifaa na mitambo mikubwa na ya kisasa katika Sekta ya Afya yenye uwezo wa kutibu magonjwa mbalimbali makubwa na yenye ghamama kubwa ambayo awali ilikuwa inawalazimu wagonjwa kupelekwa nje ya nchi. Kama ilivyoeleza awali kwenye maelezo ya ukaguzi wa miradi, Kamati imeshuhudia uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali yetu ambao Kamati inaamini kama utatangazwa ipasavyo, ni dhahiri Serikali itakuwa na uhakika wa kupata fedha za kutosha na za kigeni kutokana na kuwa Kitovu cha Utalii wa Matibabu (*Hub of Medical Tourism*) Hivyo basi, Kamati inashauri:-

- i) Serikali iweke mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutumia Balozi zetu kutangaza Huduma za kibingwa zinazotolewa na Taasisi zetu kama JKCI, MOI, Ocean Road, Hospitali ya Benjamin Mkapa na nyiningine nydingi; na
- ii) Serikali iendelee kufundisha Wataalam wake ili kuwa wabobezi zaidi katika kutumia mitambo hii ya kisasa ili kuepuka kutumia Wataalam kutoka nje ya nchi.

#### **i) Kuimarisha Huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala**

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na ongezeko la matumizi ya Tiba asili na Tiba mbadala nchini kwa sasa jambo ambalo ni jema kabisa. Kamati inapongeza wataalam hawa kwa kuwa wabunifu na kuisaidia jamii yetu.

**Mheshimiwa Spika**, Ili kuepuka uwepo wa watoa huduma hawa wasio waaminifu, Kamati inashauri Wizara iwasajili watoa huduma hawa na dawa zao ambao zimethibitika

kuwa zinatibu magonjwa mbalimbali na kuanza kuzisambaza katika vituo vyetu vya kutolea huduma za afya. Aidha, Serikali iendelee kutoa elimu kwa jamii juu ya tiba asili na tiba mbadala ambazo hazina madhara kwa watumiaji.

#### j) Hospitali ya CCBRT

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kazi kubwa inayofanywa na Hospitali ya CCBRT katika kutoa huduma za afya nchini. Hospitali hii awali ilisajiliwa kama Hospitali ya kutoa huduma za matibabu zinazolenga kuzuia ulemavu au kupunguza athari za ulemavu. Hata hivyo, Ili kuongeza mchango wake katika sekta ya afya ilikubaliwa kuanza kutoa huduma za Afya ya Uzazi na Watoto wachanga. Mwaka 2012 CCBRT ilianza kujenga miundombinu ya kutolea huduma hiyo ikiwa ni pamoja na Jengo ambalo tayari limekamilika kwa asilimia 90 na mashine na Vifaa tiba ambavyo baadhi vimeshanunuliwa tayari. Kamati imebaini kuwa, pamoja na CCBRT kupeleka maombi ya kubadili usajili wake lakini hadi sasa bado suala hili halijakamiliika. **Kamati inashauri Wizara kukamilisha usajili wa Hospitali hii mapema ili kuongeza wigo wa utaoji wa huduma za afya nchini kwani Hospitali ya CCBRT itapunguza msongamano wa wagonjwa katika hospitali za Mkoa wa Dar es Salaam na hususan Hospitali ya Taifa Muhimbili.**

### 5.2 IDARA KUU - MAENDELEO YA JAMII

#### a) Uhaba wa Maafisa Ustawi na Maendeleo ya Jamii

**Mheshimiwa Spika**, Takwimu za Wizara zinaonesha kuwa mahitaji halisi ya Maafisa Ustawi wa Jamii nchini ni 22,972. Hata hivyo, walioajiriwa ni 744 sawa na **asilimia 3.24** tu. Kwa upande wa Maafisa Maendeleo ya Jamii wanaohitajika ni **5472** ila waliopo ni **2893** sawa na **asilimia 52.9**. Ikumbukwe kuwa, Maafisa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya jamii wana nafasi kubwa ya kuleta chachu ya fikra za kimaendeleo kwa kuhamasisha jamii kutumia fursa zilizopo kujiletea maendeleo lakini pia kuiandaa jamii kukabiliana na mabadiliko na changamoto mbalimbali kwenye jamii. Upungufu huu

unaashiria kuwa jamii yetu bado haipati chachu inayotakiwa na hivyo kushindwa kuchangia kikamilifu katika Maendeleo ya Taifa letu. **Hivyo basi Kamati inashauri Serikali itoe vibali vya Ajira kwa watumishi hawa kwani Vyuo vyetu vinazalisha Wataalam hawa wa kutosha na wapo wakiwa hawana ajira.**

**b) Miundombinu ya Vyuo vya Maendeleo ya Jamii**

**Mheshimiwa Spika**, hali ya Vyuo vya Maendeleo ya Jamii nchini bado siyo ya kuridhisha, kwani baadhi ya vyuo hivi pamoja na kuidhinishiwa fedha na Bunge lako Tukufu, fedha hizo zimekuwa haziendi kabisa hali inayofanya mazingira ya kufundisha na kujifunzia kuwa magumu. Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, **Shilingi Milioni 270** ziliidhinishwa, lakini hazijatolewa mpaka wakati tulipokuwa tunachambua bajeti ya Wizara. Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, **Shilingi Milioni 360** zinaombwa kwa ajili ya ukarabati wa Vyuo sita (6) vya Maendeleo ya Jamii.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona fedha zinazotengwa kwa ajili ya ukarabati wa vyuo vya maendeleo ya jamii hazitoshi. Kamati inaendelea kusisitiza kuwa, bajeti ya vyuo hivi iongezwe lakini pia fedha hizi zinazotengwa zitolewe zote na kwa wakati hasa ikizingatiwa kuwa vyuo hivi ndiyo vinategemewa kuzalisha Maafisa Maendeleo ya Jamii ambao ni nguzo muhimu kwa Maendeleo ya Taifa letu.

**c) Usawa wa Kijinsia**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa mradi wa kuzuia ukatili wa kijinsia na afua za kuwezesha wanawake kiuchumi unategemea fedha za nje kwa **asilimia 100**. Katika Mwaka 2020/2021 fedha zilizopokelewa ni **Shilingi Milioni 90** sawa na **asilimia 9** tu kat i ya **Shilingi Bilioni 1.04** zilizotengwa. Kamati imesikitishwa na jambo hili.

**Mheshimiwa Spika**, Lengo Na. 5 la Malengo ya Maendeleo Endelevu linasisitiza umuhimu wa kuzuia ukatili wa kijinsia “**ending all discrimination against women and girls is not only a basic human right, it's crucial for sustainable future; it's**

proven that empowering women and girls helps economic growth and development”<sup>18</sup>. Hivyo basi, Kamati inashauri bajeti ya kutosha itengwe na itolewe yote na kwa wakati ili kuwezesha utekelezaji wa mipango ya kuzuia ukatili wa kijinsia.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine napenda kutoa shukrani zangu kwako kwa fursa uliyonipa ya kuwasilisha maoni haya ya Kamati lakini pia kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu Tukufu. Nawashukuru sana Waziri wa Afya Dkt. Dorothy O. Gwajima (Mb) – Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Manaibu Mawaziri wake Mhe. Dkt. Godwin Oloyce Mollel (Mb) na Mhe. Mwanaidi Ali Khamis (Mb) kwa ushirikiano wanaoipa Kamati. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Idara Kuu Afya Prof. Abel Makubi na Naibu Katibu Mkuu Idara Kuu Maendeleo ya Jamii Dkt. John Jingu pamoja na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati tangu tulipoanza kufanya nao kazi na kushiriki vizuri kwenye uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa ushirikiano mzuri ambao wanani. Wajumbe hawa ni wachapa kazi na wameshiriki kikamilifu katika uchambuzi wa Bajeti na kuhakikisha wanahoji ili kupata ufanuzi wa kina. Nawapongeza sana na naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

- |  |                |
|--|----------------|
| 1. Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo, Mb    | - Mwenyekiti   |
| 2. Mhe. Aloyce John Kamamba, Mb        | - M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb       | - Mjumbe       |
| 4. Mhe. Eng. Samwel Ilyayuma Xaday, Mb | - Mjumbe       |
| 5. Mhe. Husna Juma Sekiboko, Mb        | - Mjumbe       |
| 6. Mhe. Tecla Mohamedi Ungele, Mb      | - Mjumbe       |
| 7. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb         | - Mjumbe       |
| 8. Mhe. Kassim Hassan Haji, Mb         | - Mjumbe       |

---

<sup>18</sup> <https://www.un.org/sustainabledevelopment/gender-equality/>

- |  |          |
|--|----------|
| 9. Mhe. Francis Leonard Mtenga, Mb       | - Mjumbe |
| 10. Mhe. Jumanne Abdallah Sagini, Mb     | - Mjumbe |
| 11. Mhe. Latifa Khamis Juwakali, Mb      | - Mjumbe |
| 12. Mhe. Kabula Enock Shitobela, Mb      | - Mjumbe |
| 13. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb      | - Mjumbe |
| 14. Mhe. Bernadeta Kasabago Mushashu, Mb | - Mjumbe |
| 15. Mhe. Fatma Hassan Toufiq, Mb         | - Mjumbe |
| 16. Mhe. Neema Kichiki Lugangira, Mb     | - Mjumbe |
| 17. Mhe. Mussa Ramadhani Sima, Mb        | - Mjumbe |
| 18. Mhe. George Ranwell Mwenisongole, Mb | - Mjumbe |
| 19. Mhe. Dkt. Paulina Daniel Nahato, Mb  | - Mjumbe |
| 20. Mhe. Salome Wycliffe Makamba, Mb     | - Mjumbe |
| 21. Mhe. Abdallah Dadi Chikota, Mb       | - Mjumbe |
| 22. Mhe. Khamis Kassim Ali, Mb           | - Mjumbe |
| 23. Mhe. Khalifa Mohamed Issa, Mb        | - Mjumbe |
| 24. Mhe. Hassan Ziddu Kungu, Mb          | - Mjumbe |
| 25. Mhe. Nashon William Bidyanguze, Mb   | - Mjumbe |
| 26. Mhe. Hamisi Shabani Taletale, Mb     | - Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wetu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema. Pamoja nae namshukuru Mkurugenzi Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein na Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Gerald Magili kwa ushirikiano wanaoipa Kamati yetu wakati wote. Aidha, tunawashukuru sana Makatibu wa Kamati yetu Ndg. Pamela Pallangyo na Ndg. Nyamwanja Chilemeji pamoja na msaidizi wa Kamati Ndg. Jane Ndulesi kwa kuhakikisha shughuli zote za Kamati zinatekelezwa kikamilifu ikiwemo Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja **Fungu 52** jumla ya **Shilingi 1,034,133,295,000.00** na **Fungu 53** jumla ya **Shilingi 43,625,929,000.00**.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha, naunga mkono Hoja.

Stanslaus H. Nyongo (Mb),

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII**

11 MEI, 2021

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati kwa taarifa hii ambayo umeiwasilisha.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tutaendelea na uchangiaji. Nimepata majina hapa ya Wabunge mbalimbali ambao wanahitaji kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Tutaanza na Mheshimiwa Josephat Gwajima, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara na Mheshimiwa Grace Tendega, ajiandae.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi kuchangia. Namshukuru pia Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Dorothy pamoja na Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dakika chache sana nizitumie dakika zangu vizuri. Nataka kuzungumza kwa habari ya chanjo zinazoitwa *corona vaccine*.

Mheshimiwa Nainu Spika, niseme kwa ufupi kwamba mimi siko kinyume na chanjo za *corona*, hapana, wala siko kinyume na chanjo yoyote ile. Kwenye mazungumzo yangu, mtu asininukuu kwamba napinga chajo, hapana, kwa sababu tayari Tanzania tulishachanjwa; chanjo ya Kifua Kikuu tayari tulishachanjwa; chanjo ya Surua tayari; chanjo ya Kifaduro tayari; chanjo ya Polio tayari; na sasa hivi kuna chanjo zinaendelea kama chanjo ya Homa ya Ini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, siko kinyume na chanjo kwa sababu tayari chanjo ziko Tanzania na watu wanaendelea kuchanjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho niko makini nacho sana ni aina ya chanjo inayoitwa chanjo ya *corona virus* ilivyokuja na *study yake*. Chanjo hii ni tofauti na chanjo nydingine zote ambazo zimekuwepo duniani. Dunia imekuwa na aina ya chanjo zinaitwa *attenuation*. Maana yake ni kwamba *virus wa corona* wanapunguzwa nguvu, wanaondolewa *properties*, halafu wanaingizwa ndani ya mwili wa mtu, halafu *antibodies* zina-react, *immunity* inatengenezwa. Hii ndiyo aina ya chanjo ambayo imekuwepo miaka yote na siku zote. Chanjo hii kukamilika inagharimu miaka minane mpaka kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, chanjo hii inayoitwa chanjo ya *corona* ni chanjo ya mwendokasi, miezi miwili, miezi mitatu au miezi minne tayari. Unapajaribu kuuliza kwamba hii chanjo kwa nini imekuwa na haraka sana? Kuna magonjwa mengi kama Malaria na mengine ambayo tungetegemea mfanye haraka haraka kupata chanjo ili watu waokolowe. Wanasema sababu ya kwanza, kwa sababu teknolojia imeongezeka; sababu ya pili, wame-*mobilize resources* kutoka kwenye makampuni mengi duniani; na sababu nydingine ni kwamba ni kwa sababu ni *pandemic*, nami sikatai.

Mheshimiwa Naibu Spika, teknolojia ya chanjo hii inaitwa *MRA*. Maana yake, ni aina ya chanjo ambayo wanachukua *generic material* ya *virus* halafu wanaingiza kwenye *MRA* ya mtu, baadaye mtu, wanasema kwamba hataingilia na *gene*, lakini wanasema wanaingiza kwenye *genetical material* yaani *genetical material* za *virus* zinaingizwa kwenye *cell* ya mtu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti ya mtu na mnyama ni *RMA*, *DNA* na *G/NOS* ambazo ndio *genes*. Huo ni utu wa mtu tofauti na mnyama. Chanjo hii inaingia mpaka kwenye *RNA*, chanjo hii inaingia kwenye *DNA*, kwenye *G/NOS*, kwenye utu wa mtu. Hatujajua baada ya chanjo hii atazaliwa mtu wa namna gani baada ya miaka kumi, baada ya miaka mitano, baada ya miaka sita, hatujajua mpaka leo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya sana, nifunguke kidogo na hekima yako ikikuruhusu utaniongezea muda kidogo kama ukiisha, kwa sababu hoja yangu ina *national concern*. Mashirika duniani kwa mfano, Marekani kuna shirika ambalo linaruhusu dawa zianze kuitishwa, linaitwa *CDC (Center for Disease, Control and Prevention)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, shirika lingine linaitwa *FDA* ambayo ni *Food and Drug Administration*; haya ndiyo mashirika ya Kimarekani yanayo-*authorize* dawa zote kwa ajili ya matumizi ya binadamu. Chanjo hizi zote unazoziona, hazijawa *authorized*na mashirika haya. Kuna kishirika kidogo ambacho kinaitwa *Emergency Use Authorization*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki kishirika kinaidhinisha dawa ambazo ni dharura, ambazo zinatakiwa ziende haraka. Sheria ya hawa *Emergences Use Authorization* ni kwamba kwa sababu dawa hajifanyiwa utafiti wa kutosha miaka mingi, kwa hiyo, inaruhusiwa *emergence* kwa sababu ya uhitaji wa dunia. Madhara yatakayowapata wale, *liability* haziko juu ya hii kampuni, ziko juu ya mtumiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa najaribu kuwaza, nikiangalia kwa mfano chanjo ambazo ziko tayari zimesharuhusiwa kuanza kwa mfano, kuna chanjo ya kwanza inaitwa *Jonhson Johnson*, imeruhusiwa na Wamarekani ambayo tarehe 27 Februari, 2021 ndiyo ilikuwa *authorized* kutumika *emergency*, lakini kwenye *website* yao, watengeneza chanyo wenyewe wanasesma madhara au *side effect* ya chanjo hii: kwanza, kushindwa kupumua sawasawa; pili, kuvimba kwenye uso na kwenye *throat*; tatu, mapigo ya moyo yanakwenda haraka; nne, *bad rush* kwenye mwili; tano *dizziness*; na sita, damu kuganda kwenye mwili. Hii ni kwenye *website* yao. Sasa kama watengenezaji wa chanjo wenyewe wanaonesha kwenye *website* yao kuna shida hiyo, ni vizuri sasa tuwe makini. Najua Mheshimiwa Rais kwa hekima yake ameunda Kamati inayofuatilia hayo, lakini mimi kama Mbunge nina haja ya ku-*discuss* na ku-*alert* kwamba wawe makini wanapochagua aina ya chanjo hizi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nyingine ya pili inaitwa *AstraZeneca*, ambayo imetengenezwa *Oxford* kule *UK*. Yenyewe kwenye website yao wanasema *side effect* yake ya kwanza ni damu kuganda; na ya pili ni kifo. Ni kifo ndiyo. Wanasema, kwenye kifo hapa, wanawenza kufa watu labda kumi *out of hundred*, lakini kwenye website yao wanaonyesha kwamba *death may occur*, lakini dunia bila kufanya *research*, bila kuwaza watu wanakimbilia kupata chanjo kwa sababu ya *fear* ya *corona*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyingine inaitwa *Moderna* ambayo ni ya *USA* na nyingine inatiwa *Pfizer* ambayo ni ya Ujeruman. Kwa ujumla chanjo hizi zote zinaonyesha *side effect* ni kuganda damu, kushindwa kupumua na kifo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni kweli, tukikataa chanjo tunaweza kuwekewa *ban* ya kusafiri kwenda Ulaya kwa sababu hatujachanjwa. Tunakabiliwa na uchaguzi mbaya sana; tuchanjwe kitu tusichokijua sawa sawa au tusichanjwe tuzuiwe kwenda Ulaya. Naomba sana Wizara ya Afya wajaribu kuangalia kwa makini sana kwenye suala ya chanjo. Waangalie madhara ya sasa, madhara ya siku zijazo na madhara ya Taifa. Jambo hili ni la muhimu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu kidogo niongeze kidogo. Matatizo tuliyonayo ni kufikiri kila kinachotoka Ulaya kinafaa kwetu; *and this is a problem we face. Our colonizers* (watawala wetu) walitujengea ufahamu kwamba kikitoka kwao kinafaa. Jana kuna mtu mmoja anaitwa Dkt. Edward Fleming ambaye ni kati ya watu walioshiriki kutengeneza mojawapo ya chanjo, alikuwa ameandika barua kwa Rais wa Marekani, nina rekodi, amesema, anashauri hizi chanjo ziachwe mara moja kwa sababu madhara yake ni makubwa kuliko faifa yake kwa *prevention*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali yangu siku pamoja na Wizara ya Afya, *before we venture in to what kind of vaccine we should take*, tunatakiwa tuwe na wataalam wetu wa hapa. Namba moja, *wa-analyse content*. Haya majina ya chanjo ni *business name*, lakini kuna

*generic name that includes the content*, kuna nini ndani ya chanjo, *wa-analyse* matatizo yatakayotupata sisi tutakaochanjwa na watoto wetu baadaye. Kwa sababu shida ikiingia kwenye DNA na kwenye gene na RNA, ndiyo utu wa mtu. Ina-send message miaka ijayo mtu azaliwe wa namna gani? Madhara yanaweza kuwa siyo leo, *but in 20 or 30 years to come* tunaweza kuwa na Watanzania wasioweza kufikiri vizuri, wasio na maamuzi mazuri na Taifa letu litashindwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Wizara ya Afya, *before we know which method we implement*, tufanye due-diligence ya kuifua tilia hii chanjo ni ya namna gani? Pia tusome website.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niongezee jambo moja kwamba *anything* kule Marekani au kule Ulaya; Ulaya kuna organization inaitwa EMA maana yake ni European Medicine Agents ambayo na yenewe ina-authorize dawa zote ndiyo zinatumika. Hizi agencyzote; agencyya Ulaya na agency za Marekani hazija-authorize zenewe, zimebekwa kwenye ka-institution kanakoruhusiwa kuwa-authorize emergence kule na matokeo ya kuwa-authorize emergence, huyo aliyetengeneza dawa hana madhara, kwamba ni wewe mwenyewe, utajjua wewe mwenyewe; na wanasema kwamba iwe inatumika huku inafanyiwa uchunguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ujinga kuruhusu Taifa zima kuwa experiment ya majoribio, eti kwa sababu tuna haraka ya Corona. *I know Corona is dangerous, yes but it is more dangerous for us to allow the all natives*, Watanzania wote milioni 50 wachanjwe eti ndiyo tuwe tunaangalia matokea, tunaripoti kwenye hizi institution. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana hili suala liangaliwe kwa makini, lifanyiwe kazi na mwisho wa siku kila silaha itakayofanyika juu yetu haitafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara atafuati na Mheshimiwa Grace Tendega na Mheshimiwa Mchafu Chakoma, ajlandae.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nami nichukue nafasi hii kuchangia katika maeneo kama matatu hivi. Kwanza kabisa, nitachangia kuhusu upandikizaji wa watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwanamke au familia kukosa mtoto linaumiza sana. Mwanamke asipokuwa na mtoto anaumwa mno, na ni ugonjwa. Kisaikolojia na hata maisha kwa ujumla kwake hayana amani. Sasa kuna huu upandikizaji wa watoto nje ya nchi. Mtu hana mtoto, anajaribu kwa madaktari hapa, wanasema wewe lazima ukafanyiwe upandikizaji. Sasa hii ya upandikizaji inachukua fedha nyingi mno. Wanawake hawawezi kwenda China wala *South Africa*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kupitia Wizara ya Afya, hebu tuwasaidie wanawake kama tunavyosaidia magonjwa ya moyo na figo, watu wanasaidiwa, wanakwenda nje. Basi hata kama ni shilingi milioni 20, Serikali ichangie angalau nusu na yule mtu aambiwe na wewe saidia ongeza kiasi. Kwa kufanya hivyo, tutasaidia wanawake wengi sana.

Pia Serikali ianze kujipanga. Tutakwenda kutafuta watoto huko nje mpaka lini? Ndiyo maana kunatokea maneno kwamba unajuaje kama zile mbegu ni za mume wako? Kwa sababu unaenda kupandikizwa kule nje, labda watachukua mbegu nyingine, wataweka ili mradi mtu arudi na mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali ianze kujipanga katika utaalam huo, tuwe na maabara hapa Tanzania, nasi tuanze *test tube babies*, tuienze wenyewe hapa Tanzania. Haya mambo ya kwenda nje yatatuletea matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, naipongeza sana Serikali, ilipofanya zoezi la tohara hasa kwa watani zangu kule Tabora, Mwanza, nasikia hata huko Sumbawanga, hili jambo lilikuwa ni zuri kwa manufaa ya afya na hasa katika kupungiza maambukizi ya Ukimwi. Sasa wamefanya hiyo kazi ya tohara ya wanaume vizuri sana, naomba sana Serikali ijjipange kumaliza kabisa tatizo la ukeketaji wa wanawake katika mikoa ambayo bado ukeketaji unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepata ushahidi kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Mara, anasema licha ya juhud zile zote; *seminars* na *workshops* bado watoto wanakeketwa. Sasa Mheshimiwa Ummy alifanya, alijitahidi sana, mimi leo nawomba na wanaume mtusaidie kupiga kampeni kwamba msichana au mwanamke aliyekeketwa hataolewa. Mkianza ninyi, itasaidia kwa sababu asili ya mwanamke kukeketwa ilitokana na wanaume kutaka kuwagandamiza wanawake wasipate hisia katika tendo la ndoa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kidogo nieleze, tunalionna hili jambo ni rahisi sana au la kawaida. Nimefanya utafiti, hawa wanawake waliokeketa ukiongea nao inasikitisha. Kwanza wana madhara yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanamke aliyekeketwa anapewa ulemavu makusudi. Unamkata mtu kidole hiki cha mwisho makusudi tu, hawezi kufa lakini hawezi kushika ugali vizuri. (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sina nia ya kuwachekesha lakini nasema ukweli kisayansi. *Imagine* mtu akikukata ulimi hapa mbele, hutakufa lakini huwezi kuonja. Kwa hiyo, wanawake hao kwanza wanapata ulemavu, kwa sababu wanaondolewa kiungo ambacho akipaswi kuondolewa. Yaani ile ni kama kufyeka; na sehemu nydingine wanafyeka mpaka zile *labia minora* sasa hilo ni tatizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maumivu makali, ulemavu, halafu wanawake hao wakiingia katika kuolewa, wanabakwa kwa sababu hawasikii kabisa, nisemeje kwa

Kiswahili? Hawasikii hisia na hawafikii *orgasm*. Sasa huyo mwanamke anaishi maisha yote. Mmoja aliniambia, nimezaa watoto watano mwanangu, sijui mnachosema eti kuna raha na furaha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni shida sana. Wengi hupata ulemavu, maumivu makali wakati wa kujifungua, wakati mwininge lile kovu sasa linaweza likachanika. Hawa wanaweza kupata Ukimwi, kwa sababu vile visu siyo kwamba wanabadiisha. Sijui wanatumia visu au mapanga, mimi sijui. (*Kicheko/Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Eeh! (*Kicheko*)

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wengine wanapata Ukimwi, *tetanus*na magonjwa mengine. Halafu *waki-bleed*sana lazima watakuwa *anemic*. Kwa hiyo, hayo ni madhara. Naiomba sana Serikali sasa hivi itoe tamko, Wizara ya Afya pamoja na Katiba na Sheria, mtoe tamko la kutokomeza kabisa kama tulivyoweza kutokomeza wale waliokuwa wanawachinja *albino*. Wale wanaowaita mangariba, bado wapo na huo ukeketaji umehama kwenye ile mikoa huko mpaka Dar es salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu wengi mnajua kuna kundi lile ambalo linatoka Mara, liko Ukonga na Segerea. Kuna watoto kule walitoroka; nina uhakika na nina Ushahidi kwamba watoto wawili walitoroka kukimbia kukeketwa. Kwa hiyo, naliomba sasa ulibebe Waziri wa Afya tufanye kampeni, tuandike andiko zuri kutumia hata *celebrity* wetu, hilo litapotea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, Kituo cha Afya, *Mkwawa University* kinahudumia watu zaidi ya 50,000. Namwomba sasa Waziri, ikiwezekana tuongozane akaangalie pale. Kinatakiwa kipandishwe sasa kiwe Hospitali kwa sababu kinahudumia watu wengi. Hiyo itasaidia sana kupunguza msongamano kwenye ile hospitali ya mkoa pamoja na Hospitali ya Rufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho tiba asili zinatusaidia, tiba mbadala zinatusaidia, lakini sasa hivi hizo dawa ni ghali mno. Mtu akishindwa kupata dawa hospitali, akaenda kule anaambiwa shilingi 50,000, au shilingi 100,000. Kwa hiyo, naomba Wizara hapo ikae vizuri na hao watu wa tiba asili hizi ambazo mmezitambua, bei zao zishuke. Maana yake mtu anakubali kwenda kule ili aishi. Sasa bei yao ni kubwa sana kuliko hata bei ya dawa za hospitali ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Grace Tendega, atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma na Mheshimiwa Riziki Lulida ajiandae.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ambayo ni ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema naomba ninukuu dira na dhima ya Wizara ya Afya. Dira yao inasema hivi; ni kuwa jamii yenye afya bora na ustawi inayochangia kikamilifu katika maendeleo ya mtu mmojammoja, jamii na Taifa. Dhima ya Wizara ya Afya inasema hivi; kutoa huduma endelevu za afya zenye viwango vinavyokubalika kwa wananchi wote bila kikwazo cha fedha kwa kuzingatia uwiano wa kijiografia na usawa wa jinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nimesema nitangulize dira na dhima ya Wizara ya Afya? Ni kwa sababu ya mambo ambayo yanaendelea kutendeka katika utoaji wa huduma wa Wizara hii. Nakwenda kwa CHF iliyoboreshwa ambayo ndio inayopatikana katika mazingira tunayotoka na wananchi wetu ndio wanayoipata. Sasa CHF iliyoboreshwa iko hivi; wananchi wanatoa ile 30,000, wanaambiwa watakwenda kutibiwa kwenye zahanati, lakini kinachotokea, wakifika pale kwenye zahanati wanaandikiwa

tu na Daktari waambiwa dawa nenda katika dirisha lile pale uende ukafuate.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo imetokea kwenye mazingira yetu, mimi natoka Kalenga mazingira yako hivyo; Isimani hivyo hivyo na maeneo mengine iko hivyo hivyo. Kwa hiyo kunakuwa na uhaba wa dawa, hawapati dawa kwa *CHF* hiyo iliyoboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii inasababisha nini; unakuta kwamba mtu anakwenda pale labda ana 10,000 ambaye siyo mtu anayepata ile huduma ya *CHF*, anahudumiwa na Daktari pia pale, tena hao wanashughulikiwa harakaharaka na akienda pale ananunua dawa kama yule. Sasa watu wameona kwamba hivi huduma ya afya ni bure ama ni ya kulipia hata kama una *CHF* au *NHIF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kuna hata hii bima ya *NHIF* ambayo watumishi wapo katika kada hizo, Walimu na watumishi wengine walipo katika sekta hizo vijijini wanalamika kukosa dawa katika zahanati. Ukiposa unaambiwa uende mjini ukadai, kuna fomu ukajaze ukijaza hiyo fomu ndio utakwenda kuchukua dawa. Sasa *Imagine unatokea Pawaga* ama *unatoka Magulirwa*, umekwenda Kalenga ambayo unafika kwanza mijini halafu unakwenda Kalenga hizo *kilometers*. Sasa unakwenda kule kwenye zahanati unatibiwa unarudi tena mijini uandikiwe na hao Maafisa Afya ambao wako Gangilonga pale Iringa Mjini; natolea mfano wa Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inaleta gharama kubwa sana kwa wananchi. Matokeo yake wameona kwamba hii *CHF* ni kama siyo msaada kabisa, hata *NHIF*. Kwa hiyo niishauri Wizara kutokuwepo kwa dawa ni changamoto kubwa sana na hii inafanya wananchi wasiiamini Serikali au *NHIF* kwa sababu hakuna dawa, watu hawatajiandikisha wengi kwenda huko. Ukiangalia unakuta kwamba kuanzia mtoto wa mwaka mmoja, mtoto anayezaliwa mpaka miaka mitano kupata kile kitambulisho cha *NHIF* ni siku 90. Kwa hiyo unakuta

wanaona kwamba kuna changamoto; naomba wabadiilishe na waboreshe hicho kwa sababu ni changamoto kubwa ambayo wanaipata wananchi wanaona kwamba hakuna haja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunataka twende kwenye Bima ya Afya kwa Wote na Waziri amezungumza hapa, tunataka Bima ya Afya kwa Wote. Bahati nzuri sisi wakati huo Bunge liliopita, mimi nilikuwa katika Kamati ya Huduma, tulikwenda Rwanda, wengine walikwenda Ghana na wengine walikwenda mahali pengine, lakini tulikuta wenzetu wamefanikiwa kuwa na bima ya afya kwa wote, waliweka mkakati maalum kwa nchi yao kuhakikisha wananchi wanapata bima ya afya kwa wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona kuna fedha imetengwa pale kwa mchakato, lakini tuliambiwa kwamba ni Bunge lile utakamiliaka lakini tumekuja hapa naona Waziri tena ameweza mchakato. Watueleze lini wanakamilisha ili tuwe na Bima ya Afya kwa Wote na wananchi wetu waweze kupata huduma ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja katika kipengele cha watumishi wa afya; tuna changamoto kubwa ya watumishi wa afya; sekta ya afya vijijini na mijini nadhani, kuna changamoto kubwa. Unakuta kuna mganga mmoja ndio anayehudumia wananchi wote walioko pale. Uzuri Kamati imetoa takwimu kwamba ni asilimia 53 ya uhaba wa watumishi wa sekta ya afya. Mheshimiwa Waziri atueleze wanaajiri lini ili waweze kukimu hii asilimia 53 ya watumishi wa afya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote hayo, hawa watumishi wa afya wamekuwa wakipata adha nyingi; wamekuwa hawapandishwi mishahara, hawalipwi marupurupu yao na changamoto hizo ambazo zipo. Wanakosa morali ya kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna zile *call allowances* walikuwa wanapata, tunaomba wawape; kuna *postmortem*

*allowance*, wanafanya kazi kubwa mno hawa Madaktari wetu, kazi ni kubwa. Ukiwa mgonjwa ndiyo utajua kazi kubwa wanayoifanya hawa Madaktari; wawape hiyo *allowance* na motisha nyingine ambazo zinapaswa wapate hawa Madaktari, wanafanya kazi kwa weledi mkubwa na mazingira yao ni magumu, tunaomba wawape hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja katika kipengele cha wazee. Wazee wa nchi hii ni watu ambaao wamechangia sana katika maendeleo ya nchi yetu, lakini pamoja na kuchangia maendeleo ya nchi yetu Serikali bado haiwatambui katika huduma ya afya. Wazee wanakwenda kwenye madirisha yale, tulisema kutakuwa na madirisha ya wazee, naomba Wizara ituambie ina madirisha mangapi mpaka sasa katika Halmashauri mbalimbali zilizopo nchini ya kupata dawa za wazee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi, Serikali imechukua hatua gani kwa wale ambaao hawajatekeleza hilo agizo katika halmashauri zetu? Maana wazee wanakaa wanahangaika huko tunakotoka. Ni lini Serikali sasa itagharamia kuwapa bima ya afya wazee ili waweze kutibiwa. Tunajua wazee wanapofikia umri huo magonjwa na maradhi yanakuwa ni mengi mno; tunaomba Wizara ilivilie mkazo suala hilo la wazee.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti wanayopata hii Wizara ya Afya ni ndogo sana na haitoki kwa wakati. Unakuta kwamba wamepewa asilimia chache sana kwa maendeleo....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha, ahsante sana.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofii)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Saidi Lulida na Mheshimiwa Nora Mzeru ajiandae.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Tutakubaliana wote hapa kwamba afya ndiyo msingi wa maisha ya binadamu licha ya kwamba kumekuwa na ongezeko la magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza ambayo yanababisha vifo vya wapendwa wetu. Sekta ya afya ndiyo mahususi kutoa huduma kwa jamii, lakini imekuwa na changamoto kadha wa kadha zikiwemo upungufu wa watumishi na vifaa tiba pamoja na uhaba wa dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Pwani tuna uhaba wa watumishi takribani asilimia 52, watumishi wa sekta hii ya afya tullionao kwa sasa ni asilimia 48 tu ambayo kimsingi ni ndogo, hawatoshi kutoa huduma iliyokuwa bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wetu wa Pwani halmashauri inayoongoza kwa uhaba wa watumishi wa sekta ya afya ni Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji yenye upungufu wa watumishi wa sekta ya afya takribani asilimia 75, ikifuatwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti yenye upungufu wa watumishi wa afya kwa asilimia 71 pamoja na Halmashauri ya Mafia ambayo ina watumishi wa afya asilimia 78 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri aziangalie kwa macho matatu halmashauri hizi tatu, tuone namna bora ya kuwaongezea watumishi hawa wa sekta ya afya, hususan Halmashauri ya Wilaya ya Mafia ambayo kimsingi ni kisiwa, watumishi wakipelekwa kule huwa hawakai.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo naomba kuishauri Serikali tuangalie tuje na mpango kabambe wa kuhakikisha tunaandaa motisha. Tutoe motisha ya makusudi kwa hawa watumishi ambao wanafanya kazi katika mazingira magumu; maeneo ya visiwa, maeneo ya *Delta* na maeneo ya kule ndani ndani (*remote/interior*). Serikali ikitoa motisha kwa

watumishi wetu hawa tutawafanya wavutiwe kubaki katika hayo maeneo, lakini sambamba na hilo, kutoa huduma iliyokuwa bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, haikubaliki watumishi wa sekta ya afya Kinondoni na Ilala na wale watumishi wa sekta ya Afya kule Jibondo, Mafia ama wale wanaotoka kule *Delta*, Kibiti, wote kulipa sawasawa. Hiyo siyo sawasawa. Tena tunaambiwa kwa hawa watumishi waliokuwa Kinondoni na Ilala wenyewe wana motisha ya *overtime* kwa kuwa wanaona wagonjwa wengi, lakini tumewafikiria hao wanaotoka humo pembezoni. Usafiri mpaka kufika huku mjini kupata zile huduma za kijamii wanapanda kivuko, wanashuka, wanapanda bodaboda wanashuka, wanapanda magari wanashuka na bado wanatembea umbali mrefu. Mishahara yao yote inaishia kwenye nauli. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Serikali kama ambavyo busara na taratibu waliotumia kuwaongeza watumishi wa mijini kwa kuwa wanaona wagonjwa wengi, busara hiyo hiyo itumike kwa watumishi ambao wanatoka kwenye visiwa, *delta na remote areas*. Kwa hiyo naomba ushauri huo Serikali iuchukue na iufanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Bagamoyo, Halmashauri ya Chalinze; tunaishukuru sana Serikali mmetupatia gari la wagonjwa (*ambulance*), lakini *TANROADS* ikisimamiwa na Wizara ya Afya wanao mradi wa kujenga huduma za majengo ya dharura katika barabara kuu. Kituo cha Afya Chalinze ni mionganoni mwa vituo vilivyokuwa barabara kuu lakini pia ni mionganoni mwa vituo ambavyo vimepatiwa mradi huu. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri wakati anakuja ku-*wind up* atuambie mradi huu umeishia wapi? Unaonekana kusuasua, hatujui *status* yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu mradi ni muhimu sana kwa sababu hii leo ukipata ajali katika maeneo ya Chalinze pale Kibaha ina maana kupata huduma za dharura wewe mpaka ukimbizwe Mloganzila ama Muhimbili. Kama

tungekuwa na huduma za dharura ama hapa Chalinze ama pale kwenye Hospitali ya Mkoa Tumbi, ina maana tungeweza kuokoa maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tuna changamoto ya foleni sisi, maana foleni ile tulioi-*clear* pale Ubungo ile barabara nane yote inatapikia Kibaha. Kwa maana hiyo tunaomba sana Serikali waje na majibu, watujibu, maana Wanapwani na Watanzania kwa ujumla ambao wanaitumia ile barabara kuu tunataka kujua mradi wa ujenzi wa majengo ya huduma ya dharura umekwamia wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, alifanya ziara yake katika Hospitali ya Mkoa pale Tumbi; majengo yalishaanza kujengwa, yamechakaa na kuchakaa. Kwa hiyo nitaomba atuambie kwamba ule mradi gharama zake ni kiasi gani na wana mpango gani na mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu huu mradi utatusaidia Wabunge tunaoishi Mkoa wa Pwani, Wabunge wa Dar es Salaam, Wabunge wa Lindi, Wabunge wa Mtwara, Wabunge wa Ruvuma pamoja na Wabunge kutoka Zanzibar. Sisi ndio wasafiri wakuu kuja Dodoma kwenye vikao na kurudi majimboni. Mungu aepushie mbali, lakini *once tukipata ajali kusema tukimbizwe mpaka Mloganzila ama Muhimbili, ama hakika mradi huu utakwenda kuokoa maisha ya Watanzania.*

Mheshimiwa Naibu Spika, imezungumzwa na Dkt. Thea hapa kuhusiana na masuala ya ukeketaji, lakini pia naomba niseme jambo moja; wanaume wa nchi hii wanapenda sana kujadili mpira na wanapenda sana kujadili siasa kuliko ambavyo wangeweza kujadili masuala ya kuhamasishwa kwenda kupima Virusi Vya UKIMWI. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani ukiwakuta kwenye mijadala ya mpira, mijadala ya ukewenza pamoja na mijadala ya masuala mazima haya ya siasa; wanagetumia *effort* hiyo kuhamasishana kwenda kupima Virusi Vya UKIMWI leo hii tungesaidia akinamama. Maana wanaume hawa kwenda kupima UKIMWI wanasubiri mwanamke ashike

ujauzito akapime ndiyo wao wapate majibu yao na wakati kila mtu ana *immunity* yake, kila mtu ana kinga zake. Kwa hiyo nataka niwaombe sana kaka zangu, baba zangu na marafiki zangu, ile nguvu wanayotumia kujadili Simba na Yanga, ile nguvu wanayotumia kujadili siasa na ile nguvu wanayotumia kujadili ukewenza ihamisheni ipelekeni kwenye masuala ya kupima UKIMWI na Virusi Vya UKIMWI. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Thea kule amezungumza kuhusiana...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mchafu, kuna taarifa, sijajua ni Mbunge gani allomba kutoa taarifa.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Sawa, Mheshimiwa Twaha Mpembenwe.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa tu mzungumzaji kwamba asilimia 99 ya wanaume ambao ni Wabunge katika Bunge hili la Kumi na Mbili, taarifa zilizopo ni kwamba wamepima UKIMWI. Ahsante. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Twaha, naona hata wenyewe wanakushangaa maana hawajapima na kama wamepima hawajachukua majibu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Hawa Mchafu.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru; siipokei taarifa ya Mheshimiwa Twaha kwa sababu kama anasema kweli, hicho anachokisema wakihamishe sasa kwenye majimbo yao wakawatangazie na wananchi

wao ili waweze kufanya hivyo hivyo, kwamba tukipata asilimia 90 ya wananchi wanaume kwenye jimbo lake wamepima, sina shaka Tanzania tutakuwa tuko vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado niko hapohapo kwa wanaume wa nchi hii, kwamba tumeambiwa madhara ya ukeketaji, lakini wanaume hawa ndio watu wa kutusaidia sisi. Wakitoka huko nje wakasema aliyekeketwa na ambaye hakukeketwa nani yuko vizuri, lakini wanaume hawa wakisema kwamba hawa waliokeketa hawatawaoa, sina shaka itakuwa ni njia, itakuwa ni mwarobaini wa kusaidia kupunguza ukeketaji. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, natoka sasa hapo kwa wanaume, mchango wangu mwингine ni kuhusu suala zima alilozungumza Mheshimiwa Askofu Gwajima kuhusiana na chanjo ya *Corona* na madhara yake. Nikiwa kama Mjumbi wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI tulipata fursa ya kutembelewa na watu wenye hii dawa inaitwa...

(*Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Dakika moja, hebu elezea dawa gani. (*Makofi*)

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nilikuwa nataka kuizungumzia hii dawa *Phyt Exponent*. Imeonekana kusaidia watu wengi sana kwenye masuala ya Corona. Kwa bahati nzuri Mkemia Mkuu ameicheki na amethhibitisha kwamba inafaa kuwa ni *medicine*, lakini inatambulika kama *supplementary* na inauzwa ghali, shilingi 150,000. Ili kuwasaidia Watanzania waweze kuipata hii dawa, iklanza kufahamika kama ni *medicine*, madaktari wakiweza kui-prescribe ina maana itauzwa madukani kwa bei rahisi, tutaweza kusaidia watu wetu na janga zima la *Corona*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nikushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nadhani tunarudi pale kwenye umuhimu wa hizi dawa zetu za asili pamoja na kutambua dawa zote zinazoweza kutusaidia katika hali janga.

Hapana, sitawazungumzia wanaume, naona kuna mtu ananiambia huku nizungumzie wanaume. (*Kicheko*)

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Riziki Lulida, atafuatiwa na Mheshimiwa Norah Mzeru na Mheshimiwa Tecla Ungele ajiande.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nikushukuru. Nimshukuru pia Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kunijalia kupata afya njema nami kuwepo hapa na kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile leo ni mara yangu ya kwanza, nitoe pole kwa familia ya Hayati Dkt. John Joseph Magufuli na Watanzania wote, kwa kweli nimeguswa na msiba wake na mimi ni mmojawapo wa wateule kwa nafasi ambayo nimekuwepo hapa Bungeni. Nitaendelea na kuwaomba Watanzania tuendelee kumwombea dua kwa vile alifanya mengi mazuri ambayo sasa hivi tunayaona, ili Mwenyezi Mungu amlaze na ailaze roho yake pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni Ujeruman na America wametoa pongezi kubwa kwa aliyepeleka *research* yake kule kuhusu suala la *Corona*, kwa kweli ile *research* yake dunia wameipongeza sana. Wanakuja kumpongeza sasa hivi Hayati ameshaondoka. Wakati ule anapambana walikuwa kama wanambeza kwa vile suala la *Corona* na mambo mengine ni biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nitaongelea suala la *malaria*. Mimi ni Mwenyekiti wa

Kupambana na Malaria ndani ya Bunge. Kwa sasa hivi katika taarifa tulizokuwa nazo, kwa siku Watanzania 104 wanakufa kutokana na *malaria*. Ni gongwa zito na kubwa na tishio kuliko hata *Corona Virus*. Kwa maana nyine kwa mwezi Watanzania zaidi ya 3,000 wanakufa kwa ajili ya *malaria*. Sasa jiulize kwa nini sana wao wanatulazimisha tutumie hizi chanjo ya *Corona* wakati tunahangaika na kupambana na kutokomeza ugonjwa wa malaria. Zero malaria naanza na mimi, lakini kila Mtanzania nataka tuhakikishe tunapambana na tunatokomeza malaria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, malaria kuna mikoa sita ambayo ina maambukizo makubwa ya malaria; kwanza, Kigoma, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Geita na Kagera. Na tumeambiwa tena Mkoa wa Geita utakuwa wa kwanza katika Tanzania kwakuwa na maambukizo makubwa ya malaria kwa ajili ya machimbo yallyokuwepo kule Geita. Inamaana wachimbaji wanachimba, lakini hawaangalii athari zake kwa vile mikataba ya *EIA (Environemt Impact Assessment)* haikufanyika, hivyo watabakia jamaa zangu wasukuma kuwa ni wagonjwa ambukizi wakubwa wa malaria na watapata vifo vingi kwa kupitia katika machimbo hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jiulize kama sisi tunakufa Tanzania ni nchi ya kumi katika nchi kumi na moja duniani ambayo inamalaria, maambukizi ya malaria makubwa sana mojawapo ni Tanzania, katika zile nchi kumi. Lakini sisi leo tunalazimishwa kufanya *vaccination* ya Corona, lakini hawajataka kutupa ufumbuzi, je, tutatokomezaje janga kubwa ambalo ni tishio kuliko hata Corona. Hapa lazima utajua kabisa hapa kuna biashara, zinaenda na hizi biashara tuziangularie kwa makini sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeambiwa wanatangaza Tanzania tunapeleka dola milioni 45 kwa ajili ya kutokomeza malaria. Pesa zote zinazokuja za UKIMWI tunaziona katika Halmashauri na nyie Wabunge ni mashahidi hasa katika *Local Government*. Je, hizi hela za malaria zinakwenda wapi? Hizi hela zinakwenda kwa hao kutuletea

dawa na vyandarua lakini hawana nia kabisa ya kutokomeza malaria kwa vile biashara zao ziendelee kufanyika ili na sisi tuwe wahanga wa vifo nya malaria. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefungua kiwanda kikubwa Kibaha cha viuadudu wa malaria, lakini kwa vile wao wanafanyabiashara kile kiwanda kimeambiwa kuwa hakijakubaliwa na *World Health Organization* hivyo tumekaa na kiwanda ambacho ni kizuri nchi za wenzetu wanachukua dawa sisi tumeshindwa kutokomeza malaria wakati kiwanda kipo Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu, Mheshimiwa Waziri wewe ni pacha wangu, hakikisha hal mashauri zote zinanunua dawa kwa kupitia, za kuua wadudu maambukizi kwa kupitia kiwanda cha Kibaha. Itakuwa ni dharau kubwa wanahela za ndani za kununua dawa hawanunui na hata wakinunua hawafanyi kazi hii ya kupulizia na kuhamasisha ili angalau tutokomeze hili janga la malaria. (*Makof*)

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lulida kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Josephat Gwajima.

## TAARIFA

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumtaarifu tu Mheshimiwa Mbunge anaongea mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira. Tumetembelea hicho kiwanda cha hapo Kibaha ambacho kina utaalim wa ajabu, mzuri ambaa haupo mahala popote Afrika Mashariki. Wacuba wametengeneza hicho kiwanda kwamba, wanatengeneza *bacteria* wanapowala hawa mbu, mbu wanakufa wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini cha kusikitisha tulifika kwenye kiwanda hicho wafanyakazi wa hapo hawajalipwa miezi ya kutosha, wafanyakazi wanazunguka zunguka,

kiwanda ambacho kingeondoa malaria kuna watu wanapambana nacho kwasababu malaria ikiondoka maana yake dawa za kupulizia zimeharibika, *prescription* za malaria hazipo. Kwa hiyo, namjulisha mjambe kwamba anapambana na wafanyabiashara wanaopata fedha kupitia mradi wa malaria. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Riziki Lulida unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli naipokea taarifa yake kwa vile yeye naye ni mzalendo kama mimi. Wazalendo kama *Mr. Gwajima* ni lazima tuwapongeze na nikubali maana yake kuna Wabunge wangetaka kutumika wakataka kukidharau lakini nimeona Mheshimiwa Gwajima ni *champion* na Mama Gwajima naye vilevile ni *Champion* kuhakikisha kuwa Tanzania bila malaria inawezekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bima ya Afya, kama walivyozungumza Wabunge wenzangu ninamasikitiko makubwa sana na Bima ya Afya. Bima ya Afya haimlengi mtu na ni hii wazee zaidi ya miaka sitini, wazee wa miaka sitini ili atibiwe mahali popote inabidi atoe 936, tukiwemo humu Wabunge, Mbunge haruhusiwi kumtibu mzazi wake inabidi atumie mwenyewe kumtibu mzazi wake, sheria hii inatoka wapi? Na kama ipo naomba iletwe Bungeni tuibadilishe hii kanuni wazazi wetu nao wafaidike na matibabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta mzee anaumwa mimi nitoe laki tisa nimtibu mzee wangu wakati bima yangu mimi ni bima ambayo ni ya *VIP*. Lakini vilevile la pili, nataka Mama Gwajima unisikilize mara mbili mbili na hoja hii naileta. Hospitali ya Aghakan...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lulida ngoja kwanza.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, haya.

**NAIBU SPIKA:** kwa sababu kina Gwajima wapo wengi sasa ukimwita Mama Gwajima hapa hatuelewi unamwita mama wa Askofu ama Mheshimiwa Waziri hapa. Kwa hiyo ye ye mwite Mheshimiwa ili tutofautishe na kina Mama Gwajima.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, haya, Mheshimiwa Waziri, Waziri wa Afya, nataka nimwambie, Bima ya Afya katika hospitali kubwa ya Aghakan na *Regency Hospital* haiwataki wajawazito. Lakini ukichukulia malaria waathirika wa kwanza ni wajawazito na wanapeleka bima kule wanasema sisi hatupokei bima za afya za wajawazito. Je, ni maana moja wanawadharau wanawake na kama wanadharau wanawake, wanawake hatukubaliani nalo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wanawake ndiyo tunazaa Watoto, lakini leo unaambiwa pale hutakiwi kupewa nafasi ya kwenda kutibiwa kwa vile nini, utakuwa na gherama ya kwenda kupimwa pimwa mpaka kujifungua. Je, hii huoni kama inawakandamiza wanawake? na kulikuwa na haja gani ya kuwapa ruzuku mataasisi haya, wanaleta madawa na kila kitu wanapewa faida ya ruzuku lakini wanawakataa wanawake, tumeungana na wanawake Wenzangu wabunge wanataka uje utupe jibu kuhusu suala la Aghakan na *Regency*na vilevile waje watufanyie semina ya kututaarifu je, hizo hoja ni kweli na kama si kweli waje watuambie katika semina maalum hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Bima ya Afya ambayo tunakuwa nayo sasa hivi, ukienda Aghakan kama Mbunge tunalipa bima kubwa sana lakini tunakwenda kulazwa na watu wa kawaida wanaotoa shilingi 70 na kila kitu. Wanasema sisi hatuwezi kuwapa bima ya *VIP*lakini hii yote ni kutunyanyapaa na kutuweka katika mazingira magumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba ukae na hizi taasisi ambazo zinachukua hela za walipa kodi watanzania na iwatendee haki watanzania kwa kuwapa haki sawa kwa

wote. Wasijione wao wamekaa kule wanatoa gharama kubwa na kuwaacha wagonjwa wengine ambaao wanahitaji bima za afya zao wanazitenga kutokana na wanavyotaka wao. Kama si hivyo, pelekeni Bima ya Afya Muhimbili, boresheni Muhimbili, tutakimbilia katika mahospitali yetu ambayo ni ya walala hoi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia changamoto za walemovu, walemovu ndiyo kundi maalum ambalo linahitaji msaada mkubwa sana katika tiba. Na katika tiba hizi hawa walemovu mpaka sasa hivi wanahangaika hawana Bima za Afya. Na kama hawana Bima za Afya hawa walemovu wengi wananyanyasika tu hawana mahali pa kukaa, hawana mahali pa kuishi. Lakini je, Bima ya Afya inasema nini kuwasaidia hawa kundi maalum ambaao ni walemovu. Hatuna ma-desk ambayo yanasaidia walemovu hata katika mahospitali, leo anakwenda mlemauvu ambaye ni kiziwi anataka kujifungua au ana matatizo lakini akienda pale hapati nafasi ya kusikilizwa, wanamchukulia kama mtu ambaye hana thamani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba hakikisha kuwa katika kila eneo la kituo cha afya, polisi ni lazima tuwe na desk maalum kwa ajili ya kusaidia kundi maalum la walemovu. Walemovu wanahitaji msaada wa kupata tiba kama watu wengine, walemovu wanahitaji kusaidiwa kama wengine, leo zinagawiwa chandarua Tanzania nzima lakini haimgusi mlemauvu, kwa mara moja...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, sasa tuliweke vizuri hili jambo la *Regencyna Aghakan* kwa sababu zimetajwa taasisi humu ndani na wakati ukimalizia hoja yako kuhusu hospitali hizi mbili ukasema Mheshimiwa Waziri atueleze kama ni kweli hiso taarifa ulizonazo au si kweli.

Sasa Mheshimiwa Mbunge kwasababu kanuni zetu zinataka yaani kama hivi ukizisema hizi taasisi na huna uhakika kama ni kweli au hapana, tutakuwa hatujawatendea haki humu ndani kwa mujibu wa hizi kanuni zetu. Na wao wanaweza wakaleta malalamiko dhidi ya bunge kwa maana ya kwamba wamesemwa vibaya humu ndani.

Sasa ujipime wewe mwenyewe kama ulichosema ni uhalisia ili tusianze kumpa waziri kuja kusema ni kweli hapana ili taarifa rasmi za bunge zikae vizuri tusije tukaingia kwenye mgogoro wa kujadili taasisi wakati hatuna uhakika na hizo taarifa. Mheshimiwa Lulida dakika moja.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mbunge wa vipindi vitatu na zaidi ya hapo. Ninalolizungumza nimepewa taarifa za uhakika kuwa kinachofanyika ni hiki, hivyo sikuja hapa kama nimekuja kubuni na kuja kuropoka hapana. Nimeambiwa wanakataa kabisa bima za wajawazito. Lakini kama nitakapokuwa tayari twende tukakae chemba maana bado ninahaki ya kukaa chemba, nimuite huyo anayehusika tena anatoka katika NHIF azungumze mbele yenu kama Ushahidi kwa hili ninalozungumza.

**NAIBU SPIKA:** Nilichotaka uliweke vizuri ukishakuwa wewe na uhakika maana yake utakuwa na ushahidi wale watu watakapoleta malalamiko. Hicho tu, si hoja ya wewe kuropoka hayo maneno ni wewe unasema mimi sijasema kuhusu uropokaji, mimi nimeeleza kama wewe unaouhakika na hizo taarifa basi ni sawa kama huna uhakika ndo maana nilikupa nafasi, kwa kuwa unahakika basi tulache likae hivyo, halafu tutaenda nalo.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninauhakika nacho ninachokizungumza hivyo tunataka kifanyiwe kazi paletwe marekebisho. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Haya, niwakumbushe tu, Waheshimiwa Wabunge hizi kanuni zetu tuwe tunazipitia, tuwe tunazipitia, ili tusije tukajikuta mazingira ya kutatanisha. Lakini Mheshimiwa

Lulida amesema ye ye anaouhakika na hizo taarifa zilivyotolewa kwa hivyo ni muhimu upande wa Serikali ikajaribu kuangalia kwasababu hii ni Bima ya Afya ambayo ni ya Serikali kimsingi.

Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Norah Mzeru atafuatiwa na Mheshimiwa Tecla Ungele, Mheshimiwa Jacqueline Kainja ajiandae.

**MHE. NORAH W. MZERU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo pili nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii muhimu na adhimu kwangu kwa kuweza kusimama kwa mara ya kwanza katika Bunge lako hili tukufu na kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Watoto na Wazee.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake kwa kazi nzuri wanayoifanya. Tatu, nichukue fursa hii kuishukuru Serikali kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kutatua kero na changamoto za wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wote ni mashahidi kutohana na kazi nzuri aliyoifanya Hayati Dkt. John Pombe Magufuli katika kipindi cha mwaka 2015/2020. Wakati akilihutubia Bunge Novemba, 2020 alielezea mafanikio kadhaa wa kadha ambayo yote ukiyatilia maanani yamewagusa kwa asilimia mia moja Wanawake, Vijana na Watoto, Kiuchumi, Kijamii, Kisiasa, wote tulikuwa mashahidi tulisisimkwa kwa furaha kuona namna gani Taifa letu limepiga hatua kubwa za kimaendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwelekeo huu wa Bajeti ya Serikali tunajadili kwa mwaka 2021/2022 unaelekea katika maandalizi ya bajeti ya sita tangu Rais Mama Samia Suluhu aingie madarakani. Ambapo ukifuatilia kwa umakini utaona namna gani bajeti zote zilivyojikita katika kugusa maendeleo ya wananchi lakini zaidi kwa namna moja ama nytingine kugusa zaidi wanawake na Watoto nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siku zote wanafalsafa utuambia Uongozi Bora ni kupigania maslahi ya wengi lakini ili uwe Kiongozi Bora lazima ujielekeze kwenye utayari. Kujianaa katika upeo na uwezo wa kiuongozi kadri unavyotafakari, katika kuwafanyia mambo mema unaowaongoza, aina hiyo ya uongozi siku zote hutoa majawabu ya utatuzi wa shida na kero za wananchi bila kujali maneno, maneno ya upotoshaji wa wachache. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri Serikali katika bajeti ijayo ya mwaka 2022,2023 kuendelea kuwekeza katika kusomesha, kuajiri na kupeleka waganga, wauguzi na wakunga katika maeneo ya vijijini ili kuokoa Maisha ya akinamama Wajawazito sambamba na kutoa huduma bora za afya na tiba. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufikia malengo ya *millennium* kuna ulazima wa kuhakikisha Maisha ya akinamama wajawazito yanawekewa utaratibu bora wa kiuhuduma kwa kupewa ushauri na maendeleo yao nyakati za ujazito. Wakipata huduma bora katika vituo vyta huwezi ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wanawake wote wa Mkoa wa Morogoro nimpongeze sana Rais wetu, Mama yetu kipenzi, Mama Samia Suluhu Hassan kwani jinsi alivyojipanga na Serikali yake ya Awamu ya Sita kwa ajili ya kuendelea kushamirisha maendeleo nchini ambayo yametugusa moja kwa moja Wanawake, Vijana na Watoto. Katika Taifa lolote ulimwengu huu tulionao huwezi kuzungumzia maendeleo hayo bila kuwagusa wanawake. Nashauri bajeti hii tuendelee kukumbukwa kinamama hasa katika masuala ya elimu, afya uwezeshaji wa kiuchumi ili tuweze kujajiri na fursa za kiuongozi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu uongozi wa Rais Mama Samia Suluhu umetuhemisha sana wanawake na tunaamini kuwa ataendelea kutuheshimisha zaidi kutokana na dhamira yake njema kwetu. Kipaumbele ni kuweka mazingira bora kuanzia Halmashauri ya Wilaya hadi Serikali

Kuu ili kusomesha, kuajiri na kupeleka Wakunga, Waganga na Wauguzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati ya maendeleo, uimarishaji huduma za msingi za kijamii lakini lazima sasa iibuliwe katika ngazi za halmashauri za Wilaya kabla ya Serikali Kuu haijaweka mkono wake. Viongozi tushirikiane kutenga muda wa kushughulikia na kuondosha kero mapema katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali Kuu haiwezi kufanya kitu katika Vitongoji, Vijiji, Kata na Wilaya kwenye wilaya kazi hiyo lazima ifanywe na halmashauri zetu, wakiwemo watalaam na usimamizi ili liende sambamba na usimamizi mzuri wa matumizi bora ya fedha. Tukifanya hivyo maendeleo na mafanikio kila Kijiji tutayaona na Taifa litaendelea kupiga hatua kubwa za maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali kwa Wizara ya Afya, Wazee, Jinsia na Watoto tumekuwa tukishuhudia jitihada za Serikali katika kuboresha makazi ya wahudumu wa kada mbalimbali, lakini katika kada hii ya afya tuna wataalam wengi sana Waganga, kama vile Waganga wa Kinga, Wakunga na Wauguzi ambapo katika mazingira wanayoishi wengine wapo vijiji ambapo ndipo kwenye changamoto nyingi. Serikali inamkakati gani wa kujenga nyumba bora za kisasa? Ghorofa?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. NORAH W. MZERU:** Ambazo Waganga Wakunga na Wauguzi wataishi na kuridhika hasa maeneo ya vijiji ambapo miji inapanuka. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Norah Mzeru kuna taarifa.

**MHE. NORAH W. MZERU:** Mheshimiwa Naibu Spika, *ok.*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nora Mzeru kaa kidogo, kaa kidogo Mheshimiwa.

## TAARIFA

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa mchangiaji kwa mujibu wa kanuni haitakiwi anapochangia asome anachangia vizuri lakini anasoma. Ahsante. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, ngoja ngoja Waheshimiwa Wabunge msiwe na haraka. Kwanza taarifa si jambo la kuvunjwa kwa kanuni kwa hiyo kama kanuni imevunjwa unasi mama kwa kanuni zinazohusu utaratibu, kwamba kuna kanuni imevunjwa humu ndani. Mheshimiwa Nora Mzeru hasomi anachangia lakini anaangalia sehemu ambayo ameweka ule mchango wake. Mheshimiwa Norah Mzeru. (*Makofi*)

**MHE. NORAH W. MZERU:** Mheshimiwa Nailbu Spika, ahsante sana. Mwisho napenda kumpongeza Rais Mama Samia Suluhu Hassan pamoja na uongozi wake wa juu ikiwemo Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na timu nzima ya utawala kwa jinsi wanavyofanya kazi kubwa ya maendeleo kwa kushirikiana Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tecla Ungele atafuatiwa na Mheshimiwa Jackline Kainja, Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava ajiandae.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia hoja kwenye Wizara hii muhimu sana Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupongeza kazi kubwa inayofanya na Wizara hii. Mheshimiwa Waziri Dkt. Dorothy Gwajima na timu yake yote, Katibu Mkuu na timu yote mpaka kule kwenye vituo vy'a afya na zahanati wanafanya kazi kubwa sana kuokoa maisha ya watoto, akina

mama na wananchi wote kwa ujumla. Pia naipongeza Serikali nzima kwa ujumla kwa kazi kubwa inayofanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia muda, naomba nijikite kwenye mambo makuu mawili. La kwanza, upungufu wa watoa huduma katika sekta ya afya lakini la pili, uhaba wa vitendea ikiwepo *ambulance* na vifaa vingine katika hospitali zetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kwa ufupi hii suala la *ambulance*. Tunaona maeneo mengi yako mbali na hospitali za wilaya na huko kwenye maeneo hayo ya vijijini na kwenye kata kunatoa huduma mbalimbali lakini hakuna huduma ya *ambulance*. Nkitolea mfano kuna sehemu ambayo kuna zaidi ya kilomita 70 lakini inapotokea tatizo hakuna *ambulance*, mfano Nachingwea tuna *ambulance* moja ambayo ni mpya kwenye Kituo cha Afya Kilimarondo lakini zile *ambulance* zilizoko katika Hospitali ya Wilaya ni chakavu, hapa na hapa zinapata *breakdown* kiasi kwamba hata mgonjwa mwenyewe anaweza akafia njiani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye upungufu wa watumishi kwenye sekta ya afya, tumeona hapa Kitaifa kuna upungufu zaidi ya asilimia 53, hicho ni kiasi kikubwa sana. Nikienda kwenye Mkoa wa Lindi nkitolea mfano Wilaya kadhaa, Wilaya ya Ruangwa tulipaswa tuwe na watoa huduma 840 lakini waliopo ni 257 sawasawa na asilimia 31, upungufu ni asilimia 69. Nachingwea mahitaji ni 1,077 waliopo sasa hivi ni 305 tu upungufu ni 772. Wilaya ya Liwale wafanyakazi wa sekta ya afya ni 510 lakini waliopo ni 221 tu, upungufu ni 289. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama nilivyokuwa nimesema siku moja nilivyochangia mchango wangu hapa kwamba zahanati nyingi zinahudumiwa na *medical attendants*. Nasema hivi pamoja na upungufu huo, kwa mfano Wilaya ya Liwale mpaka kufika Hospitali ya Wilaya zahanati na vituo vya afya vingine viko mbali sana na ndipo pale tunapokuja kutoa mchango kwa kusema kwamba kuna

tembo huko na kadhalika. Kwa hiyo, anapokuwepo mto huduma mmoja kwenye *health facility* fulani anapokuja kupata mshahara na kupeleka taarifa mbalimbali kwenye Hospitali ya Wilaya, humo njiani anakabiliana na mambo mbalimbali ikiwepo na wanyama wakali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya afya kunapokuwa na upungufu wa rasilimali watu matokeo yake ni kutokutoa huduma nzuri au huduma hafifu matokeo yake yanatokea pale pale, haisubiri baadaye. Labda ni mtu kutokuhudumiwa jambo fulani ni pale pale. Naamini kabisa kuna sekta zingine kama leo kukitokea kupata huduma hafifu matokeo au madhara yake yanatokea baadaye lakini kwenye sekta ya afya kama hakuna huduma nzuri matokeo yake yanatokea pale pale. Kama ni vifo vitatoka pale, kama ni mtu ana changamoto gani ni pale pale haisubiri baadaye. Kwa hiyo, jambo hili la kuwa na rasilimali watu wa kutosha kwenye *health facilities* ni muhimu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Nimeona baada ya kutoa changamoto hiyo niseme nini kifanyike? Ya kwanza nimeona, Waziri wa TAMISEMI ametangaza hapa ajira kama zaidi ya elfu mbili kwenye sekta ya afya. Naona jambo hili likitekelezwa kwangu ni faraja kubwa kweli na naamini kabisa Waziri wa TAMISEMI akiungana na Waziri wa Afya watasaidia kuangalia Mikoa ya Lindi na Mtwara na kwingineko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suluhisho lingine ni mikataba ya ajira. Miaka iliyopita Wizara ya Afya iliungana na sekta binafsi kama vile bima na *HITECH* kupata ajira ya mkataba kwa ajili ya maeneo ya pembezoni, ile ilisaidia sana sijui ile program inaendelea au namna gani? Naomba Wizara ya Afya wajipange kutafuta kama ni wadau wengine kunusuru tatizo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine naomba Wizara husika itoe vibali kwa halmashauri zetu ziajiri kwa mkataba lakini pia kutumia *own source* kwa ajili ya kuwa-*retain* wale wafanyakazi. Mara nyingi vijana wanaajiriwa kwenye maeneo yetu lakini kutokana na mazingira fulani baada ya

miaka miwili au mitatu wanaomba kuhama. Kwa hiyo, naomba jambo hili la *retention* liangaliwe sana. (*Makofii*)

Sisi tulifanya *research* kuangalia ni jinsi gani itasaidia kuwa na *retention mechanism* Mikoa ya Lindi na Mtwara kwa kutumia vyuo vyetu vya afya na halmashauri husika na hili jambo liliwezekana. Naomba jambo hilo liwezekane Wizara husika ya Utumishi itoe vibali vya kutumia *own source* kwa ajili ya *retention mechanism*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jacqueline Kainja atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, Mheshimiwa Joseph Mkundi ajiandae.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii niweze kuchangia Wizara hii ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kwa moja mchango wangu niuelekeze kwenye *Universal Health Coverage* kwa maana ya Bima ya Afya kwa Wananchi Wote, ambayo tuliinadi katika llani yetu ya Chama cha Mapinduzi kwamba Watanzania wote wapatiwe bima ya afya. Hata hivyo, tukiambatanisha na Sera yetu ya *PPP - Public Private Partnership* ili kuweza kuondoa changamoto na matatizo ambayo yanalikumba Taifa letu la upungufu wa dawa na vifaa tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaifafanua hiyo bima ya afya pamoja na Sera yetu ya *PPP*, naomba niishauri Wizara kuangalia *explorer option*ya kutokutunza dawa za wagonjwa wa nje au hospitalini tunasema *outpatient*, ili kuondoa mkanganyiko ambao unatokea kwamba Wizara inatoa taarifa kwamba kuna wizi wa dawa na upotevu wa vifaa tiba. Tukiimarisha bima yetu ya afya kwa wananchi wetu wote, bima ambayo ina tija ambapo mwananchi akienda *private sector* atapata huduma zote na akiingia hospitalini

za Serikali atapata huduma zote. Kwa kufanya hivi inaweza ikatuondolea mkanganyiko huo wa kuona kwamba watoa huduma za afya *pharmacist, doctors* wanaiba dawa au vifaa tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tungalie sisi kama Wizara au Serikali kazi yetu ni kutoa huduma au tunahitaji tufanye *business?* Hii ni katika eneo hili la upotevu wa dawa na upungufu wa dawa na vifaa tiba. Naongea hivyo kwa maana tunaona kwamba *private sector* zinafanya vizuri ukilinganisha na vituo vyta afya na zahanati za Serikali. *Private sector* anachojali ni kuangalia ana-provide service nzuri kwa mgonjwa au kwa mteja wake, hakuna suala la dokezo, hakuna kwamba dawa imeisha lazima niandike dokezo kwa Mganga Mkuu Mfawidhi au kikao cha *management* kiweze kupitia zile taratibu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukaenda *private sector* kununua dawa hata kama hana, anakuambia subiri naenda *store* lakini kiuhalisia sio kwamba anaenda *store* anaenda kuangalia duka la jirani ili aweze kum-*maintain* huyu mgonjwa. Kwa hiyo, tuiangalie ni namna gani hii bima ya afya ikifanya kazi vizuri na tukajitahidi kuwa tuna-*store* dawa kwa ajili ya *inpatient* kwa maana ya wagonjwa ambao wamelazwa hospitali lakini wale wagonjwa ambao ni *outpatient* wapate bima yenye tija ili waweze kwenda nje kwenye *private sector* waweze kuhudumiwa, bima ambayo itakuwa na tija kwa maslahi ya mwananchi na sio kwa maslahi ya labda *system*, Serikali au Wizara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta kama Serikali au Wizara tunakuwa na mzigo mkubwa ku-*store* dawa ambazo wakati mwininge ni *brand*. Unakuta kuna dawa ambazo ni *brand* ziko pale hospitali na tukiangalia kiuhalisia yale mafungu yetu matatu ambayo ni ya *exemption* kwa maana ya wazee, watoto na mama wajawazito zile *brand* ambazo tumezi-*store* pale hospitali kwa maana tumefungua duka la dawa la hospitali siyo yale makundi yanapata zile dawa na bado hatuweki kwa wingi unaotakiwa kumfanya yule mgonjwa akifika pale apate dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile *clinicians* anapata shida anapokuwa ana-*prescribe medicine*, labda anataka ampeleke mgonjwa kwenye *third generation* ya *antibiotic*, kwa sababu dawa zilizoko *pharmacy* *first generation* inabidi ampatie hiyo iliyopo. Tunajua kiuhalisia sisi Watanzania wote huku majumbani ni madaktari, *before* hujaenda hospitali umeshajitibu sana huku nyumbani. Kwa maana umeshaji-*diagnosis* wewe mwenyewe umeshakuwa mfamasia, ukisikia tumbo linauma unakunywa dawa *metronidazole* tunatengeneza *resistance* kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapokwenda kwa daktari tumeweka *essential drugs* ambazo ziko hospitali pale kwamba sisi kama hospitali au kama Wizara tumeweka *item* zetu ni 30 hizi hapa tukipungua chini ya hapo tutasema kwamba dawa hakuna lakini kama Wizara inapoenda kufanya *supervision* inakuta zile *essential drugs* ziko pale tunaambiwa kwamba dawa zinapatikana lakini kiuhalisia tungeweka *bar yetu items* za *essential drugs* zifike *bar hata* kwenye mia tukifika sabini ndio tuseme basi dawa zipo lakini sio tumeweka 30 *and then* tunasema kwamba dawa hapa zinapatikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo kwenye suala la bima ya afya na kuchanganya na hizi *PPP*, naomba niende kwenye suala la bima ya afya ya *CHF* iliyoboreshw. Hii *CHF* iliyoboreshw bado haijawa na msaada kwa wananchi wetu, ina msaada wa kuonana na *clinician's* au vipimo. Pia na yenye we ina vipimo ambavyo haiwezi ku-*clear* na inampa shida mtoa huduma. Mfano kama kuna sehemu amekosea ku-*request* wanakatwa makato makubwa zaidi kiasi kwamba unakuta kituo kinarudi nyuma kwenye mapato. Mfano, ame-*claim* labda Sh.900,000/= lakini anakuja kupewa Sh.90,000/= jambo ambalo linamrudisha nyuma kuendesha shughuli za kituo. Wakati huo hapo kuna *exemption* za makundi matatu ambayo yanatakiwa yapate *free medicine* na kituo kinatakiwa kijienteshe na pesa zote zimelala huku *CHF*. Nimuombe Waziri aangalie hii *CHF* basi hata iwe *supported* na *NHIF* ili hawa *NHIF* ambao wamesha-*master* vizuri

kuangalia *claim form* zao zinakaaje na kama mto huduma amekosea wanajua namna gani ya kumwambia kwamba amekosea sehemu hii na hii tofauti na CHF.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye suala zima la bajeti. Suala siyo tatizo la bajeti, tatizo pesa hizi hazifiki kwenye vituo kama inavyotakiwa. Kwa hiyo, unakuta kama ni bajeti ya familia kwa mfano umepanga labda familia yangu inatakiwa kula kwa siku Sh.10,000/= baba ameacha shilingi 200 tunategemea nini? Kwa hiyo, haitaweza kufikia malengo, haya matatizo ya dawa na vifaa tiba kukosena yataendelea mara kwa mara. Tutajikuta hatutaweza kutatua tatizo kama kila siku tutakapokuwa tunakaa hapa kujadili bajeti mambo ni yale yale. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee vituo vya afya ambavyo wananchi walijenga kwa nguvu zao wenyewe na Serikali kuna wakati imeweka mfuko ikakamilisha lakini majengo bado hayajakamilika. Kwa mfano, Kituo cha Igalula kimekamilika lakini hakina dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Nashukuru sana. Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Mkundi, Mheshimiwa Luhaga Mpina ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipatia nafasi ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Afya. Kwanza niwapongeze sana Waziri pamoja na Naibu Waziri wa Afya na Watendaji wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitajikita katika suala zima la miundombinu. Ni dhahiri kwamba Serikali yetu imekuwa ikifanya vizuri sana katika miundombinu ya afya hususani majengo. Ukiangalia katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Msalala kulikuwa hakuna hospitali, lakini Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeweza kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hiyo. Hivi ninavyoongea majengo matatu

yanaendelea kukamilika, Serikali imetoa zaidi ya shilingi bilioni moja kwa ajili ya ujenzi huo. Pamoja na kwamba ili hospitali iweze kukamilika majengo yanayohitajika ni 22 hivyo, tutaendelea kuiomba Serikali yetu sikuvi iendelee kutenga fedha za kutosha ili kuweza kukamilisha ujenzi wa hospitali hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini kwa masikitiko makubwa sana katika Halmashauri ya Msalala kuna Kituo cha Afya cha Ngaya, kimekamilika mwaka 2018, kina wataalam Iakini hakuna vifaa tiba. Kwa hiyo, naomba Wizara ya Afya pamoja na taasisi ambazo zinahusika ziweze kukamilisha kutoa vifaa tiba ili Kituo cha Afya cha Ngaya kiweze kuhudumia wananchi wake. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza na kumkumbuka sana Hayati Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa aliyoifanya katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama. Halmashauri ya Manispaa ya Kahama imejenga jengo la *OPD* kwa fedha za ndani, imekwisha kutumia zaidi ya shilingi bilioni 2.7 na inaendelea na ujenzi na tunategemea kufikia mwezi Juni, jengo la hili liwe limekwishakamilika ambalo litatumia zaidi ya shilingi bilioni 3.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli, nawapongeza sana viongozi wote wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama kwa juhudhi kubwa walizofanya kuhakikisha kwamba wanajenga hospitali kubwa ya kisasa kwa kutumia mapato ya ndani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka Mheshimiwa Waziri wa Afya aliahidi mbele ya Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli kwamba hospitali ile itapandishwa hadhi iwe na hadhi ya hospitali ya mkoa kutokana na kwamba inatibu watu wengi sana kutoka kwenye Wilaya mbalimbali ikiwemo Urambo na Wilaya za Kigoma zote zinakujua Kahama. Hospitali ya Kahama wagonjwa wa nje (*outpatient*) kila siku wana-*attend* wagonjwa 800-1,000. Kama hiyo haitoshi, Hospitali ya Kahama ina vitanda 218 Iakini wagonjwa wanaolazwa kila siku kwenye ni zaidi ya 300. Kwa hiyo, bado

tuna upungufu mkubwa sana wa vitanda katika Hospitali ya Manispaa ya Kahama. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiaangalia kwa muundo wa Halmashauri ya Hospitali ya Wilaya ya Kahama, kwa ikama inaonekana watumishi wanatosha, lakini kwa uhalsia idadi ya watumishi hospitali ya Kahama hawatoshi. Kwa sababu ya hiyo takwimu niliyoitoa kwamba wana-*attend* wagonjwa wengi kwa siku kuanzia 800 mpaka 1,000, lakini wanalaza wagonjwa wengi na vitanda ni vichache. Kwa hiyo, bado tunahitaji watumishi wa kutosha kukidhi mahitaji ya Hospitali ya Wilaya ya Kahama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mama na mtoto, Hospitali ya Kahama ina vitanda 18 vya kujifungulia wanawake, lakini kwa siku wanawake wanaojifungua katika Hospitali ya Kahama ni 35 mpaka 55. Tunaona jinsi ambavyo kuna uhitaji mkubwa wa kuboresha miundombinu katika hospitali ya Kahama.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke Kahama ipo barabara kuu ya kwenda Burundi na kwenda mikoa mingine ya Geita; Kagera pamoja na Kigoma. Pale pana msongamano mkubwa sana wa watu. Kwa hiyo, inachukua idadi kubwa sana kuhudumia watu wengi kutoka sehemu nyiningine mbalimbali. Kwa hiyo, napenda Wizara ya Afya iiangalie Hospitali ya Manispaa ya Kahama kwa jicho la kipekee kutokana na idadi ya watu wengi waliopo mahali pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazidi kuipongeza Serikali na kukumbusha kwamba kuna ahadi ilitolewa na Mheshimiwa Rais ya shilingi milioni 500 kama mwanzo wa kununua vifaa tiba. Tunaomba fedha hiyo Serikali yetu sikivu iweze kutoa ili wananchi wa Wilaya ya Kahama waweze kupata vifaa tiba na hospitali iweze kufanya kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaipongeza Serikali, kwa kweli imeweza kujenga vituo vya afya kama Mwendakulima,

Nyasubi, kuna waganga, kuna waunguzi, lakini tatizo linarudi pale pale kwenye vifaa tiba. Tunaomba sana vifaa tiba viweze kutolewa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo haitoshi, katika Halmshauri ya Wilaya ya Kishapu, tuna Kituo cha Afya cha Nobola cha toka enzi za Mwalimu. Kituo kile kinahudumia Kata tisa na pembedi yake hakuna kituo kingine chochote cha afya. Vile vile kutoka pale Nobola kwenye Makao Makuu ya Wilaya ni zaidi ya kilometra 40 mpaka 50. Naiomba Serikali iweze kuboresha na kujenga kituo cha afya kingine katika Kata nyiningine aidha Talaga au Lagana ili wananchi wa Wilaya ya Kishapu nao waweze kupata huduma ya afya kwa usahihi na kwa manufaa mazima ya afya zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijiini, kuna *Health center* ambazo zimejengwa vizuri, tunamshukuru Mwenyezi Mungu, tunawashukuru wataalam wetu na tunaishukuru Serikali kwa kutukumbuka watu wa Shinyanga. Kituo cha Afya Samuye pamoja na Tinde vinafanya kazi. Tinde kinafanya kazi vizuri sana, lakini Samuye kimejengwa, kina *theatre*, kina wafanyakazi, lakini hakuna vifaa, huu ni mwaka wa tatu sasa. Kwa hiyo, tunaona Serikali iweze kukukumba.

Mheshimiwa Naibuy Spika, kuna wananchi wa Kata ya Solwa, wamejenga kituo cha afya kwa nguvu zao, kuna wodi mbili wameshajenga, kuna *OPD* nzuri, lakini kupandishwa hadhi kutoka kwenye zahanati kuwa kituo cha afya bado Wizara inasuasua. Tunaomba mwafikirie wananchi hawa ambao wametumia fedha zao nyangi kujenga miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nitapenda kuzungumzia suala la magonjwa yasiyoambukiza. Kumekuwa kuna mlipuko wa magonjwa yasiyoambukiza kwa wananchi, mengi sana. Mfano, kisukari, magonjwa ya moyo na magonjwa mengine, lakini afua ambazo zinatekeleza *intervention* hizo zimekuwa zikisuasua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana Wizara ya Afya kuitia Kitengo cha Tiba Mbadala. Tunaomba sasa dawa ambazo zinagundulika kwamba zinafanya kazi, ziweze kutolewa kwa bei nafuu, ziweze kupewa vibali ambavyo vinastahiki. Mfano hiyo *Phyt Exponent*, tunaomba hiyo dawa iweze kupunguziwa masharti, iweze kupunguziwa masharti, iweze kusajiliwa kama dawa ya tiba mbadala kuliko kuwa na *Dietary supplement*. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Mkundi, tutamalizia na Mheshimiwa Luhaga Mpina.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa fursa hii. Nawapongeza kwanza Mheshimiwa Waziri, Naibu na Watendaji wote kwenye Wizara hii. Kwa muda huu mchache nitachangia kwenye maeneo matatu kama muda utaniruhusu. Kwanza, ni kuhusu upatikanaji wa madawa kwenye vituo vyetu vya kutoa huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatambua juhudini kubwa zilizofanywa na Serikali kujenga miundombinu kwenye maeneo ya kutolea huduma za afya; hospitali zimejengwa, vituo vya afya na zahanati. Kama miundominu hii itakuwepo katika mazingira yaliyo mazuri, lakini kukawa na shida ya upatikanaji wa madawa, bado haitakuwa na tija sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na shida kubwa sana ya upatikanaji wa madawa bado. Pamoja na kwamba tumeongeza bajeti ya huduma za afya hasa kwenye eneo la madawa, lakini bado kuna shida kubwa sana ya upatikanaji wa madawa kwa watu wetu kwenye vituo vya kutolea huduma za afya. Hili linachangiwa sana na deni

lililoko *MSD*. Nikitolea mfano *case studyya* Ukerewe; Ukerewe ili tuwe na madawa ya kutosha kwa mwaka mzima, tunahitaji karibu shilingi milioni karibu 80, lakini mpaka mwezi Desemba mwaka 2020 ndiyo wamepata shilingi milioni 20. Kwa hiyo, utakuta kuna shida kubwa sana ya madawa kwenye Hospitali yetu ya Wilaya, kwenye zahanati na vituo vya afya.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Hospitali yetu ya Wilaya inahudumia watu mpaka wanaotoka eneo la Bunda kutoka Kisolya wanakuja kutibiwa pale. Sasa yanahitajika madawa mengi sana. Kwa hiyo, kunapokuwa na tatizo la kibajeti kunakuwa na shida sana kwa wananchi wetu. Kwa mfano, kwenye hospitali yetu ile, wanakwenda kununua madawa, wanakuta *MSD* kule madawa mengi hawana, wanawaelekeza kwenda kununua kwa Mshiriri. Wanapokwenda kwa mshiriri, anataka pesa *cash*, hospitali hawana. Matokeo yake sasa kunakuwa na shida kubwa sana ya madawa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali, pamoja na jithada zinazofanyika kudhibiti matumizi matumizi mabaya kwenye mnyororo huu wa madawa, lakini tuhakishe tunapata *solution* ya haraka ili madawa yawe *available* kwenye hospitali zetu ili wananchi wetu wapate huduma hizi kwa kiwango kinachotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukizingatia tuko kwenye jithada za kushawishi watu wetu wajunge na Mfuko wa Afya ya Jamii, kama wanakwenda kwenye vituo vya kutolea huduma za afya na hawapati madawa, inawakafisha tamaa hata kujiunga na Mifuko ya Afya. Hata hili tunaloendelea nalo la kutaka tutengeneze Sera ya Afya ya Jamii kwa watu wote, tunaweza tukapata kikwazo sana kwa sababu wananchi wanakosa imani kwamba hata wakiwa wanachama, basi zile huduma wanazozitarajia watazipata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili, naipongeza Serikali kwa kukubali ombi letu la kupandisha Kituo cha Afya cha Bwisya kuwa Hospitali ya Wilaya na Hospitali yetu ya

Wilaya ya Nansio angalau sasa kuwa *Referral Hospital*, ni jambo jema.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naiomba tu Serikali, zile taratibu ambazo zimebaki, ziweze kukamilishwa ili basi vituo hivi viweze kutoa huduma kwa wananchi wetu, kwa sababu dhamira ni kufanya Visiwa vya Ukerewe hasa kwa changamoto za kijigrafia, iwe kama eneo linalotoa huduma kama *self-contained*. Huduma zote ziweze kupatikana kwa sababu ikitokea changamoto ya kiafya Ukerewe, kumpeleka mgonjwa kwenye *Referral Hospital* kwa mfano Sekou Toure ni changamoto kubwa sana. Kwa hiyo, tukiwa na huduma zote kwenye kisiwa kile, angalau itasalimisha na itaokoa maisha ya wananchi wetu wengi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu sasa, pamoja na jitihada ambazo zinaendelea, najua kuna timu imepelekwa pale kufanya tathmini kuona upungufu uliopo. Naomba hasa wodi ya uzazi ya akina mama ina matatizo makubwa sana. Katika maboresho yatakayofanyika, liangaliwe kwa kipekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, jengo la mama na mtoto ambalo limejengwa kwenye miaka 1960 huko nyuma lina hali mbaya sana, nalo vile vile liangaliwe liweze kuboreshwa, lakini hata idadi ya watumishi kwenye maeneo yetu yale, bado yaangaliwe sana hasa kwenye Hospitali yetu ya Wilaya ili kuwe na *staffing* ya kutosha kuweza kuhudumia watu wetu na hasa kama itakuwa *Referral Hospital*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hili litafanikiwa kufanya Hospitali ya Nansio ambayo ni Hospitali yetu ya Wilaya kuwa *Referral Hospital*, itahitaji vituo vingine vya afya kwa ajili ya ku-*support* eneo hili. Ndiyo maana nimekuwa ninaomba Mheshimiwa Waziri mtusaidie Kituo cha chetu cha Afya cha Nakatunguru ambacho kimejengwa mwaka 2012 chenye upungufu kidogo wa majengo na vifaa tiba, kiweze kukamilika ili kiweze ku-*support* hospitali yetu hii ya Wilaya. Kama itakamilika, mzigo mkubwa uwe unaelemea huku ili Hospitali yetu ya Wilaya iwe kweli ni *referral hospital*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, kitakwimu ukienda hospitali ya *Ocean Road* kuna wagonjwa wa *cancer* wengi, lakini asilimia kubwa ya wagonjwa waliopo pale wanatoka Kanda ya Ziwa. Ndiyo maana mwaka 2009 Hospitali ya Bugando ikaanza kuhudumia wagonjwa wa *cancer*. Wakati ule ilianza na wagonjwa takribani 300, lakini hivi leo ina hudumia wagonjwa karibu 14,000 kwa mwaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2017 imeanza kutoa huduma ya mionzi, lakini bado ina upungufu wa miundombinu. Ina vitanda 20 pekee na kwa siku wanapokea wagonjwa karibu 200; ni wagonjwa wengi sana. Bado kuna upungufu mkubwa sana. (*Makofii*)

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkundi, kuna taarifa kutoka Mheshimiwa Ester Bulaya.

## TAARIFA

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nampa taarifa mchangiaji na mchango wake mzuri, naamini mkakati wa Serikali ilikuwa ni kuhakikisha hizi mashine za mionzi zinakwenda katika hospitali zote za Kanda, kwa sababu tatizo la *cancerya shingo* ya uzazi limekuwa ni kubwa sana hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa hivi, wewe unajua Mbeya pale, kwenye Hospitali ya Mbeya, kuna tatizo na mashine haipo na iliahidiwa kupelekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nampa taarifa mchangiaji.

**NAIBU SPIKA:** Sasa hiyo taarifa sijaelewa kama niipokee mimi au mchangiaji. Mheshimiwa Mkundi unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, maadam ina dhamira njema, haina shida. Ninachotaka kusema, Serikali ione namna ya kuisaidia Hospitali ya Bugando. Sasa hivi wana ujenzi wa wodi ambapo itasaidia kupokea wagonjwa wengi zaidi, basi Serikali ifikirie maombi yao katika bajeti waliyonayo ya karibu shilingi bilioni tano, wodi ile iweze kukamilika. Iwasiaidie mashine za ku-backup za mionzi ili zile zilizopo zikiharibika, kuwe na mashine nyingine kwa ajili ya ku-support. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo ambayo vituo vimekamilika na hospitali zimekamilika, Serikali ipeleke vifaa tiba na wataalam viweze kufanya kazi. Kama nilivyosema, Kituo chetu cha Nakatunguru kinahitaji kuwezeshwa, majengo yaliyobaki yakamilike, vifaa viwekwe ili kiweze kutoa huduma kwa wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna eneo kwa mfano llemela, hospitali yao ya Wilaya imekamilika muda mrefu, kimebaki kuwekwa tu vifaa na watumishi kiweze kufanya kazi, iweze kuwasaidia wananchi. Naomba Serikali vilevile kama ilivyo Hospitali ya Wilaya ya llemela, kama ilivyo Vituo vya Afya cha Nakatunguru Ukerewe na vingine vyote nchi nzima, basi vipelekewe vifaa na wataalam viweze kuanza kutoa huduma kwa wananchi wetu ili wananchi wapate kile ambacho tunakitarajia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana kwa nafasi, Mwenyezi Mungu akubariki sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Luhaga Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi uliyonipa ili nami niweze kuchangia hii Wizara muhimu sana. Nami niungane na wenzangu kuwapongeza sana watoa huduma wote wa afya hapa nchini kwa kazi nzuri sana wanayoifanya ya kutibu watu wetu na kuwapatia maisha mapya. Pia naipongeza Serikali

kwa hatua nzuri ilizozichukua kuongeza idadi ya madaktari na kuhakikisha kwamba vifaa tiba pamoja na vitendanishi vinapatikana katika maeneo mbalimbali nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo shida kubwa kweli kweli hapa nchini ya upungufu mkubwa sana wa zahanati. Kama tunavyofahamu, zahanati hizi ndiyo huko huko kabisa kwenye msingi wa afya ya mwanzo, lakini hapa nchini kwa takwimu tulizonazo toka uhuru, tumeweza kujenga zahanati 6,120. Maana yake mpaka sasa hivi tuna upungufu wa zahanati 6,197. Kwa hiyo, tuna vijiji 6,197 havina zahanati. Kwa hiyo, asilimia 50.3 ya wananchi hawana huduma hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hii hali, inaendelea kusababisha adha kubwa sana kwa wananchi wetu, akina mama wajawazito hawawezi kujifungua, mpaka watembe kilometra 10 mpaka 20 kupata huduma hiyo. Watoto wadogo wanapoteza maisha kwa kuchelewa kufika kwenye huduma kutokana na hizo kilometra ndefu za kufuata huduma hiyo kwenye vijiji jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili limekuwa likileta shida kubwa, hata sasa hivi tumepiga hatua kubwa, kwa mfano, kupunguza vifo vya watoto chini ya miaka mitano ambapo sasa hivi tunazungumza kwamba katika vizazi hai 1,000 watoto wanaopoteza maisha ni 50.3. Pia katika wajawazito 100,000 tunapoteza akina mama 321. Sasa hizi takwimu pamoja na safari ndefu tuliyotoka kule tumeweza kuzipunguza, lakini bado idadi hii ni kubwa na idadi hii sababu yake kubwa ni upungufu wa hizi zahanati katika vijiji vyetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu huu; na tunajua magonjwa hayana likizo na wala hayana *week-end*, lakini utaratibu wa Serikali tulionao sasa hivi na sisi wote ni kwamba zahanati mpaka tujenge jengo kwanza, likimalizika, mjenge nyumba ya mganga kwanza iishe, halafu mkimaliza, ndiyo sasa mfikirie kupeleka waganga, mfikirie kupeleka dawa. Hivi kuna shida gani leo hii tukiamua vijiji 6,197 ambavyo havina

huduma ya afya, tukapeleka daktari, tukapeleka muuguzi, tukapeleka na dawa, watu wakaanza kutibiwa leo hii, badala ya kusubiri jengo lijengwe mpaka likamilike ndiyo tupeleke huduma. Kwa nini miundombinu itangulie badala ya huduma kutangulia? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zahanati hizi kwa awali zinaweza tu zikaanzishwa hata kwenye nyumba ya kupanga tu, wananchi wakaanza kupata huduma badala ya kusubiri majengo. Sasa leo tuna miaka 61 ya Uhuru, wananchi wanasubiri jengo likamilike ndiyo wapate huduma. Miaka 61 hakuna huduma ya msingi kwenye kijiji husika, tunasubiri mpaka tujenge zahanati, tunasubiri nyumba ya mganga ikamilike, tunasubiri jengo la zahanati likamilike: Kwa nini haya tunayaruhusu yafanyike?

Mheshimiwa Naibu Spika, mbaya zaidi ni pale ambapo hawa wananchi wameshamaliza kujenga majengo, daktari hakuna, huduma hakuna. Mimi ninayo mifano ya vijiji nadhani karibia nane, ambayo zahanati imejengwa na imekamilika, ina nyumba ya mganga, kuna zahanati imekamilika, lakini hakuna huduma, leo miaka nane. Ukienda Kijiji cha Semu, Ukienda Mwageni, ukienda Mwagai, Mwanduitinje, Igigijo, Tindobuligi na Malwilo, zahanati zimejengwa zimekamilika, lakini hakuna huduma. Sasa haya mambo kwa nini tunayaruhusu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri *strongly* kwa Serikali, Wizara ya Afya pamoja na TAMISEMI tuamue sasa wananchi hawa kuwamalizia tatizo lao. Vijiji 6,197 vipelekewe madaktari, vipelekewe dawa, vipelekewe wauguzi, zianze kutoa huduma mara moja. Vile vile mahali ambapo zahanati zimejengwa na kukamilika, watumishi waende mara moja, vifaa viende mara moja, huduma zianze kutolewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni wizi wa dawa. Nimesoma hotuba ya Waziri kuhusu suala hili. Nadhani ipo ukurasa wa 61. Suala hili la wizi wa dawa linavyoripotiwa, ni kubwa sana, lakini nimeona kwenye hotuba ya Waziri pale imeandikwa kama *para* moja tu. Nataka niseme kwa ufupi

kwamba, tatizo hili ni kubwa, dawa zinaibiwa. Songwe mlitangaza, nadhani Waziri mwenyewe alisema ni dawa karibia za shilingi milioni 13.5 ziliibiwa. Pia Ukerewe dawa za shilingi milioni 200 ziliibiwa; na kwenye taarifa yake huku ya tathmini anakiri kwamba wizi huu unasababisha huduma za dawa zisiwafikie wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kweli leo hii Serikali imeshindwa kabisa kudhibiti hawa wezi wa dawa? Mpaka leo hii wanaendelea kuiba dawa? Nani anayeiba dawa hizi? Anafanikiwaje kuiba dawa katika Serikali ambayo imejipanga kuanzia kwenye Kitongoji, kwenye Kijiji, kwenye Kata, kwenye Tarafa, kwenye Wilaya na ina vyombo yya dola kila sehemu, hawa wezi wa dawa ni akina nani ambao hawawezi kukamatwa na kuadhibiwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Waziri hapa angetuambia amekamata wezi wangapi toka ianze vita dhidi ya wezi wa dawa? Hakuna, nani ameiba dawa? Anafanikiwaje kuiba dawa? Dawa hizi zinaibiwa zinaenda kuuzwa wapi? Nani ananunua dawa hizi? Mtandao wa wizi huo nani anaufadhili kiasi kwamba tushindwe kukomesha suala hili?

Sasa watu wanaiba dawa, leo tunaenda kuidhinisha bajeti ya dawa zikaibiwe. Ni shida sana kupitisha bajeti ya Waziri huyu ambaye yeye mwenyewe anakiri kwamba kutokana na wizi huu, dawa haziwafikii wagonjwa. (*Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama dawa haziwafikii wagonjwa, Bunge hili lijishirikishe kikamilifu kuhakikisha kwamba kwanza tunamaliza tatizo la wizi wa dawa, halafu ndiyo tupitishe bajeti, kwa sababu kinyume cha hapo tutakuwa tunawaongopea Watanzania. Ukitoma kiambatisho cha sita ambacho Waziri amekisema yeye mwenyewe, ukisoma yale matukio, ukiukwaji mkubwa wa manunuvi, watu wanunua dawa wanavyotaka wenyewe, watu wameiba dawa, watu wamefanya kila aina ya hujuma, hatua kwa nini hazichukuliwi? Kwa nini hatuambiwi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulitegemea kwamba wezi wa dawa hawa tungekutana nao kila siku wana pingu mkononi kila kunapokucha. Serikali hii haiwezi kushindwa kudhibiti wezi wa dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeweza ufisadi, tumeweza uvuvi haramu, tumeweza madawa ya kulevyta, leo hii tunakuja kushindwaje suala la wizi wa dawa? Kuna mtu hapa hajawajibika sawa sawa. (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililila kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha kwanza kwa siku ya leo. Nitaje majina machache ya Waheshimiwa Wabunge watakaoanza kuchangia mchana. Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Mheshimiwa Regina Qwaray, Mheshimiwa George Malima, Mheshimiwa Martha Mariki, Mheshimiwa Michael Kembaki, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Hawa Mwaifunga na Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza. Tutaendelea na majina mengine kadri uchangiaji utakavyokuwa hiyo mchana.

Baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni leo.

*(Saa 7.03 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilitrudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na majadiliano ya hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Tutaanza na Mheshimiwa Ritta Kabati, atafuatiwa na Mheshimiwa Regina Qwaray na Mheshimiwa George Malima ajiandae.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili kuwa mchangiaji wa kwanza jioni hii ya leo. Naomba nimirangulize Mwenyezi Mungu katika mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuwapongeza Waziri, Mheshimiwa Dkt. Gwajima na Naibu Mawaziri Mheshimiwa, Dkt. Mollel na Mheshimiwa Mwanahamisi. Kwa sababu leo ndiyo siku hii Wizara inayohusika na mambo ya wanawake, naomba kwa kweli nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan.

Kwanza kabisa kwa kuwa Rais ambaye amekuwa akituwakilisha vyema, lakini nimpongeze pia kwa hotuba yake ambayo alikuja kuhutubia hapa Bungeni kuhusiana na mambo ya afya. Ametuhamasisha sana. Vile vile, nampongeza kwa kumteua Naibu Waziri ambaye anashughulika na masuala ya wanawake, wazee na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya masuala siku zote tulikuwa tunaona yanamezwa na masuala ya afya, kwa sababu katika Wizara hii kuna mambo mazito mengi ya wanawake, watoto na wazee ambapo tulikuwa tunaona hata sisi wenyewe tukichangia tunaenda moja kwa moja kwenye afya. Sasa tuna imani Naibu Waziri wetu

attachangamsha kuhakikisha kwamba anasikiliza changamoto zinazohusu wanawake, wazee na watoto. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Rais. Amewateua wanawake kwenye nafasi nyeti sana. Kwa hiyo, nampongeza na nina imani kabisa tutawaunga wenzetu mkono na watafanya kazi vizuri akiwemo dada yetu Mheshimiwa Jenista, Mheshimiwa Ummy, Waziri wa Wizara ya Mambo ya Nje na wote waliochaguliwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niwapongeze hata Wabunge waliochaguliwa katika Majimbo wakiongozwa na wewe mwenyewe. Kwa kweli, tunaona kazi kubwa mnayoifanya na tunawatia moyo na tuna imani kwamba wananchi waone kazi ya mwanamke, wanawake tunaweza na tunasema kwamba mzigo mzito mpe mwanamke, atauweza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja sasa kuna vitu viwili nataka kusema. Jamani wanaume mpo? Wanaume mpo? (*Kicheko*)

**WABUNGE FULANI:** Tupo.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na wale waliosema jamani, hiki ni kipindi cha wanaume sasa kupima UKIMWI. Tulikuwa na Balozi wetu Waziri Mkuu ametuwakilisha vizuri sana kuhakikisha anawahamasisha wanaume kupima, lakini bado hawapimi, wanatupimisha sisi wanawake. Wanaume wengi wanaishi na virusi lakini wanatuficha na wakati mwingine wanameza dawa hawatuelezi, wanaweka sehemu nyingine.

Kwa hiyo, niombe kwa kweli kupitia Bunge hili leo hii tuhamasishe wanaume wote wakapime na tuanze na Wabunge wote wanaume muwakilishe wanaume wenzeni kwenye majimbo yenu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu maambuzi mapya ni asilimia 40, utakuta kwamba asilimia 80 ni watoto wa kike. Sasa niseme kwamba unaona kwa watoto wa kike wengi wanaambukizwa kwa sababu pia wanabakwa sana. Watoto wa Iringa, tuna kesi zaidi ya 400 wamebakwa, kuna mwanaume mmoja alibaka watotosaba amewabaka siku moja. Kwa hiyo, kwa kweli niombe kabisa pengine hata sheria ije. Naomba kwa kweli sasa hili liangaliwe. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kule China watu wakiiba wanauawa, lakini sasa hawa sijui tuangalie adhabu gani maana kitu kinachosababisha watoto wetu wabakwe kiangaliwe vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema kwamba nyumba ni choo. Sasa kulikuwa kuna kampeni ile ya kuhamasisha vyoo bora vijengwe kwenye vijiji vyetu. Kunapokuwa na vyoo bora inasaidia kupunguza hata maambukizi yale ya katika maji, kwa sababu bado kwenye vijiji wananchi wanatumia maji ya kwenye mabonde na mito, kwa hiyo unakuta maambukizi yanakuwa mengi sana. Nimwombe Waziri mwenye dhamana ahakikishe kwamba ile kampeni inaendelea kwa sababu bado kuna kaya hazina vyoo bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nielezee kuhusu Bima ya Afya. Niombe, naona leo wengi wameongelea kuhusu Bima ya Afya, lakini niombe Bima ya Afya iongeze wigo wa matibabu. Kuna magonjwa ambayo yanawatesa sana wananchi hasa magonjwa ya figo na magonjwa ya saratani. Unaona wananchi wanatumia pesa nyingi sana, wengine ni watumishi tu wa kawaida, wengine hata sio watumishi unaona bima zile bado hazimwezeshi huyu mgonjwa kwenda kutibiwa kwenye hospitali zetu. Wamekuwa wakipata shida, wanakuwa wakienda kule kwenye matibabu inatakiwa watafute nyumba za kupanga. Niombe Serikali yetu hii iangalie wanyonge hawa ambao kwa kweli mara nyingi wamekuwa wakipata mateso makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijikite kwenye changamoto za Mkoa wangu wa Iringa. Jambo la kwanza ni Hospitali yetu ya Mkoa ina *shortage* kubwa sana ya Madaktari Bingwa kwa magonjwa mbalimbali. Karibu Madaktari saba wanahitajika katika hospitali yetu ya Mkoa wa Iringa. Pia, hii *CT scan machine* nilishawahi kuleta hata swalii ni tatizo kubwa sana kwa wagonjwa wetu pale Mkoani Iringa. Nishukuru kwamba Serikali imesema kwamba itaanza kuleta hizi mashine katika hospitali za rufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nielezee changamoto nytingine, ambayo ni upungufu mkubwa sana wa watumishi wa Sekta ya Afya. Unaona karibu asilimia 62 ya mkoani kwetu bado tuna upungufu mkubwa na katika hata baadhi ya Wilaya kwa mfano Kilolo hospitali imeshakuwa tayari kabisa lakini tatizo ni watumishi wa afya. Niombi Wizara sasa iende sambamba na hizi hospitali zinazojengwa, iweke watumishi ili kuondoa changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile hawa watumishi wamekuwa wakifanya kazi kwenye mazingira magumu sana. Unaona wanafanya kazi kwenye maeneo hatarishi, hata wakati wa *covid* vifaa havikuwepo vya kutosha. Kuna wengine walipoteza maisha. Naomba pia Serikali iangalie pia na suala la vifaa tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie pia kuhusiana na dawa *MSD*. Kuna malalamiko kwamba watu hawapati dawa wanalazwa lakini dawa hawapati. Inabidi tena waende wakatafute sehemu nytingine. Mimi niombi kwamba *MSD* ijithahidi kwa sababu ilibidi nifanye ziara kwenye hii Hospitali ya Mkoa na wakasema kwamba wanapeleka asilimia 50 ya yale makusanyo lakini dawa wanazohitaji kule hakuna.

Sasa iwe kama zamani kwamba kama hakuna dawa basi waangalie labda kwa wale washitiri, kwa maana waruhusiwe kwenda kununua hiso dawa, kwa sababu limekuwa ni tatizo kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nitoe pongezi kubwa sana. Tumekuwa na watu ambao wanachangia Wizara yetu ya Afya lakini bado sijajua kama Serikali inawatambuaje. Kwa mfano, kwenye Mkoa wetu wa Iringa tunayo majengo ambayo yamejengwa na wadau wa maendeleo. Kwa mfano, nimpongeze Mheshimiwa ASAS, labda nitaje tu baadhi ya majengo ambayo amejenga. Kuna jengo la Benki ya Damu, Wodi ya Watoto Njiti na vifaa vyake, *ICU unit*, Jengo la Kiwanda cha Viungo Bandia, jingo la Kituo cha Ustawi wa Jamii na mengine mengi. Kwa kweli, naomba tutambue michango ya wadau ambao wamekuwa wakisaidia hata bajeti yetu ya Wizara ya Afya...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, kengele imegonga.

**MHE. DKT. RITTA E. KAKABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Regina Qwaray atafuatiwa na Mheshimiwa George Malima na Mheshimiwa Martha Mariki ajiandae.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa nafasi uliyonipatia nami niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Kwanza nianze kupongeza Wizara hii ikiongozwa na Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Mawaziri na watumishi wote wa Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya kuhakikisha huduma hii ya afya inaendelea kuboreshwa. Pia, nippongeze Serikali yetu kwa kazi kubwa inayofanya kuhakikisha huduma ya afya inaendelea kuboreka ili wananchi wetu waweze kupata huduma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kuhusu huduma ya mama na mtoto. Niombe Wizara itueleze wazi dhana halisi ya huduma bure kwa akinamama wajawazito na watoto wa chini ya umri wa miaka mitano. Huduma hii

imebaki kuwa nadharia, akinamama wengi wanapokwenda kujifungua wanatakiwa waje na vifaa vyao ili waweze kupata huduma hiyo ya kujifungua, wakati tunasema kwamba huduma hii ni bure kwa akinamama wajawazito, wanapokwenda kujifungua wapewe huduma stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, ukienda kwa upande wa watoto chini ya miaka mitano, huduma hii si bure kwa sababu hawapati dawa. Watoto hawa wanapata huduma ya kuwaona Madaktari lakini linapofika suala la dawa wanatakiwa wajigharamie na kwenda kununua.

Mheshimiwa Naibu Spika, basi nniombe Wizara ituweke wazi ni namna gani sasa huduma hii ya akinamama wajawazito inapatikana bure, lakini huduma kwa watoto chini ya miaka mitano inapatikana bure. Katika eneo letu mfano, hususan Mkoa wetu wa Manyara, jilografia yetu ni ngumu na ya mazingira magumu mno. Sasa inapofika hatua mama anaambiwa aje na vifaa vyake anapoenda kujifungua, inabaki akinamama wengine wala hawaendi hospitali, wanajifungulia nyumbani, kitu ambacho kinahatarisha maisha yao. Hatimaye akinamama wengi wanapoteza maisha kwa sababu fedha za kumudu gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu mama mjamzito, kwanza kutoka kwenye eneo lake analoishi kwenda kwenye hospitali ni zaidi ya kilometra 70, 80 hadi 100. Sasa mama wa kijiji unapomwambia sasa aje na vifaa, kwanza akiangalia gharama zile za usafiri, aje agharamie vifaa vya kwenda kujifungulia, kiujuimla wanashindwa kumudu hizo gharama. Kwa hiyo, naomba iwekwe katika utekelezaji, tusibaki katika nadharia, iwekwe kwa vitendo kwamba akinamama wapatiwe huduma na watoto wale chini ya miaka mitano wapatiwe huduma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hospitali zetu za Wilaya na vituo vyetu vya afya hakuna vyumba vya kuhudumia watoto njiti. Watoto njiti wanapopatikana wanahudumiwa *locally*, lakini naomba sasa Serikali ihakikishe vituo vyetu vya afya,

hospitali zetu za Wilaya, vyumba vile vya kuhudumia watoto njiti pamoja na wataalam wale wa kuwahudumia wale watoto. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo kuna huduma ya *phototherapy unit*, wale watoto ambao wanapata homa ya manjano. Maeneo yetu mengi hasa Mkoa ninaotoka mimi, watoto hawa wanapopata tatizo hilo la homa ya manjano kiukweli hawapati hiyo huduma inayostahili kwa sababu hatuna mazingira wezeshi, hatuna vifaa, hizo *phototherapy unit* hazipatikani. Kwa hiyo, Serikali ione namna gani basi angalau hata hospitali zetu za wilaya na rufaa ambazo ni hospitali za mikoa ziwepo hizo *phototherapy unit* watoto wetu wanapopata tatizo hilo basi wahudumiwe kitaalam zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijikite zaidi kwenye huduma ya wazee. Kiukweli huduma hii ya wazee bado niishauri Serikali ione namna bora ya kuwahudumia hawa wazee wetu wa miaka 60 kwenda juu. Wazee hawa wanateseka mno wanapofika kupata huduma hizo katika hospitali zetu. Ukizingatia hospitali zenyewe hizi bado tuna upungufu mkubwa wa dawa, lakini yule mzee anapohitaji ile huduma akijua kwamba Serikali yetu inamhudumia bure, anapofika ile huduma haipati, kiujumla wananyanyasika na kufedheka hawa wazee. Naomba tuwatunze hawa wazee wetu kwa sababu na wenyewe walikuwa vijana kama sisii. Sasa wanapofika katika ule umri mkubwa, naomba Serikali itusaidie basi kuhakikisha ile huduma inapatikana kikamilifu ili wazee wetu nao waendelee kuishi wakiwa na afya njema. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niungane na wenzangu walioongolea suala la Bima ya Afya. Kiukweli hili suala la Bima ya Afya ni kilio kikubwa. Hii Bima ya Afya *CHF* ambayo inatakiwa kwa wananchi wote bado kuna tatizo kubwa. Bado kuna tatizo kubwa. Tunaomba Wizara sasa ione mkakati upi wa namna gani ya kuboresha hiyo huduma ya Bima ya Afya. Utaona hata mwitikio kwa wananchi unaenda kuwa mdogo kwa sababu mtu anapokata ile Bima ya

Sh.30,000 akitegemea anapata huduma katika zahanati au kituo cha afya, matokeo yake hapati dawa. Anabaki na ile hali kama ni mgonjwa atabaki na ugonjwa wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hata unapompa rufaa kwenda hospitali ya wilaya anapata tabu ya kwenda hospitali ya wilaya kwa sababu hata nauli ya kwenda huko hana. Kwa hiyo, yule mtu anaendelea kupata tabu huku akiwa mgonjwa, anahitaji kuhudumiwa lakini huku anahitaji kutoa fedha zake ili aweze kupata huduma hiyo. Naomba huduma hii ya Bima ya Afya iboreshwe ili walau kama kweli tunahitaji wananchi wetu wapate huduma kwa kuititia Bima ya Afya, tuwe *serious* na jambo hili ili huduma hii itolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye suala la *NHIF*. Ukiangalia huduma ya *NHIF*, watu wengi wamezungumzia humu ndani. Ni kwamba huduma hiyo bado inatakiwa iangaliwe tena upya. Kuna baadhi ya dawa ambazo ni muhimu, zinatakiwa ziwepo kwenye huduma hiyo ya Bima ya Afya. Mfano kuna dawa za sukari, *pressure* ambazo ni muhimu wananchi wapate. Tena ikiwezekana wapate bure maana ni magonjwa ambayo yanajitokeza, sio magonjwa ya kuambukizwa. Kwa hiyo, unakuta hiyo huduma haipo kwenye Bima ya Afya na inalazimu watu wanaanza kununua zile dawa kitu ambacho sasa ni gharama. Mtu anajiliza kwa nini anakuwa na Bima ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nishauri, kama itapendeza Serikali ione namna ambavyo yule ambaye ni mchangiaji tunakuwa na wale wategemezi. Sasa wale wachangiaji unakuta mtu hana mtoto, hana baba, mama, hana mume, hana mke lakini yeye ni mchangiaji namba moja. Wakati huo huo anakuwa na mtu ambaye anamtegemea kama mlezi wake aliymlea, bima inamkataa yule mtu. Nafikiri tuangularie mfumo upya kwa sababu yule mtu ataendelea kuwa mtegemezi kwake na ataendelea kumhudumia na wakati huo yule mtu anaendelea kuchangia bima ya afya lakini hanufaiki, atanufaika yeye peke yake wategemezi watakuwa hawajanufaika na huduma hiyo ya bima ya afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo naomba nichangie suala la ukosefu wa vituo vya afya katika maeneo yetu. Pamoja na jitihada kubwa ya Serikali, lakini bado katika maeneo yetu tuna changamoto kubwa ya ukosefu wa vituo vya afya. Natolea tu mfano katika Mkoa wetu wa Manyara, Wilaya ya Kiteto pale tuna vituo viwili vya afya. Sasa ukizingatia vituo viwili vya afya na zahanati 23 katika kata 23 kiukweli wananchi wetu bado wanafuata huduma mbali sana. Huduma hizi zisogezwe karibu na wananchi. Mheshimiwa Naibu Spika,

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile hata kwa zahanati zilizopo hatuna vifaatiba, wananchi bado wanateseka kwa sababu vifaa tiba havipo na dawa hazipo na wakati huo huo tuna upungufu mkubwa sana wa watumishi wa huduma ya afya. Kuna zahanati zingine hata Madaktari tu hawapatikani, wamebakti kuwa watoa huduma. hivyo inawalazimu watu kwenda hospitali zingine na wengine kukosa hiyo huduma ya afya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana na naomba niunge mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa George Malima, atafuatiwa na Mheshimiwa Martha Mariki na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga ajiandae.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na wenzangu kuipongeza Wizara hii ya Afya kwa kazi nzuri ambayo inaendelea kufanyika. Naomba nichangie katika eneo la upungufu wa dawa. Kama ambavyo wenzangu wengi wameeleza, kuna shida kubwa sana ya dawa katika hospitali zetu lakini hasa katika vituo vya afya na zahanati. Mara nyingi vituo vya afya na zahanati viko vijijini na kule vijijini ndiko watu wengi walipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu huu umesababisha kumekuwepo na mrundikano wa maduka ya dawa katika maeneo ya vijiji. Kusema kweli maduka mengi hayana sifa ya kuwepo. Hatari iliyopo ni kwamba hata wale

wanaohudumia kuuza dawa zile, hawana utalaam wa kuuza dawa na kwa sababu wako vijijini hawafuatili. Kwa hiyo, watu wengi wanakunywa dawa ambazo wakati mwingine zimepitwa na wakati, *zime-expire*, lakini hakuna mtu anaweza kufuutilia mambo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wamechukua *advantage* kwa sababu ya upungufu wa dawa, wanajua kabisa kule kijijini hakuna dawa, kule kwenye zahanati hakuna dawa, kwa hiyo wanapeleka maduka na hawaweki hata watu *professional*. Anajua akimweka *professional* kwanza hataaka kijijini lakini pia hawezi kumlipa mshahara, hivyo, anaweka mtu ni mtu. Kwa hiyo, yule anakuwepo pale, mtu akienda kutafuta dawa anachofanya anapiga ramli kwamba huyu anahitaji *paracetamol*/lakini ukweli ni kwamba hajui na hiyo ni hatari tunaweza kujikuta tumeua watu wetu kwa sababu ya jambo hilli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa nashauri Serikali maduka haya ya vijijini ya dawa yafuatiliwe. Kwanza kujua hawa watu wanaouza dawa wana utaalamu wa kuuza dawa hizo? Wanafahamu hizo dawa? Wana A, B, Cs za dawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia wafuutilie waone hizo dawa hazijapitwa na wakati? Kwasababu kule mambo yanajiendea hivyo sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia ni upungufu wa watumishi. Hili ni tatizo la nchi nzima, hospitali nydingi za wilaya, vituo vya afya, watumishi hawatoshi. Kwa mfano hospitali yangu ya Wilaya ya Mpwapwa ina upungufu mkubwa sana wa watu. Hospitali ile inatakiwa kuwa na wafanyakazi 310, lakini waliopo sasa hivi ni 152 ambayo ni sawa na asilimia 49. Ina upungufu wa wafanyakazi 158 ambayo ni sawa na asilimia 51; upungufu huu ni mkubwa sana na ndio maana unaona huduma hii pamoja na nia njema ya Serikali hakuna *efficiency* kwasababu, watumishi hawatoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri sana Wizara hii iangalie uwezekano wa kupata watumishi wa kutosha. Na hasa katika hospitali zile ambazo watu wengi wanazitegemea kama hospitali za wilaya na mikoa na zile hospitali za rufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia ni miundombinu chakavu katika hospitali zetu karibu zote. Ukienda katika hospitali za wilaya karibu nchi nzima, za mikoa, utakuta majengo mengi ni chakavu, lakini hakuna vifaa tiba. Kwa mfano ukienda katika hospitali ya Wilaya yangu ya Mpwapwa jengo lile la *OPD* limechakaa san ahata unasema hapa mazingira hayaruhusu kabisa kutoa huduma ya afya pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna majengo mengine, miundombinu ya maji-taka na maji-safi yote ni ya zamani na imeharibika, lakini pia umeme hakuna umeme wa uhakika, lakini hospitali ile ya Mpwapwa mpaka leo haina *X-Ray, just imagine*. Haina *X-Ray* wakati mwingine wanaazima kutoka kwenye kituo cha afya, *X-Ray* ya kizamani sana, lakini hospitali kama hadhi kama ya wilaya inahitaji kuwa na *Digital X-Ray*. Kwa hiyo, naomba sana Wizara iangalie sana Mpwapwa hakuna *X-Ray* tunaazima kutoka kituo cha afya ndio inakuja kutumika na *X-Ray* ile haina efficiency yoyote ni mbovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huwezi kuhudumia watu wa wilaya nzima kwa kutumia vitu vya kubahatisha kama hivi. Kwa hiyo, Wizara nashauri sana hivi vitu vya miundombinu ni muhimu, hospitali zetu ziwe na vifaa tiba vya kisasa, ili tuweze kuendana na wakati, lakini pia huduma kwa watu wetu iweze kufanyika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningetaka kuchangia ni juu ya bima ya afya kwa ajili ya wazee. Sera hii imetungwa siku nyngi, lakini sioni kama kweli Wizara inatoa hizi bima kwa wazee. Katika Wilaya yangu ya Mpwapwa nadhani ni katika wilaya chache ambazo hazina, wazee wengi hawana bima ya afya. Pamoja na bima ya

afya, lakini pia wazee wetu hata wale wanaokwenda kwenye Dirisha la Wazee huduma haipo. Wazee wenye umri mkubwa unakuta wamesongamana msururu akifika kwenye dirisha anaambiwa dawa hii hamna kanunue mahali fulani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni jambo pia la kuliangalia sana, kama hakuna dawa ni afadhali wasipange foleni. Kwa nini wapange foleni watu wenye umri mkubwa wanarudi wanaumwa na dawa hawakupata? Si ijulikane moja kwamba, hakuna dawa wazee wasiende kupanga foleni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wizi Mheshimiwa mmoja amezungumzia sana habari ya wizi wa dawa. Na nimeona ukienda katika vijiji utakuta maduka ya dawa ni ya baadhi ya watumishi wasio waaminifu. Yeye ndiye anayeandika dawa kwa hiyo, anaandika dawa na anaelekeza nenda kanunue mahali fulani, lakini kijijini ni watu wangapi wanaweza kununua dawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, wana bima ile iliyoboreshwa, lakini dawa pale hamna. Dawa zinaharibiwa na baadhi ya wahudumu ambao sio waaminifu kwa hiyo Serikali lazima iwe makini sana na wahudumu wa namna hii vinginevyo tutapigizana kelele hapa kila siku, huduma hazitakuwa nzuri, watu wetu wataendelea kuathirika na utaratibu huu ambao sio mzuri. Wizi wa dawa nijambo kubwa sana linaloendelea sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Martha Mariki, atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga. Mheshimiwa Michael Kembaki ajiandae.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu, Wizara ya Afya. Awali ya yote

namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kipekee sana napenda kuishukuru Serikali ya Awamu ya Tano kwa jinsi ambavyo ilivyotutendea mambo makubwa wananchi wa Mkoa wa Katavi kwa kuhakikisha kwamba, imetekeleza llani ya Chama Cha Mapinduzi kwa kutupatia hospitali kila wilaya, iliahidi na ilitekeleza. Wananchi wa Mkoa wa Katavi wanasema ahsante sana Serikali ya Awamu ya Tano iiliyopita, lakini kipekee tunamshukuru sana Mama yetu Samia Suluhu kwa jinsi ambavyo anaendelea kuchapa kazi na kuhakikisha kwamba, huduma za afya nchi nzima zinaboreshw. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Mkoa wa Katavi kwanza tunatoa shukrani za dhati kipekee kwa kupata zahanati nyingi na vituo vya afya katika Mkoa wetu wa Katavi. Tumepatiwa zahanati za kutosha, lakini vituo vya afya vya kutosha katika Mkoa wetu wa Katavi katika wilaya zetu mbalimbali. Lakini changamoto kubwa tuliyonayo wananchi wa Mkoa wa Katavi katika wilaya zetu tumepatiwa vituo vya afya, lakini vituo vile vya afya tuna ukosefu mkubwa sana wa watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wetu wa Katavi takribani mkoa mzima tuna upungufu wa watumishi katika kada ya afya takribani asilimia 72 ambapo watumishi tulionao ni sawa na asilimia 28. Kwa jinsi Mkoa wetu wa Katavi ulivyo na muingiliano wa watu wengi utaona watumishi hawa ni wachache sana kuhakikisha kwamba, wanaenda kutatua changamoto katika kuhakikisha wananchi wa Mkoa wa Katavi wanapata huduma zilizo bora katika afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wananchi pia wa Mkoa wa Katavi katika vituo vyetu vya afya kuna upungufu sana wa vifaa tiba. Tuna upungufu wa vifaa tiba takribani asilimia 60, ambao sisi tunao ni kama takribani asilimia 40. Tunaiomba sana Wizara ya Afya waweze kutupatia watumishi ili waweze kwenda kutatua changamoto katika vituo vyetu

vya afya kwa kuhakikisha wananchi wetu wa Mkoa wa Katavi wanaenda kuhudumiwa ipasavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wananchi wa Mkoa wa Katavi tunaomba sana Serikali yetu sikivu, Serikali yetu tukufu, huduma ya *MSD* tunaomba katika Mkoa wetu wa Katavi iweze kuboreshwa. Serikali imekuwa ikitenga pesa kwa ajili ya dawa katika Mkoa wa Katavi, lakini *MSD* wanatuambia baadhi ya dawa hakuna. Sasa tunaomba sana Wizara ya Afya wahakikishe kwamba, wananchi wa Mkoa wa Katavi tumakwenda kupata dawa ili wananchi wa Mkoa wa Katavi waweze kupata huduma ilio bora katika kuhakikisha kwamba, afya zao zinaenda kuwa safi ili waweze kwenda kuchapa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi pia wa Mkoa wa Katavi tunasema asante sana Serikali yetu kwa jinsi ambavyo imeona umuhimu ikaamua kutujengea hospitali ya Mkoa wa Katavi ambayo kwa jinsi ninavyoionna ile ramani, jinsi ilivyokaa niiombe sana Serikali, hospitali ile isitumike kama hospitali ya Mkoa hospitali ile kwa ramani jinsi inavyoonesha inafaa kuwa hospitali ya rufaa. Ukiangalia mwananchi wa Mkoa wa Katavi tunatumia gharama kubwa sana kwenda kufuata rufaa katika Mkoa wa Dar-es-Salaam katika Hospitali ya Muhimbili, lakini kwenda Ikonda pia ni mbali sana, lakini ukiangalia kwenda Bugando ni mbali sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Mkoa wa Katavi wamekuwa wakitumia gharama nyingi sana kufuata rufaa katika mikoa hii ambayo ni mbali sana na ukizingatia miundombinu yetu katika Mkoa wa Katavi bado ni mibovu. Hivyo, niiombe sana Serikali kwa kuwa, walitenga hela katika Hospitali hiyo ya Mkoa wa Katavi ambayo ina hadhi kabisa ya kufanywa kuwa hospitali ya rufaa au hospitali ya kanda kwa watu wanaotokea katika mikoa hiyo ya Katavi.

Niwaombe sana Serikali, hospitali hiyo ilikuwa ikabidhiwe Januari tarehe 21. Sasa niwaombe tunaiuliza Serikali, ni kwa nini mkandarasi sasahivi hayuko *site* na hakuna kitu chochote kinachoendelea katika hospitali ile? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na ile hospitali ni muhimu sana kwa wananchi wa Mkoa wa Katavi, lakini kwa wananchi wa mikoa ya jirani, jirani zetu pale watatumia hospitali ile kama ya rufaa ili kuondokana na adha ya kufuata hospitali za rufaa ikiwepo Ikonda, ikiwepo Muhimbili, ambapo ni gharama kubwa nyingi sana. Niwaombe sana Serikali yetu Sikivu, tunaomba hospitali hii iweze kumalizika, ili wananchi wa Mkoa wa Katavi waweze kupata huduma iliyoboreshwa kwa ukaribu ili waweze kuchapa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukizingatia Mkoa wetu wa Katavi wananchi wale ni wazalishaji wazuri sana wa kilimo wanahitaji huduma ilio bora, lakini ukizingatia Mkoa wetu wa Katavi Rais wetu aliyepita, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, aliona umuhimu wa mkoa ule akaamua atajenga bandari, alisema kwamba, atajenga bandari na bandari imeshaanza kujengwa. Kuna bandari inayojengwa Wilaya ya Tanganyika ambayo inaenda kutuunganisha na wananchi wa Kalemii, Kongo, ambako kuna dhahabu nyingi sana. Hivyo yote hiyo naeleza haya ili muweze kuona umuhimu wa hospitali ile kuweza kumalizika, ili iweze kutibu wananchi wengi sana wanaokuja katika Mkoa wetu wa Katavi kuhakikisha fursa nyingi sana za uchumi zinaenda kunyaaliwa katika Mkoa wetu wa Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, niiombe sana Serikali hospitali ile ni muhimu sana wananchi wa Mkoa wa Katavi wanaihitaji sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ambalo napenda kuchangia katika Wizara ya Afya, niwaombe sana, kumekuwa na sintofahamu akinamama wanapoenda kujifungua. Mama zetu wanapoenda kujifungua wanakutana na ghadhabu sana wanaambiwa kwamba, wanatakiwa wachangie damu, ila hata pale wanapopata watu wa kwenda kuwachangia damu wanaambiwa kwamba, ile mifuko ya kuchangia damu inauzwa, takribani wanatoa mpaka 16,000/=. Niwaombe sana Serikali waangalie jambo hilo aikinamama ni waaminifu sana na akinamama wana upendo mkubwa na Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe Serikali muweze kuwaangalia akinamama hawa waweze kwenda kujifungua. Ikiwezekana kama Serikali ilivyosema akinamama watajifungua bure, basi kweli waende kutekeleza hiyo kwa vitendo. Akinamama wa Mkoa wa Katavi na akimama wa Tanzania nzima tuhakikishe kwamba, wanajifungua salama na wanajifungua kwa bei nafuu, ikiwezekana ni bure kabisa kama Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu jinsi alivyo tuahidi. Hivyo, niiombe sana Serikali kupitia Wizara ya Afya m jitahidi jamani, akinamama wa Mkoa wa Katavi wanahitaji huduma iliyoboreshwa ili kuhakikisha akinamama wanajifungua na kuzaliana, tuweze kwenda kuzaliana tuongeze nguvu kazi katika Taifa hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia, niiombe sana Wizara ya Afya, kutokana na huu upungufu ambao umeonekana ni mkubwa sana, hapa nitazungumzia Hospitali yetu ya Wilaya ya Mpanda ambayo kwa sasa inatumika kama Hospitali ya Mkoa. Hospitali ile jamani ina ufinyu sana wa maeneo kiasi ambacho kwamba, hata upasuaji imekuwa ni kitendawili kufanyika maeneo yale.

Niwaombe sana Wizara ya Afya wakati tunasubiri hospitali hii ya rufaa iweze kukamilika niwaombe sana waiboreshe hiyo Hospitali yetu ya Wilaya ya Mpanda ambayo inabeba wagonjwa wengi sana, waiboreshe kwa kuangalia kukarabati miundombinu, lakini kuleta vifaa tiba. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyoeleza hivi hata huduma tu ya *CT-Scan* katika Mkoa wetu wa Katavi haipo. Niwaombe sana Wizara ya Afya mtuangalie wananchi wa Mkoa wa Katavi. Naongea hivi kwa uchungu sana mtuangalie kwa sababu, mama zangu na baba zangu wanapata tabu sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ambalo napenda kuchangia katika Wizara hii ya Afya niwaombe sana. Kwa kuwa, Serikali yetu imeahidi wazee watapata huduma bure, niwaombe sana mtuboreshee wazee waweze kupata huduma iliyo bora na salama. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge huyo ni Mheshimiwa Martha Mariki, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Katavi. Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, atafuatiwa na Mheshimiwa Michael Kembaki. Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma ajiandae.

**MHE. HAWA S. MWEIFUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika Wizara hii. Kwanza kabisa ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia uhai na afya tele nimeweza kusimama hapa muda huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ningependa kuzungumzia utekelezaji wa bajeti ya maendeleo katika Wizara hii kwa miaka mitatu iliyopita. Utekelezaji wa bajeti ya maendeleo katika Wizara hii umekuwa hafifu mno kwa miaka mitatu iliyopita. Kwa mujibu wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya 2018/2019 fedha za miradi ya maendeleo hadi kufikia mwezi Machi, 2019 zilikuwa zimepelekwa kwa asilimia 16 peke yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2019/2020, na haya sio maneno yangu yapo kwenye randama za Wizara ya Afya za miaka hii mitatu, fedha zilitotengwa zilikuwa jumla ya shilingi bilioni 544.137 lakini hadi kufikia mwezi Machi mwaka 2020 kiasi cha fedha kilichokuwa kimetolewa ni shilingi bilioni 83.06 peke yake sawa na asilimia 15.3 tu. Mwaka 2020/2021 bajeti iliyotengwa ilikuwa ni kiasi cha shilingi bilioni 360.9 lakini mpaka mwezi Machi mwaka 2021, mwaka huu, fedha zilitokuwa zimepelekwa ni shilingi bilioni 83.1 peke yake. Kwa hiyo, utaona ni kwa namna gani fedha zinatengwa lakini haziendi kutekeleza yale ambayo tumekubaliana katika Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na hii inaonesha kwa miaka yote mitatu fedha zimekuwa zikipelekwa angalao kwa asilimia 18 tu kila mwaka. Sasa uone ni namna gani

changamoto za afya zinavyozidi kujitokeza kwasababu, fedha zile zilizokusudiwa haziendi kama ambavyo tumezipangia bajeti. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na changamoto kubwa sana katika maeneo yetu. Mimi natokea Mkao wa Tabora, Jimbo la Tabora Mjini; kuna suala la wanawake kwenda kujifungua na kulipa gharama. Unapojifungua mtoto wa kiume utorialpa 50,000/= na unapojifungua mtoto wa kike utorialpa 40,000=/. Hili jambo lipo katika hospitali za Mkao wa Tabora, ikiwepo Hospitali ya Kitete ya Rufaa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na hata juzi hivi ninavyozungumza kuna ndugu yangu katoka kujifungua, amelipa 50,000. Sasa huyo amejifungua mtoto wa kiume, sasa huyo ana uwezo wa kulipa hiyo 50,000/= lakini kuna mwananchi mwengine wa kawaida ambaye uchungu umempata, anakwenda hospitali hana hiyo fedha ya kulipa, vifo vinatokea. Na hii sio uwongo ndio ukweli uliopo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ningeomba sana Serikali atakapokuja kwenye majumuisho Mheshimiwa Waziri aje na majibu, hii ni sheria? Ni utaratibu? Ama ni waraka wa Wizara uliokwenda kwenye baadhi ya hospitali wanatakiwa wachangie fedha hizi? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwasababu hata sisi wawakilishi wa wananchi tukihoji tunaambiwa hay ani maelekezo. Sasa tunataka tujue hayo ni maelekezo kutoka wapi? Mheshimiwa Waziri aje aseme hapa, ili wananchi wa Tabora wapate kupona kwasababu hii imekuwa kero kubwa sana katika Jimbo la Tabora Mjini na Mkao mzima wa Tabora. Na ninaamini kabisa kuna baadhi ya mikoa mingine fedha hizi wanalipa wakati wanawake wanakwenda kujifungua. Hii ni kero kubwa sana kwa wananchi wa Jimbo la Tabora na Mkao mzima wa Tabora. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tabora Mjini hatuna hospitali ya wilaya, lakini tuna kituo cha afya. Kituo hiki cha afya hakina vifaa tiba, hakina wauguzi, hakina madaktari,

hakina dawa. Hivyo, inasababisha wananchi wa Jimbo la Tabora Mjini wengi kwenda kusongamana katika Hospitali ya Rufaa ya Kitete na hivyo kusababisha msongamano kuwa mkubwa zaidi kwa sababu, ile ni hospitali ya rufaa. Sasa tunaiomba sana Serikali iweze kusaidia kituo kile cha afya, tunaomba mkakiboreshe, muweze kuweka vitu kwa ajili ya wanawake kujifungua. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu anatoka kwenye Kata kwa mfano ya Ikomwa, Ikomwa ni kata ambayo iko mbali sana na pale maili tano. Kwa hiyo, mtu anatoka pale anaafika pale maili tano anaambiwa dawa hakuna, anaambiwa hakuna vipimo, anaambiwa hakuna, kwa hiyo, mwananchi anajikuta amechoka kwelikweli kiasi kwamba, anakuwa hana jinsi inabidi arudi jinsi ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningeomba sana Serikali itusaidie iende ikaboreshe kile kituo cha afya. Mnafahamu kabisa Jimbo la Tabora Mjini limegawanyika katika sehemu mbili, kuna kata za mjini kuna kata za vijijini na kituo cha afya kinachotegemewa ni hicho kilichopo maili tano. Sasa tungeomba kama Wizara kuna uwezekano basi tuongezewe vituo vya afya, ili angalao viendane na maeneo ambayo tupo kwasababu, maeneo mengi yako pembezoni na ni makubwa mno na kuna wananchi wanaishi kule, lakini wanapata changamoto kubwa sana ya huduma za afya. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na kule kwenye maeneo mengine ya kata za pembezoni hakuna hata zahanati. Watu wanateseka, watu wanapata shida kwelikweli kwasababu ya ukosefu wa huduma za afya. Ningeomba sana Serikali iuangalie mkoa wa Tabora, iangalie Jimbo la Tabora Mjini tuna changamoto kubwa sana katika huduma za afya. Na haya niliyokueleza ni changamoto ambazo zinatukabili siku hadi siku. Hasa hasa pia, hata hii Hospitali yenyewe ya Kitete ambayo nimezungumza haina vifaa tiba. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2018/2019, bajeti ilitengwa hapa kwa ajili ya kufanya ukarabati kwenye vituo

vya wazee. Pale Tabora tunacho Kituo cha Wazee Ipuli, kwa kweli kinahitaji ukarabati. Tunahitaji kuwasaidia wale wazee ili na wao angalau waweze kuishi kama wapo sehemu ambapo wanalelewa na Serikali. Kwa hiyo, naomba sana zile fedha ambazo zilitengwa na kama zilikuwa hazijafika basi wajitahidi kuweza kuboresha vituo hivi ili viweze kutunza vizuri wale wazee kama ambavyo Serikali tumekusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Michael Kembaki atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma na Mheshimiwa Maimuna Mtanda ajiandae.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika Wizara hii ya Afya ambayo ni muhimu sana katika Taifa letu. Mtu yejote asipokuwa na afya nzuri hawezi kuzalisha au kuwa na amani kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa ambayo imeifanya katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Kwa sababu wameweza kujenga zahanati zaidi ya 423 na vituo vya afya zaidi ya 449 na Serikali imeweza kukarabati Hospitali za Halmashauri zaidi ya 22 na Hospitali za Rufaa zaidi ya 23. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali imetumia zaidi ya shilingi bilioni 102.9 kwa ajili ya kukarabati na kujenga Hospitali za Rufaa katika Mikoa ya Geita, Katavi, Njombe, Simiyu na Mara. Kwa hivyo, ninayo sababu ya kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa ambayo imeifanya katika kipindi hiki cha miaka mitano. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ninayo machache ambayo napenda kuishauri au kuisemea Serikali ili iweze kufanya marekebisho. Kwa mfano, katika Jimbo langu la Tarime Mjini tunayo hospitali moja ya Halmashauri, kituo cha afya kimoja na zahanati tatu, ukilinganisha na idadi ya watu iliyopo na jiografia ilivyo bado vituo hivi vya afya

havikidhi mahitaji katika kuhakikisha kwamba watu wa Tarime wanakuwa na afya nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda katika Hospitali ya Bomani mara nyingi kilio kinakuwa hakuna dawa, hakuna siku mgonjwa atakwenda pale aweze kupata dawa na matibabu yaliyostahili lakini sababu kubwa ya ukosefu wa huduma hii nzuri ni kama zifuatazo. Moja, tulihitaji madaktari zaidi ya 16 katika hospitali ile lakini madaktari waliopo ni watano peke yake na unajumlisha pamoja na *DMO*. Sasa ukiangalia idadi ya watumishi hawa haitoshelezi, mtu anafanya kazi usiku na mchana kiasi kwamba anachoka hata kuhudumia, wagonjwa wanapata wakati mgumu sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ipo changamoto, kwa kipindi hiki ambapo barabara imematika na mawasiliano ya barabara hayapo, unakuta hakuna zahanati za kutosha ambazo zinaweza zikahimili watu kupata huduma kwa karibu. Kutokana na hali hiyo watu wengine hufia njiani na akina mama hujifungulia njia kwa kukosa huduma ya afya kwa karibu. Kwa hivyo, nashauri tupate zahanati katika kila kata kwa mfano Kata za Kebaga, Ketare, Nyandoto, Bomani, Nyamisangura, Kenyamanyori pamoja na Sabasaba. Zahanati hizi zitaweza kutoa huduma karibu badala ya watu wote kusongamana katika Hospitali ile ya Bomani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu nyingine inayopelekea huduma kuwa siyo nzuri katika hospitali ile ni kutokana na hospitali ile kuwa kongwe, toka miaka mingi iliyoita ni hospitali ambayo Halmashauri zaidi ya tatu zimetoka pale: Hamashauri ya Rorya, Halmashauri ya Tarime Vijiiji imetoka pale na Tarime Mjini. Watu wana imani sana na hospitali ile na hivyo basi wengi wanakuja kutibiwa pale, kwa hiyo, dawa zinazokuja katika hospitali ile zinachangiwa na Halmashauri zote tatu. Naomba hospitali ile ikiwezekana ipandishwe daraja iweze kuwa Hospitali ya Kanda ili *at least* iweze kupata dawa na madaktari wa kutosha ili watu wetu waweweze kupata huduma inayostahili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda katika hospitali ile unakuta hakuna damu na sababu kubwa si kwamba watu wa kuchangia damu hawapo isipokuwa damu inapopatikana pale lazima ipelekwe Bugando ili iweze kupata vipimo na iweze kurejeshwa. Hata hivyo, ili majibu yaweze kurudi inachukua zaidi ya mwezi mmoja na kusababisha damu kukosekana katika hospitali yetu ya Tarime. Naomba Waziri aweze kutujengea kituo pale Mkoani ili huduma hii ya kupima damu iweze kupatikana kirahisi hatimaye kusiwepo na upungufu wa damu katika hospitali zetu. Hii si kwa Mkoa wa Mara peke yake ninaamini katika nchi nzima damu bado ni changamoto. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kuhusu huduma inayotolewa kwa akina mama wajawazito, wazee pamoja na watoto. Hii imekuwa ni kero na kila Mbunge anayesimama hapa anaongelea kuhusu suala hilli. Mimi nilikuwa naona kama Mheshimiwa Waziri huduma hii hawezu kuitoa vizuri basi tuangalie namna nyingine ambayo tunaweza kufanya ili wazee, akina mama wajawazito na watoto waweze kupata huduma kama inavyostahilli. Wanakwenda pale wanaandikishwa lakini bado hawapati dawa na hatimaye wanarudi nyumbani bila kupata matibabu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba nizungumzie kuhusu huduma inayotolewa na watumishi wetu. Kwa mfano, katika Hospitali yetu ya Tarime hakuna wahudumu wanaotosheleza inafikia hatua mpaka wagonjwa wanafanya usafi. Mimi nikifika jimboni kila mtu ninayekutana naye analalamika kuhusu hospitali, tafadhalii sana Mheshimiwa Waziri tunaomba sana uangalie hospitali yetu kwa jicho la pekee *at least* watu wale wapate huduma inayostahili, watu wengi wanafia pale kwa kukosa huduma inayostahili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho naependa kukizungumzia na kuishauri Serikali ni kuhusu kuongeza watumishi. Ukiangalia katika vituo vingine ambavyo viro pembezoni bado watumishi hawatoshelezi

kutoa huduma katika vituo au zahanati zile zilizo pembezoni.  
*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.  
*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Maimuna Mtanda atafuatiwa na Mheshimiwa Bahati Kenneth Ndingo, Mheshimiwa Abbas Tarima ajiandae.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipatia fursa hii ili niweze kuchangia katika Wizara hii ya Afya. Nianze kuwapongeza Waziri na timu yake lakini pia nimpongeze Waziri kwa uwasilishaji mzuri wa hotuba yake. Kipekee, niishukuru Serikali pamoja na Wizara kwa kutupatia fedha shilingi bilioni moja sisi Newala Vijiji kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, Wizara ya Afya inakabiliwa na changamoto nyingi sana hasa kwenye maeneo yetu. Nianze na suala la ukosefu wa nishati ya umeme katika yale maeneo ambayo huduma za afya zinatolewa lakini hawajafikiwa bado na miradi ya umeme au pia mradi wa REA nao haujafika, kuna changamoto kubwa sana katika utoaji wa afya katika maeneo hayo. Katika maeneo mengi unakuta kuna zahanati zinatumia solar ambazo hazikaguliwi kiasi kwamba zinakufa matokeo yake wagonjwa wanaokwenda kupata huduma pale wanakosa huduma ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, akina mama wajawazito muda wa kujifungua haupigi hodi au hauchaguzi wakati mwingine wanakwenda kupata hizo huduma nyakati za usiku matokeo yake kituo kina giza lakini mama mjamzito anatakiwa ajifungue hapo. Inambidi mama mjamzito pamoja na uchungu alionao awashe tochi yake ya siku ammulikie mtoa huduma anayemsaidia kwa wakati huo. Mimi ni mzazi najua uchungu ulivyo, napata shida sana wakati mwingine wa kutambua namna gani mama huyu anaweza kumulika

tochi amsaidie mzalishaji wakati yupo kwenye maumivu makali. Kwa hiyo, niiombe sana Wizara iangalie kwa jicho la kipekee maeneo kama hayo ili ufumbuzi upatikane akina mama wapate huduma vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, dunia sasa hivi imekumbwa na magonjwa mengi ya milipuko ikiwemo suala la Corona. Wanaotoa huduma katika maeneo yetu ni madaktari wetu tunatambua lakini sijaona mkakati wa Serikali wa kutafuta *PPE* ya kuwakinga madaktari wanaokwenda kutoa huduma kwa wagonjwa. Matokeo yake madaktari wana-*risk* maisha, wanununa *PPE* wenyewe, kama hana uwezo anaingia kichwa kichwa kwenda kutoa huduma. Hii ni changamoto kubwa na tunawakatisha tamaa. Namuomba Mheshimiwa Waziri wakati wa kuhitimisha hoja yake aje na mpango mkakati wa namna gani atawasaidia madaktari kuwapatia *PPE* ili waweze kuwashudumia wagonjwa bila kupata shida au kuwa na hofu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nami niungane na wenzangu kuongelea yale makundi yaliyobainishwa katika Sera ya Afya kwamba watapatiwa huduma za afya bure. Hata kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi imebainishwa kwamba wazee zaidi ya miaka 60 watapata huduma bure, akina mama wajawazito pamoja na watoto chini ya miaka mitano. Hata hivyo, suala hili limekuwa ni kinyume kila ukienda kwenye mikutano sijui kama ni kwangu peke yangu unakutana na kero hiyo. Wazee wanalamika hawapati vitambulisho matokeo yake wanashindwa kupata huduma ya afya. Sasa hawaelewi wapo kwenye *dilemma*, je, kilichoongeleta katika llani ilikuwa ni kwa ajili ya kuombea kura au kweli Serikali ilikuwa na nia thabiti ya kuwasaidia wazee hawa? Niombe sana Serikali pamoja na Wizara ijipange vizuri wazee wabainishwe wapewe zile kadi wapate huduma za afya kama llani ya Chama cha Mapinduzi ilivyoeleza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala la akina mama wajawazito limekuwa ni changamoto kweli kweli, kuanzia kadi za kliniki wanatakiwa wanunue wao wenyewe. Kadi ya

kliniki ambapo ndiko tutaona maendeleo ya ukuaji wa mimba yake anatakiwa anunue lakini tumeshaji nasibu sisi kwamba tutawapatia huduma za afya bure. Kwa hiyo, inaleta mkanganyiko sana kwa sababu akina mama hawapati hizo huduma bure wala Watoto. Kwa hiyo, tunapokwenda tukasema kwamba huduma zinatolewa bure tunakuwa hatueleweki. Niungane na wenzangu Mheshimiwa Waziri wakati wa kuhitimisha hoja tunaomba uje na mpango mkakati utueleze namna gani au nini kauli ya Serikali kuhusiana na kundi hili la wanufaika wa huduma bure za afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niungane na wale walioongelea suala la *CHF Iliyoboreshwa*. Mkakati ulikuwa mzuri lengo la Serikali lilikuwa zuri lakini wale waliokata kadi kwa ajili ya kupata hizo huduma hawapati ...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, kengele imegonga.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo atafuatiwa na Mheshimiwa Abbas Tarimba, Mheshimiwa Anna Lupembe ajandae.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kupata fursa ya kuchangia katika Wizara hii ya Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuipongiza sana Wizara kwa kazi nzuri na nzito ambayo wameendelea kuifanya. Pia nimpongeze Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan kwa hotuba yake aliyoitoa tarehe 7 kuhusiana mambo ya masuala mazima ya wazee. Kwa kweli, hotuba

ile iliwapa matumaini makubwa wazee na tunashukuru kwa kutambua thamani kubwa ya wazee wa Taifa hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua tuna Sera ya Wazee iliyotungwa mwaka 2003 lakini mpaka sasa hatujaitengenezea sheria ya kusimamia utekelezaji wake. Hata kama tuna mipango mizuri na mikubwa kwa ajili ya wazee wetu kama tunakosa sheria ya kusimamia utekelezaji wa sera hizi, itakuwa ni ngumu sana changamoto za wazee kupata muarobaini. Kwa hiyo, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anakuja ku-*windup* atuambie ni lini ataleta Bungeni sheria ya kusimamia utekelezaji wa Sera hii ya Wazee. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze sasa kwenye vituo vya kulelea wazee vinavyomilikiwa na Serikali. Nitambue kwamba Serikali inafanya kazi kubwa kwa ajili ya wazee wetu na sasa hivi tuna vituo takriban 16 nchi nzima vya kulelea wazee, lakini hali ya vituo hivi kwa kweli inasikitisha. Mimi binafsi nimeshatembelea baadhi ya vituo vya kulelea wazee, niliwahi kwenda pale Fungafunga Morogoro miundombinu ya pale si rafiki. Ilani ya Chama cha Mapinduzi imetuelekeza kwamba wataenda kukarabati vituo 5 kama ifuatavyo: Kituo cha Kolandoto (Shinyanga); Kituo cha Nunge (Dar es Salaam); Kituo cha Njoro (Kilimanjaro); Kituo cha Magugu (Manyara) na Kituo cha Fungafunga (Morogoro). (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wanapokwenda kufanya maboresho ya vituo hivi pia waangalie sana miundombinu ambayo itakuwa rafiki kwa wazee. Kwa mfano, pale Fungafunga (Morogoro) ukiangalia kile Kituo cha Wazee vyoo vyao viko nje kabisa ya sehemu wanazolala na wale wazee wanahitaji kusaidiwa kwa sababu ni watu ambaa umri wao umekwenda sana.

Mheshimiwa NaibU Spika, kwa hiyo, niombe sana wanapofanya marekebisho ya vituo hivi waangalie miundombinu rafiki ambayo haitakuwa vikwazo kwa wazee wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na miundombinu kuwa rafiki vifaa vya kuhudumia wazee kwenye hivi vituo hakuna, hata *gloves* za kuwasaidia wale wazee hakuna. Kwa hiyo, niombe sana sana Serikali vifaa viwepo kwenye vituo hivi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kwenye vituo hivi vya Serikali huduma zinazotolewa mle ndani ni huduma za kwanza yaani mzee atapewa tu *Panadol*, ndio zinazokuwepo pale lakini ile huduma angalau inakuwa ni ngumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi vituo vingi vyao vipo nje sana ya miji na kusababisha wazee wengi kupoteza maisha kwa sababu ya umbali. Kwa mfano, hiki cha Fungafunga (Morogoro) kwa sababu nimeshakwenda hata barabara ya kufika pale kituoni hakuna, watu wanapita chini ya lile bomba la reli, hata gari zikifika pale kuleta dawa wanaenda na pikipiki wanavuka wanachukua ndio wanakuja kuzileta kituoni. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri muangalie sana miundombinu ya hivi vituo vya wazee. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilifurahi kusikia kwamba mna utaratibu wa kuanzisha *uniform* kwenye vituo vyetu vya afya, kwamba watu wanaohudumia wazee mtatoa *uniform* maalum ili mzee akifika pale ajue hawa ndio wanaohudumia wazee. Naomba katika utaratibu huo mwaangalie pia walemauvu na viziwi ili wajue kabisa, kama mtaweka sare hizo kwa wazee muweke na sare pia kwa watu wengine ambaao wanauhitaji maalum. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, naomba niongelee kuhusu mambo ya vyoo. Magonjwa mengi sana yanatokana na ukosefu wa vyoo; usambazaji wa uchafu kutoka vyooni. Kuna kampeni moja ilikuwa inaongelea "Nyumba ni Choo." Kampeni ile ilifanyika, lakini kwa vijijini kule bado suala la vyoo ni shida. Kwa hiyo, naomba sana, kampeni hizi za nyumba ni choo iendelezwé ili iweze kuleta tija mpaka kule vijijini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kule vijijini hakuna vyoo na maradhi mengi yanatokana na kukosa vyoo. Endapo Serikali mtaichukulia uzito hii Kampeni ya Nyumba ni Choo na vyoo vikawepo kwenye kila maeneo, itatusaidia sana kupunguza magonjwa mengi na itaisaidia pia Serikali kutopoteza fedha nyingi kwa sababu ya kukosekana magonjwa ambayo ni hatarishi. Kwa hiyo, niwaombe sana Serikali m jitahidi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, kengele imeshagonga.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Shukurani sana. Mheshimiwa Abbas Tarimba atafuatiwa na Mheshimiwa Aisha Ulenge na Mheshimiwa Agnesta Lambert, ajiandae.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia katika hotuba iliyoko mbele yetu. Kwanza napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, yeye pamoja na wasaidizi wake kwa kazi nzuri. Hotuba yake hii imejaa matumaini mazuri sana kwa wananchi wetu wa Tanzania. Naamini kwa kuwa yumo ndani ya Serikali Sikivu, basi hata haya ambayo sisi Waheshimiwa Wabunge tunachangia, atayachukulia kwa uzito unaostahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu nitaupeleka katika huduma za watoto yatima, nitazungumzia kidogo suala la maiti na nilikuwa nizungumzie Kampeni ya Nyumba ni Choo, lakini bahati nzuri Mheshimiwa Mbunge aliyejita ameshalizungumzia. Hata hivyo, kama nitapata nafasi, naweza nikaligusia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri na pia nimepata nafasi ya kuisoma tena. Kuna maeneo ambayo yananisikitisha kwamba hotuba hii

haijataja kwa uwazi kabisa watoto yatima. Hili ni eneo ambalo, katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri ameligusia, watoto ambao wapo katika mazingira magumu, lakini nadhani ingekuwa busara tukawataja, kwa sababu nchi hii sasa hivi ina watoto yatima ambao wametokea tu katika lile kundi ambalo wazazi wao wamefariki kwa *HIV*, wako takribani 1,400,000 ukiachilia wale wengine ambao wazazi wamefariki wao katika magonjwa mengine na *acts of God* wameondoka, yawezekana kuna watoto wengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali hii, naomba sana Mheshimiwa Waziri afikirie. Yawezekana Taifa hili sasa linahitaji kuwa na sera *specific* kwa ajili ya watoto yatima. Kwa nini nasema haya? Nasema hivi kwa sababu najua kuna Sera ya Maendeleo ya Watoto ile ya mwaka 2008, lakini kutokana na hali halisi ambayo sisi Waheshimiwa Wabunge tunakumbana nayo katika Majimbo yetu, utaona ni hakika watoto yatima wanahitaji watu wa kuwasemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwishoni mwa wiki nilipata nafasi ya kutembelea vituo vinne vya kulelea watoto yatima katika Jimbo langu la Kinondoni. Nilikwenda katika Kata ya Hananasifu, nikaenda kwenye Kata ya Mzimuni, Kata ya Tandale na Ndugumbi. Niliyoyaona kule yawezekana kabisa yanaakisi hali ya watoto yatima katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa sababu hii napenda niwapongeze kwanza wale wananchi ambao wamejitoa, kwa sababu hawa ni wananchi wa kawaida na wengi wao ni akina mama ambao ni watu wazima, lakini wamejitoa kwa hali na mali. Wengine wana watoto 50, wengine wana watoto 200, wengine wana watoto 300, wanategemea wafadhili na wana kazi ngumu sana ya kuwapeleka shule watoto hawa, kuwafundisha tabia njema na utashangaa watoto wanajua dini, wana tabia njema pengine tofauti na hata watoto wetu ambao wako majumbani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naangalia ni kwa jinsi gani Serikali inaweka mkono wake pale? Hili mtanisaidia Mheshimiwa Waziri, ni kwa jinsi gani Serikali inasaidia watoto

yatima ambao wanalelewa katika mazingira ya kijamii. Labda niseme kitu kimoja, kuna hali ambayo badala ya wale watu wa ustawi wa jamii kusaidia na kuwapa moyo wale ambao wamejitolea, kuna wakati mwengine wanawakatisha tamaa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, nilifika katika kituo kimoja kinaitwa cha Bi Maunga pale Hananasifu; katika kukagua kagua nilikuwa namwuliza kuhusu upakaji wa rangi, maana kuna baadhi ya sehemu hazijapakwa rangi vizuri. Akasema suala hili pia liligusiwa na watu wa Ustawi wa Jamii, lakini badala ya kunisaidia, wamenitisha. Wanasema kama sikupaka rangi, watakifunga kile kituo. Kauli kama hizi siyo nzuri kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya, mfano wakifunga kile kituo, wale watoto 100 wanakwenda wapi? Sasa lazima wafanyakazi wetu wa Ustawi wa Jamii wawe ni vijana au wawe ni akina mama au wawe ni watu wa rika lolote lile, wajifunze kuwa na *customer care* nzuri sana wanapozungumza na watu kama hawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na changamoto nydingine na wengi wameizungumza, sasa sijui katika Majimbo mengine; watoto hawa wakipelekwa shule kuandikishwa, wanahitajika kuwa na *Birth Certificate* (zile hati za kuzaliwa) ambazo watoto wale ambao ni yatima waliopatikana katika mazingira ambayo mengine ni magumu, hawana hizo hati. Wanapata matatizo, hawapelekwi shule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iangalie katika zile haki za Watoto, mojawapo ni haki ya kuendelezwa; haki ya elimu. Naiomba Serikali itoe kauli, naye atafute njia rahisi ya kuweza kusaidia watoto hawa kuweza kupata hati za kuzaliwa. Pale ambapo itakuwa na ugumu, angalau waanze kuruhusiwa kusoma huku taratibu nydingine zikitafutwa ili waweze sasa kupata elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, wakati nazunguka nilikutana na wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wanaosoma Saikolojia, walikuwa wanakwenda pale kuwapa nasaha wale watoto ambao wanajitambua. Jambo lile limenifurahisha sana. Kwa hali hiyo, naiomba Serikali itoe wito kwa vijana wanafunzi ambao wanasoma katika vyuo kama hivi wakipata nafasi watembelee maeneo ya yatima, wazungumze nao na kuwapa *encouragement* kwamba kuwa yatima siyo mwisho wa maisha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo moja la mwisho ambalo napenda nilizungumze kuhusu huduma za maiti. Huduma za maiti kule kwetu Kinondoni wakati tunafanya kampeni lilikuwa ni suala moja zito sana. Maneno ni kwamba, watu wanapofariki miili haitolewi mpaka watu walipie. Sawa, ni haki kabisa kulopia, lakini jambo kama hilli linatakiwa Serikali ilitolee mwongozo ambao utasaidia kupunguza machungu ya watu wanaofiwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza kuruhusu watu wakapewa miili ile, yaani maiti wakaenda kuzika na kukawa na utaratibu mwingine wa kuweza kuzipata zile fedha, ama njia nydingine zozote ambazo zinawezekana. Ila lugha ambayo ilikuwa inatumika jamani, ni kwamba Serikali inatuuzia maiti. Maiti wanauzwa! Kwa maana huwezi kumpata maiti mpaka ulipe pesa. Nilikuwa naomba tu Serikali iweze kutafuta njia ambayo inaweza ikasaidia kuondoa machungu haya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Agnesta Lambert, atafuatiwa na Mheshimiwa Zakaria Paul Essay na Mheshimiwa Dkt. Pauline Nahato, ajiandae.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili nami kwa uchache niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu. Mchango wangu

wa leo utajikita katika ripoti ya CAG ukurasa Na. 223 na ukurasa Na. 226.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imekumbwa na ugonjwa wa hatari ambao umeua watu wengi duniani kote wakiwemo ndugu zetu, jamaa zetu na marafiki zetu. Kila nchi imeweka mkakati madhubuti wa kupambana na ugonjwa huu wa *corona*; na nchi yetu Tanzania pamoja na mikakati mingine ambayo iliweka, ilijikita zaidi kuhakikisha Watanzania tunajikinga kwa kutumia barakoa na siyo tu kwa kunawa mikono.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo mwezi Mei, 2020 Serikali kupitia *MSDiliagiza* mtambo wa kutengeneza barakoa hapa nchini. Mtambo huu umegharimu dola za Kimarekani 270,314 sawa na shilingi milioni 600 *plus*. Mtambo huu according to CAG ultitarajiwa kuzalisha barakoa milioni nne kwa mwezi. Hata hivyo, *management* ilikaa na kukubaliana kwamba badala ya kuzalisha barakoa milioni nne kwa mwezi, basi izalishe barakoa 504,000 tu kwa mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeyasema haya kwa mujibu wa CAG. Pamoja na kwamba *management* ilijipanga kuzalisha barakoa 504,000 malengo haya hayajatimia kabisa. Ukumbuke, nimesema kwamba uwezo wa mtambo huu ulipaswa kuzalisha barakoa milioni nne kwa mwezi. Mpaka sasa nimesimama mbele zako, mnamo mwezi Agosti mtambo huu umezalisha barakoa 76,500 tu. Mwezi Septemba mtambo huu umezalisha barakoa 244,000 tu which means hata yale malengo waliyojiwekea ya kuzalisha barakoa 504,000 yameshindikana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa CAG, anasema katika ukurasa 223, kwamba changamoto hii ya mashine hii kushindwa kuzalisha milioni nne kwa mwezi ilitokana na *compressor* iliyokuwepo kutolefanya kazi vizuri na hivyo basi, ikabidi iletwe *compressor* nyingine ili kuongeza nguvu na hatimaye angalau uzalishaji ufikie malengo yale ya *management* iliyokuwa imejiwekea ya 504,000. Mpaka hivi sasa, kwa mujibu wa CAG mtambo huu wa kuzalisha

barakoa umefanya uzalishaji kwa asilimia nne tu ya uwezo wa mtambo huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema kwamba ilifungwa *compressor*nyingine ili iongeze nguvu kwamba sasa angalau uzalishaji uweze kuwa mkubwa. Cha kushangaza...

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

## TAARIFA

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Agnesta Lambert, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nimemskiliza mzungumzaji, anazungumza kuhusu suala la uzalishaji wa barakoa. Nilitaka kumpa tu taarifa kwamba kitu chochote kinachotengeneza vitu kibiashara, kinategemea na mahitaji yanayotakiwa. Sasa ukiangalia hata humu Bungeni, namwona dada yangu Mheshimiwa Halima peke yake ndio amevaa barakoa. Sasa hata tungezalisha hizo milioni nne, yeye mwenyewe mwongeaji, yuko *empty*ingekuwaje? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Agnesta Lambert, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, siipokea taarifa hiyo, lakini nadhani alikuwa hanisikilizi vizuri. Nilisema mchango wangu utajikita katika ripoti ya CAG. Haya siyo maneno yangu mimi Agnesta Lambert, ni maneno na ripoti ya CAG. Kwa hiyo, taarifa hiyo ingekuwa ni vyema kama ungemtafuta CAG ukampatia ili aweze kukupatia majibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niendelee. Nimesema mtambo huu siyo tu kwamba umeshindwa kukidhi matakwa ya kuzalisha milioni nne kwa mwezi, imeshindwa hata kukidhi matakwa ya kuzalisha barakoa 504,000 which

*means* hapa kuna shida. Kuna utata! Ni wazi Watanzania tumeuziwa mbuzi kwenye gunia.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Agnesta Lambert, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Getere.

## TAARIFA

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampa taarifa mzungumzaji kwamba suala la uzalishaji wa barakoa ni biashara inayoweza kufanya, kwa sababu kuna *demand* na *supply*. Sasa *demand* ya biashara ya Tanzania ni kidogo sana, lakini pia tulisharuhusu badala ya Serikali kutengeneza barakoa, tutengeneze wenyewe. Kwa hiyo, ye ye asihangaike na mambo ya CAG, atengeneze tu kwa njia yake. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Agnesta Lambert, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza siipokei hiyo taarifa, lakini pili naomba niwe wazi, niko hapa kuwatetea Watanzania zaidi ya milioni 60. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili nimalize kwa kusema hivi, lazima ufanyike uchunguzi kabisa wa moja kwa moja ili kuangalia mambo makuu mawili. Kwanza, tuhakiki kama kweli mtambo huu ulinunuliwa kwa thamani hiyo ya dola za Kimarekani 270...

*(Hapa kengele ya kwanza ililia)*

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee nimalize kwa kusema hivi, kwa mwaka mmoja mashine hii au mtambo huu ulipaswa kuzalisha barakoa milioni 48, lakini mpaka sasa hivi nimesimama mbele zako *MSD* wamezalisha barakoa 320,000 tu. *It is a shame.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende moja kwa moja ukurasa 226 wa ripoti ya *CAG*. Katika mchango wangu nilipokuwa nachangia katika Wizara ya Ofisi ya Waziri Mkuu niliongelea moja kwa moja juu ya usugu wa Serikali kutokulipa madeni ya *MSD*, jambo ambalo limesababisha *MSD* siyo tu kwamba imeshindwa kuagiza madawa, lakini Watanzania wengi wanakufa na wanakosa huduma kwa sababu tu ya madeni ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo nimeweka tu kumbukumbu lakini hoja yangu ya msingi imejikita...

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hiyo itakuwa taarifa ya mwisho. Mheshimiwa Agnesta Lambert, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Patrobas Katambi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru. Napenda kumpa taarifa msemaji, suala la malipo ya *MSD* lilitolewa ufanuzi na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, kwamba liko kwenye hatua ya uhakiki wa madeni na taarifa na kama tunakumbuka katika Bunge la wiki iliyopita taarifa hiyo ilielezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi katika eneo la uzalishaji wa barakoa; uzalishaji wa barakoa unaendana na kusudio kwa maana ya mahitaji. Zingezalishwa barakoa unazozihitaji kwa kipindi hicho, kungekuwa na *query* tena ya *CAG* kwa utaratibu ule ule. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda tu kumpa taarifa kwamba awe anachunguza zaidi katika kuangalia haya mambo kabla hajaleta hoja mezani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Agnesta Lambert, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kiti chako kilinde muda wangu, nafikiri umeona jinsi ambavyo Waheshimiwa Wabunge wame-*interfere* sana.

Mheshimwia Naibu Spika, naomba niende kwa *point* yangu ya pili. Hoja yangu ya pili ni kuhusiana na usugu wa Serikali uliokolea sasa kwa kutokupeleka bajeti ilioidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwenda *MSD*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka wa fedha wa 2019/2020, Bunge lako hili Tukufu lilipitisha bajeti ya bilioni 200 kwenda *MSD*, lakini pesa hii haijaenda hata shilingi moja. Matokeo yake *MSD*wameshindwa kuagiza madawa pamoja na vifaa tiba venye thamani ya millioni 119, yote haya Serikali ni kwa sababu inashindwa kupeleka fedha bilioni 200 kwenye *MSD*kupambana kuhakikisha Watanzania wanakua na afya njema, lakini wanapata huduma bora...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa, ahsante sana.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipe sekunde moja ili ni-*finalize* wamechukua muda wangu.

**NAIBU SPIKA:** Sekunde 30.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nimalizie kwa kusema kwamba kwa kipindi cha miaka mitano Bunge lako Tukufu limeidhinisha kiasi cha fedha za Kitanzania trilioni 1.04 kwenda *MSD*, lakini mpaka hivi sasa nimesimama mbele yako Serikali imepeleka bilioni 315 tu. *This is the shame*, hii ni asilimia 30 ya bajeti nzima ya *MSD*.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Zacharia Paul Issaay, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Paulina Nahato na Mheshimiwa Salim Alaudin Hasham, ajandae.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza niungane na Watanzania wote na Waheshimiwa Wabunge kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa majaliwa yake kwetu sote. Nafasi hii ya pumzi na uhai ni rasilimali na rehema za Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru pia Serikali kwa kazi kubwa iliyofanya, Serikali ya Awamu ya Tano katika kipindi kilichopita kupitia sekta hii ya afya, kwa kweli kuna miradi mingi na mageuzi makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije kwenye kuchangia hoja iliyopo mezani. Nizungumzie Bima ya Afya kama wenzangu walivyozungumza, Bima ya Afya ni changamoto, ni changamoto kweli kweli. Bima ya Afya ambayo mtumishi amekatwa fedha zake lakini anakwenda hospitalini hakuna dawa. Kama Bunge tunatakiwa kujitafakari, kujitathimini na nini angalau Serikali ichukue hatua za mahususi kwa ajili ya jambo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya afya ni sekta muhimu sana na ugonjwa hauna hodii, unapoouga wala hakuna maandalizi yanayotokea. Kwa hiyo eneo hili lina changamoto, hakuna dawa na kwa wakati wowote ule mtu anapata madhara lakini akifika kwenye sehemu ya huduma hawezni kuhudumiwa kwa sababu wa ukosefu wa dawa na vifaa tiba. Kwa hiyo, nashauri kama itawezekana, kuna haja kubwa sana ya kufanya tathmini kwenye huduma ya afya na fedha nyingi zinatumika kwenye huduma ya afya kwa kulipia gharama ambazo hazina uhalisia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, ukienda sekta binafsi, huduma ambayo kwenye sekta ya Serikali unapata kwa laki moja au na laki na nusu; kwa sekta binafsi ni kati ya

laki tano mpaka sita. Mifano ya wazi iko kwenye miwani, mifano ya wazi ipo kwenye vipimo na unasaini *form*, lakini wakati unasaini *form* ukilinganisha na huduma unayopata Serikalini kuna tofauti kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili linahitaji Serikali itazame upya na ione uwiano au utofauti huu uliopo ni kwa kiasi gani tunaweza kuwa na tofauti ya kawaida. Sioni sababu za msingi za gharama hizo kuwa kubwa kwa sekta binafsi wakati kwetu sisi haipo. Ninavyoona ni vile kwenye vituo vyetu tunakosa kabisa huduma hizi na tunapokwenda sekta ya binafsi basi wao wana maamuzi yao binafsi juu ya utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili lilitusumbua sana, kama alivyozungumza Mheshimiwa Abbas Tarimba, wakati wa uchaguzi hoja nyingi zilizopunguza kura za CCM ilikuwa huduma za afya; huduma ya afya kwa wenyewe bima, huduma ya afya kwa wananchi, huduma ya afya kwa wazee, huduma ya afya kwa watoto na huduma ya afya kwa mama na mtoto. Hapa tusipapase wala kupaka mafuta kwa mgongo wa chupa. Tunalo tatizo kwenye huduma ya afya kwa sababu sera inazungumza tofauti na hali halisi iliyoko kwenye maeneo ya huduma. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inatakiwa itazamwe kitaalam nini kifanyike, kwa mfano, kwenye jimbo la Mbulu Mji, tulikuwa na wakati mgumu sana wa kutetea kura za CCM kwa sababu *ambulance* ambayo inamsafirisha mgonjwa wa rufaa anayetoka Hospitali ya Mji wa Mbulu kwenda Haidom lazima awe na laki moja ya mafuta ya *ambulance*, vinginevyo mgonjwa huyu hata angekuwa amepata matatizo hasafirishwi haraka ili kuokoa maisha yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninachozungumza ni kwamba, wakati fulani tunapotoa huduma nadhani kuna haja ya kuwasikiliza wale wanaopokea huduma nao wanasesma nini kuhusu huduma tunayotoa sisi kama Serikali. Kwa nini nazungumza hivi? Kijana anayepata ajali wa bodaboda, familia ya kwao unakuta haina uwezo ya kulipa

hiyo *ambulance* kwa laki moja. Sasa mgonjwa huyu hatahudumiwa kwa wakati na kwa umuhimu ulioko ili aende kwenye kituo cha afya au kwenye hospitali ya rufaa ili aweze kuhudumiwa. Kwa hiyo, nadhani eneo hili litazamwe, Serikali haifanyi biashara inatoa huduma na kama tunatoa huduma kuna maeneo nyeti ya kutazama.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni eneo la huduma ya mama na mtoto. Kuna ushahidi wa wazi hususani jimbo la Mbulu Mji, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wapokee taarifa hii nimeshawaeleza hata tukiwa wenyewe kwamba kuna haja kubwa ya kutazama upya Hospitali ya Mji wa Mbulu na huduma inavyotolewa. Tunalo tatizo unakuta akinamama wajawazito wanaingia kwenye gharama; analipia vifaa tiba pamoja na gharama mbalimbali ili aweze kuhudumiwa kwa ajili ya kujifungua salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ninayoyazungumza nina ukweli nayo, nimekwenda hospitalini mara kadhaa kuwaauliza walioko kwenye huduma na wameniambia tunalo tatizo na wanasema nisiwe naondoka ondoka niwe nafika hospitalini kila siku. Sasa kwa kweli kazi Mbunge ni kukaa geti la hospitalini ama kwenye wodi ili kwa kuwa yupo ndio waweez kutoa huduma bora. kwa hiyo, nadhani hili jukumu ni muhimu sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ziara ya Kamati; Kamati zetu zinapopita, ziende basi kuwasikiliza pia wapokeea huduma, wafanye hata namna ya kusikiliza wanaopewa huduma wanasesmaje, kuliko kupita tu kukagua majengo ya hospitali, kukagua vitu mbalimbali, waende pia kwenye upande wa upokeaji wa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia vitambulisho vya wazee, wazee ndiyo walitolitumikia Taifa hili, naomba sana vitambulisho vya wazee walivyogawiwa havina huduma hospitalini, hakuna dirisha la wazee, hakuna afisa anayewashika mkono awapeleke wanapaswa kwenda wapi na kuangalia sehemu gani. Sisi kama Wabunge kuingia kwenye jengo hili kunatufurahisha sana, lakini tuangalie sana

kuingia kwenye jengo hili ni kwa ridhaa ya wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba hata Wizara ya Waziri, wawe wanafanya vikao Waziri na Naibu Waziri, wasipite tu barabarani, wasikilize wananchi wanasesma nini katika maeneo wanayofanya ziara ili wasikie huduma ya afya ikoje. Eneo hili ni muhimu sana, sisi Mbulu tuna vituo vitatu, tuna hospitali ya mji, hatuna gari la *ambulance*, hatuna mafuta, hata *Nurse* anataka alipiwe, tunakwenda wapi? Tunapokwenda ni wapi? Nadhani kuna maeneo tunakosea sana. Maeneo yetu ya kisera na maeneo ya wale wanaopokea huduma wanatushauri nini ili tukafanye vizuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa watumishi kwenye sekta hilo umeathiri sana huduma bora kwa akinamama, watoto na wazee kwa sababu eneo lao halifikiwifikiwi zaidi ya wale wagonjwa ambao wanamwona Daktari na Muuguzi, lakini eneo hilo la wazee, eneo hilo la akinamama na watoto, eneo hilo la watu wa bima ambao ndiyo watakaohamasisha bima ipendwe nchini, halina watumishi kwa kiasi kikubwa sana katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo kwa uchache sana kutokana na muda ni eneo hili ambalo nataka kuwaeleza kwamba, wakati fulani tunapotoa huduma hizi za afya, sisi tuwe kama kioo au kama kauli nzuri kwa sababu unakuta *Nurse* aliyeko hospitalini badala ya kauli yake kuwa sehemu ya tiba, anakuwa sehemu ya kuongezea ugonjwa. Tatizo ambalo si nzuri sana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, kengele imeshagonga.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitashika shilingi. Naunga mkono hoja. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt Paulina Nahato, atafuatiwa na Mheshimiwa Jumanne Sagini na Mheshimiwa Esther Midimu, ajiandae.

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili nichangie katika Wizara ya Afya. Awali ya yote napenda kumshukuru Waziri wa Afya kwa kutuwasilishia taarifa yake nzuri. Naomba nichangie katika sehemu moja tu ambayo ni elimu ya afya kwa jamii na hususani nitachangia katika sehemu ya tabia au tuna sema *behavior change*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kabisa kwamba magonjwa mengi ambayo yanaikumba jamii yetu yanaepukika. Tatizo kubwa ni kwamba wananchi wengi hawajui na kwamba kwa sababu hawajui hata tabia zile ambazo ni tabia hatarishi ambazo zinaweka katika mazingira ya kupata magonjwa, wananchi wengi hawajui hususani wananchi wanaoishi vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, magonjwa yapo, lakini watu hawajui, hawajui kwa kiwango gani magonjwa yapo na hata kama yapo hawajui yaani hakuna ufhamu wa kutosha kuhusu aina mbalimbali za magonjwa. Magonjwa aina zote; magonjwa ya kuambukiza na yale yasiyo ya kuambukiza. Kwa hiyo, watu wanaishi tu kwa sababu hawajui, mpaka mtu anapofikia sasa anaumwa ndiyo anaanza kushtuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba niishauri Serikali kuimarisha kitengo hiki Elimu ya Afya ya Jamii (*public health*), watu sasa wafikie kupata taarifa sahihi kwamba magonjwa yako kwa kiasi gani. Elimu itolewe; kwanza watu wajue kuna aina gani ya magonjwa na nini kisababishi cha haya magonjwa, tuna magonjwa mengi ambayo yanayosababishwa kutoka kwa mtu, mengine ni kutokana na mawasiliano ya wanyama na watu, mengine ni wadudu wengine ya kwenda kwa watu, lakini watu hawajui. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanaishi na Wanyama, hawajui kwamba wanyama wanaambukiza

magonjwa *zoonotic diseases* watu hawajui na kwamba hata yale magonjwa mengine ambayo yanatokana na maziwa, watu wanakunywa maziwa bila kuchemsha, hawajui kwamba ni rahisi kupata magonjwa fulani. Kwa hiyo, kunahitajika elimu kwanza ya kujua kuna aina gani ya magonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kwamba pia elimu itolewe ya kutosha kuhusu watu kubadili tabia zao, tabia ambazo zinaweza kuwaweka katika mazingira hatarishi ya kupata magonjwa. Kila mtu akishajua hivyo ni rahisi kujichunga na kama mtu mmoja atajichunga basi jamii yote ni rahisi kujikuta kwamba inakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu magonjwa. Kwa hiyo hatutalalamika sana kuhusu tiba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ni kwamba, watu wanaweza kujua juu ya magonjwa, lakini hawajui faida za kwenda hospitali. Wengi wanakwenda hospitali wakati magonjwa mengi yameshafikia katika *stage fulani* ambayo ni mbali. Kwa mfano magonjwa labda ya kansa hivi, magonjwa mengine, mtu anakwenda hospitalini akifika kule unakuta imeshakwenda imefikia *stage four*, sasa pale ndiyo tiba inakuwa ni ghali sana, wakati ambapo huyu mtu angejua dalili za awali, akaenda hospitali huyu mtu angetumia pesa kidogo tu kwa matibabu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo utamaduni wa tabia ya kwenda hospitalini ya kucheki afya mara kwa mara unakuwa haupo hata kwa watu wenye kipato hasa wenye kipato cha juu. Kwa hiyo matatizo haya ya ukosefu wa dawa yanakuja kwa sababu watu wanakwenda hospitali wakati tayari hali imekuwa ni mbaya. Kama ni presha imeshafika juu, kama mtu angekuwa na tabia ya kucheki afya mara kwa mara huenda angeshajigundua ana *BP* mapema, angechukua hatua mapema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusisitiza juu ya *behavior change*, kubadili tabia. Hivyo, basi vitengo katika Wizara ya Afya vijikite katika kuimarisha kubadili tabia

*behavior change aspect.* Baada ya hii watu kujua faida zake pia wajue changamoto ambazo wanaweza kuwa nazo. Mtu akiwa na afya anaweza kwenda hata Mumbai kwenda kucheki afya yake na mtakubaliana na mimi kwamba mtu anaweza akawa anaumwa kichwa, kuumwa kichwa siyo ugonjwa, ni dalili ya ugonjwa fulani, hasa huyu mtu anaumwa kichwa anakunywa *panadol* anajiona yuko sawa, hafanyi mazoezi anaendelea na shughuli zake, akisikia usingizi anakwenda analala, kumbe huyu mtu ana tatizo kubwa. Anapokuja wanashangaa huyu mtu ameanguka akiletwa hospitalini, huyu mtu yuko *ICU* matibabu ni makubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tujaribu pia kuimarisha hivi vitengo vya kuangalia tabia za watu, wajue pia ni changamoto gani watakazokumbana nazo wanapokwenda hospitali. Kwa hiyo kujengwe na hiyo tabia ya watu kucheki afya zao. Pia wanahitaji kukumbushwa mara kwa mara, watu wakumbushwe mara kwa mara. Hapa sasa siyo Wizara ya Afya tu, tunaingia Wizara ya Maji, yaani Wizarani ichanganyike na Wizara nydingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Michezo iwakumbushe watu faida za michezo; Wizara ya Maji iwakumbushe watu, Wizara ya Mifugo iwakumbushe watu kutokuchangamana na mifugo; na Wizara ya Uvumi iwakumbushe watu kutokutumia yale maji ambayo ni machafu. Kwa hiyo watu wapate kukumbushwa mara kwa mara na hivi vyombo vya habari vitumike hususani *television, radio, simu, mawasiliano* ya mara kwa mara ili watu wakumbushwe wajue hatari na mazingira yaliyoko kwamba ni hatarishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho Wizara pia iangalie suala la kuhakikishwa kwamba watu wanabadili tabia zao na kuwa na tabia zile ambazo zitawafanya wawe na afya ambayo tunaita *safe efficacy*, ni muhimu sana. Kama hivi vitu vyote Wizara itaviangalia kwa macho matatu, basi uwezekano wa kupunguza magonjwa mengi katika jamii zetu utakuwa ni mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sisi Wabunge ni vizuri kusoma mara kwa mara ili pia tutumike kama chombo cha kufikisha ujumbe wa masuala ya afya kwa jamii. Katika mikutano yetu, tusiongelee mambo yetu ya siasa tu, tuweke kipaumbele katika elimu na sisi tupate elimu, tuwe na shauku ya kujua magonjwa, maambukizi na jinsi magonjwa yanavyokuja na hatua za magonjwa ili watu wetu katika majimbo yetu iwe ni gumzo. Itakapokua ni gumzo tutajenga jamii ambayo itakua na afya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kutenga fedha za kutosha katika Idara hii ya *Health Promotion and Health Education* ili iweze kupata fedha za kutosha na pesa hizi zitumike katika kufikisha elimu ya afya kwa jamii ili watu waweze kuchukua hatua za kubadili tabia ambazo zinawaweka katika mazingira hararishi ya kupata magonjwa, tutaweza kuokoa fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia katika Wizara hii. Naunga mkono hoja. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jumanne Sagini, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Midumu na Mheshimiwa Agness Mathew Marwa, ajiandae.

**MHE. JUMANNE A. SAGINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia kwenye sekta hii ya afya ambayo ni muhimili wa amani na utulivu na maendeleo watu wenye afya watafanya vizuri kwenye shughuli za kilimo shughuli za elimu shughuli za ujasilliamali na nyinginezo. Na mimi kwa kuanza niungane na Wabunge wote waliopongeza juhudzi za Serikali na Wizara ya Afya mahususi katika kuimarisha sekta hii ya afya kwenye Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, karibu kila Mbunge yeoyote aliye koko hapa na asiyekuwepo anapotoka kuna athari ya jambo jema lili ofanywa na Wizara ya Afya kwa kushirikiana na sekta ya TAMISEMI. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, natoka Mkoa wa Mara, kule kuna Ushahidi wa jambo kubwa ambalo Awamu ya Tano na ya Sita watakumbukwa na wananchi wa mara hususani juu ya hiyo Hospitali ya Rufaa ya Mkoa. Hospitali ile ina historia ndefu ujenzi wake kwanza waliweka jiwe la msingi mwaka 1975, ujenzi ukaendelea mpaka mwaka 1987 ukasimama lakini kwa maamuzi yenye tija ya mpendwa wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli mwenyezi mungu amweke roho yake mahala pema peponi 2018/2019 waliweza kufanya uhamuzi wa kutoa zaidi ya bilioni 15 kwa ajili ya kuhakikisha hospitali ile inakamilishwa. Na sote sasa tunaona hospitali ile inapendeza bahati nzuri imejengwa kwenye mwinuko wa Mlima Mkendo ina vutia sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sasa, Serikali ikamilishe majengo machache yaliyobaki ili huduma muhimu za rufaa ngazi ya mkoa ziweze kuanza kutolewa kwa ukamilifu. Lakini hilo la muhimu kwa majengo yaliyokamilika ambayo yanaweza kuanza kutoa huduma za rufaa ngazi ya mkoa, ni vizuri tupate vifaa tiba majengo yale ukifika utakuta maeneo mengi yanayotakiwa kuwepo vifaa tiba hakuna vifaa tiba ndio maana hadi sasa huduma zinaendelea kutolewa kwenye hospitali iliyokuwa inatumika kimsingi ni hospitali ya wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni watumishi Wabunge wengi waliozungumza wameonyesha upungufu wa watumishi maeneo yote sasa na huku ambako tumejenga hospitali hizi mpya, ni vizuri kuwe na mkakati maalum kama wa ajira kwa ajili ya watumishi wa kada zote za sekta za afya zinazohitajika. Wakiwemo madaktari, madaktari bingwa, wauguzi wafamasia wataalam wa usingizi nakadhalikadhalika. Kwa hospitali hii ya rufaa ya Mkoa wa Mara ina upungufu mkubwa sana, niombe wizara kwa jambo jema mlilolifanya likamilishwe kutuletea wataalam wa kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ninalotaka kuzungumza kwenye sekta ya afya ni mafunzo ya watalaam wa afya hususani madaktari bingwa, uzoefu unaonyesha

kuwa hospitali kubwa za mijini hasa majiji makubwa ya Dar es salaam, Arusha, Mbeya, Mwanza, Tanga nakadhalika, wanaomadaktari na madaktari bingwa wakutosha, kuliko mikoa inayoonekana ni ya pembezoni, kiasi kama mkoaa wangu wa mara. Nakumbuka miaka michache iliyopita wizara ilifanya uhamuzi wa kufanya *rationalization* ya kuhamisha bahadhi ya madaktari bingwa kutoka jijini Dar es salaam, na kuhamishia mikoa ya kusini na mikoa yetu kama kule Simuyu nakadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilivyoonekana wataalam bingwa waliokwisha zoea Dar es Salaam si rahisi sana kukubali kwenda kufanya kazi kwenye mikoa hii ya pembezoni. Taarifa nilizonazo wengi wa madaktari wale waliamua *ku-resign* waliamua kuacha kazi na kurudi Dar es Salaam. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri sasa kwenye hilo tufanyaje, ninadhani wakati umefika sasa tuzisaidie hizi Hospitali za Rufaa za mikoa huko zilizo wawe na utaratibu wakuwaendeleza watumishi wao mabingwa, kama mtu ameshazoea kuwa Musoma kule ukienda ukampeleka ni rahisi kurudi lakini aliyezoewa Dar es Salaam ukwamwambia nenda Musoma anaona kama vile katupwa hivi na wengi wanasema nimetupwa Mara nimetupwa Mtwara, nimetupwa Katavi wakati kule kuna watanzania wanaohitaji huduma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwenye hili naomba niwapongeze *of course* Katibu Tawala wetu wa Mkoa wa Mara pamoja na *medical officer incharge* huyu Dr. Johakimu Eiyembe na *RMO* wake kwa uhamuzi wakutraini maafisa wataalam wao wanne. Lakini kwa uamuzi ule wa kutumia mapato yao ya ndani wizara ikaamua kuwasaidia kuwasomesha mmoja vitu vyaa aina hii vikiendelea vitatupunguzia mahitaji makubwa ya madaktari bingwa kwenye hizo hospitali za pembezoni. Kwa hiyo, hili niwasifu Wizara kwa kulifanya kwa ajili ya wataalam wetu kutoka kule Mkoa wa Mara, lakini liendelee kufanyaika mara kwa mara ili kujenga uwemo wa hospitali hizi za pembezoni pia kupata wataalam wanahitajika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni makusanyo ya mapato ya ndani, ukipitia taarifa ya wizara ya utekelezaji utaona kwamba kwa sehemu kubwa, taasisi za Wizara hazikusanyi vya kutosha mapato yao ya ndani. Na nimeona zipo taasisi chache kwa idhini yako nizitaje zimefanya vizuri sana. Hospitali ya Mloganzira kwa mfano imekusanya zaidi ya asilimia 99 ya malengo yake lakini ipo Hospitali ya Benjamin Mkapa hii imevuka malengo kwa asilimia 118 ambako imekusanya zaidi ya shilingi bilioni 13, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili imekusanya zaidi ya asilimia 74 sawa na bilioni 45, taasisi ya chakula na lishe asilimia 73 lakini taasisi nydingine zinazobaki zinasuasua sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili pia lipo kwenye hospitali za Rufaa za Mkoa, pia kuna mapungufu ya ukusanyaji, ushauri wangu kwenye hili wizara iweke utaratibu wa watu kwenda kujifunza kwenye hizo hospitali zilizofanya vizuri ili uzoefu huu usaidie kuimarisha mapato ya ndani kwenye hospitali zingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkona hoja nawatakia heri katika utekezaji wa majukumu yao. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ester Midumu tutamalizia na Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hili niwese kuchangia kwanza kabisa nampongeza Waziri na Naibu waziri kwa hotuba yake nzuri iliyosheheni matumaini ya watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali yangu ya Chama Cha Mapinduzi kwa kutupatia pesa bilioni 5.4 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali za Wilaya, Wilaya ya Busega Bariadi DC na Itilima. Mchanganuo wake kila wilaya tumepata bilioni 1.8 lakini pia tunachangamato ya ukosefu wa vifaa tiba pamoja na madawa. Changamoto hii ni kubwa sana katika vituo vyetu vya afya pamoja na Hospitali za Wilaya wananchi

wanatoka vijijini kwenda kutibiwa kwenye Vituo vya Afya wakifika wanakosa madawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo inasikitisha sana mwananchi akitibiwa anaambiwa kwenda kununua dukani kuna wananchi wengine wana hali duni hawana uwezo wa kununua dawa, naiomba Serikali iweze kutuletea dawa za kutosha katika hospitali zetu. Lakini pia katika vituo vyetu vya afya mkoa wa Simiyu hatuna *x-ray* mashine, hiki kifaa ni muhimu sana ikiwezekana naiomba Serikali ibaini vituo vyote vya afya nchi nzima ambavyo havina *x-ray* mashine ili waweze kufunga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wetu hawa wa bodaboda wanapata ajali, wakienda kwenye kituo cha afya wanapewa tiba ya dharula ambayo ni ya mwanzo kwamba atibiwe halafu baadaye aende katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa. Kwa vile vijana wetu wanaimani potofu wanaendea kwa waganga wa kienyeji hatimaye kidonda kinaoza wengine wasukuma wetu kule anawenza akapata ugonjwa wa *TB* hajapigwa *x-ray* anaenda kwa waganga wa kienyeji anatumia dawa za kienyeji akienda kwenye kituo cha afya hamna kipimo cha *x-ray* anaishia kutumia madawa ya kienyeji anaathirika naiomba Serikali ifanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine katika vituo vyetu vya afya hatuna umeme mbadala ambaao ni jenereta, daktari akiwa anamfanyia mama mjamzito *operation* umeme ukikatika inakuwa ni shida naiomba Serikili ifanye utafiti katika vituo vya afya vyote ambavyo havina umeme mbadala ambayo ni jenereta ili waweze kufunga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia katika vituo vyetu tuna upungufu mkubwa wa madaktari hasa madaktari bingwa wa magonjwa ya akina mama, sisi akina mama tuna maradhi mengi, ukienda hospitali huwezi ukatibiwa na daktari wa kawaida kuna malazi mengine ambayo unatakiwa umwone *specialist* wa magonjwa ya wanawake. Sisi Mkoa wa Simiyu tuna mmoja tu ambaye yupo Somanda, na katika Mkoa wa Simiyu tuna Wilaya tano huyo daktari anahudumia

wilaya tano unakuwa msongamano mkubwa, daktari anachoka tunaiomba Serikali ituletee madaktari bingwa katika hospitali zetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hospitali yetu ya mkoa, kwanza niipongeze Serikali kwa kutupatia pesa kujenga hospitali yetu ya Mkoa katika hospitali yetu ya mkoa bado hajakamilika hatuna wodi ya akinamama, hatuna wodi ya watoto, na hatuna wodi ya akina baba. Jengo la mama la mtoto bado halijakamilika na pesa ipo sijui tatizo ni nini, Mkandarasi anasua sana tunaiomba Serikali waziri akija aje na majibu kwa nini hilo jengo linasuasua na pesa ipo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hospitali yetu ya mkoa hatuna uzio kabisa, na hospitali ikikosa uzio ni hatari sana hospitali yetu ya Mkoa wa Simiyu iko karibia na barabara ya lami, wagonjwa katika hospitali wanaenda wa kila aina kuna mwingine anaweza kwenda amerukwa na akili anakimbilia kwenye lami anagongwa gari lakini pia uzio unadhibiti hata kuibwa madawa na vifaa tiba. Naiomba Serikali itupatie pesa ili tuweze kujenga uzio. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali kwa kutuboreshea hospitali ya Maswa tuna *theatre* nzuri na tuna wodi nzuri za kulaza wagonjwa lakini tatizo *mortuary* ni ndogo inachukuwa watu watatu Tunaomba tupatiwe friji ili tuweze kuipanua hiyo *mortuary*. Lakini pia katika Vituo vya Afya vya Mkoa wa Simiyu hauna friji za kuhifadhi maiti. Tunaiomba Serikali iweze kutuletea friji katika vituo vyetu vya afya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hospitali inayotibu saratani ni moja tu hiko Dar es salaam ambayo ni *Ocean Road* na wagonjwa wengi wanatoka kanda ya ziwa, tunaomba Serikali iboreshe hiyo hospitali ya Bugando ili kuweze kurahisha matibabu wananchi wanaotoka vijijini kanda ya ziwa watibiwe hapo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia wizara hii kwanza niwapongeze sana waziri na watendaji wote katika wizara hii, lakini pia nimpongeze kipekee dada yangu kwa awamu iliyopita daktari wa *covid* Mheshimiwa Waziri Ummy kwa kazi kubwa aliyoifanya kipindi kilichopita pamoja na Serikali nzima akiwemo Mheshimiwa wetu Hayati John Pombe Magufuli pamoja na mama yetu Samia kwa kazi nzuri waliyoifanya kipindi kilichopita ambayo sasa mama anaiendeleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwa kweli hotuba ya juzi ya mama alipokuwa na wazee nampongeza sana Mheshimiwa wetu Rais kwa moyo huohuo Mwenyezi Mungu amwongezee sana na azidi kumpa hekima na sisi tunamuombea sana aliposema kwamba huduma ya afya kwa wazee iboreshwa. Naamini kabisa mama yetu wewe ni mama na bahati nzuri ulianza na baba, baba katuacha na wewe, kwa hiyo, tunaamini kabisa wazee hawa wanategemea faraja kutoka kwako kama ulivyosema Mheshimiwa Rais wetu kwamba huduma hii itaboreshwa tunaamini kabisa suala hilo litasimamiwa vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuombe waziri na watendaji wako, Mheshimiwa Rais ametoa maagizo huduma kwa wazee iboreshwa sio sasa mpaka aje kuanza kutumbuatumbua ndio muanze kufanya vizuri. Niwaombe sana hili suala mliangalie kwasababu hawa wazee pia watoto wao ni wapiga kura wenu na wao wenyewe ni wapiga kura wenu lakini pia kwa kura za kishindo walizozitoa sasa hivi watananzania wanasubiri na kutegemea matokeo chanya kwa wabunge wao na kwa serikali yao. Kwa hiyo, niseme tu naamini kabisa Mheshimiwa Waziri uliyechaguliwa

ni jembe na ninaamini kabisa wewe ni mtendaji mzuri, hawa wazee watapata faraja kutoka kwako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nikuombe sana, Mheshimiwa Waziri sasa aangalie hili suala la watoto wa chini ya miaka mitano. Kule kwetu Mkao wa Mara na hasa katika hospitali nilizokwenda kukutana na malalamiko haya kwamba watoto wa chini ya miaka mitano wanalipishwa wakati watoto wale wanatakiwa wapate huduma bure. Nafikiri sio jambo zuri Mheshimiwa Waziri lifatilie na ikikupendeza naomba tuongozane nikakupeleke maana ushahidi ninao na baadhi ya stakabadhi walizolipia nilichukuwa kabis ushahidi ninao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ila tu ukifika usiwatumbue urekebishe tu mambo ili yakae sawa kwa hiyo niseme tu kwa kweli wananchi wetu wanaumia, tusimamie vitu tunavyokuwa tunaviahidi lakini pia tufanya kwa kadri ya mapenzi ya Mungu tukiwa tunajua kwamba kesho ahera tutajibu nini, sio tu watupigie kura wakimaliza kutupigia kura watanzania hawa vitu vingine tunakuwa kama vile hatuwaatendei haki wakati sisi wenyewe ndio tumeahidi kutoka midomoni kwetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niishukuru sana Serikali yangu ya Chama Cha Mapinduzi kwa kipindi kilichopita na sasa hivi kwa kutejengea hospitali nzuri sana ya rufaa hospitali ile kwa kweli ilikuwa na muda mrefu sana na sasa imejengwa iko vizuri, na imeanza kutoa huduma lakini tu kama alivyosema Mbunge mwezangu Mheshimiwa wetu waziri tungeomba sana kwasababu Mkao wa Mara kiukweli ni kwamba ni mkao ambao mnatakiwa muuweke ukae kimkakati kwasababu ndio mkao uliomtoa Mhasisi wa Taifa hili Hayati Mwl Julius Kambarage Nyerere. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, basi ile hospitali ya rufaa irekebishe vitu viliviyobaki ili kusudi sasa na mkao wa mara wale wanaojua wale watu wanaojua maana kule sisi kuna bibi zetu ambao mpaka leo wanajua Mwl Nyerere yupo Butiama hawajui kama ameshakufa mpaka leo ukienda kule

vijijini saa nyingine wanakuambia ah sisi tunaenda kuchagua chama cha Mwl Julius Kambarage Nyerere. Sasa kwasababu hiyo basi mazingira yaboreshwa hata sisi tuonekane kwamba akina Agnes tunatoka Mkoa wa Muhasisi wa Taifa hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa wangu waziri ufanye kweli nakuamini sana waziri najua utafanya kweli. Lakini kipekee zaidi niseme tu hivi sasa, hivi tumejenga hospitali nyingi sana na nzuri sana tena za kimkakati zinazoweza kuwasaidia wananchi wengi sana, katika sehemu zote mikoa yote vijiji vyote hospitali zetu jamani ni nzuri sana. Lakini Vituo vya Afya vimejengwa vingi sana. Mheshimiwa Waziri kama vilevile ardhi waliyyokaa kamati nane, basi Mheshimiwa Waziri na wewe pia ukakae chini na waziri au Wizara ya Ujenzi ili muangalie hizi hospitali ziweze kufikika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mama anataka kwenda hospitalini lakini sasa unakuta sehemu zenyewe hazipitiki ni mabonde kuinama sasa kama ni mabonde kuinama inakuwaje yani mabonde kuinama namaanisha kwamba hapa kuna shimo mara hapa kuna mtaro umekaa vibaya mara hapajarekebishwa. Kwa hiyo, niombe sana hii Serikali yetu naamini ni Serikali Sikivu, na haya mambo ambayo tunayashauri naamini kabisa yatakekelezeka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe sana mama yetu Mheshimiwa Rais mama yetu kipenzi Raisi wa kwanza mwanamke Tanzania kwa mambo haya yote tunayoyasema hapa mawaziri wake kama watayaafuata na kuyashikiria naamini kabisa wakiyatekeleza, na hizi pesa zitoke kwa wakati sio tu tuwe tunaongea hapa maneno tunasema weeee! Pesa mara zimetoka kidogo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa kengele imeshagonga.

**MHE. AGNES M. MARWA:** ...mara mkandarasi, nashukuru sana naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa siku yetu ya leo niwapongeze kwa Wabunge waliopata fursa ya kuchangia namuona Mheshimiwa Waziri hapo anaandika kwa bidii kabisa.

Jambo moja dogo Mheshimiwa Waziri wakati mnaboresha hii miundo mbinu sehemu nyingine mmepeleka madaktari wazuri kabisa kwenye ngazi ya Vituo vya Afya. Ambao wana hadhi ama ule utaalam wao unalingana na aliyepo kwenye Wilaya na aliyeko kwenye hospitali ya rufaa ya mkoa. Sasa mazingira kama hayo akiwekewa yale masharti ya dawa yale mliyonayo kituo cha afya ye ye hawezi kuandika wakati ye ye analingana kabisa na daktari aliyepo kwenye Hospitali ya Wilaya au Hospitali ya Rufaa ya Mkoa. (Makofi)

Kwa namna hiyohiyo Kituo cha Afya kinakuwa hakiwezi kufanya kazi vizuri na bima yetu ya afya kwasababu sasa inabidi mtu ashauriwe aende kwinge hili akapate dawa huko kwasababu daktari liyeko pale hawezi kutoa huduma wakati mmeboresha hicho kituo cha afya kina kila kitu. Lakini sasa hawezi kutoa hizo huduma kwasababu mmeweka yale masharti ya dawa hapo. Kwa hiyo, tujitahidi na hilo nalo kuliangalia kwa hapo baadaye kurekebisha hapa na pale sehemu ambap vituo afya ni vikubwa kama hospitali za wilaya basi wawewe kutoa huduma vizuri ili wananchi wasilazimie kwenda mbali. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.02 Jioni Bunge lilahirishwa hadi siku ya Jumatano  
Tarehe 12 Mei, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*